Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 3 Julai, 2009**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI :-**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2009/2010.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:-**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza maswali ningependa kutoa taarifa hii kwamba jana ilitolewa hoja ya kuahirisha mjadala wa kupitisha Makadirio ya matumizi ya Wizara ya Miundombinu hadi baada ya kipindi cha maswali leo ili kutoa nafasi kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kufikiria hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Athony Diallo, juu ya kusudio lake la kufanya mabadiliko kwenye baadhi ya vifungu vya Wizara.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 30 Kanuni Ndogo ya Sita ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, nainukuu. « Shughuli za Bunge katika kila Kikao zitatekelezwa kwa kufuata Orodha ya Shughuli ya siku hiyo au kwa kufuata utaratibu mwingine ambao Spika ataagiza ufuatwe kwa ajili ya uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge.

Baada ya kushauriana na Serikali na kutafakari uzito wa suala hili nimeona ni busara kutoa nafasi tena kwa pande zote mbili Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Serikali kuendelea na mazungumzo ambayo yataleta tija kwa manufaa ya nchi yetu na kwa kuzingatia kwamba hatuwezi kupoteza siku nzima ya leo tukisubiri uamzi wa suala hili nimeona ni vema tuahirishe mjadala wa hoja ya Wizara ya Miundombinu hadi tarehe 4 Julai, 2009 siku ya Jumamosi na badala yake Bunge liendelee kama kawaida kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuwasilisha bajeti yake leo kama ilivyokuwa imepangwa kwenye ratiba ya jinsi ya Wizara kuwasilisha Bajeti zake.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ninachokisema hapa tunaendelea na utaratibu wa siku ya leo. Lakini kesho saa tatu tutaendelea na Wizara ambayo tumeahirisha. Sasa tunaingia kwenye maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, atauliza swali la kwanza.

Na. 152

**Mgogoro wa Ugawaji mali na watumishi wa Halmashauri Mpya**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya Halmashauri zinapogawanywa hutokea migogoro juu ya mgawanyo wa mali na watumishi:-

Je, ni utaratibu gani na Sheria ipi hutumika katika mgawanyo wa mali hizo pamoja na watumishi ?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kugawanywa kwa Halmashauri huanzia kwenye Halmashauri yenyewe kujenga hoja na kuijadili kwenye vikao vyake vyote kwa mujibu wa Sheria. Vikao hivyo ni pamoja na Baraza la Madiwani la Halmashauri husika na Baraza la Ushauri la Wilaya *(DCC)* na lile la Ushauri la Mkoa *(RCC).* Makubaliano ya mapendekezo hayo huwasilishwa kwenye Mamlaka ili kuweza kuridhia maombi na mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayosimamia mgawanyo wa mali mara Halmashauri inapogawanywa ni Sheria inayotoa utaratibu wa kuanzisha Halmashauri. Sheria hiyo ni Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 kwa Halmashauri za Wilaya na Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288 kwa Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji. Kifungu cha Saba (7) cha Sheria hizo ndicho kinachompa Madaraka Waziri Mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kutoa Amri *(Order)* ya kugawa Halmashauri na kuanzisha Halmashauri nyingine. Katika Amri (*Order)* hiyo, Waziri ataeleza utaratibu wa kugawa mali na madeni. Endapo hatafanya hivyo katika *Order* inayoanzisha Halmashauri; atatoa Amri nyingine itakayoelezea utaratibu wa mgawanyo wa mali na madeni *(Division of Assets and Liabilities).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya Waziri Mwenye Dhamana kutoa Amri ya mgawanyo wa mali na mali na madeni huitaka Halmashauri kufanya yafuatayo:-

(i) Kufanya tathimini ya mali na madeni;

(ii) Kuainisha umiliki wa mali *(ownership);*

(iii) Kuanzisha mgawanyo wa mali na madeni kwa kuzingatia mahitaji na uwezo wa kila Halmashauri itakayoundwa (yaani Halmashauri Mama na ile Halmashauri mpya);

(iv) Uwezo wa mapato kwa Halmashauri zinazotarajiwa kuundwa *(Financial Capacity);* na

(v) Kuainisha mgao wa watumishi kwa kuzingatia Ikama na mahitaji ya kila Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchakato huo, mapendekezo hayo huwasilishwa kwa Waziri Mwenye Dhamana ili yawekwe kwenye Amri *(Order)* ya kugawa mali, yaani *Local Government Authorities (Division of Assets and Liabilities) Order*. Kimsingi mgawanyo wa mali unapaswa kuzingatia Amri yaani *Order* ya Waziri japo pale ambapo hakuna mgogoro mgawanyo unaweza ukafanyika.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri zinapogawanywa hugawanywa pia watumishi na hivyo kupelekea Ikama ya Wakuu wa Idara kupungua katika Halmashauri Mama na ile Ndogo inayoanzishwa. Je,

Mheshimiwa Waziri unazisaidiaje Halmashauri zilizogawanywa kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Nanyumbu na Mji Mdogo wa Masasi kuweza kupata Wakuu wa Idara ambao wenye sifa?

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mgawanyo huu wa Halmashauri unapofanyika vile vile hugusa katika mali. Je, kwa kuwa kunakuwa na mali ambazo hazihamishiki, Serikali huzisaidiaje zile Halmashauri Mpya zinazoanzishwa ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya kujenga majengo ya Ofisi, nyumba za watumishi na kadhalika ili kuharakisha maendeleo ya Wilaya zile mpya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kumpa pole Mheshimiwa Mariam Kasembe kwa kufiwa na mwanawe, nilisahau kuisema mwanzoni na najua limeshapita hili lakini tutamtakia kheri na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe moyo wa subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapokuwa tunagawanya Halmashauri zimekuwa ni mbili, nimeeleza utaratibu wake unavyofanyika. Mnawachukua wale watumishi wote walioko pale na mnaanza kuwagawanya katika Halmashauri zote mbili kufuatana na wale watumishi walioko katika hiyo Halmashauri Mama, unasema tunaanza hapa na *DO* kwa mfano, unasema *DO* anakwenda Masasi yule anayemsaidia *DO* pale kuna Maofisa wanaomsaidia pale anakwenda Nanyumbu, mnatoka hapo nmakwenda nafasi nyingine, mnasema *DALDO* mnachukua mmoja anakwenda Nanyumbu mwingine anakwenda Masasi. Mnawagawanya wale hivyo hivyo mpaka wanamalizika pale wanakuwa wameondoka.

Ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Kasembe inawezekana kabisa katika mgawanyo ule ikaonekana kwamba kuna nafasi nyingine ambazo zinaonekana hazijajazwa hasa katika Halmashauri Mpya na ninasema maneno haya kwa sababu mimi mwenyewe kwa zile Halmashauri Mpya ambazo ziliundwa Wilaya ya Siha iliundwa pamoja na Wilaya ya Nanyumbu. Inapotokea sasa pale wamekuwa na tatizo hilo kinachofanyika sasa ni kuwasiliana na Wizara na Wizara sisi tunawasiliana na wenzetu wa Utumishi ili kuona hizo nafasi ambazo zinaonekana kwamba hazikupata watu ili wale waweze kupatikana na ili waweze kusaidia katika hizo Halmashauri zinazohusika.

Pia amezungumzia kuhusu mali ambazo hazihamishiki, Nanyumbu-Masasi. Masasi huwezi kusema hili Boma lihame sasa liende Nanyumbu kwa sababu liko pale. Huwezi kusema hii hospitali ihame hapa iende Nanyumbu, kwa sababu iko pale. Vitu ambavyo watagawana pale Mheshimiwa, lakini ambavyo vitazingatia pia kwamba ni vitu gani vimebakia pale ni vile ambavyo vinahamishika. Kwa mfano walipokuwa wanagawana wenzetu hawa Masasi na Nanyumbu maeneo ambayo yalibakia yalikuwa maeneo yale yanahusu suala la greda, suala la *VX* pamoja na Kijiko wakafikia uamzi wakasema mambo yafuatayo:-

Wakasema kwamba greda libakie Masasi na wakasema kijiko kiende Nanyumbu na wakasema na *VX* ile ambayo ilikuwa imechakaa nayo iende Nanyumbu. Hawakuweza kuelewana katika jambo lakini tumezungumza na *RAS* inaonekana sasa watafikia mwisho ili waweze kugawana. Vinginevyo Serikali nayo inasaidia katika kuanzisha Mamlaka Mpya na ndiyo maana unaliona Boma la Nanyumbu limejengwa pale na zile nyumba nyingine na huduma nyingine ambazo zinahitajika Serikali huingia na kusaidia pamoja na wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Lakini kunakuwa na mgogoro kweli kweli. Hata wewe unajua hata Njombe kuko hivyo hivyo. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kuniona ili niweze kuuliza swali lingine dogo la nyongeza. Kwa kuwa ni kweli kabisa migawanyo hii ya Halmashauri kwa kipengele cha mali zisizohamishika imekuwa ikileta migogoro mikubwa kama ule mgogoro ambao uko sasa hivi kati ya Halmashauri ya Songea na Namtumbo na hasa katika eneo la mali zisizohamishika ambazo ziko Songea na lakini Namtumbo pia nao nafikiri kwamba wangepata kufaidika na mali hizo.

Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuliambia Bunge hili na kuiambia Halmashauri ya Wilaya ya Songea Halmashauri Mama kwamba kama mgogoro huo kwa namna ulivyo hitimishwa hautakuwa ukii-*favour* Halmashauri Mama ambayo ni mlezi, yuko tayari kupokea rufaa na kuangalia upya namna ya kusuluhisha mgogoro huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo analizungumzia Mheshimiwa Jenista Mhagama tunalifahamu na tatizo hili limeletwa Ofisini kwetu likaletwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo.

Hili nalo ambalo wanalizungumzia hapa ni eneo ambalo ni majengo ambayo yako katika Manispaa ya Songea na walipofika mahali wakaamua kwamba sasa wanataka kugawana ile mali, yalionekana majengo yanayozungumzi hapa kulikuwako na soko na jengo lingine ambalo linatumika kama hoteli kama sijasahau. Wakakubaliana kwamba mmoja abakie na biashara hii na mwingine abakie na biashara hii na hao wanafahamu. Wanaelewa hilo jambo.

Sasa Mheshimiwa mimi niseme hapa, hapa mimi siwezi kufanya maamuzi mengine nje ya maamuzi yale ambayo yalishafanyika na majibu tulishayatoa hapa.

Nikifanya hivyo nitakuwa nakosea sana na kama kuna jambo lolote ambalo wanafikiri Mheshimiwa Waziri atatakiwa aingilie kati tunaweza tukafanya hivyo, lakini nakumbuka Mheshimiwa Vita Kawawa alilileta na tukalitolea maelezo. Sina maelezo mengine nje ya yale ambayo tulimpatia. *(Makofi)*

Na. 15

**Kukarabati Bwawa la Maji-Kihanga**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Bwawa la Kihanga ni muhimu sana kwa uvuvi wa wanavijiji vya Kihanga, Mninga, Igowole Ibatu, Nziri na Nyololo na kwa kuwa kuta zinazozuia maji katika Bwawa hilo zimelika kutokana na kujengwa tuta la udongo na hivyo kuwa hatari sana kwa vijiji vilivyo chini ikiwa bwawa litabomoka kutokana na wingi wa maji:-

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya hali hii?

(b) Je, Serikali iko tyayari kukarabati bwawa hilo liwe salama zaidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la Kihanga ni muhimu sana kwa shughuli za uvuvi kwa wananchi wa Vijiji vya Kihanga, Mninga, Igowole Ibatu, Nziri na Nyololo.

Shughuli za uvuvi husaidia kuwaongezea kipato wananchi, wanapambana pia na umaskini na kuwapatia lishe. Iwapo kuta zinazozuia maji katika bwawa hilo zitabomoka ni hatari kwa wananchi wanaoishi jirani na Bwawa hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kubaini uwezekano wa tuta la Bwawa la Kihanga kubomoka na kuruhusu maji mengi kutoka, Halmashauri ya Wilaya Mufindi imeamua kuchukua hatua zifuatazo:-

(i)Kuzuia shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo, na makazi katika umbali usiopungua mita 60 kutoka kingo za Bwawa na mita 20 kutoka vyanzo vya maji kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004.

(ii) Kuhakikisha usafi wa mara kwa mara unafanyika katika mifereji ya kupunguzia maji ili kuondoa uwezekano wa maji kupita juu ya tuta.

(iii) Kwa kuzingatia ongezeko la maji katika Bwawa na madhara yanayoweza kujitokeza siku za usoni kwa wananchi, Halmashauri ya Wilaya katika Bajeti yake ya mwaka 2009/2010 imetenga kiasi cha fedha shilingi milioni 8.6 kwa shughuli za ukarabati wa Bwawa la Kihanga.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jibu zuri sana la Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi binafsi nilitembelea bwawa lile. Lile

bwawa linahitaji *design* ya *retaining walls* ili kwamba zile kuta ziwe na nguvu kwa maana hiyo hizi milioni 8.6 nina hakika hazitoshi. Je, Serikali iko tayari kwenda Wizara yenyewe kwenda kutathmini gharama halisi ya bwawa lile na kusaidiana na Halmashauri ya Mufindi ili waweze kulijenga?

Swali la pili, lile bwawa la Kihanga, ni tofauti na bwawa la Ngwazi, lile bwawa la Kihanga lina samaki wadogo wadogo sana kiasi kwamba wavuvi hawa hawapati samaki wazuri na wenye faida. Je, Serikali iko tayari kupanda kwa kusaidiana na wananchi wa Ngwazi na vijiji vinavyohusika ili kwamba waweze kupandwa samaki watakaokuwa wakubwa na wenye lishe ya kutosha na wenye faida kwa wavuvi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mhesihmiwa Naibu Spika, kwanza mimi mwenyewe binafsi naomba nikiri kwamba hil Bwawa sijaliona na kwa hiyo Mbunge kama anasema *retaining wall* inaonekana ni dhaifu, siwezi kumpingia hapa. Maana yake yeye ni mamlaka atakuwa anajua vizuri zaidi kuliko mimi hapa ninayezungumza. Siwezi kupinga hapa kwa sababu nikipinga hapa bwawa likabomoka pale watu wakafa mimi hapa nitawekwa kitimoto.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba jitihada tuliyoifanya hapa ni hiyo ya kutenga milioni 8.6 ambazo kwa mujibu wa Mbunge anavyotueleza hapa anaona kiasi hiki hakitoshi. Kwa hiyo kuna haja ya kwenda kuangalia tena upya ili tuweze kuona kwamba tunafanya nini katika jambo hilo. Hili mimi silikatai, mimi nitaondoka hapa na Mheshimiwa Malangalila tukaenda kule, nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba niende nikaangalie jambo hilo na kama kutakuwapo na haja ya kusaidia kwa sababu linahusu na maisha ya watu, sina tatizo kabisa na hilo.

Kwa hiyo, kiasi kilichotengwa ni hicho lakini kama kutakuweko na gharama zaidi basi tunaweza tukasaidiana wote kwa pamoja na wananchi na Halmashauri tukaangalia tutafanya nini.

Kuna hili analozungumza la kuona kwamba samaki wale walioko pale ni wadogo kwa hiyo labda tungeongeza aina nyingine. Hili sasa nikijibu hapa linahitaji wataalam sasa. Wataalam watushauri vizuri, watuelekeze vizuri watuambie kwamba je, ukiingiza samaki hao humo ndani hawatawamaliza wale wadogo halafu baadaye mkaja tena mkalaumiwa. Lakini naomba nimkubalie kwamba tutakwenda tukakae na wataalam tuzungumze halafu tutaona huo ushauri anaouleta wa kuingiza samaki wa aina nyingine ambao wataleta tija zaidi. Kwa kweli nadhani litahitaji utaalam kidogo. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nakushukuru Naibu Spika kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa haya mabwawa yaliyoko kwenye Halmashauri zetu yanasaidia sana wananchi na kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba ingefanya mpango wa kukarabati bwawa la Kinampundu na Miganga, je, Waziri yuko tayari kufuatilia ahadi hiyo imefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tupate nafasi ya kwenda

kuangalia, tuangalie wote kwa pamoja lakini ukweli bado linabakia kuwa ni suala la Halmashauri, lakini mimi nataka niseme hapa kwamba tutakuwa tayari kwenda kuliangalia na kuona jinsi ambavyo tunaweza tukasaidia.

Na. 154

**Mahitaji ya Umeme – Kibondo**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa ahadi ya Serikali ya kuwapatia wananchi wa Kibondo umeme wa kuaminika haijatekelezeka, na kwa kuwa, Shirika la kuwahudumia wakimbizi *UNHCR* lililoko Wilayani Kibondo linalo jenereta kubwa linalotoa umeme wa *KVA 60* na kusambaza umeme huo kwa watu wachache tu Wilayani na hivyo kutonufaisha wananchi wengi:-

Je, Serikali haiwezi kuzungumza na watu wa *UNHCR* ili wakubali kuwasambazia wananchi umeme wakisubiri utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kupeleka umeme kwa Wilaya za Mkoa wa Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme unaotokanana jenereta la Shirika la kuwahudumia Wakimbizi *UNHCR* ni la ukubwa wa 60 KVA (na wala sio 60 KV kama ilivyoandikwa kwenye swali).

Umeme wa *60 KVA* ni mdogo kiasi kwamba hautoshelezi kukidhi mahitaji ya umeme kwa wananchi wa Kibondo Mjini. Umeme huo unatosheleza matumizi yao pale *UNHCR* peke yao na baadhi ya seheu chache tu Wilayani hapo.

Katika upembuzi yakinifu *(feasibility study)* uliofanywa na Mshauri *SWECO* mwaka 2006 kwa kupeleka umeme Mkoa wa Kigoma pamoja na Wilaya zake, mji wa Kibondo ulitathminiwa na kukadiriwa mahitaji ya umeme kufikia 5,000 *KVA.* Kutokana na utafiti huo, umeme wa *UNHCR* usingetosha kabisa kwa kusambazwa kwa wananchi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa kupeleka umeme wa uhakika Mkoani Kigoma pamoja na wilaya zake ikiwemo Wilaya ya Kibondo, ili kuharakisha maendeleo ya wananchi wa mkoa huo.

Juhudi hizi zimezungumzwa mara kadhaa hapa Bungeni na nje ya Bunge, kwa miaka yote ya Bunge lako hili, Serikali imerudia na kusisitiza nia yake hiyo ya kupeleka umeme Kigoma na Wilaya zake. Ili kuhakikisha utekelezaji wa azma hii, serikali kupitia Wakala wa Nishati vijijini *(REA)* imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa laini za kusambaza umeme mjini Kibondo, kazi itakayofanyika mara tu baada ya Mkandarasi kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa mji wa Kibondo hivi sasa hauna umeme, hata hivyo kuna jenereta 17 zenye uwezo wa kuzalisha *MW 1.25* kila moja, zilizoombewa fedha Serikalini, kwa ajili ya miji ya Kibondo, Kasulu, Loliondo, Sumbawanga na Kigoma mjini.

Kati ya hizo, mbili ni kwa ajili ya mji wa Kibondo. Kwa kusema kweli mpaka sasa ni jenereta tano tu za Kigoma mjini ndizo zilizopatiwa fedha. Jenereta zilizobaki zinasubiri upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Aidha *TANESCO* iko katika hatua za mwisho kuandaa zabuni za ununuzi na ufungaji wa jenereta za mjini Kibondo, ili punde fedha hizo zitakazopatikana, kazi ya ufungaji wa jenereta hizo zianze mara moja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukrani kwamba yule mwananchi wa Kibondo ambaye ni mpiga kura wangu atapata umeme, nashukuru sana naipongeza Serikali.

Lakini swali la nyongeza la msingi litabakia pale pale kwamba kwa sababu kwa kuwa Serikali inakuwa mstari wa mbele wakati wakimbizi wanapoingia mahali popote na siyo lazima iwe Kibondo, na kwa kuwa Serikali inawajibika kuangalia ni jinsi gani wakimbizi wameleta madhara katika maeneo hayo, ikiwa ni pamoja na mali zao ambazo zinaweza zikawasaidia wananchi wa eneo hilo.

Sasa kwa kuwa mimi ninaelewa taratibu za wakimbizi kwamba maeneo yote yanayokuwa *affected* kutokana na ujio wa wawakimbizi yanatakiwa yapate fidia mara baada ya wakimbizi kuondoka. Je, Serikali haioni kwamba haikutekeleza hivyo na kusababisha hawa watu walio *NHCR* waondoke na vifaa vyao ikiwa ni pamoja na jenereta ninayoizungumzia ?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, hukumwelewa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani kimsingi wote tunaelewa kwamba nchi yetu inatoa sadaka kubwa kwa kupokea wakimbizi hawa na madhara yanayotokana na naamini kwamba madhara ya wakimbizi na utaratibu ambao Serikali imejiwekea ya kufanyia kazi masuala haya yako kwenye mamlaka mengine kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Ndani na kadhalika.

Lakini hili suala la kwamba kulikuwa na jenereta pale *UNCHR* na kwamba wameondoka nalo siwezi kusema hapa mkataba wa kuwepo kwa *UNCHR* pale kwenye kambi za wakimbizi na mali zao zilikuwaje. Lakini hata hivyo napenda tu kurudia tena kwamba hivi ki-jenereta kingekuwepo pale hata kisingesaidia kwa lolote. Mkakati wa Serikali ni kuleta jenereta mbili, na tayari zimeombewa fedha hapa Bungeni na Bunge limeridhia, na kwa sasa hivi utaratibu unategemea upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Katika jenereta 17 tayari tumepata jenereta tano, tunasubiri hizo jenereta zingine Hazina watakapotuambia wamepata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jenereta hizo kwa pamoja zitazalisha megawati 2.5 kwa Wilaya ya Kibondo na umeme huo ni mwingi sana kwa mahitaji ya Kibondo kwa hivi sasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mporogomy, maana yake ni wa huko huko.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika kunipatia nafasi. Kwa kuwa katika Wilaya ya Kasulu ziko *mini-hydros* kama tatu hivi zinazofanana fanana na zile zingine ambazo ziko Kibondo kule.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuniambia na kuwahakikishia wananchi wa Jimbo la Kasulu Magharibi na Kasulu Mashariki kwamba *mini-dyros* za Mwoga, Kabanga na Heri Mission, zinaweza zikafungiwa umeme, wananchi wanaoishi karibu na hizo *mini-hydros* wakapata umeme hivi sasa? Maana kilio cha umeme katika Mkoa wa Kigoma ni kikubwa sana. Naomba Mheshimiwa Waziri, anipe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kufanyia tathmini *mini hydros,* unabuniwa na Wabunge kama hivyo na unakuja *REA* na *REA* wanazifanyia kazi. Na kwa kweli, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mporogomyi, kwasababu hili suala la *mini hydros,* yeye ameshaliwasilisha *REA* na jana nimezungumza na Mkurugenzi Mkuu wa *REA,* Dr. Makehesye na amenihakikishia kwamba hili suala la *mini hydro* ya Heri Misheni analifanyia kazi; isipokuwa ni lazima niseme kwamba *mini hydro,* ni umeme

mzuri kwasababu ni umeme nafuu ni umeme unaotegemewa, lakini tunasubiri bado tathmini ya utekelezaji wa kazi hiyo ili tujue ni kiasi gani cha umeme kitakachozalishwa, kwa gharama gani na kwa muda gani. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba masuala ya *mini hydros* kwenye maeneo hayo ikiwa ni pamoja na ile ya Rusumo kule Kibondo unafanyiwa kazi.

Na. 155

**Malipo ya Pensheni na Mirathi**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa malipo ya pensheni na mirathi bado unasuasua na ni kero sugu kwa wastaafu na waliofiwa na kwa kuwa Serikali mara kwa mara imekuwa ikidai kwamba, hali hiyo husababishwa na upungufu katika nyaraka za madai:-

(a) Je, kuanzishwa kwa Mfuko wa Pensheni kumesaidia kwa kiasi gani kurekebisha hali hiyo na kwa sasa huchukua muda gani kulipwa kwa madai sahihi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kuchelewesha kulipa pensheni au mirathi wahusika ni kukiuka taratibu za Utawala Bora na mkataba wa huduma kwa mteja ?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya pensheni na mirathi ni haki ya mhusika na ni kweli kwamba inapochelewa kulipwa hugeuka kuwa kero. Kuchelewa kwa malipo hayo mara nyingi husababishwa na upungufu wa nyaraka za madai zifuatazo:-

(i) Barua ya kuajiriwa;
(ii) Hati ya mshahara wakati wa kusajiliwa na mfuko;
(iii) Barua ya mwajiri ya kumkubalia mwajiriwa kustaafu;
(iv) Fomu ya kuomba mafao iliyosainiwa na mwajiri na mwajiriwa; na
(v) Barua ya cheo cha mwisho na mshahara wake na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara ya Fedha na Uchumi imetoa mafunzo kwa maafisa wanaoshughulikia mafao ya pensheni na mirathi kutoka Wizara, Mikoa, Halmashauri na Mahakama. Mafunzo hayo yanahusiana na uwekaji na uchambuzi wa kumbukumbu za waajiriwa pamoja na taratibu za ulipaji wa mafao.

Usahihi wa kumbukumbu za mtumishi utamsaidia sana mstaafu kuweza kupata malipo yake kwa wakati, tangu kuanzishwa kwa mfuko wa pensheni wa watumishi wa umma mnamo mwaka 1999, Mfuko umesaidia sana kutokana na kujiwekea utaratibu wa utendaji wa kulipa, mafao ya wastaafu kwa kipindi kisichozidi muda wa siku saba.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza, sio nia ya mfuko kuchelewesha malipo ya mstaafu au warithi, kuchelewa kwa malipo ni matokeo ya kuwa na nyaraka, pungufu Mfuko kutokuwa na Afisa/Ofisi kwa kila Mkoa, kutokueleweka kwa taratibu za ufunguaji wa mirathi, na baadhi ya wakati waajiri kuchelewa kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hata hivyo, Wizara yangu imeshaanza kuyapatia ufumbuzi baadhi ya matatizo yaliyopo kwa nia ya kuondoa kabisa tatizo la ucheleweshaji wa mafao.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kunipa majibu mazuri, ningependa kujua lifuatalo; nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Hivi karibuni tumepitisha sheria kwamba kiinua mgongo au malipo ya wastaafu kwa mwezi yatafikia kiasi cha shilingi hamsini. Je, malipo haya yataanza lini? Kwa kuwa, mara nyingi pakiwa na malipo ya aina hii panakuwa na suala la kuhakiki na nini na nini. Na wananchi au wastaafu hao, wako katika hali ngumu. Tungetaka siku kamili au mwezi kamili ambao unaweza kujulikana, waweze kufuatilia. Vinginevyo tuarifiwe ni namna gani ya kufuatilia endapo watakuwa hawajapata, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Kwa kuwa, serikali imekiri kwamba kwa upande fulani Serikali yenyewe inachelewesha, aidha kiutendaji. Je, isingekuwa vizuri kuanzia sasa kwa wastaafu waandaliwe hundi zao miezi mitatu kabla ya kuastaafu? Vinginevyo aendelee kufanya kazi mpaka siku ile anapata hundi yake ya mkupuo. *(Makofi).*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kigwalilo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ametaka kujua hiki kiwango tulichokitangaza cha *minimum pension* ya shilingi 50,000/= itaanza lini. Nataka nimhakikishie kwamba *minimum pension* itaanza mwezi wa saba, yaani mwezi huu kwa wastaafu wote na kitaendelea mpaka kiwango kingine kitakapowekwa; hayo makisio yapo na tumeshayaweka katika Bajeti zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili; ametaka kuandaliwe cheki ya mstaafu miezi mitatu kabla ya kustaafu. Nataka nimhakikishie kwamba kwa utaratibu wa sasa hivi sidhani kama kutakuwa na ucheleweshaji kwasababu taarifa zote za wastaafu,

tutaanza kuzikusanya miezi sita kabla. Kwa maana hiyo uwezekano wa kuwa na taratibu hizi kukamilika upo na utaandaliwa hundi yake katika kipindi husika. *(Makofi).*

**MHE. BALOZI DR.GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, kuna maeneo yaliyo mbali sana na Makao Makuu ambako kunafanyika shughuli hizi kama Wilaya ya Ukerewe. Je, Waziri atakubali kutuma Timu Maalum, ambayo itasaidiana na mimi kuzunguka vijijini, kuwaona wale wote ambao wanangoja pensheni zao? Wengine wameandikwa wamekufa na wakati hawajafa na taarifa tumeleta na hakuna majibu?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE.OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Balozi Mongela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nilidhani Balozi ataniomba na mimi nifuatane naye, lakini kwasababu amehitaji watendaji tu, nakubaliana naye. *(Makofi).*

Na. 156

**Mfuko wa Pensheni Wa Mashirika ya Umma**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma, *PPF,* umefanikiwa vizuri kwa kutoa huduma kwa wanachama wake na pia kutoa mikopo ya muda mrefu kwa Serikali kwa ajili ya majengo ya uwekezaji; na kwa kuwa, Mfuko huo una changamoto nyingi kama wanachama wake kuugua *UKIMWI,* waajiri kutowasilisha makato ya watumishi kwa wakati:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kunusuru Mfuko na wanachama wake?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Jimbo la Mkwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mzee Ngwali, Mbunge wa Jimbo la Mkwajuni kwamba Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma, *PPF,* kwa kiasi kikubwa umefanikiwa kutoa huduma nzuri kwa wanachama wake. Huduma hizo ni pamoja na kulipa mafao kwa wakati, kutoa mikopo kwa wanachama wake, malipo ya ada ya shule kwa wanafunzi baada ya wazazi wao kufariki dunia wakiwa wanachama wa Mfuko pamoja na kutoa mikopo ya muda mrefu kwa Serikali kwa ajili ya majengo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto zinazoukabili Mfuko na juhudi za kunusuru Mfuko, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Mfuko kutakiwa kuwa na sera ya kupambana na *UKIMWI* mahali pa kazi. Lengo ni kuwaelimisha wanachama wa mfuko katika kujikinga na ugonjwa wa *UKIMWI*.

(ii) Kuifanyia marekebisho Sheria ya Mfuko, kwa lengo la kuwachukulia hatua za kisheria, waajiri wote wasiowasilisha michango ya wafanyakazi wao kwa mujibu wa sheria.

(iii) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, imeweka utaratibu wa kudai taarifa za ulipaji wa michango ya wafanyakazi kutoka kila taasisi ya umma kwa kila baada ya miezi mitatu. Utaratibu huu una lenga katika kuhakikisha kuwa hakuna mlundikano wa malipo.

(iv) Serikali kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo itasaidia kuboresha utendaji wa Sekta hii.

(v) Serikali kuruhusu Mfuko kutumia sehemu ya fedha zake kuwekeza kwa lengo la kupata faida zaidi.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo tu ya nyongeza. Kwa kuwa, Mfuko huu au Serikali imeanza mchakato kwa muda mrefu sana wa kuhakikisha kuwa unakuwa na Mamlaka moja. Je, ni lini Mamlaka hii itamalizika ili ifanye kazi zake vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mheshimiwa Waziri amesema kuwa kuna baadhi ya sheria zina mapungufu na upungufu huo baadhi ya waajiri wanautumia. Je, haoni ipo haja wakati umefika kwa hiyo sheria iletwe ili iafanyiwe marekebisho?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba mchakato wa kuunda Mamlaka upo katika hatua za mwisho. Sasahivi tunajaribu kuangalia vigezo ambavyo ni vya kuweza kumteuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka pamoja na kupata Ofisi pamoja na majengo mengine ili Mamlaka iweze kufanya kazi zake kwa uhakika zaidi. Namwomba avute subira tu, hatua hii itakamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu sheria ambazo zinatakiwa zije zifanyiwe marekebisho; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba sheria hizo tunazingalia na tutazileta hapa ili ziweze kuja kufanyiwa marekebisho.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma hutoa huduma kwa wanachama na pia mikopo kwa Serikali. Je, ni lini mfuko huu utatoa mikopo ya kujenga nyumba za gharama nafuu kwa wanachama wake?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sote ni mashahidi, nikipindi kifupi tu kilichopita Serikali imepitisha sheria ya *Mortgage Financing.* Sheria ile ndiyo inayoipa nguvu Benki pamoja na mifuko kuweza kutoa mikopo kwa ajili ya wanachama wao.

Kwa hiyo ninadhani tukishamaliza kuweka Kanuni, zikishakuwa tayari nadhani hii Mifuko itakuwa na uwezo wa kuangalia fedha walizonazo ili waweze kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba kwa wanachama wao.

Na. 157

**Afya ya Msingi – MMAM**

**MHE. OMAR ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, lengo la mpango wa Afya ya Msingi, *MMAM,* ni kupunguza idadi ya vifo kwa mama wajawazito na watoto, *Martenal Mortality Rate and Infant Mortality Rate:-*

Je, idadi ya vifo vya akina mama na watoto ikoje kati ya mwaka 2007 – 2008?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za vifo vya akina mama wajawazito na watoto zinapatikana katika utafiti maalum unaofanyika nchi nzima, *Demographic Health*

*Survey.* Tafiti hizi zinafanyika kila miaka mitano, muda ambao ni muafaka kuweza kupima kama afya zilizopangwa kutekelezwa zimefanya kazi au la.

Hapa nchini tafiti zilifanyika mwaka 1999 na 2004. Tafiti zilizofanyika mwaka 2007/2008 zilijumuisha magonjwa ya *UKIMWI* na malaria na watoto wakati utafiti wa vifo vya wajawazito utafanyika mwaka huu 2009. Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa moja ya malengo yaliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, *MMAM,* ni kupunguza vifo vya kina mama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa zitokanazo na *demographic health surveys'* idadi ya vifo vya watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1,000 imepungua kama ifuatavyo; 147 mwaka 1999, 112 mwaka 2004 hadi 91 mwaka 2007/2008. Aidha vifo vya watoto wachanga, umri chini ya mwaka mmoja, vimepungua kama ifuatavyo: 99 (1999), 68 (2004) na 58 (2007). Mafanikio haya yanaashiria kwamba kwa mwenendo huu kuna uwezekano mkubwa wa kufikia lengo la nne la maendeleo ya milenia, *MDG4.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vifo vinavyotokana na uzazi, takwimu tulizo nazo ni 529 mwaka 1999 na 578 mwaka 2004 kwa kila vizazi hai 100,000. Aidha kwa mwaka 2009 viashiria vinaonesha kwamba vifo hivyo vimepungua. Hata hivyo taarifa rasmi ya kupungua kwa vifo hivyo itatolewa baada ya kufanya tathmini ya kisayansi ambayo inatarajiwa kufanyika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Wizara imetoa maelekezo kwa waganga na viongozi wa vijiji na kata kwamba vifo vya wajawazito ni matukio ambayo lazima yatolewe taarifa. Zoezi hili litasaidia Wizara kupata takwimu sahihi ya vifo hivi vinavyotokea hospitali na vijijini. Vilevile sababu zitabainika na hatua za kitaalamu, kinidhamu na kiutawala kuchukuliwa. Ni matarajio yetu kuwa utekelezaji thabiti wa mikakati iliyoainishwa kwenye Mpango wa *MMAM* pamoja na afua nyingine za kuboresha afya ya uzazi na mtoto zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuendelea kupunguza idadi ya vifo vya wajawazito na watoto.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, huko Kanda ya Ziwa mitaa ya Geita na Mara, kwenye milipuko. Kuna taarifa kwamba mamba nyingi zinatoka kutokana na mshituko. Na kwa kuwa, mazingira ya huko pia yamechafuka na maji; Je, Serikali sasa ipo tayari kwenda kufanya utafiti maalum kuthibitisha kwamba milipuko inayofanyika huko na mazingira ya huko inasababisha mimba nyingi zitoke?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**Mheshimiwa naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, anazungumzia maeneo ya ziwa huko na kwamba kuna matatizo yametokea huko, mambo ambayo ninavyofahamu kwa *debate* iliyopo hapa ni kwamba Serikali inafuatilia mambo haya na kwamba itatoa taarifa kwamba ni nini kilichotokea kule. Najua kwamba Waziri wa Madini amekwenda kule, najua kwamba Naibu Waziri wa mambo ya ndani pia amekwenda kule, kama ni haya anayoyazungumzia.

Lakini kuhusu sasa hawa akina mama wajawazito pamoja na watoto; mimi nadhani kikubwa hapa tunachokiona na hii taarifa anayotueletea hapa ni elimu zaidi na hizi huduma ambazo nimezielezea hapa ambazo zinatolewa za karibu zaidi. Na kubwa zaidi ambalo nimezungumza katika mpango huu ambao tunauzungumza sasahivi na ambalo ni jipya kama sikusikika vizuri; ni kwamba tunahitaji sasa mama na baba wawe wanafuatana kwenda kule Hospitali, ili mama kama miguu imevimba, baba aweze kujua kwamba huyu mama labda tatizo hili linatokana na nini. Kwahiyo kumeanzishwa utaratibu mpya sasa ule wa *RSH* badala ya *MCH* utakaosaidia katika mambo haya. *I hope* utasaidia katika haya maeneo yanayozungumzwa ya ziwa kama kuna tatizo kama hilo.

**MHE. NURU AWADH BAFADHIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kuniona. Kwa kuwa, kina mama wengi wajawazito wanaishi vijijini; na kwa kuwa, kina mama hao wanakuwa na umbali kuzifikia zahanati au vituo vya afya wakati wa kujifungua.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafundisha wakunga wa jadi ili wawasaidie hawa akina mama ambao wanaishi mbali na vituo vya afya au zahanati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII I:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nuru Bafadhil, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wetu sasahivi kwa nchi, kwa maana ya sera za Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma hizi zinakwenda karibu sana na wananchi. Ndio maana hapa tunayo sera innayozungumza sasa kwamba kila kijiji kiwe na zahanati yake pale. Hakuna ubaya wowote wa kuwaelimisha na kuwasaidia hawa wakunga wa jadi, kwasababu na wao wana *play role* kubwa, lakini ni lazima wafanye kazi hii chini ya wataalamu.

Ukisema tu unawaacha wao wenyewe *it is a problem.* Najua kwamba wame-*play role* kubwa sana, wamekuwa wanasaidia lakini pia ni muhimu kwa maana ya sasa kwamba mambo yanabadilika na matibabu yanabadilika na shida tulizonazo za akina mama zinaongezeka. Kwa sababu ya teknolojia bado utahitaji watu ambao wana utaalamu ambao wataweza kusaidiana na hawa wakunga wa jadi kusaidia katika jambo hili. *(Makofi)*

Na. 158

## Kukarabati Jengo La Mahakama Ya Mwanzo Igamba

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, jengo la Mahakama ya Mwanzo Igamba limechakaa sana:-

Je, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria ina mpango gani wa kukarabatai jengo hilo ili Hakimu, Watumishi na wahusika wa kesi Mahakamani hapo wawe kwenye mazingira safi na salama zaidi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya kukarabati na pengine kujenga upya jengo la Mahakama ya Mwanzo Igamba. Mahakama ina nia ya dhati ya kukarabati Mahakama hiyo kama ilivyo kwa Mahakama zake zingine 762 hapa nchini. Hata hivyo Mahakama iya mwanza i na ufinyu wa Bajeti katika kutekeleza nia yake hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunasubiri nafuu ya kibajeti naomba nichukue fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge, aishirikishe Halamashauri yake na hata Wananchi wa Jimbo lake wasaidie ama kukarabati au kujenga jengo la Mahakama hiyo kama inavyofanyika katika kujenga majengo mengine ya taasisi za kutoa huduma za jamii, ikizingatiwa kuwa utoaji haki huduma ya jamii kama zilivyo huduma zingine za jamii; hili limefanyika katika sehemu kadhaa hapa nchini ikiwemo Kata ya Itaka huko Mbozi, ambako wananchi wamesaidia kujenga jengo la Mahakama.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza. Wananchi wa Mbozi na kwa kweli wananchi wa mahali pengine katika nchi hii, wamekuwa wanajitolea sana katika kuchangia maendeleo katika maeneo mbalimbali ikiwa ni ujenzi wa Sekondari, zahanati, na kadhalika.

Hivi sasa tunataka tena tuwahamishie wananchi kwamba waendelee kuchangia katika Mahakama? Hatuoni kwamba Serikali inakwepa wajibu wake wa msingi katika maeneo mengi na kwa maana hiyo kuwapa wananchi mzigo mkubwa zaidi? *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni kweli wananchi wa Itaka wamejitolea sana kujenga jengo lile mpaka lilipofika, lakini vifaa kama mabati, nondo, saruji,

sementi, misumari, imekuwa ni jukumu la Serikali. Na leo asubuhi nimeongea na Hakimu wa Wilaya, Ndugu Matembele, amesema sasahivi wanahitaji shilingi milioni 13 ili waweze kumalizia ujenzi wa jengo la Mahakama ya Mwanzo itaka. Je, serikali itakuwa tayari kuwapa pesa ili waweze kumalizia jengo hilo katika mwaka huu wa fedha?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikwepi wajibu wake, Serikali inakusudia kujenga Mahakama zote hapa nchini. Lakini tunachosema ni kwa sasa hali yetu kifedha sio nzuri. Kwa hiyo tunaomba na nimesema kabisa tunamwomba Mheshimiwa, kama ikiwezekana washirikiane na wananchi wafanye kazi hii. Lakini la sivyo, basi tusubiri tu mpaka hapo uwezo utakapopatikana, tutaijenga tu na tunakusudia kuijenga kama hizi nyingine 762 nazo pia tunakusudia kuzijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwamba wananchi wa Itaka wamejitolea na ni kweli wamejitolea na wamejitolea vizuri. Na mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali itatimiza wajibu wake kwa kutafuta vifaa ambavyo wanananchi hawawezi kujitolea; ni wajibu wetu kujenga Mahakama hizi na tunakusudia kuzijenga. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, baada ya Serikali kusitisha shughuli za Mahakama ya Mwanzo ya Msangano, Jimboni Mbozi Magharibi, ambayo kwa wakati huo ilikuwa ikihudumia Kata za Chiwezi, Chilulumo, Chitete na Msangano yenywe; Mahakama hii ya Mwanzo ya Igamba, ambayo ipo Jimbo la Mbozi Mashariki, ndio ilichukua jukumu la kuhudumia Tarafa zote mbili kwa maana ya Igamba na Msangano zenye wananchi zaidi ya 200,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali haioni sasa kwamba ni muhimu ikawapunguzia hawa wananchi mchakato wa kujitolea kwa kuwapa hiyo pesa ili waweze kuendelea na shughuli zao za ujenzi wa zahanati, shule za sekondari pamoja na vituo vya afya badala ya kuzidi kuwabebesha huo mzigo?

**NAIBU SPIKA:** Wewe unaulizia Mahakama, vituo vimeingiaje hapa? Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Siyame kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nafahamu wananchi wa Itaka wanayo matatizo ya Mahakama. Na nimesema tunayo matatizo ya Mahakama katika mahakama nyingine 762 hapa nchini; zote ni jukumuletu kuzijenga na tuna kusudia kuzijenga.

Tunaposhindwa kuijenga Itaka kwa sasahivi si kama hatutaki, ni kwamba kwa muda huu bado hatujafikia hapo; mwaka huu tunajenga 20 tu, mwaka ujao labda tutapata uwezo wa kujenga nyingine. Na tunaweza tukaiweka hiyo ya Msagano, ya Itaka, kama Mheshimiwa Mbunge, anavyotaka.

Na. 159

**Kilimo cha Umwagiliaji Rorya**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANGO K.n.y. MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeweka kipaumbele katika kilimo cha Umwagiliaji kwa lengo la kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula na kuuza ziada; na kwa kuwa Wilaya ya Rorya inazo hekta 1,380 zinazofaa kwa kilimo cha Umwagiliaji zenye uwezo wa kutoa tani 6.373 za Mpunga kwa mwaka lakini hadi sasa ni hekta 219 tu, zinazolimwa na kutoa tani 861 za mpunga kwa mwaka:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha skimu za umwagiliaji katika mabonde ya Rwag’enyi, Nyathorogo, Nyabwarongo na Kirongo kwa ajili ya kilimo cha mpunga?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mbunge wa Rorya, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na mfuko wa Kimataifa wa kuendeleza kilimo, *IFAD*, ilitekeleza mradi uliojulikana kwa jina la *Mara Region Farmers’ Initiative Project - MARA-FIP* kati ya mwaka 1996 – 2003. Mradi huo uliendeleza miradi ya umwagiliaji kwa kutumia teknolojia ya kuvuna maji kwa njia ya ujenzi wa mabwawa madogo na malambo yaliyojulikana kama *Mara bunds*.

Jumla ya mabwawa matano na *Mara bunds* 11 zilijengwa katika mkoa wa Mara na kati ya hayo, mabwawa matatu ya Sakawa, Nyanjage na Irienyi pamoja na *Mara bunds* mbili za Ochuna na Chereche zilijengwa katika wilaya ya Rorya.

Mabwawa ya Sakawa na Nyanjage, ni maji kwa matumizi ya binadamu; Bwawa la Irienyi na malambo ya Ochuna na Chereche, ni kwa jili ya umwagiliaji wa maeneo ya hekta 100 na hekta 250 sawia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mpunga na kipato cha wakulima. Ongezeko

la uzalishaji kutokana na umwagiliaji ni kutoka tani moja na nusu kwa hekta hadi tani tano kwa hekta kwa zao hilo la mpunga.

Kwa mfano katika *scheme* ya Chereche, uzalishaji umeongezeka kutoka magunia 18 kwa heka hadi magunia 40 kwa heka. Uzoefu uliopatikana katika miradi hiyo itatumika kusanifu na kujenga marambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naapenda kujibu swala la Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mafanikio ya *scheme* za Rorya, Wizara yangu kupitia Ofisi ya umwagiliaji, Kanda ya Mwanza imekamilisha usanifu wa miradi ya Rwang'enyi na Kirogo. Usanifu wa *scheme* ya Nyathorogo uko katika hatua za mwisho ili utekelezaji uweze kufanyika katika mwaka wa fedha 2009/2010. Wizara yangu imepanga kutekeleza *scheme* za Rwang'enyi na Nyathorogo katika mwaka huu wa fedha.

Pamoja na azma hii ya Serikali; napenda kuishauri Halmashauri ya Rorya kwamba miradi ya Kirogo na Nyaborongo ambayo iliibuliwa katika mipango ya maendeleo ya vijiji, iwekwe katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya yaani *DADIPS,* ilikupatiwa fedha za utekelezaji.

Baada ya hapo, Halmashauri ipeleke maombi *TAMISEMI* ili *scheme* hizi zifanyiwe tasmini ya kupata fedha za nyongeza kutoka mfuko wa maendeleo *DIDF,* baada ya kukidhi vigezo kwa kukamilisha utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Rorya kutayarisha maandiko mbalimbali ya kuombea fedha kutoka vyanzo mbalimbali kama vile *TASAF* na *Japan Food Aid Company Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mabwawa yaliyojengwa katika wilaya ya Rorya ni kwa ajili ya matumizi mengi ikiwa ni pamoja na matumizi ya binadamu.

Tarehe 24 Juni, 2009 nilipokuwa natoa kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini niliitaarifu Bunge kwamba Serikali ingetuma kwa Halmashauri zote nchini fedha za ziada kwa ajili utekelezaji wa *program*. Nafurahi kulitaarifa Bunge lako tukufu kwamba tarehe Juni, 2009 Serikali imetuma kwa Halmashauri zote jumla ya shilingi bilioni 27.4 na hivyo kutekeleza ahadi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Sarungi Mbunge wa Rorya kwa kazi nzuri ya ufuatiliaji wa miradi hii. naahidi kumpa yeye na Waheshimiwa Wabunge, ushirikiano mkubwa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Baada ya majibu mazuri sana ya Profesa Mwandosya ningependa niulize maswali mawili.

(a)Kwa kuwa *scheme* ya mabonde ya Rwagenyi, Nyathongo na Kilongo yamefanana sana na *scheme* ya umwagiliaji ya Rungwe Mpya huko Kasulu na ni majuzi tu Mheshimiwa Waziri Mkuu amefungua *scheme* ile. Je, Mheshimiwa Profesa atakubaliana na mimi kwamba wakati umefika sasa atupelekee watalaam ili wakashirikiane na Halmashauri kutafuta vyanzo vingine ile scheme awamu ya pili iweze kuendelea?

(b)Kuna ombi limepelekwa Ofisi ya Maji ya shilingi milioni 42 za dharura kumalizia awamu ya kwanza iliyoanza ya kumilizia awamu ya kwanza iliyoanza ya kukamilisha mfereji. Nilitaka kujua je, Mheshimiwa Profesa Mwandosya hiyo barua umeshaiona, kama umeiona hizo fedha unatuletea lini Kasulu? Nashukuru ahsante.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu scheme ya Rungwe Mpya kupatiwa watalaam namuahidi kwamba tutatuma watalaam kushughulikia awamu ya pili. Si kwa Rungwe Mpya tu hata kwa Rungwe ya zamani Wilaya ninakotoka. Kuhusu Ofisi ya Maji kuombwa shilingi milioni 40 nitalifuatilia hilo ombi nina hakika tutatafuta hizo fedha ili tuwapatie wananchi maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na maswali yaliyobakia tunachukua muda ule tuliotoa matangazo ulikuwa dakika kama 10.

Na. 160

**Uhamishaji wa Watu kwenye maeneo ya Hifadhi na Mipaka.**

**MHE. TATU M . NTIMIZI** aliuliza:-

Kwa kuwa, watendaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii walioko mikoani hufanya kazi ya kuhamisha wananchi waliokaa kwenye maeneo ya mipaka ya hifadhi au ndani ya hifadhi nyakati za masika:-

(a) Je, ni kwanini zoezi la kuwahamisisha wananchi hao linafanyika wakati wananchi hao wamekwishalima na kupanda na mazao yao yamekwishaiva tayari kwa matumizi yao?

(b) Je, kwanini watendaji hao wasiwahamishe wananchi hao baada ya kuvuna?

(c) Je, kwanini watendaji hao wanachoma nyumba za makazi ya wananchi pamoja na vifaa vyote na chakula wakati wa operesheni hiyo? Je, huo sio unyanyasaji na dhuluma kwa wananchi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mbunge wa Igalula lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 26 cha Sheria namba 14 ya misitu ya mwaka 2002 na sheria ya wanyamapori sura 283 na mapitio yake ya mwaka 2002 pamoja na mambo mengine vinazuia mtu yeyote kufanya shughuli za kilimo, kuingiza mifugo na kuweka makazi katika hifadhi hapa nchini.

Aidha kifungu cha 14(1) na 4(a) cha Kanuni ya misitu kinazuia kabisa kutoa kibali kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makazi katika misitu ya asili hasa vyanzo vya maji na ardhi oevu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu swali la dada Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Utekelezaji wa sheria ya misitu na wanyamapori kama sheria nyingine hapa nchini hutekelezwa wakati wowote wa majira ya mwaka pale uhalifu unapogundulika bila kujali kama wahalifu hao wanavuna au wanapanda mazao, lakini kiubinadamu huwa wanaruhusiwa kuondoka na mazao pamoja na mali zote zinazohamishika.

Mheshimiwa Spika, kabla ya zoezi la kuhamisha wananchi katika eneo linalokusudiwa kuwa hifadhi wananchi hupewa taarifa rasmi ya siku 90 ili wajiandae kutoka na kuwalipa fidia kwa mali zao, lakini kwa wananchi waliovamia maeneo ambayo tayari ni hifadhi huwa hakuna muda maalum. Muda unaotolewa mara nyingi ni kwa wananchi hao kuondoa mazoa yao ya kilimo yakisha komaa na mali nyingine zinazohamishika na baada ya hapo hutakiwa kuondoka kwa hiari yao.

Hata hivyo zoezi la kuwaondoa wavamizi kwenye maeneo ya hifadhi linahusisha mamlaka nyingi katika eneo husika kuanzia Mkoa, Wilaya hadi kuiui kwa msingi huo, pale mamlaka hizo zinaposhindwa kuwashawishi wananchi ndipo taratibu stahili za kisheria zinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya hifadhi ya mazingira ni jukumu la kila mmoja kuanzia wananchi wa kawaida, viongozi na sisi Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawaikilishi wa wananchi wetu katika sehemu zetu zinazohusika. Kwa sababu madhara ya uharibifu wa mazingira hayachagui.

Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote akiwemo na dada yangu Tatu Ntimizi kwamba tusaidiane katika kuwaelimisha wananchi wao umuhimu wa kuhifadhi wa mazingira yetu pia tuwahimize kuhusu kuheshimu maeneo yaliyohifadhiwa kwa faida yetu sisi wote na vizazi vyetu vya baadaye kwa ajili ya jamii nzima ya Tanzania na dunia nzima kwa jumla.

**MHE. TATU M . NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa watu katika nchi hii ya Tanzania maeneo ya hifadhi yamepungua. Katika Jimbo la Igalula waliotolewa na kuchomewa nyumba wamekaa zaidi ya miaka 20.

(a) Je, Maafisa Misitu walikuwa wapi toka wafanye kazi waliyoifanya?

(b) Kuelimisha Wabunge ndiyo kazi zetu, kazi za Maofisi wa Misitu wanakuwa wapi ambapo wametengewa Wilaya za kufanyia kazi hawaendi mpaka wapate maelekezo kutoka Makao Makuu ndiyo wanakwenda kuchomea watu nyuma na kwenda kuchoma vyakula. Je, ndiyo kazi hizo walizowekewa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu kwa pamoja maswali mawili ya Mheshimiwa Dada Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mara nyingi baada ya amri kutolewa ya watu kuondoka inachukua muda mrefu mpaka watu waanze kuondoka. Hiyo inatokana na sababu mbili, sababu mojawapo ni kwamba sheria nyingi ambazo zinatumika katika vijiji vyetu na sheria hizo ni kama zifuatazo:-

Kuna sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, kuna sheria ya ardhi namba 4, kuna sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999 na kuna sheria ya misitu namba 14 ya mwaka 2002. Wakati mwingine sheria hizi zinagongana ndipo unakuta kwamba hata wananchi wanakuta kwamba hawajui wafuata sheria ipi.

Pia na sisi wenyewe wakati mwingine wanasiasa pomoja na Serikali katika ngazi mbalimbali tunashiriki katika kuhakikisha kwamba mambo haya hayatekelezeki kwa sababu ya kutoa sisi amri za pembeni ambazo mtu akienda na yeye anaamua mambo yake yawaje.

Kwa hiyo, ni kwamba siyo watendaji peke yao, hata sisi ngazi mbalimbali za siasa na za Serikali tunachangia katika kuhakikisha mambo haya hayafanyiki. Lakini hata hivyo pia na wananchi napenda nitoe mfano katika miaka 2001 mpaka 2007 tumekuwa tukiwahamisha wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu yawe mafupi muda hautoshi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba tu nimalizie kwamba na wananchi wenyewe wanakuwa na visingizio wanashindwa kuhama. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 161

**Kuboresha Uwanja na Michezo wa Namfua Uliopo Singida**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete amesaidia sana Watanzania katika kuboresha kiwango cha mpira wa miguu nchini kwa uamuzi wake wa kumleta kocha wa kigeni wa timu ya Taifa Ndugu Maximo, ambaye kwa muda mfupi ameleta mafanikio makubwa kisoka; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais pia ameahidi

kusaidia kuboresha mchezo wa riadha ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa kocha mzuri, viwanja vizuri vya riadha vya kimataifa.

Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuboresha uwanja wa michezo wa Namfua - Singida, ili uwe uwanja wa kimataifa wa riadha kwa kuwa na sifa hiyo na kwamba mkoa wa Singida upo katikati ya nchi yetu na wapo wakimbiaji wazuri mkoani Singida na Mikoa ya jirani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ipo haja ya kuboresha uwanja wa michezo sio tu wa Namfua uliopo Mkoani Singida, bali pia na viwanja vingine vilivyopo katika Mikoa mbalimbali hapa nchini ili viwe vya kisasa zaidi na katika viwango vya kimataifa na hivyo kuweza kutumika kwa michezo mbalimbali ukiwemo wa riadha.

Kuboresha kwa viwanja hivi hapa nchini na kuwa katika viwango vya kimataifa kutasaidia kuwaweka wanamichezo wetu katika mazingira ya kuvizoea na hivyo kuweza kufanya vizuri zaidi wanaposhiriki katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, jambo ambalo kwa miaka mingi limekuwa ni mojawapo ya changamoto wanazokabiliana nazo wanamichezo wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo baada ya Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kueleza azma yake ya kuendeleza mchezo wa riadha hapa nchini kama alivyofanya kwa mchezo wa mpira wa miguu, Wizara yangu imeanza kupanga mikakati mbalimbali itakayaoweza kufanikisha utekelezaji wa azma hiyo ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya hali ya viwanja vya michezo, kupata walimu na kuendelea kuhamisha vijana kupenda mchezo na riadha na kushiriki katika mchezo huo.

Mwezi Machi Mwaka huu, Wizara yangu kupitia idara ya Maendeleo ya Michezo ilimtuma mtaalamu wa viwanja vya michezo kwenda mkoani Singida kufanya tathmini ya hali ya Uwanja wa Namfua ambao mara nyingi umekuwa ukitumika kwa mashindano ya mchezo wa riadha kitaifa, ili kutambua maeneo yanayohitaji maboresho na kuufanya uwanja huo kuwa wa kisasa na wenye hadhi ya kimataifa. (*Makofi*)

Kwa vile kiwanja cha Namfua kinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM), taarifa ya mtaalamu aliyetumwa kufanya tathmini ya uwanja huo imekabidhiwa kwa uongozi wa Mkoa wa Singida ili uweze kukaa pamoja na uongozi wa CCM mkoa kujadili taarifa hiyo kwa ajili ya kuangalia namna ya kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ipo tayari kutoa ushirikiano kwa uongozi wa CCM na Serikali ya Mkoa wa Singida na Mikoa mingine kwa ujumla katika

kuhakikisha kwamba viwanja vya michezo vinaboreshwa na kuwa katika hali ya kisasa na viwango vya kimataifa jambo ambalo litasaidia kusukuma mbele maendeleo ya michezo hapa nchini.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Lakini pamoja na majibu hayo naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa uwezo wetu kifedha ni mdogo na tatizo mara nyingi ambalo ni kutawanya fedha hizi kidogo kidogo kwenye maeneo mbalimbali ndiyo maana hatufanyi vizuri katika baadhi ya miradi. Serikali haioni kwamba ingetafuta kiwanja kimoja au viwili kama kile cha Namfua kika-*invest* pale kwa ajili ya mchezo wa ridhaa badala ya kusema kwamba watangalia viwanja vingi waweze kuvitengeneza wakati uwezo wetu ni mdogo.

(a) Je, haoni bado ni muhimu ku-*invest* katika kiwanja cha Namfua badala ya kutawanya fedha ndogo ambayo tunayo? (*Makofi*)

(b)Kwa kuwa Watanzania tumepata bahati ya kuwa na Rais ambaye anapenda michezo na ameonyesha kwa vitendo namna anavyopenda kusaidia katika mpiga wa miguu na sasa kama nilivyosema ameweka nia ya kusaidia mchezo wa riadha.

Je, Wizara haioni kwamba ingetengeneza utaratibu wa kumkutanisha Mheshimiwa Rais na viongozi mbalimbali wa michezo kwa awamu kwa maana ya mpira wa miguu, riadha, ngumi ili Mheshimiwa Rais apate nafasi ya kupata maoni na mawazo mengine kutoka kwa hawa watu ambao wako kwenye *field* ya michezo kwa shabaha ya kupata msaada wa Mheshimiwa Rais, katika kuinua michezo mbalimbali hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (K.n.y. WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vizuri pia kuwa na viwanja mbalimbali Mikoani ili vijana waweze kushiriki huko huko waliko na kiwepo kiwanja kama mfano sasa hivi kiwanja cha Taifa kinatumika kimataifa lakini siyo vibaya pia Namfua na vingine viwepo ili kuimarisha riadha katika nchi yetu. Kwa hiyo, Kiwanja cha Taifa kipo lakini pia kuna haja vingine viwepo.

La pili nakubaliana na wazo kwamba si jambo baya kwa Rais kukutana na viongozi mbalimbali wa Michezo kwa sababu hii ni sehemu ya kazi zake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na umepita sana. Sasa nina wageni katika kumbi zetu za hapa Bungeni.

Tunao wageni wa Mheshimiwa John P. Magufuli Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ambao ni watendaji mbalimbali wa Wizara wanaongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara Dr. Nyamlunda. Ahsante wako kule juu. Karibuni sana leo mnayo kazi.

Tunao Waheshimiwa Haroub S. Masoud ambao ni Bi. Nasra Majid Said, Bi. Ubwa Said maarufu kama mama Ngina, yuko bwana Amour Abdallah na Bwana Abdallah Musa. Karibuni sana. Kumbe kuna akina Mama Ngina hapa hapa. (Makofi)

Tuna Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ambaye pia ana wageni wa *TAPAC* kutoka *future group. Future group* ni mradi unaofadhiliwa na *USAID* unahusu na mambo ya sera za afya ni Mr. Mileti Obaso yeye ndiyo mwakilishi nchini hapa. Makao yake yako Dar es Salaam. Pia yuko Miss Angelina Sparo yeye ni mwakilishi *Regional Director* kwa *East Africa.* Karibu. Tunaye Mrs. Fortunate Temu yeye ni *consultant capacity building* ya mradi huo.

Huyo alikuwa mwanasheria wangu nilipokuwa Waziri wa *Gender.* Halafu yuko Mr. Rose Amolo yeye ni *Senior Technical Advisor* wa *HIV Aid, Center Development and Population Activities*. Anatoka Marekani. Tunawakaribisha najua mna mikutano na *TAPAC* na baada pia mna mkutano na *TWPG* mimi kama Mwenyekiti.

Tuna mgeni Wageni wa Mheshimiwa Stephen Galinoma ambao wanatoka jimboni kwake na Wilaya. Kutoka Jimboni ni Bwana Martin Mhanjila Mwanafunzi wa *St. Gasper University Dar es Salaam*. Halafu yupo pia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Ndugu Fundi Mihayo. Karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

Halafu tuna wageni wa Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa huyu ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Iringa ndugu Deo Sanga maarufa Jaa People mtu wa watu. Anafuata na Ndugu Mwapinga, ambaye ni Kaimu Katibu wa CCM Mkoa wa Iringa. Yupo pia ndugu Godfrey Mosha yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Mufindi. Pia Mwenyekiti Mtendaji wa Chama cha Mazingira. Hawa wamekuja kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Iringa, pamoja na mimi maana na mimi natoka huko kwa mashauri yanahusiana na Chama chetu kule Mkoani. tunawakaribisheni sana. *(Makofi)*

Nadhani safari yenu imekuwa ya mafanikio na tunaomba mwendelee kushika hatamu huko ya Chama ili siku ya siku tujisikie tuna viongozi wetu. Karibuni sana.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Felix Mrema ambao ni Kwaya ya Mtakatifu Secilia ya Mjini Arusha. Naomba wasimame wote wana kwaya. Nilikuwa nashangaa mnatoka wapi kumbe ndiyo ninyi. Tunaifahamu kwaya yenu ni maarufu sana katika nchii hii na tunapenda kuisikiliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Lakini wameongozana na Padri Kadrun Olelesikoni. Baba Padri karibu. Yupo na Ndugu Novatus Rumanyika, Mdhamini wa Kwaya. Halafu yuko Bi. Donat Kibonge Mwenyekiti wa Kwaya. Ahsanteni sana. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Idd Azan, ambao ni jumla ya walimu 30 kutoka shule ya msingi Victoria iliyoko Dar es Salaam naomba wasimame. Ahsanteni sana. Wanaongozwa na Mwalimu Bi. Agnes Simbambili Mkuu wa Shule na Bwana Richard Mbogo Makamu Mwenyekiti wa Shule na Bi. Margreth Omar Makamu Mkuu wa Shule. Vile vile Mheshimiwa Idd Azan ana wageni wengine ambao ni jumla ya wanafunzi 15 na

walimu 6 kutoka shule ya Msingi Hanasifu iliyoko Kinondoni Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. Sasa hawa wanaongozwa na Mwalimu Mndulwa Mwalimu Mkuu na Ndugu Esha Lima, Mwalimu Mkuu Msaidizi pamoja na Ndugu E. Kahwa, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wa Mheshimiwa Janeth Massaburi ambao ni wajasiria mali kutoka Wilaya ya Temeke Mkoa wa Dar es Salaam wanajihusisha na utengenezaji wa chaki sabuni na kilimo cha uyoga. Naomba wajasilia mali wetu wasimame wako wapi? Hao ni Halima Masoud Kiongozi wa Msafara, yuko Ndugu Fujo Mzinga na Ndugu Habiba Kandoro na Ndugu Agripina Almasi. Halafu tunao wanafunzi 50 kutoka Chuo cha *Assembly of God Bible College* kilichopo hapa Dodoma. Tunaomba wasimame walipo. Nadhani wako kwenye g*a*lley au watakuja kesho karibu wote Bunge letu ni wazi kwa kila mtu. Kuna wengine hatujawatambulisha si maana yake hawana umuhimu unaostahili wote mnakaribishwa ni Bunge lenu mnaweza kulisikiliza wakati wote. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi. Kwanza Mheshimiwa William Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa leo tarehe 3 kutakuwa na kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika ukumbi Namba 231 jengo la utawala saa 8.00. Halafu Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM Mheshimiwa Ali Ameir anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi kwamba saa 7.00 kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa kila siku.

Halafu saa mbili usiku baada ya kuahirisha Bunge hili kutakuwepo na Kikao cha Wabunge wote wa CCM katika ukumbi wa Pius Msekwa. Hii ni baada ya kuahirisha jioni usiku. Hiki kingine ni saa saba mchana. Kwa hiyo, haya ni matangazo wanachama wazingatie.

Halafu kuna tangazo linatolewa na Ofisi kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuona na kula bidhaa za maziwa kutoka chama cha Wasindika Tanzania. Sasa nadhani yako mengi, maana yake mkienda wote mkila lazima yawe mengi. *TAMPA* wapo hapa kwa ajili ya maonyesho ya bidhaa zao mbalimbali katika viwanja vya Bunge kwa siku moja tu kwa mwaliko wa Mheshimiwa John P. Magufuli, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Waheshimiwa Wabunge wote wanahimizwa kuhudhuria katika maonyesho hayo kwa kuwa bidhaa zote zinatolewa bure. Kwa hiyo, mnakula bure. Msemo wao ni kwamba kunywa maziwa kwa afya yako yaliyosindikwa ni bora zaidi. Kwa hiyo, mwende mkale huko maziwa kwa wakati. *(Makofi)*

Baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na shughuli za leo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo ikiwa ni Bunge la Bajeti la Nne kwa Serikali ya Awamu ya Nne.

Aidha, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji inayohusu Wizara, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka 2008/2009 baada ya kushinda katika chaguzi ndogo ambao ni Mheshimiwa Charles Mwera Nyanguru kutoka Jimbo la Tarime, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjali kutoka Jimbo la Mbeya Vijijini na Mheshimiwa Lolensia Bukwimba kutoka Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu; Hayati Richard Said Nyaulawa, aliyekuwa mbunge wa Mbeya Vijijini; Hayati Faustine Kabuzi Rwilomba aliyekuwa mbunge wa Busanda na Hayati Phares Kashemeza Kabuye aliyekuwa mbunge wa Biharamulo Magharibi.

Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi wa majimbo waliyokuwa wanayawakilisha. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. Aidha, Naomba pia, nitumie fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali mbalimbali katika kipindi cha mwaka 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa waliotupatia katika maandalizi ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara itaendelea kuzingatia na kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yatakayotolewa na Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda**,** Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa, hotuba yake nzuri ambayo kwa ufasaha imetoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa Sekta mbalimbali pamoja na kazi zitakazotekelezwa na Serikali katika mwaka 2009/2010.

Aidha, nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo**,** Mbunge wa Kilosa pamoja na Mawaziri wote waliotangulia kwa hotuba zao nzuri ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana kwa karibu katika kutoa huduma za kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini.

Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia masuala ya Maendeleo ya Sekta za mifugo na uvuvi kupitia hotuba zilizotangulia.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Milenia Na Utekelezaji wa Mkukuta, Sekta za mifugo na uvuvi ni kati ya sekta zenye umuhimu mkubwa katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Umaskini nchini (MKUKUTA). Mkakati huu unazingatia Dira ya Taifa 2025 na Malengo ya Kimataifa ya Kuondoa Umaskini (*Millenium Development Goals* - *MDGs*).

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Malengo ya Milenia, Serikali iliandaa Mkakati wa Kuinua Uchumi na Kupunguza Umaskini **(**MKUKUTA**)** kama mkakati wake wa muda mfupi. Katika mkakati huo, Sekta za mifugo na uvuvi zimepewa majukumu ya kuinua kipato cha mfugaji na mvuvi pamoja na kuchangia uhakika na usalama wa chakula, kutoa ajira na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Ccm ya Mwaka 2005 Na Utekelezaji Wake Hadi Mwaka 2008/2009. Kwa kutambua mchango unaoweza kutolewa na Sekta za mifugo na uvuvi katika kuwapunguzia wananchi umaskini na kuongeza pato katika uchumi wa Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza sekta hizo kutekeleza maeneo muhimu yafuatayo:-Sekta ya Mifugo.

(a) Kujenga Mazingira ya Kuvutia Uwekezaji katika Viwanda vya Kuongezea Thamani Mazao ya Mifugo kama vile Ukataji Nyama, Usindikaji wa Maziwa na Utengenezaji wa Bidhaa za Ngozi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuandaa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mkakati wa Kutekeleza Sera hiyo wa mwaka 2009;

(ii) Kuanzisha Bodi ya Maziwa na ya Nyama ili kusimamia ubora wa maziwa na nyama;

(iii) Kupitia na Kuandaa Sheria zikiwemo: Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006; Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008; Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008; na

(iv) Kuandaa Kanuni 21 chini ya Sheria ya Veterinari (3); Sheria ya Magonjwa ya Mifugo (2); Sheria ya Maziwa (6); Sheria ya Ngozi (6); na Sheria ya Ustawi wa Wanyama (4).

Katika kuendelea kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongezea thamani mazao ya mifugo, Serikali inaandaa Rasimu za Sheria za Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo; Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo; Uanzishwaji wa Maabara Kuu ya Mifugo; Uanzishwaji wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo; na Sheria ya Uzalishaji wa mbari bora za wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuwepo kwa mazingira yanayovutia uwekezaji, sekta binafsi imejenga viwanda vya kusindika nyama, maziwa na ngozi kwa lengo la kuongezea thamani ya mazao ya mifugo ambapo:-

(i) Viwanda vya kusindika nyama vya *Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds Industries (SAAFI) na Tanzania Pride Meat,* vyenye uwezo wa kuchinja jumla ya ng'ombe 350 kwa siku vimejengwa na vinafanya kazi;

(ii) Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Shinyanga kimebinafsishwa kwa Kampuni ya *Triple "S" Beef Limited*;

(iii) Serikali imeuza asilimia 51 ya thamani ya mali za machinjio ya kisasa, Dodoma, kwa Kampuni ya *National Investment Company Limited (NICOL)* na kubakiza asilimia 49 chini ya Kampuni ya Ranchi za Taifa – NARCO;

(iv) Machinjio za kisasa za kuku za *Mkuza Chicks Limited* (Pwani), *Interchick* na *Tanzania Pride Meat* (Morogoro), zenye uwezo wa kuchinja jumla ya kuku 30,000 kwa siku zimejengwa na zinafanya kazi;

(v) Viwanda vya kusindika maziwa vimeongezeka kutoka 22 mwaka 2005/2006 na kufikia 39 mwaka 2008/2009. Hata hivyo, uwezo wa usindikaji wa maziwa umekuwa ukishuka na kupanda, ambapo mwaka 2005/2006 ulikuwa lita 150,000, 2006/2007 lita 56,580**,** mwaka 2007/2008 lita 65,930 na lita 88,940 kwa siku mwaka 2008/2009. Kushuka kwa usindikaji wa maziwa kumetokana na kutofanya kazi kwa viwanda vya Royal Dairies, Tommy Dairies na Azania Dairies. Aidha, kupungua kwa ukusanyaji wa maziwa kutoka maeneo ya uzalishaji na gharama kubwa za uendeshaji kumesababisha kushuka kwa usindikaji;

(vi) Usindikaji wa ngozi uliongezeka kutoka kilo milioni 1.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 mwaka 2005/2006 na kufikia kilo milioni 5.6 zenye thamani ya

shilingi bilioni 16.0 mwaka 2007/2008. Ongezeko hilo limetokana na kuanza kutekelezwa kwa Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Ngozi nchini. Katika mwaka 2008/2009, usindikaji umefikia kilo milioni 3.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 7.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanashawishiwa kula nyama na mayai na kunywa maziwa kwa wingi zaidi, kwa ajili ya kujenga afya zao na kukuza soko la ndani la bidhaa hizo. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, imeendelea kuhamasisha utumiaji wa mazao ya mifugo kwa kuandaa promosheni mbalimbali, ikiwemo Wiki ya Unywaji Maziwa, ambayo huadhimishwa Kitaifa mwanzoni mwa mwezi Juni ya kila mwaka. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, maadhimisho hayo yamefanyika katika Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Rukwa na Dodoma. Kutokana na uhamasishaji huu, unywaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 39 mwaka 2005/2006 hadi lita 42 mwaka 2008/2009 kwa mtu kwa mwaka.

Aidha, Mradi wa Majaribio wa Unywaji Maziwa Shuleni (*School Milk Pilot Scheme*), uliozinduliwa mwaka 2004 umeendelea kutekelezwa katika shule 73 za Wilaya za Mbeya, Hai, Moshi Vijijini, Tanga na Njombe. Mradi huo unafadhiliwa na wazazi, wasindikaji wadogo, makampuni ya *Fukeni Dairy Company Ltd, Peach Software Company Ltd, Tanga Fresh, Panges Omnus* na Shirika la Maendeleo la Italia – CEFA. Kutokana na mpango huo, jumla ya wanafunzi 53,742 wamenufaika.

Pia, uhamasishaji wa ulaji wa nyama na mayai umeendelea ambapo ulaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai 53 mwaka 2005/2006 hadi 64 mwaka 2007/2008 na sasa 2008/2009 umefikia mayai 72 wakati ulaji wa nyama umepanda kutoka kilo 10 hadi kilo 11 kwa mtu kwa mwaka katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*), Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*PADEP*), Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*DASIP)* na Mfuko wa Jamii Tanzania (*TASAF),* imechangia ujenzi wa malambo 583, visima virefu 21 na mabwawa makubwa mawili katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, *Mwongozo wa Ujenzi Bora wa Vyanzo vya Maji kwa Mifugo na Miundombinu Inayoambatana Nayo* umesambazwa kwa Halmashauri zote nchini. Pia, majosho 134 yamejengwa na 303 yamekarabatiwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wameendelea kuelimishwa kufuga kisasa na kibiashara, kwa kuzingatia uwezo wa ardhi kupitia mashamba darasa 21 yaliyoanzishwa Nzega, Uyui, Manispaa ya Tabora, Urambo, Kilindi, Korogwe, Same, Hai, Arusha, Karatu, Meru na Mvomero na wafugaji 84,630 wameelimishwa mbinu za ufugaji bora ikiwemo umuhimu wa kuuza mifugo yao ili kujiongezea kipato.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga na Dar es Salaam, imeendelea kuhamasisha utekelezaji wa mpango wa unenepeshaji wa mifugo ya nyama ili kuiongezea thamani. Mpango huu pia

unatekelezwa katika Ranchi za *Glienshils Ranch* (Morogoro), *Mark Taylor Farm* na *Kisolonza Farm* (Iringa), *Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds Industries (SAAFI)*, Manyara, Kongwa, Ruvu na Mzeri na wafugaji wadogo. Kutekelezwa kwa mpango huu, kumewezesha kupanua wigo wa soko kwa wafugaji wadogo, ambapo jumla ya ng'ombe 62,000 walinenepeshwa ili kuzalisha nyama bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imemilikisha (*sub-lease*) jumla ya Hekta 289,069 za NARCO kwa wawekezaji wananchi, kwa lengo la kuanzisha na kuendesha ufugaji wa kibiashara katika ranchi (*Commercial Ranching*). Jumla ya vitalu 124 vimemilikishwa kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira katika jamii za wafugaji wa asili ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za asili kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha ufugaji wa mifugo kulingana na uwezo wa ardhi, malisho na maji;

(ii) Kuendeleza na kuhimiza njia za asili za hifadhi ya malisho kama vile *ngitiri* na *ololili; na*

(iii) Kuaandaa Sheria ya Matumizi ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo ili kuweka matumizi endelevu ya ardhi na kuhifadhi mazingira katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali chini ya uratibu wa Wizara ya Nishati na Madini, Asasi ya *SNV – Tanzania na CAMARTEC*, Wizara imeshiriki katika uanzishwaji na utekelezaji wa programu ya matumizi ya nishati mbadala ya biogesi katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara, kwa lengo la kupunguza matumizi ya kuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imejenga jumla ya minada mitatu ya upili ya Nyamatara (Misungwi), Meserani (Monduli) na Kizota (Dodoma); na kukarabati minada 12 ya upili. Aidha, mfumo wa utoaji wa taarifa za masoko ya mifugo (*Livestock Information Network Knowledge System - LINKS*), umeanzishwa katika minada 45 ambayo hutoa taarifa za bei na aina ya mifugo iliyouzwa kwa madaraja kwa kutumia ujumbe wa simu. Vilevile taarifa za LINKS zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara http://www.lmistz.net na http://www.mifugo.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ushauri ziliendelea kutolewa kwa wafugaji ili kuwawezesha kuongeza ubora wa mifugo na mazao yatokanayo na mifugo; hivyo kuongeza tija na mapato. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wafugaji kupitia vipindi 208 vya redio na 48 vya runinga. Pia, mabango 60,130, vipeperushi 230,110 na vijitabu 18,200 kuhusu ufugaji bora, kinga na tiba ya mifugo, uvunaji wa maji ya mvua na uboreshaji wa malisho, vilitayarishwa na kusambazwa kwa wadau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo imeandaliwa na kutekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Ugonjwa wa Sotoka umedhibitiwa na nchi yetu imetambuliwa na kupewa cheti na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani cha kutokuwa na virusi vya ugonjwa huo tangu mwaka 2007;

(ii) Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (RVF) umeendelea kudhibitiwa kwa kusambaza jumla ya dozi milioni 5.5 za chanjo, ambapo jumla ya ng'ombe milioni 4.9 wamechanjwa na ugonjwa haujaripotiwa nchini tangu mwezi Juni 2007;

(iii) Udhibiti wa Mafua Makali ya Ndege unaendelea kwa kujenga uwezo wa kutambua na kufuatilia ugonjwa huo kwa kuchunguza jumla ya sampuli 22,042 za kuku na ndege pori. Hadi sasa ugonjwa huo haujathibitika kuwepo nchini;

(iv) Ugonjwa wa Homa ya Mapafu umeendelea kudhibitiwa kwa kusambaza jumla ya dozi milioni 13.6 ambapo ng'ombe milioni 10.1 wamechanjwa. Tathmini imeonesha kupungua kwa maambukizi ya ugonjwa huo nchini;

(v) Ugonjwa wa Mdondo unadhibitiwa kwa kuendesha kampeni za chanjo kwa kusambaza dozi milioni 69 za chanjo inayostahimili joto (I-2). Tathmini inaonesha kupungua kwa vifo kutoka asilimia 95 hadi 4 katika maeneo yaliyozingatia taratibu za uchanjaji;

(vi) Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa umeendelea kudhibitiwa ambapo dozi 422,000 za chanjo zilisambazwa kwenye Halmashauri mbalimbali nchini na jumla ya mbwa 383,687 walichanjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe Serikali imetoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 12.5 kwa ajili ya kununua lita 827,616 za dawa za kuogesha mifugo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha kituo cha uhimilishaji (NAIC), kwa kufanya ukarabati wa majengo pamoja na kuendeleza shamba la malisho na uzio. Aidha, madume bora 10 ya ng'ombe yamenunuliwa kutoka Afrika ya Kusini na mawili kutoka Kenya, kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mbegu bora na kufanya jumla ya madume bora kufikia 34 yenye uwezo wa kuzalisha dozi 340,000 za mbegu kwa mwaka. Aidha, vituo vidogo vinne vya uhimilishaji vimeanzishwa katika Kanda za Kati (Dodoma), Mashariki (Kibaha), Ziwa (Mwanza) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya). Jumla ya dozi 253,015 za mbegu zilizalishwa, ambapo jumla ya ng'ombe 222,206 walihimilishwa. Aidha, idadi ya wahimilishaji waliopatiwa mafunzo imefikia 529.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya mitamba aina ya Boran 536 wamenunuliwa na kusambazwa katika mashamba ya Wizara ya kuzalisha mitamba. Aidha, mashamba hayo yameendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi, kukarabati miundombinu na

watumishi kupatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Aidha, jumla ya mitamba 3,090 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.2 ilizalishwa katika mashamba ya Wizara na kuuzwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI, imeendelea kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya kuainisha, kutenga na kumilikisha maeneo kwa wafugaji na kuhakikisha yanaendelezwa. Pia, jumla ya wafugaji 259 wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa (30) na Lindi (229), wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi bora ya ardhi. Jumla ya hekta 1,391,109.41 zimetengwa kwa ajili ya ufugaji katika vijiji 240 vya Halmashauri za Wilaya 31 za Mikoa 13. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Asasi Zisizo za Serikali, inatekeleza programu ya kuelimisha wafugaji wa asili kuhusu Sheria za Ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, iliendelea na juhudi za kuwahamasisha wafugaji na wadau wengine wa Sekta ya Mifugo, kuunda vikundi na mitandao ili kuwa na nguvu ya pamoja katika kutatua matatizo yao ya ufugaji na kutafuta masoko. Mpaka sasa, jumla ya vikundi 1,728 vya wafugaji, kuweka na kukopa na uendeshaji wa majosho vimeundwa. Aidha, jumla ya mitandao 39 imeanzishwa katika Mikoa ya Tanga (15) na Kagera (24) kuhusu wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa. Pia, mitandao ya mbuzi wa maziwa aina ya *Norwegian* (NOBRA) imeanzishwa Mgeta (Morogoro) na *Torgenburg* (TOBRA) Babati (Manyara).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuwasaidia wavuvi kutumia maarifa ya kisasa yenye lengo la kuongeza ufanisi na mapato yao kwa njia mbalimbali, zikiwemo kutoa mafunzo juu ya njia bora za uhifadhi na uchakataji wa mazao ya uvuvi kwa watumishi 42 na wavuvi 1,780 katika Wilaya za Rufiji, Kilwa na Mafia. Aidha, mafunzo hayo yalitolewa kwa wavuvi, wamiliki na wafanyakazi wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi 167 katika Ukanda wa Ziwa Victoria. Pia, mafunzo kuhusu njia za kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kabla ya kumfikia mlaji yalitolewa kwa wavuvi 50 wa Mwalo wa Kasela, Mkoani Tanga. Vilevile mafunzo kuhusu uvuvi wa ndoano za kulambaza kwenye maji ya kina kirefu yalitolewa kwa vikundi 32 vya wavuvi katika vijiji vitano vya Ziwa Nyasa, Wilaya za Ludewa (2), Mbinga (2) na Kyela (1). Aidha, mialo 19 imeboreshwa na michoro ya ujenzi wa mialo 9 katika Ukanda wa Ziwa Victoria (6) na Pwani (3) imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uelimishaji na uhamasishaji wa wavuvi wadogo kuanzisha SACCOs, umefanyika katika Wilaya za Rufiji, Kilwa na Mafia na jumla ya VICOBA *(Village Community Bank)* 63 vimeanzishwa katika Wilaya za Rufiji (16), Kilwa (24) na Mafia (23).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kutengeneza mazingira mazuri yatakayosaidia upatikanaji wa zana za kisasa za uvuvi, serikali imepunguza kodi ya malighafi kufikia asilimia tano tu ya kodi halisi na kuondoa kodi ya zana za uvuvi ikiwemo boti, nyavu na injini. Aidha, Wizara kwa kupitia Mradi wa MACEMP,

imehamasisha kuanzisha miradi shirikishi katika maeneo ya Ukanda wa Pwani, itakayosaidia kuwapatia wavuvi zana za kisasa za uvuvi.  Vilevile wavuvi 654 wanaoishi ndani ya Maeneo ya Hifadhi za Bahari, wamefaidika na mpango wa kubadilishana zana haribifu kwa zana bora za uvuvi endelevu. Pia, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Mradi wa MACEMP, itaanzisha mfuko ujulikanao kama *Marine Legacy Fund,* utakaoshughulikia matukio hatarishi ya rasilimali ya uvuvi na mazingira yake katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika  juhudi za kuwavutia wawekezaji kuanzisha viwanda vya kusindika samaki hasa katika Ukanda wa Mwambao wa Bahari ya Hindi na Visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia, Wizara imefanya mapitio ya Sheria Na. 17 ya 2007 ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu na kukamilisha Kanuni za Mamlaka hiyo, ambazo zitawezesha kuwepo kwa taratibu za kuwekeza katika uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imeanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu, yenye makao makuu yake Zanzibar.

Aidha, Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2005 zimefanyiwa mapitio na zimekamilika. Vilevile, katika kudhibiti usalama na ubora wa samaki na mazao yake, Wizara imejenga Maabara ya Taifa ya Uvuvi – Nyegezi, Mwanza, ambayo imetambuliwa rasmi kimataifa. Mazingira haya yamewezesha kuanzishwa kwa Viwanda vya *Tanpesca* kilichoko Kilindoni Mafia na Sea Products Tanzania Ltd. kilichoko Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kushawishi wananchi na wawekezaji wa ndani na nje, kuwekeza katika viwanda vya zana za uvuvi ambapo Kiwanda cha Fanaka Fishnet Ltd kimeanzishwa Jijini Mwanza katika Ukanda wa Ziwa Victoria na Imara Fishnet (T) Ltd cha Dar es Salaam katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika  kupambana na uvuvi haramu, Wizara imeendelea kuzishirikisha serikali za vijiji na mitaa, kwa njia mbalimbali ikiwemo kutoa mafunzo.  Jumla ya wadau 96 kutoka Wilaya za Mafia (39), Rufiji (52), Wataalam wa Idara ya Uvuvi (2) na wa WWF/RUMAKI (3), walishiriki katika mafunzo dhidi ya uvuvi haramu na madhara yake. Aidha, jumla ya vikundi 506 vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) vilivyopo vimeimarishwa na vikundi vipya 177 viko katika hatua za mwisho za uundwaji. Pia, mafunzo ya ulinzi shirikikishi wa rasilimali ya pwani, yalitolewa kwa waraghibishi 48 kutoka Wilaya za Mafia na Rufiji na Watalaam wa Ugani 68 kutoka Halmashauri za Mkinga, Muheza, Pangani, Jiji la Tanga; Bagamoyo, Mafia, Mkuranga, Rufiji, Kilwa, Lindi Vijijini, Lindi Mjini, Mtwara Mikindani na Mtwara Vijijini. Vilevile viongozi 2,655 wa Halmashauri za Vijiji na Jamii ya Wavuvi kwenye Halmashauri za wilaya hizo walihamasishwa kuhusu kusimamia uanzishwaji wa BMUs kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kuhusu mbinu bora za uhifadhi wa mazao ya uvuvi na upunguzaji wa uharibifu wa mazao ya uvuvi ilitolewa kwa kuchapisha na kusambaza nakala 1,000 za mabango, vijarida 6,000 na vipeperushi 37,000.  Aidha,

vipindi 70 vya redio na 20 vya runinga, vilirushwa hewani kwa madhumuni ya kuelimisha umma kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilifanya jumla ya siku-kazi za doria 17,774 katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Tanganyika, Bwawa la Nyumba ya Mungu na Baharini, ambapo nyavu haramu 225,881, baruti 172, magari 31, mitumbwi 732, baiskeli 107 na Kamba za kokoro mita 511,264 vilikamatwa. Aidha, samaki kilo 4,162,340, dagaa kilo 146,640, kasa hai 20, nyama ya kasa kilo 40 na majongoo bahari kilo 7,188.50 walikamatwa. Watuhumiwa 3,635 walikamatwa na kesi 184 zilifunguliwa mahakamani. Pia, meli ya kigeni iliyokuwa na tani 296.3 za aina mbalimbali ya samaki ilikamatwa katika eneo la Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu na watuhumiwa 37 walifikishwa mahakamani.

Wizara imeendelea kuimarisha vituo sita vya doria vya Tanga, Dar es Salaam, Kigoma, Musoma, Kagera na Mwanza na kuanzisha vituo 12 vipya vya doria katika maeneo ya Mtwara, Mafia, Kilwa, Horohoro, Kipili, Kasanga, Sota, Sirari, Kasumulo, Tunduma, Kabanga na Kanyigo ili kuimarisha doria nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu lake la kuboresha ukuzaji wa viumbe kwenye maji, Wizara imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Ukuzaji wa Viumbe Kwenye Maji (*National Aquaculture Development Strategy – NADS*). Aidha, wataalam 14 wamepelekwa Morogoro (6), Ruvuma (1), Kilimanjaro (2), Tabora (1), Lindi (1), Mara (2) na Mwanza (1), kwa lengo la kuanzisha na kuimarisha vituo vya ukuzaji viumbe kwenye maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, imepandikiza jumla ya vifaranga milioni 2.1 vya samaki aina ya perege na 758 vya kambale katika Mikoa ya Pwani, Iringa, Kilimanjaro, Rukwa, Shinyanga, Mbeya, Tabora, Ruvuma, Kagera, Mwanza na Morogoro. Kati ya hivyo, vifaranga 686,280 vya samaki aina ya perege kutoka Kituo cha Kingolwira vilisambazwa kwa wafugaji wa samaki kwenye Mikoa ya Pwani, Ruvuma, Morogoro, Rukwa na Dodoma. Aidha, ufugaji wa Kambamiti kibiashara (*Prawn farming*), umeendelea kufanywa na kampuni ya *Alpha Krust* katika mabwawa 30 Wilayani Mafia, ambayo yamezalisha jumla ya tani 250 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2.3 na kati ya hizo, tani 100 zimeuzwa katika soko la Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha ugani katika ukuzaji viumbe kwenye maji, pikipiki sita zilipelekwa katika Halmashauri za Meru, Mtwara, Tanga, Songea, Lindi na Kituo cha Ukuzaji wa Samaki Kingolwira. Aidha, utambuzi wa maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki na unenepeshaji wa kaa umefanyika katika vijiji 16 vya Mikoa ya Tanga, Mtwara, Lindi na Pwani. Pia, majaribio ya uzalishaji wa lulu (*pearls*), yanaendelea katika Wilaya za Mafia na Pangani. Vilevile nakala 16,000 za Mwongozo wa Ufugaji wa Samaki zilisambazwa kwa wananchi na mafunzo ya ufugaji wa samaki yametolewa kwa wanavijiji 250 katika Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kukamilika kwa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Ukuzaji wa Viumbe Kwenye Maji (*National Aquaculture Development Strategy – NADS*), Wizara itaandaa mpango mahususi wa kuzalisha na kusambaza mbegu bora za samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha mwani kinaendeshwa katika maeneo mbalimbali ya pwani yetu kwa kuhusisha takriban wakulima 3,000. Kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2008/2009, tani 940 za mwani mkavu zimezalishwa na kati ya hizo tani 320 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 136,000 ziliuzwa nje ya nchi. Vilevile Wizara imetoa mafunzo ya ujasiriamali na uboreshaji wa kilimo cha mwani kwa wakulima 783 wa Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo ina umuhimu mkubwa katika kumwondolea umaskini mwananchi hususan katika maeneo ya vijijini. Katika mwaka 2008/2009, idadi ya mifugo inakadiriwa kufikia ng'ombe milioni 19.1, mbuzi milioni 13.6, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.6 na kuku milioni 56 *(Hali ya Uchumi wa Taifa, Juni 2008)*. Kati ya ng'ombe hao, 605,000 ni ng'ombe wa maziwa. Vilevile kati ya kuku hao, milioni 22 ni kuku wa kisasa, ambapo milioni 8 ni kuku wa mayai na milioni 14 ni kuku wa nyama. Wastani wa ulaji mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka 2008/2009 ni kilo 11 za nyama, lita 42 za maziwa na mayai 72. Ulaji huu ni mdogo ikilinganishwa na viwango vya FAO vya kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka. Aidha, katika mwaka 2008, Sekta ya Mifugo ilikua kwa asilimia 3.7 ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2007 na kuchangia asilimia 4.6 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi pia inayo fursa kubwa katika kuchangia kuondoa umaskini kwa kuwapatia wananchi lishe bora, ajira na kipato. Katika mwaka 2008, jumla ya tani 335,024 za samaki zilivuliwa nchini, ambapo tani 324,960 sawa na asilimia 97 zilivuliwa na wavuvi wadogo wapatao 170,038 na tani 10,114 zilivuliwa na meli kubwa katika Bahari kuu. Katika mwaka 2008, Sekta ya Uvuvi ilikua kwa asilimia 4.3 na kuchangia asilimia 1.3 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na kukua kwa asilimia 4.5 na kuchangia asilimia 1.6 mwaka 2007. Wastani wa ulaji mazao ya uvuvi kwa mtu kwa mwaka 2008/2009 ulifikia kilo 8.1 ikilinganishwa na kilo 10.7 zinazopendekezwa na FAO.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili sekta hizi ziweze kuchangia zaidi katika Pato la Taifa na kuboresha pato la mfugaji na mvuvi, Wizara imekamilisha kuandaa Mkakati wa Kutekeleza Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe kwenye Maji. Aidha, mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi yanaendelea. Vilevile Sheria mbalimbali zinazosimamia Sekta za Mifugo na uvuvi zinaendelea kufanyiwa mapitio ili kukidhi matakwa ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kipindi cha mwaka 2008/2009, zimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Uhaba wa maeneo ya ufugaji na miundombinu umesababisha wafugaji kuhamahama na kusababisha uharibufu wa mazingira, kuenea kwa magonjwa ya mifugo na migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi;

(ii) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi umesababisha ukuaji mdogo wa sekta hizi kuliko ilivyotarajiwa;

(iii) Kuwepo kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo, hususan ya milipuko kumeathiri maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini;

(iv) Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uhifadhi wa samaki na mazao ya uvuvi, uzalishaji duni na ukosefu wa masoko ya uhakika kumepunguza mchango wa sekta hizi katika Pato la Taifa;

(v) Kutokuwepo kwa taasisi za mikopo zenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi kumesababisha washindwe kupata mitaji ili kuzalisha kibiashara;

(vi) Gharama kubwa za pembejeo za mifugo na uvuvi zikiwemo chanjo za mifugo na zana za uvuvi kumesababisha wafugaji na wavuvi kushindwa kuzimudu na hivyo kupunguza uzalishaji wenye tija na kupunguza mapato kwa wafugaji na wavuvi;

(vii) Kuendelea kuwepo kwa uvunaji na matumizi ya rasilimali za uvuvi yasiyo endelevu; na

(viii) Matumizi duni ya teknolojia sahihi za ufugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake na Wadau wa Sekta, iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kubuni na kutayarisha sera, sheria, kanuni na miongozo; kutayarisha mikakati na programu za kisekta na kusimamia utekelezaji wake. Majukumu mengine yaliyotekelezwa ni pamoja na kukusanya na kusambaza takwimu na taarifa muhimu za sekta; kutoa huduma za ushauri kwa wadau; kufanya na kuimarisha tafiti mbalimbali; kutoa mafunzo kwa watumishi na watarajali na wadau; kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo na uvuvi; kudhibiti na kukagua ubora wa zana, pembejeo, usalama na viwango vya mazao ya mifugo na uvuvi, pamoja na masoko; kusimamia Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu; kukusanya maduhuli na kuendeleza rasilimali watu.

Majukumu hayo yametekelezwa kwa kuzingatia malengo ya kitaifa, ambayo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (Vision 2025), MKUKUTA na Mkakati wa Msaada Tanzania (*Joint Assistance Strategy for Tanzania - JAST*), Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 1997. Aidha, Wizara imezingatia miongozo na kanuni za Kimataifa kama Malengo ya Milenia (MDGs),

Mikakati na Makubaliano ya Mashirika mbalimbali ya Kimataifa yanayohusu Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 9,334,915,000. Kati ya hizo, shilingi 1,269,492,287 ni kutoka Sekta ya Mifugo na shilingi 8,055,421,000 ni kutoka Sekta ya Uvuvi. Hadi kufikia mwezi Mei 31, 2009, jumla ya shilingi 6,191,036,863 zilikusanywa ikiwa ni asilimia 67 ya lengo la makusanyo. Vilevile kiasi cha shilingi 1,368,098,460 kilikusanywa ikiwa ni mauzo ya asilimia 51 ya thamani ya machinjio Dodoma na kufanya kiasi kilichokusanywa kufikia shilingi 7,559,135,323. Kati ya hizo, shilingi 2,462,517,284 ni kutoka Sekta ya Mifugo na shilingi 5,096,618,039.4 ni kutoka Sekta ya Uvuvi. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 11,267,731,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, iliidhinishiwa jumla ya shilingi 54,557,250,390. Kati ya hizo, shilingi 34,184,743,390 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 20,372,507,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 23,761,804,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine (OC) na shilingi 10,422,939,390 kwa ajili ya mishahara (PE). Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, shilingi 7,723,810,000 zilikuwa fedha za ndani na shilingi 12,648,697,000 fedha za nje.

Hadi kufikia mwezi Juni, 2009, jumla ya shilingi 32,570,307,814 (asilimia 95.3) zimetolewa. Kati ya hizo, shilingi 11,343,273,914 ni mishahara na shilingi 21,227,033,900 ni matumizi mengineyo. Vilevile shilingi 21,402,082,251.50 zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Kati ya hizo, shilingi 6,995,000,000 ni fedha za ndani (asilimia 90.6) na shilingi 14,357,082,251.50 ni fedha za nje.
Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Ili kufikia azma hiyo ya Serikali, kazi zifuatazo zitapewa kipaumbele katika utekelezaji:-

Sekta ya Mifugo:

(i) Kuendelea kutoa ruzuku ya dawa, chanjo na pembejeo za mifugo.

(ii) Kuboresha miundombinu ya mifugo.

(iii) Kuimarisha huduma za uhimilishaji mifugo na utafiti wa mifugo.

(iv) Kutoa elimu ya wataalam wa ugani wa sekta ya mifugo.

(v) Kupanga matumizi ya maeneo ya malisho ya mifugo.

Sekta ya Uvuvi:

(i) Kuimarisha miundombinu ya kupokelea, kuhifadhi, kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi.

(ii) Kudhibiti uvuvi na biashara haramu na kuhifadhi mazingira.

(iii) Kuimarisha utoaji wa huduma za ufugaji wa samaki na ukuzaji wa viumbe wengine kwenye maji (*Aquaculture*).

(iv) Kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Uvuvi na ukusanyaji wa takwimu.

(v) Kutoa elimu ya wataalam wa ugani wa Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 1997, ambapo rasimu ya awali imekamilika. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itakamilisha maandalizi ya Sera hiyo na kuiwasilisha Serikalini. Aidha, Mkakati wa kutekeleza Sera hiyo utaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 inawafikia wadau ambao ndio watekelezaji wakuu wa Sera hiyo, Wizara imesambaza jumla ya nakala 4,500 za Sera hiyo kwa wadau mbalimbali nchini. Pia, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera hiyo kupitia matukio ya kitaifa yakiwemo; Sikukuu ya Wakulima Nane Nane, Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa, Wiki ya Utumishi wa Umma, pamoja na mikutano mbalimbali ya kitaaluma. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imekamilisha kuandaa Mkakati wa Kutekeleza Sera ya Taifa ya Mifugo. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itafanya tafsiri ya mkakati huo katika Lugha ya Kiswahili na itausambaza kwa wadau na kuandaa Mipango ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Sheria ya Ngozi (*Hides, Skins na Leather Trade Act*) Na. 18 ya Mwaka 2008 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*Animal Welfare Act*) Na. 19 ya 2008, zimepitishwa na Bunge lako Tukufu na zimeanza kutumika tarehe 1 mwezi Mei, 2009.

Aidha, mapendekezo ya kutunga sheria nyingine yapo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo *(Grazingland and Animal Feed Resources Act*) na Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo (*Livestock Identification, Registration and Traceability*) zimewasilishwa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kujadiliwa na kwa hatua zaidi; na

(ii) Sheria ya Maabara Kuu ya Mifugo (*Central Veterinary Laboratory Act*) na Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo (*National Livestock Research Institute Act*) zimewasilishwa kwenye Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, inaendelea kuandaa na kufanya mapitio ya sheria zifuatazo:-

(i) Rasimu ya awali ya Sheria ya Uzalishaji wa Mbari Bora ya Wanyama (*Animal Breeding Act*) ya mwaka 2009 imeandaliwa;

(ii) Rasimu ya kwanza ya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(Marine Parks and Reserves Authority Act*) Na. 29 ya mwaka 1994 imekamilika;

(iii) Rasimu ya kwanza ya mapitio ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (*Tanzania Fisheries Research Institute Act*) Na. 6 ya mwaka 1980 imekamilika; na

(iv) Rasimu ya Sheria ya Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeandaa kanuni mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kanuni za Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi Bahari Kuu Sura Na. 388 zimekamilika na kuanza kutumika tarehe 06 Machi, 2009 na kupewa GN. Na. 48 ya mwaka 2009; na

(ii) Rasimu za Kanuni zifuatazo zinaendelea kufanyiwa kazi na Serikali:-
- Kanuni za Sheria ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008.
- Kanuni za Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008
- Kanuni za Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 mwaka 2003
- Kanuni za Sheria ya Veterinari Na. 16 ya 2003.
- Kanuni za Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006.
- Kanuni za Kudhibiti Mbung'o.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kukamilisha sheria na kanuni zilizotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kuratibu Bodi tano zinazosimamia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Bodi ya Nyama, Bodi ya Maziwa, Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) na Baraza la Veterinari Tanzania. Pia, Wizara imeendelea kusimamia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo – Mpwapwa, Maabara ya Mifugo Temeke na Maabara ya Uvuvi – Nyegezi. Utekelezaji wa majukumu ya Bodi na Taasisi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), imeendelea kuzalisha nyama kupitia ranchi zake 10 za mfano, zenye jumla ya ng'ombe 34,859. Katika mwaka 2008/2009, NARCO ilizalisha jumla ya ndama 9,265 kati ya ng'ombe wazazi 12,834, sawa na asilimia 72 ya uzalishaji na kuuza ng'ombe 6,748 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.7. Aidha, kampuni ilinunua ng'ombe 2,954 wenye thamani ya shilingi milioni 599 kwa ajili ya kunenepesha. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni kwa sasa imekamilisha upimaji wa vitalu kwa ajili ya kuwamilikisha wawekezaji wazalendo katika Ranchi ya West-Kilimanjaro na mchakato wa kuwapata wamilikishwaji unaendelea. Pia, Wizara imewezesha upatikanaji wa hati miliki ndogo kwa vitalu 91 kati ya 124 katika ranchi za Mzeri (8), Missenyi (10), Mkata (11), Uvinza (21), Usangu (18), Mabale (6) na Kagoma (17). Utoaji wa hati kwa vitalu vya Ranchi za Mkata, Kalambo na Kitengule unaendelea. Ranchi zilizomilikishwa kwa wawekezaji wazalendo zinaendelea vizuri kwa kuwa wamejenga miundombinu ya mashamba zikiwemo nyumba za wafanyakazi, malambo, visima na ofisi kufuatia notisi ya miezi sita ya kuwanyang'anya vitalu kwa wale wasioviendeleza. Nasisitiza tena kwa wote waliopewa maeneo hayo, kuwekeza kulingana na uwezo wa maeneo. Wizara yangu haitasita kuwanyang'anya wale wote watakaoshindwa kuyaendeleza mashamba hayo na kuwapatia wananchi wengine wenye nia na uwezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imemilikisha machinjio ya Dodoma kwa kampuni ya *Tanzania Meat Company,* ambayo imeundwa kwa ubia kati ya NARCO yenye hisa 49 na *NICOL* hisa 51, kwa lengo la kuchinja ng'ombe, kondoo na mbuzi kutoka NARCO, wafugaji wadogo na wafanyabiashara wa mifugo kwa ajili ya kuuza nyama kwenye soko la ndani na nje ya nchi. Aidha, NARCO imeingia mkataba na Kampuni ya ujenzi ya SUMA ya Jeshi la Wananchi Tanzania, kujenga machinjio ya kisasa katika Ranchi ya Ruvu kwa gharama ya shilingi bilioni 10.7. Machinjio haya yatakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 800 na mbuzi/kondoo 400 kwa siku na machinjio haya yatakuwa mojawapo ya machinjio kubwa nchini. (*Makofi*)

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaiwezesha NARCO kufanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na ujenzi wa machinjio katika Ranchi ya Ruvu;
(ii) Kunenepesha ng'ombe 3,000 kwa ajili ya kupata nyama bora;
(iii) Kusimamia na kushauri ufugaji bora katika ranchi ndogo zilizomilikishwa kwa wawekezaji wananchi;
(iv) Kukamilisha utoaji wa hati za vitalu katika ranchi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Nyama Tanzania imeundwa chini ya Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006. Bodi hii imezinduliwa rasmi mwaka 2008, ikiwa na jukumu la kusimamia sekta ndogo ya nyama nchini. Katika mwaka 2008/09, Wizara ikishirikiana na Bodi, imeandaa Mpango Mkakati wa Sekta ndogo ya nyama.

Katika mwaka 2009/2010, Bodi ya nyama itaajiri sekretarieti, kusajili wadau na kuwahamasisha kuhusu sheria ya nyama na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Maziwa Tanzania, ina jukumu la kusimamia sekta ndogo ya maziwa kupitia Sheria ya Maziwa Na. 8 ya Mwaka 2004. Katika mwaka 2008/2009, Bodi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* imehuisha viwango saba vya maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa nchini ili vifanane na vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Bodi imefanya mapitio ya viwango 24 vya bidhaa

zitokanazo na maziwa. Vilevile Bodi ya maziwa ikishirikiana na Bodi ya Maziwa ya India, imepeleka wadau wa maziwa na wataalamu 25 India, kujifunza mbinu za kuanzisha na kuendesha ushirika wa uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na uuzaji wa maziwa. Ziara hii imesaidia kuwapa wadau na wataalamu, uzoefu na mbinu sahihi za kuendeleza ushirika wa maziwa nchini. Pia, Bodi ya maziwa imeendelea kusimamia na kuratibu Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni, inayofanyika kwenye shule 73 ambapo jumla ya wanafunzi 53,742 wanafaidika na programu hiyo kwa kunywa maziwa. *(Makofi*)

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa, itasajili wadau wa maziwa 200 wakiwemo wazalishaji, wakusanyaji, wasafirishaji, wasindikaji na wauzaji wa maziwa. Aidha, Bodi itarasimisha wachuuzi wa maziwa 100 kwa kuwapa mafunzo na leseni za kufanyia biashara. Pia, Bodi itaendelea kuratibu programu za unywaji wa maziwa shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(Marine Parks and Reserves Unit - MPRU),* kimeandaa Mipango ya Jumla ya Usimamizi wa Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma na Maeneo Tengefu ya Dar es Salaam Kaskazini. Maeneo hayo yanajumuisha Visiwa vya Bongoyo, Mbudya, Fungu Yasini na Pangavini. Ujenzi wa Ofisi ya Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma umekamilika kwa asilimia 80. Aidha, michoro ya jengo la Kituo cha Utafiti kwenye Hifadhi ya Bahari ya Mafia imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kuwashirikisha wadau, imekamilisha taratibu za kulitangaza eneo la Kigombe, Tanga, kuwa Hifadhi ya Bahari ya Silikanti. Hifadhi hii itakuwa ya pili ulimwenguni, ikifuatia ile ya Afrika Kusini, ambayo inatarajia kuongeza utalii wa baharini nchini. Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia MPRU itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kukamilisha mchakato wa kulitangaza eneo la Kigombe, Tanga kuwa Hifadhi ya Bahari ya Silikanti;
(ii) Kutangaza kwenye Gazeti la Serikali, Visiwa vya Mwewe, Kirui, Ulenge na Kwale vilivyopo katika Wilaya ya Mkinga, Tanga, kuwa Maeneo Tengefu Mtambuka mpakani mwa Tanzania na Kenya (*Trans-boundary Marine Reserves*) ili kulinda mifumo ya ikolojia na rasilimali za bahari;
(iii) Kufuatilia rasilimali za bahari kama vile matumbawe na aina mbalimbali za samaki kwenye Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, kwa kushirikisha taasisi za utafiti wa uvuvi;
(iv) Kuimarisha Kitengo kwa kukipatia watumishi na vitendea kazi kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za bahari kwenye maeneo mapya ya hifadhi na kuvutia utalii na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), imeendelea kufanya utafiti wa ufuatiliaji wa

mwenendo wa rasilimali ya kambamiti ili kutathmini uwingi baada ya kufunga uvuvi huo kwa wavuvi wa meli kubwa na za kati mwaka 2008. Matokeo ya ufuatiliaji huo, yanatazamiwa kupatikana mwezi Agosti 2009. Vilevile kwa kushirikiana na watafiti wa ndani na nje, Taasisi imebaini sababu za kisayansi zitakazowezesha kuanzishwa kwa Hifadhi ya Silikanti Tanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kutekeleza maagizo ya Baraza la Mawaziri wa Nchi za Kenya, Tanzania na Uganda, lenye dhamana ya kusimamia uvuvi katika Ziwa Victoria, TAFIRI kwa kushirikiana na Taasisi za Utafiti wa Uvuvi za Kenya na Uganda imeendelea kutathmini mwenendo na uwingi wa rasilimali za samaki katika Ziwa Victoria. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Sangara walipungua kutoka tani 375,670 mwezi Februari, 2008 hadi tani 227,365 Agosti, 2008. Hata hivyo, matokeo ya utafiti ya mwezi Februari, 2009 yameonesha kuwa sangara wameongezeka hadi kufikia tani 369,498. Aidha, katika kipindi hicho, dagaa wameongezeka kutoka tani 742,289 hadi 1,261,174; furu na samaki wengine kutoka tani 518,359 hadi 820,624.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza upatikanaji wa samaki, TAFIRI imeanza utafiti wa teknolojia sahihi ya uzalishaji wa vifaranga bora kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwa kujenga mabwawa saba katika vituo vya Dar es Salaam (4) na Sota - Rorya (3).

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia TAFIRI itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kutathmini wingi wa kambamiti na nguvu ya uvuvi (*fishing effort*) inayohitajika katika uvuvi huo.
(ii) Kufanya utafiti utakaolenga kutatua matatizo ya ufugaji samaki.
(iii) Kufuatilia na kutathmini uvuvi wa kutumia ndoano za kulambaza.
(iv) Kufanya utafiti wa hali ya uvuvi katika Maziwa ya Rukwa, Eyasi, Manyara na Bwawa la Mtera na Mto Kilombero.
(v) Kuendelea na utafiti wa teknolojia sahihi ya kuzalisha vifaranga na vyakula bora kwa ajili ya wafugaji wa samaki.
(vi) Kujenga ofisi na maabara ya kituo cha utafiti cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo – Mpwapwa, pamoja na vituo sita vya Kongwa, Mabuki, Naliendele, Tanga, Uyole na West Kilimanjaro vilivyo chini ya Taasisi hiyo, viliendelea na jukumu la kufanya utafiti wa mifugo kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mifugo nchini. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya ndama 147 aina ya Mpwapwa na 127 chotara wa Boran na Mpwapwa walizaliwa. Aidha, madume bora 90 aina ya Mpwapwa yalisambazwa na kufanyiwa tathmini katika Wilaya za Iramba (40), Chunya (20), Mpwapwa (14), Bahi (12) na Dodoma (Manispaa) (4), ikiwa ni asilimia 100 ya lengo lililowekwa. Vilevile ng'ombe 14 aina ya *Friesian* walisambazwa katika Wilaya za Rungwe, Mbeya, Sumbawanga na Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhimilishaji kwa kutumia mbegu za ng'ombe aina ya *Sahiwal* ulifanyika ili kuharakisha uzalishaji wa ng'ombe aina ya Mpwapwa kituoni

ambapo ndama maalum 21 walizalishwa kutokana na njia hiyo. Katika mwaka 2009/2010, Taasisi itazalisha ndama 150 aina ya Mpwapwa na madume 100 na kusambazwa katika vijiji mbalimbali na kuwafanyia tathmini ya ukuaji na uzalishaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, utafiti na uendelezaji mbuzi wa maziwa ulifanyika na mbuzi 86 walizalishwa na kufanya idadi ya mbuzi katika Taasisi kufikia 236. Jumla ya mbuzi 91 wamesambazwa kwa wafugaji katika Wilaya za Kishapu (majike 40 na madume 10), Mpwapwa (majike 27 na madume 4) na Singida (madume 10).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzalisha na kuchambua sifa za mbuzi wa asili, majike 20 aina ya *Gogo white* walinunuliwa kutoka kwa wafugaji wa Dodoma na kutunzwa katika Kituo cha Utafiti wa Malisho Kongwa, ambapo takwimu muhimu za sifa na tabia za mbuzi hao zinaendelea kukusanywa.

Katika mwaka 2009/2010, madume bora 80 ya mbuzi yatasambazwa vijijini kwa lengo la kutathmini uzalishaji wao. Pia, mafunzo ya ufugaji bora yatatolewa na ukusanyaji wa takwimu muhimu kuhusu ukuaji na uwezo wa kuzalisha chotara wanaopatikana kwa kupandisha mbuzi wa asili na madume bora utaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Taasisi imeendelea kuzalisha nguruwe bora kwa ajili ya kusambaza kwa wafugaji vijijini ili kuboresha ufugaji wa nguruwe. Jumla ya nguruwe 97 wamezalishwa na kati ya hao, 70 wamesambazwa. Katika mwaka 2009/2010, Taasisi itaendelea na utafiti ili kubuni teknolojia zinazoongeza uzalishaji wa nguruwe kituoni na vijijini. Aidha, nguruwe 200 watazalishwa, kati ya hao 180 watasambazwa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, tathmini za uzalishaji wa kuku 378 wa asili wakiwemo *Kuchi, Kishingo, Kikwekwe/Ntewa, Sasamala na Bukini*, *Msumbiji, Kinyavu, Njachama* na kuza zilifanyika katika Vituo vya Utafiti vya Naliendele, Uyole na Mpwapwa. Matokeo ya awali ya tathmini hizo yameonesha kuwa, kuku wa asili waliopewa vyakula vya ziada waliongezeka kwa takriban gramu 500 zaidi ya wasiopewa vyakula hivyo wakiwa na umri wa majuma 24. Aidha, idadi ya mitago (*Clutches*) iliongezeka kutoka 4 ya mayai 58 hadi 8 ya mayai 112 kwa mwaka.

Katika mwaka 2009/2010, Taasisi itaendelea kuainisha na kukusanya kuku wenye sifa nzuri za uzalishaji mayai na nyama kutoka Mikoa ya Iringa na Rukwa. Aidha, utafiti utakaowezesha kuku wa asili kufikia uzito wa kilo 2 chini ya mwaka, kutaga mayai 150 kwa mwaka na uzito wa yai wa zaidi ya gramu 60 zitafanywa. Pia, Taasisi itaendelea kuhifadhi aina za kuku wa asili ambao wako hatarini kutoweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti kuhusu mbuzi na kondoo wa asili uliolenga kufahamu sifa zao na namna ya kuzitumia ili kuboresha uzalishaji ulifanyika katika Vituo vya Naliendele, West Kilimanjaro na Tanga. Mbuzi aina ya Newala 144, *Pare White* 64, *Sonjo Red* 39 na *Red Maasai* 194 walihusika. Pia, ukusanyaji takwimu ulifanyika kwa

mbuzi chotora aina ya *Blended Goats* 117 *na* kondoo aina ya *Black Head Persian* 212. Utafiti huu bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, utafiti wa kuainisha uzalishaji wa ng'ombe wa *Ankole* na *Ufipa* uliendelea katika Vituo vya Mabuki na Uyole. Matokeo ya awali yamebaini kuwa, ng'ombe aina ya *Ankole* wanahimili mazingira ya joto na mvua haba. Pia, utafiti wa kuainisha sifa za uzalishaji uliendelea kwa ng'ombe aina ya *Singida white* katika Taasisi ya Mpwapwa. Katika mwaka 2009/2010, Taasisi itaendeleza utafiti wa kufuatilia kosaafu za ng'ombe wa asili jamii za *Ankole, Ufipa, Singida white* na *Iringa Red* vituoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Taasisi ilikusanya aina 80 za malisho na kuzihifadhi katika *Genebank* ya Kituo cha Mpwapwa kwa lengo la kuzifanyia tathmini ya uzalishaji wa malisho na miti malisho. Aidha, jumla ya vinasaba 72 vya malisho mbalimbali vinaendelea kuainishwa na kutunzwa katika Kituo cha Utafiti Uyole.

Katika mwaka 2009/2010, usambazaji wa vinasaba vitakavyoonekana kuzalisha malisho na miti malisho kwa wingi utafanyika. Pia, aina nyingine 50 za malisho kutoka nje na ndani ya nchi zitakusanywa, kustawishwa, kufanyiwa tathmini na kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, jumla ya kilo 2,800 za mbegu za nyasi na 576 za mikunde ya malisho zilizalishwa katika Vituo vya Mpwapwa na Mabuki. Aidha, kilo 1,454 za mbegu za nyasi na kilo 66 za mikunde ya malisho ziliuzwa kwa wakulima kwa lengo la kutathmini uzalishaji. Pia, tathmini ya mchanganyiko wa uzalishaji wa malisho, nafaka na mabaki ya mazao, uliendelea kufanyika vituoni na katika Vijiji vya Iguguno (Iramba), Unyankhanya (Singida Vijijini) na Mtumba (Dodoma). Matokeo ya tathmini ya mbegu za malisho zilizosambazwa kwa wakulima yanaonesha kuwa, mikunde ya malisho inaweza kustawishwa pamoja na mimea ya nafaka na kuongeza ubora wa malisho bila kuathiri uzalishaji wa nafaka. Matokeo haya yanaashiria uwezekano wa kuongeza uzalishaji wa vyakula bora vya mifugo bila kuathiri usalama wa chakula katika kaya zinazolima na kufuga. (*Makofi*)

Katika mwaka 2009/2010, kilo 3,000 za mbegu za nyasi na 600 za mbegu za mikunde ya malisho zitazalishwa na kutathminiwa. Aidha, Taasisi itaendelea na utafiti wa kuboresha malisho hasa katika maeneo yenye ukame kama ya Mikoa ya Dodoma na Singida na kuongeza ubora wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, vituo vya utafiti wa mifugo viliimarishwa kwa kuvipatia vitendea kazi. Pia, majengo ya ofisi na nyumba za watumishi katika Vituo vya Mpwapwa, Kongwa, Mabuki, West Kilimanjaro, Naliendele na Uyole yamekarabatiwa. Watafiti 2 wameanza mafunzo ya uzamivu na 4 wameanza mafunzo ya uzamili. Aidha, mafunzo ya muda mfupi ya namna ya kuandaa maandiko na tathmini ya matokeo ya utafiti yamefanyika kwa watafiti wapya 27. Vilevile ziara ya mafunzo kwa wataalamu wa mifugo 5 ilifanyika nchini India, kwa lengo la kuwajengea uwezo wa namna ya kupanga na kuratibu shughuli za utafiti.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, itaendelea kuimarisha vituo vyake kwa kuvipatia vitendea kazi muhimu na mafunzo kwa watafiti ya muda mfupi 72 na mrefu 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, rasimu za Mipango ya Utafiti wa Mifugo (*Livestock Research Programmes*) wa maziwa, lishe na malisho, uzalishaji wa wanyama (*animal breeding*), kuku na nguruwe na mbuzi na kondoo ziliandaliwa.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itakamilisha maandalizi ya mipango ya utafiti na kuendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utafiti wa mifugo na utoaji huduma chini ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo - ASDP.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kuimarisha na kuiwezesha Mifuko ya Utafiti na Maendeleo ya Kanda (*Zonal Agricultural Research and Developmet and Extension Fund – ZARDEF*), iliyoundwa katika kanda 7 za utafiti nchini kwa kuzipatia jumla ya shilingi milioni 85.7 kila kanda, kwa ajili ya kugharimia miradi ya utafiti kulingana na vipaumbele vya Kanda husika. Jumla ya miradi 30 ya utafiti wa mifugo imefadhiliwa na Mfuko huo. Aidha, mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko wa ZARDEF uliandaliwa, kwa kushirikiana na Kamati za Usimamizi wa Utafiti katika Kanda zote saba. Vitengo vya mawasiliano ya utafiti vya kanda 7 *(Zonal Information and Extension Liaison Units - ZIELU*) viliundwa na Wataalamu 32 wa ZIELU walipatiwa mafunzo ya namna ya kuandika matokeo ya utafiti wa kilimo na mifugo kulingana na mahitaji ya wadau (*Client Oriented Research and Development Management Approach – CORDEMA).* Aidha, mafunzo ya *CORDEMA* kwa watafiti wakufunzi wa mifugo 15 na watafiti 71 yalifanyika. (*Makofi*)

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuwezesha Mifuko ya ZARDEF ili iendelee kufanya utafiti kulingana na vipaumbele vya kanda na mahitaji ya wadau;
(ii) Kushirikiana na Taasisi za kitaifa na kimataifa kuratibu utafiti shirikishi wa mifugo;
(iii) Kuwezesha/kuratibu utoaji mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watafiti 71 na wataalamu wa mifugo 20 katika kanda nyingine;
(iv) Kuimarisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu za utafiti wa mifugo nchini; na
(v) Kukamilisha ajenda ya utafiti wa mifugo ili kuimarisha mfumo wa utafiti wa mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo – Temeke ni pamoja na kufanya uchunguzi, utambuzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo; kufanya majaribio ya dawa mpya na chanjo za mifugo; kutengeneza chanjo mbalimbali za kuzuia magonjwa ya mifugo; kuchunguza ubora wa bidhaa zitokanazo na

mifugo; kuchunguza nguvu za dawa za majosho na kuchunguza ubora wa vyakula vya mifugo. Pia, maabara hutoa mafunzo ya ufundi sanifu maabara na stashahada ya afya ya wanyama. Katika mwaka 2008/2009, Maabara Kuu imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kufanya utambuzi wa magonjwa mbalimbali ya Mifugo kutokana na sampuli 11,079 za wanyama zilizopokelewa. Baadhi ya Magonjwa yaliyotambuliwa ni Homa ya Nguruwe, Ndigana Kali, Mkojo Mwekundu (*Babesiosis)*, Ndigana baridi *(Anaplasmosis)*, Nagana, Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Kideri *(Fowl typhoid),* Mdondo (Newcastle disease), *Mareks disease, Gumboro na* Sotoka ya Mbuzi na Kondoo *(Peste petit Ruminantia - PPR).*

(ii) Kuzalisha na kusambaza chanjo dozi milioni 23 za kuzuia Mdondo, dozi 500,000 za kuzuia Kimeta na dozi 300,000 za kuzuia Chambavu. Aidha, dozi 25,000 za chanjo ya kuzuia ugonjwa wa Kutupa Mimba zimefanyiwa majaribio ya ubora na usalama.

(iii) Kufanya uchunguzi na kuhakiki ubora wa mazao na vyakula vya mifugo, yakiwemo mabaki ya dawa na sumu kwa kutumia mashine za *High Performance Liquid Chromatograph* (*HPLC*) na *Near Infrared reflectance spectrophotometer* (*NIRS*), ambapo sampuli 480 za vyakula vya kuku vilihakikiwa ubora wake.

(iv) Kuimarisha Kituo kipya cha Udhibiti wa Mbung'o na Ndorobo kilichopo Kigoma.

(v) Kukarabati maabara ya kwanza *(Insectory block I)* kwa asilimia 80 na kukamilisha ujenzi wa jengo la kuhifadhi na kutayarisha damu kwa ajili ya mbung'o katika Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo na Nagana Tanga. Aidha, aina na idadi ya mbung'o waliofugwa katika kituo hicho ilikuwa *Glossina pallidipes* (3,800), *G. austeni* (23,350), *G. brevipalpis* (150) na *G. morsitans centralis* (3,700).

(vi) Kufanya tathmini katika Mikoa ya Iringa na Singida kuhusu matumizi ya chanjo stahimilivu joto (*I-2*) ya kuzuia mdondo. Matokeo ya awali ya tathmini hiyo yameonesha kuongezeka kwa kuku wa asili katika maeneo husika.

(vii) Kufanya tathmini katika Wilaya za Kibaha, Kilosa na Handeni kuhusu matumizi ya chanjo ya kuzuia Ndigana kali. Matokeo yameonesha manufaa makubwa kwa wafugaji kutokana na kupungua kwa idadi ya vifo vya ng'ombe vinavyosababishwa na ugonjwa huo.

Katika mwaka 2009/2010, Maabara Kuu itazalisha na kusambaza katika Halmashauri, chanjo za kuzuia magonjwa mbalimbali zikiwa ni pamoja na dozi 100,000,000 za Mdondo, 500,000 za Kimeta, 400,000 za Chambavu na 25,000 za Ugonjwa wa Kutupa Mimba. Pia, Maabara itafanya kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya uchunguzi, utambuzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali;
(ii) Kuendeleza ufugaji wa aina mbalimbali za mbung'o kwa ajili ya utafiti;

(iii) Kuchunguza na kuhakiki ubora wa mazao ya mifugo na vyakula vya mifugo pamoja na mabaki ya dawa na sumu;
(iv) Kupima nguvu za dawa za kuogesha mifugo *(dip wash);*
(v) Kuendelea na taratibu za ujenzi wa kituo cha kutengeneza chanjo za mifugo Kibaha; na
(vi) Kukarabati na kuimarisha Maabara Kuu ya Mifugo, Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Ndorobo, Tanga na kuimarisha kituo cha Udhibiti wa Mbung'o na Ndorobo Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki - Nyegezi ni kufanya uchunguzi wa sampuli za samaki, maji na matope ili kubaini vimelea haribifu na masalia ya kemikali yatokanayo na mbolea za mazao, uchafu wa viwandani na majitaka ya majumbani. Katika mwaka 2008/2009, Maabara imeimarishwa kwa kupatiwa wataalam 6 na vitendea kazi. Aidha, wataalam 4 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu ubora wa viwango na udhibiti wa maabara. Jumla ya sampuli 174 za minofu ya samaki kutoka viwandani, 101 za maji na 44 za udongo zilifanyiwa uchunguzi ili kuhakiki ubora na usalama wake.

Katika mwaka 2009/2010, Maabara itafanya uchunguzi wa sampuli 600 za minofu ya samaki, maji tope, masalia ya madawa ya mimea, *dioxins, polyaromatic hydrocarbons* na madini tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania, iliendelea kuandaa na kusimamia viwango na miongozo kuhusu utoaji huduma za mifugo. Katika mwaka 2008/2009, wakaguzi wa huduma 55 na wasajili wasaidizi 18, waliteuliwa kwa mujibu wa Sheria na kupewa mafunzo juu ya kanuni za ukaguzi. Aidha, Baraza lilisajili madaktari 22 wakiwemo 4 wa kigeni, ambao walipata usajili wa muda na kufanya madaktari waliosajiliwa nchini kufikia 593. Pia, wataalamu wasaidizi 100 wenye stashahada na astashahada waliandikishwa na kuorodheshwa na kufikia 1,006. Vilevile vituo 13 vya kutolea huduma vilisajiliwa na kufanya jumla ya vituo kuwa 304. Aidha, orodha za usajili za mwaka 2008 za madaktari wa mifugo na wataalam wasaidizi zilichapishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Jumla ya nakala 1,100 za miongozo juu ya wataalam waliosajiliwa na kanuni za ukaguzi chini ya Sheria ya Veterinari Na. 16, 2003 zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza liliandaa na kutoa mada kuhusu kanuni za maadili ya taaluma ya veterinari katika vyuo 6 vya Mpwapwa, Morogoro, Tengeru, Madaba, Temeke na Buhuri kwa wanafunzi 394. Aidha, Halmashauri 27, mashamba 7 na vyuo 7 vya mifugo, vilihamasishwa kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za mifugo. Vilevile jumla ya vituo vya kutolea huduma 15 vilikaguliwa katika Mikoa ya Dar-es-Salaam na Pwani, kwa kushirikiana na wakaguzi wa Halmashauri na Mamlaka ya Chakula na Dawa. Pia ukaguzi na uhamasishaji kuhusu viwango vya mitaala ya kufundisha wataalam wa afya ya mifugo ulifanyika katika vyuo 3 vya Kilacha, Simanjiro na Igabiro na Taasisi 2 za VETA na NACTE.

Katika mwaka 2009/2010, ukaguzi wa maadili ya watoa huduma utaboreshwa katika ngazi za Halmashauri kwa kuteua wakaguzi wapya 25 na kuhamasisha wataalam wa sekta binafsi kutoka Halmashauri 60 kushiriki katika kutoa huduma bora katika maeneo yenye mifugo. Aidha, Baraza litasajili madaktari wa mifugo 20, kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi 300 na vituo vya kutolea huduma 30 na kuhakiki mitaala na ubora wa wahitimu katika ngazi ya astashahada, stashahada na shahada ili waweze kutoa huduma kulingana na maadili ya taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 jumla ya wanachuo 1,185 wanaendelea na mafunzo ya Stashahada na Astashahada katika vyuo 6 vya mifugo vya Buhuri, Madaba, Morogoro, Mpwapwa, Temeke na Tengeru. Kati ya hao wanaume ni 854 na wanawake ni 331. Aidha, kati ya hao 608 wamemaliza mafunzo yao mwezi Juni, 2009 katika Stashahada za Afya ya Mifugo (364), Uzalishaji wa Mifugo (227) na Uendelezaji Nyanda za Malisho na Udhibiti wa Ndorobo (17) na kupangiwa vituo vya kazi katika Halmashauri zilizoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliandika mihtasari ya Stashahada za Afya ya Mifugo, Mafundi Sanifu Maabara ya Mifugo na Uzalishaji wa Mifugo pamoja na ya Astashahada ya Afya ya Mifugo na Uzalishaji kwa kuiweka katika mfumo wa moduli ili iweze kuwasilishwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Aidha, vitabu vya "*Animal Breeding & Artificial Insemination*" na "*Animal Products & By products*" vilichapishwa na nakala 1,000 kusambazwa katika Maktaba za Vyuo vya Mafunzo vya Mifugo.

Katika mwaka 2009/2010 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuweka katika mfumo wa moduli muhtasari wa Stashahada ya Utunzaji wa Nyanda za Malisho na Udhibiti wa Ndorobo kulingana na taratibu za NACTE;
(ii) Kupanua uwezo wa vyuo vya mifugo kwa kudahili wanafunzi 1,200 kwa mwaka wakiwemo 400 wa astashahada na 800 wa stashahada na kushawishi sekta binafsi kuanzisha vyuo vya mafunzo ya Mifugo ili viweze kudahili wanafunzi zaidi;
(iii) Kuboresha majengo, vitengo vya uzalishaji kibiashara, miundombinu na vifaa vya kufundishia katika vyuo 6 vya mafunzo ya mifugo ili kuweka mazingira bora ya kutoa mafunzo;
(iv) Kuendesha tathmini za mafunzo ili kubaini mahitaji mapya ya mafunzo katika soko la ajira;
(v) Kufanya ukaguzi wa vyuo mara 3 na kuratibu shughuli za mitihani;
(vi) Kupeleka wanafunzi 572 na walimu 24 katika taasisi za elimu ya juu, utafiti na mashamba ili kufanya mafunzo kwa vitendo; na
(vii) Kuwaendeleza waalimu 6 katika ngazi ya uzamili na 2 katika ngazi ya uzamivu ili kuwajengea uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya taaluma za uvuvi kwa watumishi 42, wakiwemo 5 katika ngazi ya Stashahada, 1 ngazi ya Astashahada, 7 Shahada ya Uzamivu

(PhD); 10 Shahada ya Uzamili (MSc); 13 Shahada ya kwanza (BSc) na 73 mafunzo ya muda mfupi. Pia, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya Uvuvi kwa wanafunzi 232 katika Vyuo vya Mbegani (164) na Nyegezi (68) ngazi ya Astashahada.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada kwa wanachuo 120 na Stashahada 120 katika Vyuo vya Uvuvi vya Nyegezi na Mbegani. Aidha, Wizara itagharimia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 30 na muda mrefu watumishi 5 ngazi ya Stashahada, 13 Shahada ya kwanza, 15 Shahada ya Uzamili na 7 Shahada ya Uzamivu. Pia, Wizara itagharimia ukarabati wa majengo na kununua vifaa vya kufundishia kwa ajili ya kuimarisha Vyuo vya Nyegezi na Mbegani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, uzalishaji wa maziwa ulifikia lita bilioni 1.6 sawa na ongezeko la asilimia 6.7 ikilinganishwa na lita bilioni 1.5 za mwaka 2007/2008. Ongezeko hili limetokana na kuongeza ukusanyaji wa maziwa. Kati ya kiasi hicho, lita milioni 600 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita bilioni 1.0 ng'ombe wa asili. Aidha, unywaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 41 mwaka 2007/2008 hadi lita 42 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la mahitaji ya mitamba nchini, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba yake kwa kununua ng'ombe wazazi 100. Pia, mashamba haya yameimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi. Vilevile miundombinu ikiwemo majengo, barabara na uzio katika mashamba ya Kitulo na Sao Hill vimekarabatiwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, ilisambaza jumla ya mitamba 10,095 kwa wafugaji wadogo na mbuzi wa maziwa 2,163.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika maziwa. Kiasi cha maziwa kinachosindikwa kwa siku (*operating capacity*), kimeongezeka kutoka lita 65,930 mwaka 2007/2008 hadi lita 88,940 mwaka 2008/2009, sawa na ongezeko la asilimia 34.9. Ongezeko hilo limetokana na kuimarishwa kwa usindikaji katika viwanda vya *New Musoma Dairy* na *Mara Milk (*Mara*), Tanga Fresh (Tanga), ASAS (Iringa),* pamoja na kuanzishwa kwa viwanda vidogo vya *Gondi Foods* (Dodoma), Emuhuru (Kilimanjaro), Terat, Orkesmet na Naberera (Manyara) na *Longido Women Dairy Cooperative* (Arusha).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuimarisha ukusanyaji ili kuongeza usindikaji wa maziwa kufikia lita 95,000 au zaidi kwa siku. Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kuhamasisha utekelezaji wa mpango wa kuendeleza zao la maziwa kwa kuandaa na kushiriki katika promosheni ya Wiki ya Maziwa, inayoadhimishwa Kitaifa mwanzoni mwa Mwezi Juni kila mwaka.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Maziwa, itaendelea kuandaa na kuratibu maadhimisho ya Wiki ya Unywaji wa Maziwa, ambayo itafanyika katika Mkoa wa Lindi. Maadhimisho hayo yatahusisha kongamano la wadau wa maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mifugo na kuongeza tija, mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji. Kwa sasa teknolojia hii imeanza kukubalika na wafugaji wa asili na hivyo kuongeza matumizi ya mbegu bora. Ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa mbegu bora na kuwa karibu na wafugaji, Wizara imeanzisha vituo viwili vipya vya uhimilishaji katika Kanda ya Kati (Dodoma) na Kanda ya Mashariki (Kibaha), kuweka mitambo ya kuzalisha hewa baridi ya naitrojeni kwenye kila kituo. Aidha, jumla ya madume bora 12 yamenunuliwa kutoka Afrika ya Kusini (10) na Kenya (2). Katika kipindi hicho uzalishaji wa mbegu bora za uhimilishaji kutoka NAIC umeongezeka kutoka dozi 69,085 mwaka 2007/2008 na kufikia 74,200 mwaka 2008/2009, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Pia, idadi ya ng'ombe waliohimilishwa imeongezeka kwa asilimia 24.7 kutoka ng'ombe 55,253 mwaka 2007/2008 na kufikia 68,900 mwaka 2008/2009. Kiasi cha lita 18,160 za hewa baridi ya naitrojeni zilizalishwa. Vilevile Wizara imeboresha mtaala wa mafunzo ya uhimilishaji na kutoa mafunzo kwa wataalam 307 ikilinganishwa na wataalam 137 wa mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 124.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaimarisha vituo vya uhimilishaji vya Kibaha, Mwanza na Dodoma, kwa kuvipatia vitendea kazi na kujenga vituo viwili vya Mbeya na Lindi kwa kuweka mitambo ya kutengenezea hewa baridi ya naitrogeni. Pia, Wizara itaimarisha kituo cha uhimilishaji cha NAIC kwa kukinunulia madume bora 15 yaliyohakikiwa kijenetiki kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora, ambapo dozi 200,000 za mbegu bora zitazalishwa na ng'ombe 83,000 watahimilishwa. Aidha, Wizara itafanya utafiti wa kuanzisha kituo kipya cha uzalishaji wa mbegu za mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu sekta ndogo ya nyama ikihusisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya tani 422,230 za nyama zimezalishwa, ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.8 ya tani 410,706 zilizozalishwa mwaka 2007/2008. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa idadi ya mifugo na mahitaji ya nyama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, imeendelea kuhamasisha mfumo wa unenepeshaji wa mifugo, kwa lengo la kuboresha zao la nyama. Mfumo huo umeendelea kutekelezwa katika ranchi za sekta binafsi, za Taifa na wafugaji wadogo katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Morogoro, Shinyanga na Dar es Salaam, ambapo jumla ya ng'ombe 62,000 walinenepeshwa, ikilinganishwa na ng'ombe 29,600 walionenepeshwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuku wa asili hufugwa na takriban kila kaya nchini hususan vijijini na ikiboreshwa itachangia kwa kiasi kikubwa kuboresha lishe, pato la kaya na Taifa kwa ujumla. Idadi ya kuku wa asili imeongezeka kutoka kuku milioni 33 mwaka 2007/2008 na kufikia milioni 34 mwaka 2008/2009. Ongezeko hili limetokana na mafanikio yaliyopatikana katika utumiaji wa chanjo ya mdondo ya *I-2* ambayo imepunguza vifo vya kuku kutoka asilimia 90 hadi asilimia 4 pale ambapo chanjo hii imetumika. Kwa upande wa kuku wa biashara, jumla ya vifaranga milioni 34.8 vya kuku wa kisasa vilizalishwa ikilinganishwa na vifaranga milioni 32.6 vilivyozalishwa mwaka

2007/2008. Aidha, uzalishaji wa mayai nchini uliongezeka kutoka mayai bilioni 2.69 mwaka 2007/2008 hadi mayai bilioni 2.81.

Katika mwaka wa 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa kuku, mayai na vifaranga, ambapo mayai bilioni 3.0 na vifaranga milioni 36.2 vya kibiashara vinatarajiwa kuzalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umefikia tani 36,000, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8 kulinganisha na mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2009/2010, Wizara inaendelea kuimarisha mashamba yake kwa kuyapatia nguruwe bora ili wazalishe mbegu bora.

Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kupitia Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), wameainisha na kutenga maeneo kwa wafugaji na kuhakikisha yanaendelezwa kwa ajili ya ufugaji. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya hekta 460,833 zimepimwa katika vijiji 28 vya Wilaya tano (5) za Liwale, Lindi, Kilwa, Kilosa na Nachingwea. Hadi sasa jumla ya hekta 1,391,109.41 zimetengwa kwa ajili ya ufugaji katika vijiji 240 kwenye Halmashauri za Wilaya 31 katika mikoa 13 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya mbegu za malisho ya Vikuge, Langwira, Mabuki, Buhuri, Kizota, Kongwa, Mivumoni na Sao Hill ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mbegu bora za malisho kwa wadau. Jumla ya tani 43 zimezalishwa kutoka mashamba ya serikali, ikilinganishwa na tani 42.7 zilizozalishwa mwaka 2007/2008. Vilevile marobota 929,680 ya hei yalizalishwa na kati ya hayo 509,680 yalizalishwa na sekta binafsi na 420,000 kutoka mashamba ya serikali.

Katika mwaka 2009/2010, mashamba hayo yatazalisha tani 50 za mbegu za malisho. Aidha, marobota 550,000 ya hei yatazalishwa na sekta binafsi na 450,000 yatazalishwa na mashamba ya serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuratibu usindikaji na ubora wa vyakula vya mifugo, ambao hufanywa na sekta binafsi. Kwa sasa vipo viwanda 80 vya kutengeneza vyakula vya mifugo katika Mikoa ya Pwani (6), Dar es Salaam (33), Arusha (15), Kilimanjaro (7), Mbeya (8) na Mwanza (11), ikilinganishwa na viwanda 74 vilivyokuwepo mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2008/2009, tani 801,727 za aina mbalimbali ya vyakula vya mifugo zilizalishwa, ikilinganishwa na tani 717,231 zilizozalishwa mwaka 2007/2008.

Aidha, wataalam 25 kutoka Halmashauri za Mvomero, Kibaha, Pangani, Mkinga, Morogoro, Kilosa, Kongwa, Korogwe, Mkuranga, Ulanga, Kilindi, Handeni, Bagamoyo, Kilombero, Mpwapwa, Morogoro (V), Kisarawe, Lushoto na Chamwino, walipewa mafunzo kuhusu ubora wa vyakula vya mifugo. Pia, mafunzo ya utengenezaji wa vyakula vya mifugo yalitolewa kwa wataalam wakufunzi 43 kutoka katika Halmashauri za Mkinga, Pangani, Lushoto, Korogwe (M), Korogwe, Handeni, Kilindi, Rufiji, Mkuranga,

Kibaha, Bagamoyo, Morogoro, Manispaa ya Morogoro, Mvomero, Kilosa, Ulanga, Kilombero, Bahi, Kongwa, Mpwapwa, Chamwino na Kondoa.

Katika mwaka 2009/2010, jumla ya tani 830,700 za vyakula vya mifugo vilivyosindikwa zitazalishwa. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa wakaguzi 80 wa vyakula vya mifugo. Pia, wataalam wakufunzi 40 wa Halmashauri watapewa mafunzo juu ya uzalishaji, usindikaji na matumizi ya miti malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji ya kutosha ni muhimu kwa uzalishaji endelevu wa mifugo na kwa kiwango kikubwa, uhaba wa maji umekuwa ni moja ya vyanzo vya migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine. Katika mwaka 2008/2009, Wizara imeratibu ujenzi wa malambo 68 katika Halmashauri 34 yaliyojengwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs).* Aidha, kupitia Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (PADEP), malambo 64 yamechimbwa katika wilaya 12. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, imebaini vyanzo 46 vya maji vitakavyoendelezwa kwa matumizi ya mifugo katika Mikoa 6 ya Ruvuma, Mwanza, Kagera, Lindi, Rukwa na Shinyanga.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri nchini, itaendelea kuhamasisha na kutoa miongozo ya kujenga miundombinu ya maji kwa mifugo. Aidha, Wizara itaendelea kukagua miundombinu ya maji katika Mikoa ya Singida, Manyara, Tabora, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya na Lindi. Pia, Wizara itashirikiana na Halmashauri kubaini maeneo yenye fursa za vyanzo vya maji katika mikoa 8, yenye sehemu kame ya Singida, Manyara, Tabora, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuwaandaa wafugaji kukabiliana na majanga, Wizara imeanzisha dawati la tahadhari ya majanga yanayosababisha uhaba wa malisho (*Livestock Early Warning System- LEWS*) na kutoa mafunzo kuhusu mfumo huo kwa wataalam wa mifugo 19 wa Wilaya za Nachingwea, Ruangwa, Kilwa, Lindi Vijijini, Liwale na Rufiji.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuimarisha mfumo wa LEWS katika Wilaya za Nachingwea, Ruangwa, Kilwa, Lindi Vijijini, Liwale na Rufiji na kutoa mafunzo kwa wakusanyaji wa takwimu 150.

(ii) Kukamilisha kuandaa miongozo ya matumizi endelevu ya nyanda za malisho wakati wa kiangazi na kusambaza katika Halmashauri zote nchini.

(iii) Kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa wataalam wa ugani 40 kuhusu mipango endelevu ya utunzaji na utumiaji wa rasilimali za nyanda za malisho.

(iv) Kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ya Mikoa ya Rukwa, Lindi, Pwani, Mbeya, Morogoro na Tanga kuhusu kutenga na kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na kuelimisha jamii ya wafugaji juu ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeendelea kuathiriwa kibiashara kwa kuwepo kwa magonjwa ya mifugo na hasa ya milipuko. Katika mwaka 2008/2009, Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), chini ya mpango wa *roll back plan,* uliendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Iringa, Singida, Tabora na Kigoma. Jumla ya dozi milioni 3.2 za chanjo ya CBPP zimenunuliwa na ng'ombe 2,388,098 wamechanjwa.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itanunua dozi milioni 4.2 kwa ajili ya kukamilisha chanjo kwenye Mikoa ya Singida, Tabora na Kigoma na kuanza chanjo kwenye Mikoa ya Shinyanga na Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ugonjwa wa Miguu na Midomo (*FMD*), umeendelea kusababisha nchi yetu kushindwa kupenya katika masoko ya mifugo na mazao yake ya kimataifa na hasa soko la Ulaya. Katika mwaka 2008/2009, Mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo umekamilika. Jumla ya matukio 16 ya ugonjwa huo, yaliripotiwa katika Halmashauri 12 ambapo mifugo 510 iliugua.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo kwa kufanya uchunguzi kwa ajili ya kupata hali ya ugonjwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo (*Peste des Petits Ruminants* - PPR), uliingia nchini kwa mara ya kwanza ukitokea nchi jirani. Ugonjwa huu uliathiri Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara, ambako jumla ya mbuzi 536,382 na kondoo 326,115 waliugua na kati ya hao mbuzi 96,549 na kondoo 58,701 walikufa. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la VETAID na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilinunua na kusambaza jumla ya dozi za chanjo 940,000. Jumla ya mbuzi na kondoo 658,131 walichanjwa katika Wilaya za Longido, Monduli, Ngorongoro, Siha na Simanjiro na uchanjaji unaendelea.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), itachanja jumla ya mbuzi na kondoo 5,744,334 katika wilaya zote za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga na katika baadhi ya wilaya zinazopakana na mikoa hiyo za Babati, Bariadi, Hanang, Iramba, Kondoa, Meatu, Serengeti na Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kudhibiti kupe na magonjwa wanayoeneza kwa kuhimiza ujenzi wa majosho na uogeshaji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri kupitia mipango ya DADPs, ilipanga kujenga majosho 46 na kukarabati majosho 79. Hadi sasa, jumla ya majosho 42 yamejengwa na

39 yamekarabatiwa. Aidha, kutokana na gharama kubwa za madawa ya kuogesha mifugo na nia ya Serikali kutokomeza magonjwa hayo, Serikali imetoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ruzuku ya madawa ya kuogesha mifugo nchini. Kampuni 9 zimesambaza lita 649,552 za dawa hizo, ambapo wafugaji wanazinunua kwa asilimia 60 ya gharama na Serikali huchangia asilimia 40 kama ruzuku. Pia, Sekta binafsi imeendelea kutoa chanjo ya Ndigana Kali ambapo ng'ombe 70,548 wamechanjwa katika mikoa 12, ikilinganishwa na ng'ombe 76,233 waliochanjwa mwaka 2007/2008.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, itaendelea kuhamasisha uchanjaji dhidi ya Ugonjwa wa Ndigana kali ili kuogesha idadi ya ngo'mbe kwa kupunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo. Aidha, Serikali itatoa ruzuku ya chanjo ya Ndigana Kali dozi 132,000, ambayo itatumika katika maeneo ya ufugaji wa asili unaotumia uhimilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kutokomeza mbung'o na kudhibiti Ugonjwa wa Nagana kwa kutoa mafunzo kwa wafugaji 229 waliohamia katika vijiji 21 vya Wilaya za Lindi Vijijini na Kilwa toka Ihefu na Morogoro. Pia, mafunzo hayo yalitolewa kwa wataalam wa mifugo 16 wa Wilaya za Lindi Vijijini, 5 Kilwa na watendaji wa 7 wa tarafa na vijiji kutoka wilaya hizo. Vilevile, uchunguzi wa mtawanyiko wa mbung'o umefanyika katika Wilaya za Urambo, Uyui, Sikonge, Nzega na Igunga na kuchora ramani kwa Mkoa wa Tabora.

Katika mwaka 2009/2010, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa mifugo 60 juu ya mbinu shirikishi za kutokomeza mbung'o na kudhibiti ugonjwa wa Nagana katika Wilaya za Rufiji, Kisarawe na Bagamoyo Mkoani Pwani.

(ii) Kufuatilia wafugaji walioanza kutumia teknolojia ya vyambo katika Mikoa ya Lindi, Arusha, Tabora na Kigoma.

(iii) Kufuatilia mtawanyiko na aina za mbung'o katika Mkoa wa Kigoma na Singida.

(iv) Kuanza kutekeleza Mpango wa PATTEC kwa kukusanya takwimu za awali *(baseline data)* katika eneo la Bonde la Mto Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu (*Zoonoses)*; katika mwaka 2008/2009, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Mkakati wa miaka 5 wa kudhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa unaofadhiliwa na Taasisi ya *Bill na Melinda Gates.* Tanzania imetengewa dola za Kimarekani milioni 3.9 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara na kuratibiwa na Shirika la Afya Duniani (*WHO*). Vilevile dozi 50,000 za chanjo ya Kichaa cha Mbwa zimenunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri 30 za mikoa 17, ambapo jumla ya mbwa 111,601 walichanjwa.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kudhibiti ugonjwa wa kichaa cha mbwa, kwa kununua na kusambaza dozi 400,000 za chanjo na kutekeleza mradi wa kudhibiti ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, uchanjaji dhidi ya Ugonjwa wa Bonde la Ufa uliendelea kufanyika katika maeneo yaliyokuwa kwenye hatari ya kuambukizwa na ugonjwa, ambapo ng'ombe 116,880, mbuzi 17,797 na kondoo 5,299 walichanjwa katika Halmashauri za Mbarali, Kongwa, Mpwapwa, Kondoa na katika Ranchi za NARCO. Aidha, elimu kwa umma kuhusu athari za ugonjwa huo iliendelea kutolewa.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itadhibiti Ugonjwa wa Bonde la Ufa (RVF), kwa kununua na kusambaza chanjo dozi 500,000 katika Halmashauri pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athari za ugonjwa huo na hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kupitia Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo (VICs) vya Mpwapwa, Temeke, Arusha, Mwanza na Tabora, ilichunguza ng'ombe 1,500 na mbuzi 340 dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba, ambapo ng'ombe 73 walikuwa wameathirika na walichinjwa.

Katika mwaka 2009/2010, ng'ombe 5,000 watachunguzwa dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba katika kanda zote na Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke itazalisha dozi 25,000 za chanjo za majaribio dhidi ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa Ugonjwa wa Kimeta *(Anthrax)*, uliendelea kufanywa na Halmashauri kwa kushirikiana na sekta binafsi, ambapo ng'ombe 34,482, mbuzi 8,454 na kondoo 2,740 walichanjwa katika Halmashauri za Mbarali, Mpwapwa, Nzega na Bahi, zilizopatwa na ugonjwa huo. Aidha, dozi 500,000 za chanjo ya Kimeta zimezalishwa katika Maabara Kuu ya Mifugo.

Katika mwaka 2009/2010, dozi 500,000 za chanjo ya Kimeta zitazalishwa katika Maabara Kuu ya Mifugo na kusambazwa katika wilaya mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF)* na Mradi wa Umoja Wa Mataifa wa *Joint Project* (*J.P 6.2*), imeendelea kuelimisha na kuhamasisha wataalam na jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari kuhusu athari za Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege. Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Tahadhari ya Mafua Makali ya Ndege kwa lengo la kuzuia na kudhibiti ugonjwa huu endapo utaingia nchini. Sampuli 2,300 za kuku na ndege pori zimechunguzwa na matokeo yamethibitisha kutokuwepo kwa ugonjwa huo. Aidha, Maabara Kuu ya Mifugo –Temeke, imejengewa uwezo wa kutambua viashiria vya ugonjwa huo. Vilevile elimu kwa umma wakiwemo madiwani, wataalam na waandishi wa habari imetolewa kwa njia ya mabango na vipeperushi 5,000, vitabu 1,000 na vijarida 5,000.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na *UNICEF* na wadau wengine, itaendelea kutekeleza Mkakati wa Tahadhari ya Mafua Makali ya Ndege kwa

kutoa elimu na hamasa kwa wadau. Aidha, Wizara itapitia na kuboresha Mkakati huo na kuimarisha uratibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ugonjwa wa Mafua ya Nguruwe, husababisha homa kali na vifo vichache vya nguruwe na uligunduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1918. Ugonjwa huu huathiri nguruwe wakati wote wa mwaka, lakini mlipuko hutokea zaidi wakati wa kipupwe na baridi. Hakuna ushahidi kwamba, mlipuko unaoendelea sasa ambao ulianza tarehe 22 Aprili, 2009, umesababishwa na nguruwe, aidha, hakuna nguruwe wagonjwa. Mlipuko huu umekwishaua watu 145 nchini Mexico na kusambaa katika nchi 76 zikiwemo nchi 2 za Afrika Misri na Morocco. Mlipuko huu unatofautiana kwa makali, nchini Mexico umeua watu 108 wakati nchini Marekani ni watu 17,855 wameambukizwa na watu 45 wamekufa.

Katika koo la nguruwe *(respiratory tract*), virusi vya influenza vya nguruwe, binadamu na ndege vinaweza kukaa (*bind*). Kutokana na uwezo wa virusi hivyo vitatu kuweza kuwa kwenye nguruwe kwa wakati mmoja, nguruwe ameitwa kama chombo cha kuchanganya (*mixing vessels*) katika kupatikana kirusi *(virus)* kipya cha influenza, chenye vinasaba vya influenza ya binadamu, nguruwe na ndege wakati virusi hivi vinabadilishana vinasaba *(genetic re-assortment in pigs).* Kwa tabia hii, kumekuwa na milipuko mingi ya mafua ya nguruwe yenye kutofautiana ukali. Kwa wakati huu, kuna jamii 4 za virusi vya mafua ya nguruwe ambavyo ni H1N1, H1N2, H3N2 na H3N1. Kirusi cha aina ya influenza A-H1N1, ndicho chenye madhara na ndicho kinachozunguka hivi sasa.

Kwa kawaida kirusi hiki H1N1, kilikuwa hakimuathiri mwanadamu na ni mara chache watu waliokuwa wanafanya kazi katika mashamba ya nguruwe, waliripotiwa kupata ugonjwa huu. Tofauti ya Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege na Mafua ya Nguruwe ni kwamba, Ugonjwa huu huenea kutoka kwa binadamu aliyeambukizwa kwenda kwa binadamu mwingine kwa kupiga chafya, kukohoa na kugusa makohozi (njia ya hewa). Virusi vya Mafua ya Nguruwe, havisambazwi kwa kula nyama ya nguruwe iliyopikwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili za ugonjwa kwa nguruwe ni pamoja na:-

(i) Kukohoa, kupiga chafya, kutoka makamasi, homa, kupumua kwa shida, kupungua ulaji wa chakula na uchovu (*lethargy*). Kwa wakati mwingine kutupa mimba;
(ii) Nguruwe wanapata ugonjwa (*morbidity*) hadi kufikia asilimia 100 lakini vifo ni asilimia 1-4; na
(iii) Dalili za ugonjwa na kutoa virusi mwilini (*sheding*) zinaweza kutokea saa 24 baada ya nguruwe kuambukizwa.

Athari za kiuchumi kwa mfugaji ni kuwa, nguruwe waliombukizwa hawakui haraka (*retarded weight gain*), kwa hiyo, inabidi kulishwa kwa siku nyingi mpaka kufikia uzito wa kupelekwa sokoni.

Dalili za ugonjwa huu kwa binadamu ni zile zile za mafua ya kawaida, ambazo ni homa, kukohoa, kutokwa na makamasi, maumivu ya koo, kukereketwa na koo na maumivu ya kichwa na mwili.

Jamii ya kirusi kinachozunguka sasa kinatibika zaidi kwa dawa ya Oseltamivir (Tamiflu) na Zanamivir (Relenza). Hakuna chanjo ya kuzuia mlipuko wa hivi sasa, bali watu wanaweza kutibiwa kwa dawa zilizotajwa hapo juu.

Tahadhali za kuchukua kwa binadamu:-

(i) Kunawa mikono kwa sabuni mara kwa mara.
(ii) Kuepuka makundi yasiyo ya lazima.
(iii) Kutumia kitambaa kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa na kupiga chafya.
(iv) Kusitisha kwa muda uingizaji wa nguruwe na mazao yake.
(v) Usafi wa mabanda ya nguruwe.
(vi) Kuepuka kutembelea mabanda ya nguruwe.
(vii) Kuepuka safari za nje zisizo za lazima.
(viii) Kutoa taarifa za ugonjwa wowote unaoathiri nguruwe.
(ix) Kwenda hospitali mara unapohisi dalili za mafua.
(x) Kutoa na kusambaza taarifa sahihi zinazoweza kusaidia katika kuepuka mlipuko.

Tahadhali kwa mifugo:-

(i) Kudhibiti usafirishaji wa nguruwe na mazao yake.
(ii) Usafi wa mazingira ya ufugaji (*Biosecurity*).

Hatua zilizochukuliwa:-

(i) Kuwajulisha watalaam waliopo katika Halmashauri, Mikoa na VIC kuwa katika hali ya tahadhali wanapohisi dalili za Mafua ya Nguruwe watoe taarifa VIC na CVL ili wafuatilie.
(ii) Kuwa makini zaidi na mazao ya nguruwe yanayoingizwa nchini yasitoke katika nchi zenye ugonjwa.
(iii) Tunaendelea kufuatilia mwenendo wa ugonjwa kutoka Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE). Hadi sasa haijagundulika au kuthibitika kuwa nguruwe wanahusika katika mlipuko wa ugonjwa unaoendelea kwa binadamu; hivyo, jina la ugonjwa sasa linalotambulika kimataifa ni *Influenza A (HINI)* badala ya *Swine Influenza*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha orodha ya dawa muhimu za mifugo ili itumike na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), pamoja na TRA katika kudhibiti usajili na uingizaji wa dawa za mifugo nchini. Aidha, ukaguzi wa maduka 43 yanayouza pembejeo za mifugo ulifanyika katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro na Tanga ili kudhibiti ubora ambapo pembejeo bandia, hususan tani 2.5 za

madini ya ziada (*mineral supplements*) ziligundulika katika baadhi ya maduka na hatua za kisheria kuchukuliwa. Pia, ukaguzi ulifanyika kwa mifumo baridi ya kuhifadhi chanjo za magonjwa ya mifugo katika maduka 43 ya pembejeo za mifugo katika mikoa hiyo na wenye maduka kushauriwa ipasavyo.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na TFDA na TBS itaendelea kuandaa viwango vya pembejeo za mifugo pamoja na kusimamia ubora, matumizi na hifadhi sahihi ya pembejeo hizo na kutoa elimu kwa wakaguzi 200. Pia, ukaguzi wa maduka ya pembejeo za mifugo utafanyika kati mikoa ya kanda za Kati, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, ukaguzi wa machinjio za Mikoa ya Morogoro, Mara, Singida, Iringa, Mwanza, Arusha na Dar es Salaam ulifanyika na Halmashauri husika zilishauriwa kurekebisha kasoro zilizobainishwa, ikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu na uchafu wa mazingira.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea na ukaguzi wa machinjio zote nchini na kutoa mafunzo kwa wakaguzi 200 wa nyama na ngozi kwenye Halmashauri. Aidha, vituo vya ukaguzi wa mifugo tisa vya Horohoro (Tanga), Kasumulo na Tunduma (Mbeya), KIA (Kilimanjaro), Kibaha (Pwani), Kirumi na Sirari (Mara), Mutukula (Kagera) na Namanga (Arusha) na vituo 3 vya karantini vya Kwala na Ruvu (Pwani) na Themi (Arusha), vitaimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi na mafunzo kwa wakaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (*FAO*), chini ya mpango wa kudhibiti majanga yaletwayo na magonjwa ya mlipuko ya wanyama, imeanzisha mfumo wa utoaji taarifa kwa kutumia teknolojia ya *Digital Pen.* Ili kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa za mienendo ya magonjwa, Halmashauri za Wilaya za Misenyi, Monduli, Ngorongoro, Same na Tarime, zimeingizwa katika mfumo huo. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo huo kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, imeendelea kuratibu biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje. Idadi ya mifugo iliyouzwa minadani imeongezeka kutoka ng'ombe 779,280, mbuzi 616,693 na kondoo 112,995, wenye thamani ya shilingi bilioni 216.1 katika mwaka 2007/2008 hadi kufikia ng'ombe 781,230, mbuzi 623,732 na kondoo 114,564 wenye thamani ya shilingi bilioni 319.2 mwaka 2008/2009. Ongezeko hilo la idadi ya mifugo iliyouzwa, linatokana na kuimarishwa kwa huduma za minada, mwamko wa wafugaji kuuza mifugo yao kupitia minada na kuongezeka kwa bei ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, jumla ya ng'ombe 3,264 na mbuzi na kondoo 1,834 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.1 wameuzwa katika nchi za Comoro, Kenya, Burundi na Malawi. Pia, jumla ya tani 139.8 za nyama ya ng'ombe zenye thamani ya shilingi 416,947,750, tani 35.4 za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi 120,204,477 na tani 46.7 za nyama ya mbuzi zenye thamani ya shilingi

117,330,455 ziliuzwa katika nchi za Kuwait, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Misri na Oman.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuhamasisha, kufuatilia na kuratibu uuzaji wa mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu ukusanyaji na uuzaji wa ngozi za mifugo nchini. Jumla ya vipande milioni 1.65 vya ngozi za ng'ombe, milioni 2.99 vya mbuzi na milioni 1.25 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 10.9 vilikusanywa. Kati ya hivyo, vipande vya ngozi za ng'ombe 982,668, mbuzi milioni 2.7 na kondoo 769,936 viliuzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi bilioni 12.8. Mapato kutokana na mazao ya ngozi yameshuka kwa asilimia 40.43, ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 21.5 mwaka 2007/2008 kutokana na mtikisiko wa uchumi uliojitokeza katika kipindi hiki. Kutokana na hali hiyo, ununuzi wa ngozi kutoka kwa wazalishaji umepungua na kusababisha mrundikano kwa wafugaji. Aidha, jumla ya vipande 1,514,350 vya ngozi visivyosindikwa vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.4, vimeshindikana kuuzwa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi nchini, umeendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Halmashauri 55 na Chama cha Wadau wa Ngozi. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya shilingi bilioni 1.8 zilikusanywa na Serikali Kuu kupitia TRA, kutokana na ushuru wa ngozi ghafi nje ya nchi na kufikisha jumla ya shilingi bilioni 8.1 tangu kuanzishwa kwa Mfuko huo. Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo *(Livestock Development Fund*), imeimarisha huduma za ugani kwa kununua na kusambaza pikipiki 55, baiskeli 275, visu vya kuchunia 5,500, visu vya kuwekea mikato 3,300, vinoleo 5,500 na vifaa vya kunyanyulia nyama 110 na gari moja. Aidha, jumla ya wakaguzi 160 wa ngozi wamepatiwa mafunzo ya mwezi mmoja. Pia, wafugaji, wachunaji, wawambaji na wafanyabiashara ya ngozi 1,686 katika Halmashauri 55, wamepatiwa mafunzo juu ya uboreshaji wa zao la ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Halmashauri zitakazoshiriki katika Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi zitaongezeka kutoka 55 hadi 65. Aidha, Wizara itatumia kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kujenga machinjio ndogo 3 katika vyuo vya mafunzo ya mifugo vya Tengeru, Morogoro na Mpwapwa na kujenga banda la kuwamba ngozi na ghala kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wadau wa ngozi ili kuweza kuongeza ubora wa zao la ngozi. Pia, Wizara itatoa mafunzo kwa wagani na wakufunzi wa ngozi 50 na kununua pikipiki 10, baiskeli 50, visu vya kuchunia 6,500, visu vya kawaida 3,200, vinoleo 3,250 na vifaa vya kunyanyulia nyama 130 kwa ajili ya Halmashauri zinazotekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha biashara ya mifugo, Wizara imekamilisha ujenzi wa minada ya Nyamatara na Buhigwe. Aidha, minada ya Meserani, Pugu na Kizota imekarabatiwa. Vilevile Wizara imeendelea kushirikiana na wadau

wengine kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko ya mifugo kutoka minada 29.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, itaongeza minada iliyounganishwa na Mtandao wa *LINKS* kutoka 29 hadi 45. Pia, Wizara itakamilisha Mnada wa Buzirayombo na itajenga mnada wa Kirumi na kukarabati minada 9 ya Igunga, Ipuli, Kizota, Korogwe, Lumecha, Mhunze, Pugu, Themi na Weruweru. Pia, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalam 50 wanaosimamia minada katika kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa mbalimbali za masoko ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kuhimiza utekelezaji wa mfumo wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake. Hereni za kutambua ng'ombe 15,000 katika Mashamba ya NARCO ya Kongwa na Ruvu zimenunuliwa, kuanza kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji *(traceability from farm to fork*). Aidha, Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo ya usajili wafugaji na mifugo yao, pamoja na utambuzi wa ng'ombe kwa kutumia chapa yenye namba ya kitaifa kwa Maafisa mifugo wa Halmashauri 133 na Washauri wa Mifugo wa Mikoa yote 21;

(ii) Kuchapisha madaftari ya usajili/rejesta 2015 ili kusajili wafugaji kwa kuanzia na maeneo yenye migogoro kati ya wafugaji na wakulima ili kudhibiti kuingiza kiholela mifugo katika maeneo hayo, pamoja na maeneo yaliyokithiri wizi wa mifugo;

(iii) Kutambua ng'ombe 38,725 kwa chapa ya moto yenye namba za kitaifa na kusajili wafugaji 585 kwenye daftari katika vijiji 20 kati ya vijiji 74 katika Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi;

(iv) Kununua vifaa muhimu vya kujenga mfumo wa kuhifadhi takwimu za usajili *(computerised national livestock registry database system*) na utambuzi ngazi ya kitaifa; na

(v) Kutambua wafugaji 188 wa mbuzi wa maziwa aina ya Togenburg waliojiunga katika mtandao wa *Togenburg Breeders Association* (TOBRA) Wilayani Babati Mkoa wa Manyara ili wasajiliwe.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kusambaza madaftari 2,015 kwa ajili ya kusajili wafugaji.

(ii) Kufundisha wataalam 133 wa mifugo kutoka Halmashauri kuhusu Mfumo wa Kitaifa wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo.

(iii) Kuratibu na kuwezesha ushiriki wa Siku ya Wanyama Duniani na Wiki ya Wanyama Duniani.

(iv) Kuwezesha Halmashauri kutambua mifugo kwa njia chapa, hususan katika Mikoa ya Arusha, Kagera na Mara.

(v) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi 65 kuhusu ustawi wa wanyama.

(vi) Kuanzisha na kuwezesha Baraza la Ustawi wa Wanyama kufanya vikao vinne kwa mwaka.

(vii) Kuorodhesha na kusajili vyama vya wazalishaji wa koo bora za mifugo.

(viii) Kuanzisha mtandao wa kutunza kumbukumbu za usajili wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Taasisi ya Takwimu ya Taifa *(National Bureau of Statistics*), inashiriki katika zoezi la sensa ya mifugo kwa njia ya sampuli. Ili kuwezesha kufanikisha zoezi hili, Wizara imechangia shilingi milioni 400.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itashiriki kukamilisha sensa ya sampuli na maandalizi ya sensa kamili kwa njia ya kuhesabu mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, iliendelea kutoa huduma za ushauri kwa wafugaji ili kuwawezesha kuongeza ubora wa mifugo na mazao yatokanayo na mifugo hivyo kuongeza tija na mapato. Katika kutimiza azma hiyo, Wizara ilichapisha na kusambaza kwa wadau vipeperushi 150,000, mabango 30,120 na vijitabu 13,200 kuhusu ufugaji bora. Aidha, vipindi 52 vya redio na 12 vya runinga viliandaliwa na kurushwa hewani. Pia, wafugaji 21,312 kutoka Mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Singida na Tanga, walipatiwa mafunzo juu ya ufugaji wa kibiashara kupitia vyuo vya mafunzo ya mifugo, Chuo cha Mafunzo ya Wafugaji - Mabuki na kwa njia ya sinema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu Upangaji Mipango Shirikishi ya Ugani na wafugaji vijijini *(Extension Programme Planning),* kwa wataalam 88 wa ugani kutoka Wilaya 10 za Kanda ya Kusini, 12 za Kanda ya Kaskazini na Wilaya 20 za Kanda ya Ziwa. Aidha, wataalam wakufunzi 10 wa ugani kutoka Kanda ya Magharibi, walipatiwa mafunzo ya kutumia mbinu shirikishi ya Shamba Darasa, kwa lengo la kuwawezesha kuanzisha Mashamba Darasa ya mifugo na kutoa mafunzo kwa wataalam wengine wilayani kwao.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuchapisha na kusambaza vipeperushi 52,000, mabango 30,000 na Vijitabu 13,000 kuhusu ufugaji bora.

(ii) Kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya runinga.
(iii) Kuziwezesha Halmashauri kutoa mafunzo kwa wafugaji 4,000 kuhusu ufugaji bora na wa kibiashara.
(iv) Kutoa mafunzo kwa wataalam wakufunzi 20 wa ugani kutoka Halmashauri za Kanda ya Kati na Kanda ya Kusini kuhusu kutumia mbinu shirikishi ya Shamba Darasa.
(v) Kutoa mafunzo kuhusu Upangaji wa Mipango Shirikishi ya Ugani kwa wataalam wakufunzi wa Ugani katika Wilaya 31 za Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini.
(vi) Kufuatilia na kutoa ushauri rejea wa kitaalam katika Wilaya za Kanda za Kaskazini, Kusini na Kanda ya Ziwa ambazo zimepatiwa mafunzo ya Upangaji wa Mipango Shirikishi ya Ugani.
(vii) Kusambaza kwa wadau nakala 3,000 za Mwongozo wa Kanuni za Ufugaji Bora wa Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, imeendelea kutoa elimu mbalimbali kwa wadau ikiwemo athari za uvuvi haramu, matumizi bora ya rasilimali za uvuvi, utunzaji wa mazingira na mbinu shirikishi za usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Jumla ya vipindi 50 vya radio na 20 vya televisheni vimeandaliwa na kurushwa hewani. Aidha, nakala 1,000 za mabango, vijarida 6,000 na vipeperushi 3,000 kuhusu mbinu bora za hifadhi ya mazao ya uvuvi zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau wa uvuvi. Pia, elimu dhidi ya uvuvi haramu na athari zake ilitolewa kwa wavuvi 444 kutoka Halmashauri za Wilaya za Mafia, Rufiji, Mkinga na Muheza na Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza rasilimali za uvuvi, jumla ya Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) 177 viko katika hatua za mwisho za uundwaji. Aidha, mafunzo ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi yametolewa kwa watalaam wa ugani 68 kutoka Halmashauri za Wilaya za Mkinga, Muheza, Pangani, Bagamoyo, Mafia, Mkuranga, Rufiji, Kilwa, Lindi Vijijini, Mtwara Vijijini na Mji wa Lindi, Manispaa ya Mtwara/ Mikindani na Jiji la Tanga. Pia, viongozi 2,655 wa Halmashauri za Vijiji na Jamii ya wavuvi kwenye Halmashauri za wilaya hizo, walihamasishwa kusimamia uanzishwaji wa BMUs kwenye maeneo yao. Vilevile mafunzo kuhusu uvuvi wa ndoano za kulambaza kwenye maji ya kina kirefu ya Ziwa Nyasa, yalitolewa kwa vikundi vya wavuvi 32 kutoka vijiji 5 katika Wilaya za Mbinga na Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuelimisha wananchi kuhusu uhifadhi wa rasilimali katika maeneo tengefu. Katika mwaka 2008/2009, wavuvi 80, walimu 70 na wanafunzi 120 wa shule za msingi zinazozunguka maeneo tengefu mapya ya Visiwa vya Kendwa, Sinda, Makatube, Nyororo, Shungimbili na Mbarakuni, walipewa mafunzo hayo. Aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wavuvi, wamiliki na wafanyakazi wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi 124 katika Ukanda wa Ziwa Victoria na wavuvi na wafanyabiashara 430 katika Wilaya za Rufiji, Kilwa na Mafia, juu ya usafirishaji, uchakataji na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaandaa na kurusha vipindi 6 vya uvuvi katika runinga na kufanya maonesho ya ufugaji bora wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu shughuli za uvuvi nchini katika maji baridi na maji chumvi. Jumla ya tani 324,821.1 za mazao ya uvuvi yanayokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi bilioni 371.4 yalivunwa katika maeneo mbalimbali ya uvuvi nchini. Kati ya hizo, tani 43,130.2 zilitoka ukanda wa maji chumvi na tani 281,690.9 kutoka maji baridi. Aidha, nguvu ya uvuvi (*fishing effort*), imeongezeka kutoka wavuvi 163,037 waliotumia vyombo vya uvuvi 51,704 mwaka 2007 hadi 170,038 waliotumia vyombo vya uvuvi 52,327 mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008, Wizara iliendelea kuratibu mauzo ya samaki na mazao yake katika soko la nje. Jumla ya tani 51,426.2 za samaki na mazao mbalimbali ya uvuvi na samaki wa mapambo 33,066, vyote vikiwa na thamani ya shilingi bilioni 205.1 viliuzwa nje ya nchi. Kiasi cha shilingi bilioni 6.6 zilikusanywa zikiwa ni ushuru utokanao na mauzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara ilinunua boti 4 na kutoa mafunzo kwa wavuvi ili kuimarisha usimamizi wa uvuvi endelevu katika Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Vilevile Wizara ilifuatilia hali ya uvuvi katika Ziwa Rukwa na Ziwa Kitangiri, Bwawa la Mtera na Bwawa la Nyumba ya Mungu na kubaini kukithiri kwa uvuvi haramu, ambao unasababisha kupungua kwa rasilimali za uvuvi na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa uvuvi endelevu katika Ziwa Tanganyika, unategemewa kuimarika baada ya Programu ya Maendeleo ya Uwiano katika Bonde la Ziwa Tanganyika kuanza rasmi mwezi Novemba, 2008. Programu hii ya miaka mitano, inatekelezwa kwa pamoja na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Tanzania na Zambia, kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 68.4. Hadi sasa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 1.1 zimepatikana kwa ajili ya kutekeleza kipengele cha Maendeleo ya Uvuvi kuanzia mwaka 2009/2010. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuanzisha ofisi za mradi, ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ofisi na utambuzi wa vijiji vitakavyohusika na utekelezaji wa kazi zilizobainishwa katika eneo la uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, Halmashauri na wadau wengine, ilifanya doria za nchi kavu, majini na angani katika Ukanda wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Bwawa la Nyumba ya Mungu na maeneo mengine ya mipakani yakiwemo Msimbati, Kasanga, Tunduma na Kasumulo upande wa kusini, upande wa kaskazini maeneo ya Horohoro, Sirari, Rusumo na Kabanga na Kigoma. Jumla ya siku-kazi za doria 8,943 zilifanyika nchi nzima na kuwezesha kukamatwa kwa zana haramu na mazao mbalimbali ya uvuvi, zikiwemo makokoro 7,440, kamba za kokoro mita 756,450, nyavu za utali *(Monofilament)* 9,455, nyavu zenye macho madogo 58,040 na vipande vya nyavu

hizo 62,582, ndoano 202,000, vyandarua 228, baruti 51, tambi 6 za baruti, mbolea aina ya urea kilo 133.5, vifaa vya kuzamia jozi 110, mitumbwi 443 na injini za boti 17.

Vilevile doria iliwezesha kukamatwa kwa samaki wachanga kilo 133,511, wakavu kilo 16,030, waliovuliwa kwa baruti kilo 13,412, sato waliovuliwa kwa sumu kilo 3,115, majongoo bahari kilo 3,188.5 na dagaa kilo 244,401.20 pamoja na vifaa mbalimbali haramu. Aidha, watuhumiwa 1,023 walikamatwa na kesi 184 ziko mahakamani kwa makosa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuvua bila leseni, kuvua samaki wachanga, kuvua viumbe walio hatarini kutoweka, na kutumia vyombo visivyosajiliwa katika uvuvi. Jumla ya shilingi 19,673,000.0 zimepatikana kutokana na faini na shilingi 3,474,000.0 kutokana na mnada wa samaki waliokamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia doria iliyofanyika chini ya SADC, ambapo nchi za Afrika Kusini, Msumbiji, Tanzania na Kenya zilishiriki, meli moja ijulikanayo kwa jina la TAWARIQ 1 ilikamatwa ikivua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic Zone, EEZ)* Tanzania na ilikuwa na shehena ya samaki waliogandishwa tani 296.3. Watuhumiwa 37 walifikishwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka na kesi inaendelea mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, vituo vipya 12 vya doria vimeanzishwa katika maeneo ya Mtwara Mjini, Mafia, Kilwa, Horohoro (Tanga), Kipili na Kasanga (Rukwa), Sota (Rorya), Sirari (Tarime), Kasumulo (Kyela), Tunduma (Mbozi), Kabanga (Ngara) na Kanyigo (Misenyi). Aidha, vituo 6 vya doria vya Mwanza, Musoma, Bukoba, Tanga, Dar es Salaam na Kigoma vimeimarishwa. Pia, Wizara imeandaa Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi unaohusisha Jamii ya Wavuvi wa Pwani ya Bahari ya Hindi katika ulinzi wa rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria, kwa kutoa tamko la pamoja linalotaka hatua za haraka zichukuliwe ili kunusuru kutoweka kwa samaki, hususan aina ya sangara katika ziwa hilo.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kupambana na uvuvi haramu na utoroshaji wa samaki na mazao ya uvuvi, ambapo jumla ya siku-kazi za doria 12,000 zitafanyika. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya ulinzi wa rasilimali pamoja kuimarisha vilivyopo. Pia, Wizara itaendelea kudhibiti matumizi ya zana haramu, usimamizi wa rasilimali na uchambuzi wa takwimu za uvuvi katika maji baridi. Vilevile kwa kushirikiana na wadau wengine, Wizara itaendelea kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali ya uvuvi katika maji yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kudhibiti ubora wa mazao ya uvuvi kwa kuchunguza sampuli 1,133, kati ya hizo 894 ni kwa ajili ya vimelea haribifu, 137 kwa ajili ya mabaki ya sumu, dawa na viuatilifu (*pesticides*) na 12 kwa ajili ya madini tembo. Aidha, ukaguzi wa kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao yake kabla ya kusafirishwa nje ya nchi ulifanyika mara 3,163 ambapo tani 23,885.6 zilihakikiwa.

Vilevile ukaguzi ulifanyika mara 122 kwenye viwanda 25 vya kuchakata mazao ya uvuvi vilivyopo Kanda ya Ziwa Victoria na Pwani. Pia, michoro ya ujenzi wa mialo 3 katika Wilaya za Mafia, Rufiji na Kilwa katika Ukanda wa Pwani, imekamilika.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kudhibiti, ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao yake, kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi kwa kuchunguza sampuli 600 na kufanya ukaguzi mara 2,842 wa ubora wa samaki na mazao yake wakati wa kusafirisha nje ya nchi na ukaguzi mara 84 kwa viwanda vya usindikaji wa samaki kutumia wakaguzi 70 kwa siku 11. Pia, ujenzi wa mialo 3 utaanza katika Wilaya za Mafia, Rufiji na Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendeleza ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa kuainisha mabwawa 34 na kupandikiza vifaranga vya samaki 538,500 katika Mikoa ya Pwani (21,000), Iringa (5,106), Kilimanjaro (3,400), Rukwa (2,000), Shinyanga (3,300), Tabora (2,000) na Morogoro (501,694). Kati ya hivyo vifaranga 21,000 vilitoka Kituo cha Kingolwira na 517,500 vilitoka kwa wafugaji wa samaki katika mikoa hiyo. Aidha, vifaranga 552,630 vya samaki aina ya perege kutoka Kituo cha Kingolwira vilisambazwa kwa wafugaji wa samaki kwenye Mikoa ya Pwani (15,760), Ruvuma (500), Morogoro (533,570), Rukwa (1,500) na Dodoma (1,300); na vifaranga 738 aina ya Kambale vilisambazwa Mkoani Morogoro. Pia, wataalam 16 wamepelekwa Kagera (2), Kilimanjaro (2), Lindi (1), Mara (2), Morogoro (6), Mwanza (1), Ruvuma (1) na Tabora (1) kwa lengo la kuanzisha na kuimarisha vituo vya ukuzaji viumbe kwenye maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetoa mafunzo ya ujasiriamali ya kuboresha kilimo cha mwani, ufugaji wa kaa, kambamiti na mwatiko kwa wafugaji wa samaki 783 wa Ukanda wa Pwani. Aidha, mafunzo ya ufugaji wa samaki yametolewa kwa wanavijiji 250 katika Vijiji vya Marendego, Mkwanyule, Tingi, Somanga, Njianne na Magengeni Wilayani Kilwa, wanavijiji 181 katika Vijiji vya Kanga, Kungwi, Kirongwe, Dongo, Ndagoni, Chunguruma Wilayani Mafia na wanavijiji 240 katika Vijiji vya Ndundutawa, Kikale, Kivinja A, Nyamisati, Ruma, Msindaji na Nyanjati Wilayani Rufiji. Pia, Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Kampuni ya Alphakrast iliyowekeza katika ufugaji wa samaki aina ya kambamiti Wilayani Mafia, imechimba bwawa moja na kufanya idadi ya mabwawa yaliyokamilika kufikia 30. Mabwawa hayo yamezalisha tani 250 zenye thamani ya takriban Dola za Kimarekani milioni 2.3 na kati ya hizo, tani 100 zimeuzwa kwenye soko la Jumuiya ya Nchi za Ulaya.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia ufugaji na uendelezaji wa mazao yatokanayo na ukuzaji wa viumbe kwenye maji ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuainisha maeneo yanayofaa kwa ukuzaji na ufugaji wa viumbe, kama vile, mwani, mwatiko, kambamiti, kaa na chaza;

(ii) Kuimarisha vituo 8 vya ufugaji wa samaki katika Mikoa ya Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Morogoro, Mwanza, Ruvuma na Tabora;
(iii) Kuanzisha vituo 3 vya uzalishaji wa vifaranga wa samaki wa maji chumvi katika Mikoa ya Pwani (Mbegani), Lindi na Mtwara;
(iv) Kutoa mafunzo na huduma ya ugani kwa jamii na maofisa uvuvi 20 wa wilaya juu ya ufugaji wa viumbe kwenye maji kibiashara;
(v) Kuzalisha na kusambaza kwa wafugaji samaki vifaranga 800,000 vya perege na 200,000 vya kambale; na
(vi) Kuwezesha wakulima na makampuni ya uzalishaji wa mwani katika kuongeza thamani ya zao la mwani kwa kutoa mafunzo na kuanzisha vikundi.

Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (Marine and Coastal Environment Management Project - MACEMP)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatekeleza Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani *(Marine and Coastal Environment Management Project - MACEMP),* kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Halmashauri 16 za mwambao wa Bahari ya Hindi. Katika mwaka 2008/2009, wananchi 3,062 wamewezeshwa kutekeleza miradi midogo ya kiuchumi 189 katika Halmashauri za Wilaya za Rufiji (60), Mafia (43), Kilwa (63), Lindi Vijijini (6) na Bagamoyo (17), yenye thamani ya shilingi 2,389,933,355. Aidha, miradi 191 imeibuliwa na Halmashauri 9 za Mkinga, Muheza, Pangani, Jiji la Tanga, Kinondoni, Mkuranga, Lindi Mjini, Mtwara Vijijini na Mtwara/Mikindani na miradi hiyo ipo katika hatua za kuhakikiwa. Vilevile mradi umewezesha kukamilishwa kwa Kanuni za Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu, pamoja na kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutekeleza Mradi wa MACEMP, kwa kushirikiana na Halmashauri 16 na wadau wengine katika kusimamia mazingira ya bahari na ukanda wa pwani na miradi ya kuwawezesha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, michoro na gharama za ujenzi wa mialo sita ya Bwai (Musoma Vijijini), Sota (Rorya), Kigangama (Magu), Kahunda (Sengerema), Ikumbitare (Chato) na Marehe (Misenyi) inayojengwa katika Ukanda wa Ziwa Victoria imekamilika na mkataba wa ujenzi umesainiwa. Aidha, jamii ya wavuvi imenufaika kwa kujengewa madarasa matatu ya shule ya sekondari ya Kata ya Nyahongo (Rorya) na darasa moja katika shule ya msingi Soswa (Sengerema), madarasa mawili, ofisi na nyumba ya mwalimu katika Shule ya Nyakakarango (Chato). Vilevile ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika zahanati ya kijiji cha Lugata na madarasa mawili katika shule ya msingi Soswa (Sengerema) unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni mojawapo ya nchi zinazotekeleza Mradi wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko ya Mifugo *(Strengthening Institutions for Risk Management of Transboundary Animal Diseases - TADs) in the Southern African Development Community - SADC),* ambao unahusisha nchi tano za Jumuiya ya Nchi za

Kusini mwa Afrika za Angola, Zambia, Msumbiji, Malawi na Tanzania. Mradi utatekelezwa kwa miaka mitano na unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), kwa gharama ya dola za Kimarekani 21,859,608 na kati ya hizo, Tanzania itapata dola 5,888,189. Madhumuni ya mradi ni kuimarisha maabara na taasisi zinazohusika na uchunguzi wa magonjwa ya mifugo. Mradi huu umeanza kutekelezwa mwezi Januari, 2009 na kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kugharamia mafunzo ya ukaguzi wa nyama kwa wakaguzi wa nyama 6 kutoka katika Manispaa za Temeke, Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Songea na Jiji la Mbeya yaliyofanyika nchini Botswana kwa muda wa miezi sita;

(ii) Kununua vifaa mbalimbali vya maabara;

(iii) Kuendesha mafunzo ya kushirikisha sekta binafsi kuhusu udhibiti wa magonjwa ya milipuko; na

(iv) Kuandaa mikakati ya kudhibiti ugonjwa wa Miguu na Midomo na Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zilizoanzishwa mwaka 2008/2009, ikiwa ni pamoja na kuboresha Maabara Kuu ya Mifugo - Temeke na Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 ili kuimarisha na kuboresha utendaji kazi, Wizara imepandisha vyeo watumishi 29, kuajiri 28 na kuthibitisha kazini watumishi 90. Aidha, jumla ya wastaafu 32 wamelipwa mafao yao. Vilevile mafunzo ya mfumo wa Wazi wa Upimaji na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) ndani ya Wizara yametolewa kwa Wakufunzi 87, Wakuu wa Idara/Vitengo wa Makao Makuu 50 na Watumishi 191 kutoka baadhi ya Taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha utunzaji wa nyaraka za Serikali, Wizara imetoa mafunzo juu ya matumizi ya teknolojia ya kisasa ya utunzaji kumbukumbu kwa watunza kumbukumbu 45. Aidha, makasha 1,000 ya kutunzia kumbukumbu na majalada 8,800 yamenunuliwa. Pia, maandalizi ya kuanzisha benki ya takwimu za watumishi umeanza kwa kununua kompyuta na kukusanya taarifa muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara ilizindua Mkataba wa Huduma kwa Wateja, ambapo jumla ya nakala 2,300 zilisambazwa kwa wadau. Pia, vikao 4 vya TUGHE na 2 vya Baraza la Wafanyakazi vimefanyika. Aidha, wafanyakazi 40 wa Wizara walishiriki katika mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika katika Manispaa ya Morogoro mnamo mwezi Oktoba, 2008.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuimarisha na kuboresha rasilimali watu na kuwezesha watumishi kushiriki katika michezo mbalimbali inayoratibiwa na SHIMIWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendela kushirikisha Sekta Binafsi katika utoaji huduma za ulinzi na usafi katika Makao Makuu ya Wizara na baadhi ya Taasisi zake. Aidha, katika juhudi za kupambana na rushwa, Wizara imekamilisha Mkakati wa Kuziba/Kuzuia mianya ya rushwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaajiri wataalam 199 wa mifugo na uvuvi na 16 wa fani nyingine. Aidha, watumishi 97 watapandishwa vyeo na 150 kuthibitishwa kazini. Pia, watumishi 94 wa kada mbalimbali watapatiwa mafunzo, kati ya hao 19 ya muda mrefu na 75 ya muda mfupi. Majukumu mengine yatakayotekelezwa na Wizara ni pamoja na:-

(i) Kukamilisha Benki ya takwimu (*Data Bank*) za watumishi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu.

(ii) Kushirikiana na vyama vya wafanyakazi na Baraza la Wafanyakazi ili kuwezesha watumishi kuboresha utendaji kazi na kujenga uhusiano mzuri kati ya watumishi na mwajiri.

(iii) Kuhamasisha wafanyakazi kushiriki katika michezo ili kuboresha afya zao na kuimarisha uelewano miongoni mwao.

(iv) Kuelimisha wadau kuhusu Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kufanya tathmini ya ubora wa huduma kwa wateja.

(v) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa wa Wizara.

(vi) Kuimarisha mfumo wa wazi wa kupima utendaji kazi (OPRAS) ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kuelimisha umma kuhusu majukumu yake kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano. Nakala 4,000 za majarida mawili yanayohusu Sekta za Mifugo na Uvuvi na nakala 20,000 za kalenda za Wizara ziliandaliwa na kusambazwa. Aidha, Rasimu ya Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara imeandaliwa na kusambazwa kwa wadau ili kupata maoni yao.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuboresha mfumo wa Tovuti na kusambaza nakala 4,000 za majarida na kalenda kuhusu maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rushwa, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeimarisha dawati la jinsia kwa kulipatia vitendea kazi. Vilevile viashiria vitakavyotumika katika kufuatilia na kupima mafanikio ya jinsia ndani ya Wizara vimepitiwa na kuboreshwa. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kujumuisha

masuala ya jinsia katika mipango na programu za sekta na itatoa mafunzo kuhusu masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari kupitia vikao vya wafanyakazi wote, Baraza la Wafanyakazi na mafunzo maalum. Aidha, watumishi 180 wamepewa mafunzo juu ya namna ya kujikinga na maambukizi mapya. Wizara imetoa posho ya lishe kwa watumishi 3 wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kwa mujibu wa Waraka wa Watumishi wa Umma Na 2. wa Mwaka 2006. Pia, hadidu za rejea kwa ajili ya mtaalam mwelekezi, ambaye atafanya tathmini ya hali ya UKIMWI katika Wizara zimekamilika na kazi imeanza.

Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kupima kwa hiari afya zao, kuwahudumia walioathirika na kukamilisha tathmini ya hali ya UKIMWI katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira katika jamii za wafugaji wa asili ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza kupitia sera, sheria na kanuni za sekta za mifugo na uvuvi zinavyohusiana na sera na sheria kuhusu mazingira. Aidha, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali chini ya uratibu wa Wizara ya Nishati na Madini, Asasi ya SNV - Tanzania na CAMARTEC, Wizara imeshiriki katika uanzishwaji wa programu ya matumizi ya nishati mbadala ya biogesi nchini.

Katika 2009/2010, Wizara itaendelea na mikutano ya aina hiyo katika kanda zilizobaki ili kuhakikisha kuwa, ufugaji unafanywa kwa kuzingatia utunzaji wa Mazingira. Pia, Wizara itashiriki katika uratibu wa programu ya kujenga mitambo 12,000 ya biogesi katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Mwaka wa Wataalam wa Mifugo na Uvuvi, ulifanyika tarehe 8 - 9 Oktoba, 2008 Mjini Dodoma na uliwakutanisha kwa mara ya kwanza wataalam wa mifugo na uvuvi kutoka Halmashauri zote na taasisi mbalimbali za serikali na sekta binafsi. Aidha, Mkutano wa mwaka wa Madaktari wa Mifugo *(Tanzania Veterinary Association - TVA),* ulifanyika Arusha tarehe 20 - 22 Februari, 2009 na kufunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na kufungwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeshiriki katika mikutano mitatu inayohusu usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria chini ya Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria (LVFO). Mkutano wa kwanza, ulifanyika Jinja, Uganda tarehe 27 - 29 Oktoba, 2008 na ulishirikisha Mawaziri wanaosimamia uvuvi katika nchi za Kenya na Uganda. Katika mkutano huo, Mawaziri hao walitoa tamko linalotaka hatua za haraka zichukuliwe kunusuru kutoweka kwa samaki, hususan sangara. Aidha, mkutano wa pili wa Mawaziri ulifanyika tarehe 3 - 5 Desemba, 2008 Jinja, Uganda kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya mkutano wa kwanza, pamoja na kuzindua Makao

Makuu ya Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria yaliyopo nchini Uganda na kukabidhi boti nne za doria moja kwa kila nchi na moja kwa Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika Ziwa Victoria, mkutano wa tatu wa Mawaziri wenye dhamana ya rasilimali za uvuvi kupitia Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria, ulifanyika tarehe 23 - 27 Februari, 2009 Jijini Dar es Salaam na kusaini makubaliano ya:-

(i) Kupitisha uamuzi wa kutokomeza matumizi ya zana haribifu, uvuvi wa samaki wachanga kwa asilimia 50 ifikapo Juni, 2009 na asilimia 100 ifikapo Desemba, 2009 kwa kutumia matokeo ya survey ya uvuvi ya mwaka 2008;

(ii) Kuandaa mipango kazi na kuanzisha mfumo wa upashanaji habari wa kiintelijensia ili kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki; na

(iii) Kutekeleza Mpango wa Kikanda wa Kudhibiti Uvuvi haramu *(Regional Plan of Action to deter Illegal, Unregulated and Unreported Fishing - REPOA - IUU)* na Mpango Kazi wa Kudhibiti nguvu ya uvuvi *(Regional Plan of Action to Reduce Fishing Capacity – REPOA Capacity).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara iliratibu na kushiriki maadhimisho ya matukio mbalimbali ya sekta za mifugo na uvuvi kama ifuatavyo:-

(i) Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nane Nane yaliyofanyika katika Manispaa ya Dodoma tarehe 01- 08 Agosti, 2008 yakiwa na Kaulimbiu "*Mapinduzi ya Kijani ndio Mkombozi wa Mtanzania".* Mgeni Rasmi alikuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda (Mb);

(ii) Wiki ya Unywaji Maziwa iliyofanyika Kitaifa katika Manispaa ya Dodoma tarehe 29 Mei hadi tarehe 01 Juni, 2009 ikiwa na kaulimbiu *"Kunywa maziwa kwa afya yako, yaliyosindikwa ni bora zaidi";*

(iii) Siku ya Chakula Duniani iliyofanyika tarehe 16 Oktoba, 2009 katika Manispaa ya Musoma ikiwa na kaulimbiu *"Uhakika wa chakula: Changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na nishati itokanayo na mimea";*

(iv) Siku ya Uvuvi Duniani ilifanyika katika Ziwa Victoria, katika Kisiwa cha Kalangala, Uganda, tarehe 18 Desemba, 2008, ikiwa na kaulimbiu *"Ustawi wa Uvuvi kupitia Serikali na Wavuvi katika kuitikia Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na nchi za Afrika ya Kusini, Kenya na Msumbiji, Tanzania imefanikiwa kukamata meli kubwa ya uvuvi iliyokuwa ikivua katika Bahari Kuu ya Tanzania tarehe 8 Machi, 2009, ambayo ilikutwa na jumla ya tani 296.3 za samaki wa aina mbalimbali. Jumla ya watuhumiwa 37 wamefunguliwa mashtaka na kesi iko Mahakama Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, napenda kuwashukuru kwa dhati, wale wote walioshirikiana nasi kwa njia moja au nyingine katika kutimiza majukumu yetu. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. James Wanyancha (Mb), Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Katibu Mkuu, Dkt. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Jonas Melewas, Wakuu wa Idara na Taasisi za Wizara, Wafanyakazi na Wadau wote, kwa mshikamano wao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa washiriki wetu wa maendeleo (*Development Partiners),* pamoja na wahisani wanaotuunga mkono katika kutekeleza miradi mbalimbali ya sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kuzitambua na kuzishukuru nchi za Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Serikali za Australia, Austria, Denmark, Japan, Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Ireland, Marekani, Misri, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Italia. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa mashirika ya Umoja wa Mataifa ya FAO, IFAD, CFC, UNICEF, UNDP, GEF na IAEA.

Vilevile, napenda kutambua na kuzishukuru Taasisi za Kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB); Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japani (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DfID), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama la Umoja wa Afrika (AU/IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Norway (NORAD).

Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *VETAID, Care International*, *OXFAM* na *Wellcome Trust* za Uingereza, Austro-*Project, Heifer Project Tanzania (HPT)*, *World Vision, FARM Africa, Southern Highland Livestock Development Association (SHILDA), CONCERN, SNV, Land 'O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCF), World Society for Protection of Animals (WSPA), Dryland Development Centre (DDC), Worldwide Fund for Nature (WWF)* na *International Livestock Research Institute (ILRI),* ambao wameendelea kuisaidia Wizara.

Naomba kupitia kwako Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wote hawa kwa dhati na kuwaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Biharamulo Mashariki (Chato), kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi 67,334,294,900 kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi 9,271,422,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE);

(ii) Shilingi 27,982,032,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine (OC);

(iii) Shilingi 30,080,841,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 9,723,810,000 ni fedha za ndani na shilingi 20,357,031,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani: www.mifugo_uvuvi.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Charles Keenja karibu.

**MHE. CHARLES N. KEENJA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 na Maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4 Juni, 2009, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, ilikutana kwenye Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es salaam, kupitia Taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa 2008/2009. Aidha, Kamati ilijadili Makisio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa 2009/2010. Kamati ilipata maelezo ya kuridhisha kutoka kwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Kamati ilitoa maoni na ushauri juu ya shughuli za Wizara na Makisio ya mwaka wa 2009/2010, kwa lengo la kuboresha utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Kamati ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa ili kuongeza ufanisi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi cha kuridhisha, imeyafanyia kazi maoni ya Kamati na naipongeza Wizara kwa utekelezaji mzuri. Baadhi ya maeneo ambayo yalifanyiwa kazi na Wizara ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara kutoka shilingi 41,872,573,000 kwa mwaka wa 2008/2009 hadi kufikia shilingi 67,334,267,000 kwa mwaka wa 2009/2010, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 24.5. Fedha hizi zinajumuisha shilingi bilioni 10 kutoka kwenye Mfuko wa Madeni ya Nje (EPA), zilizoidhinishwa na Bunge mwezi wa Februari, 2009 kwa ajili ya kulipia ruzuku ya madawa ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa maeneo ya ufugaji na miundombinu, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeainisha na kutenga maeneo kwa wafugaji na kuhakikisha yanaendelezwa kwa ajili ya ufugaji. Katika mwaka wa 2008/2009, jumla ya hekta 460,833 zilipimwa katika wilaya tano za Liwale, Lindi, Kilwa, Kilosa na Nachingwea na mpaka sasa jumla ya hekta 1,391,109.41 zimetengwa kwa ajili ya ufugaji katika Mikoa 13, yenye jumla ya Halmashauri za Wilaya 31 na jumla ya vijiji 240. Zoezi hili litaendelezwa katika mwaka wa 2009/2010, katika maeneo mengine yaliyotengwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwapunguzia wafugaji na wavuvi gharama za madawa, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya asilimia 40 ya bei za pembejeo hizo. Katika mwaka wa 2009/2010, kiasi cha shilingi bilioni 10 kimetengwa kwa ajili ya kutoa ruzuku ya pembejeo za mifugo na uvuvi. Aidha, Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa forodha kwenye dawa zote za kutibu magonjwa ya mifugo. Kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda, Serikali imeweka utaratibu wa kupunguza au kuondoa kabisa, kodi kwenye malighafi, pembejeo na zana za uvuvi ili kuwawezesha wavuvi kumudu kununua zana hizo kwa bei nafuu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizi ambazo zitaharakisha mafanikio ya kupunguza umaskini miongoni mwa wafugaji na wavuvi. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kusambaza madawa ya ruzuku ili kuhakikisha kwamba, yanawafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha na kuimarisha vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS), kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi. Aidha, Wizara, kwa kushirikiana na Shirika la World Wildlife Fund (WWF), chini ya Mradi wa Mfuko wa Japan wa Maendeleo ya Jamii, imeandaa mpango wa kuwasaidia wavuvi, ambapo jamii za Pwani zimehamasishwa kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa katika Wilaya za Kilwa, Rufiji na Mafia. Mpaka sasa jumla ya Benki za Jamii Vijijini (VICOBA) 60 zimeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** chini ya Mradi wa Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP), Savings and Co-operatives Union League of Tanzania (SCULT) ipo kwenye mchakato wa kuanzisha Benki ya Jamii katika Wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji ili kuwasaidia wavuvi. Aidha, mchakato wa kuanzisha Benki ya Kilimo unaendelea chini ya usimamizi wa Benki kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba, Serikali inajenga mazingira mazuri ya kuwezesha Sekta Binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi, tayari Serikali imeainisha maeneo yenye fursa za uwekezaji ambayo ni Magu, Themi, Ruvu, Bunda, Kyaka na Kiwanda cha Nyama cha Mbeya. Katika kuwekeza katika maeneo hayo, wawekezaji wanatakiwa kuingia ubia na NARCO. Hadi mwezi wa Juni, 2009, hakuna wawekezaji waliokuwa wamejitokeza na Serikali imeamua kujenga machinjio ya kisasa kwenye Ranchi ya Ruvu. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu na inashauri kwamba, kila itakapotokea kwamba sekta binafsi haijitokezi kushiriki katika utekelezaji wa shughuli ambazo ni muhimu kwa umma, Serikali isisite kutumia uwezo wake kutekeleza shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza uwekezaji katika viwanda vya maziwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maziwa na kupitia wiki ya unywaji wa maziwa inayofanyika tarehe 1 Juni ya kila mwaka, imeendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa kwa ajili ya kupanua soko la ndani. Mpaka sasa jumla ya shule 73 zenye jumla ya wanafunzi 53,742 zinashiriki katika Mpango wa Unywaji wa Maziwa, ambao unatekelezwa kwenye Wilaya za Hai, Moshi Vijijini, Tanga, Mbeya na Njombe.

Aidha, Wizara imewasilisha kwa Wizara ya Fedha na Uchumi, mapendekezo ya kupunguza au kufuta kodi zote zinazokwamisha usindikaji wa maziwa, ikiwa ni pamoja na ushuru wa forodha na VAT kwenye mitambo, vifaa na vifungashio na VAT kwenye maziwa na mazao yake ili viwanda viweze kumudu gharama za usindikaji na kuhimili ushindani wa soko. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuzingatia maoni ya Kamati kwa kupunguza kodi kwenye maziwa na mazao ya maziwa yanayozalishwa humu nchini na kuongeza ushuru wa forodha kwa bidhaa za maziwa zinazoingizwa nchini kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha uwekezaji katika ngozi, Serikali imeongeza kodi kutoka asilimia 20 hadi kufikia asilimia 40 kwa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi. Kutokana na hatua hii, viwanda vimeongeza uzalishaji hadi kufikia asilimia 80 ya uwezo wa viwanda vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, imeendelea kutoa taarifa za masoko ya mifugo kila wiki na kila mwezi kwa minada 29 iliyopo katika Wilaya mbalimbali hapa nchini kwa kutumia mfumo wa mtandao wa kompyuta, simu za mikononi, magazeti na radio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mradi wa Marine and Coastal Environment Management Project (MACEMP), Serikali ilitathmini matatizo yanayowakabili wakulima na wanunuzi wa zao la mwani na baadae kuwakutanisha ili kuangalia jinsi ya kuboresha soko la mwani. Aidha, ushauri kwa wakulima wa mwani umeendelea kutolewa, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kuanzisha vikundi vyao ili kuwa na maamuzi ya pamoja kuhusu bei, kwani ni njia mojawapo ya kuwawezesha kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2008/2009, Wizara imefanikiwa kutekeleza kazi ilizojipangia kama ambavyo Waziri mtoa hoja alivyowasilisha hivi punde. Napenda kutaja baadhi ya kazi zilizotekelezwa kama ifuatavyo:-

Sekta ya Mifugo:

a) Sheria ya Ngozi na 18 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama, zote za mwaka 2008, zilipitishwa na Bunge Novemba, 2008 na kuridhiwa na Rais Desemba, 2008 na kuanza kutumika tarehe 01 Mei, 2009. Rasimu za kanuni za sheria hizo zimekamilika na zimewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mapitio.

b) Vituo vya utafiti vya Mabuki, Kongwa, Tanga, West Kilimanjaro, Naliendele na Mpwapwa vimeboreshwa kwa kupatiwa vitendea kazi muhimu. Aidha, Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa na mafunzo kwa wataalam.

c) Ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa watumishi, hususan katika Serikali za Mitaa, wanafunzi 1,185 walipatiwa mafunzo kwa gharama za Serikali, katika vyuo sita vya mifugo nchini. Aidha, wahitimu 613 wa ngazi ya stashahada walihitimu mafunzo yao mwezi wa Juni, 2009 na kupangiwa kazi katika Halmashauri mbalimbali za Wilaya na Miji.

d) Mikakati ya kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo, hususan Homa ya Mapafu, Homa ya Bonde la Ufa, Mafua Makali ya Ndege, Kichaa cha Mbwa, Mapele, Ngozi na Ugonjwa wa Miguu na Midomo, inaendelea kutekelezwa. Aidha, katika Nyanda za Juu Kusini, mpango wa kuchanja ng'ombe kuzuia Homa ya Mapafu ulikuwa na mafanikio mazuri kwa ugonjwa kudhibitiwa na chanjo kusitishwa.

e) Maabara Kuu ya Mifugo iliyoko Temeke, Dar es Salaam ni taasisi muhimu sana katika Sekta ya Mifugo. Katika mwaka wa 2008/2009, Maabara hiyo ilifanya kazi nyingi muhimu ikiwa ni pamoja na kuzalisha na kusambaza dozi 23,000,000 za chanjo ya mdondo, dozi 500,000 za Kimeta na dozi 100,000 za chambavu. Aidha uchunguzi na uhakiki wa ubora wa mazao na vyakula vya mifugo yakiwemo mabaki ya dawa na sumu ambapo sampuli 480 za vyakula vya kuku vilihakikiwa ubora wake. Uchunguzi ulionesha vyakula hivyo kutokuwa na ubora unaotakiwa.

f) Viwanda vya kusindika vyakula vya mifugo vimeongezeka kutoka 74 hadi kufikia 79 ambapo tani 800,000 zimezalishwa katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Mei, 2009.

g) Kituo cha Uhimilishaji cha Usa River, Arusha - *National Artificial Insemination Centre (NAIC)*, kimefanyiwa ukarabati wa majengo pamoja na kuendeleza shamba la malisho. Kituo kilizalisha lita 18,160 za *liquid nitrogen* na dozi 74,200 za mbegu bora. Ng'ombe 68,900 walihimilishwa katika mashamba mbalimbali ya wafugaji. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wahimilishaji kutoka katika Halmashauri za Wilaya 142 na asasi za kijamii 165.

h) Usindikaji wa maziwa kwa siku umeongezeka kutoka lita 65,930 kwa mwaka 2007/2008 hadi kufikia lita 88,940 kwa mwaka 2008/2009 na hii imetokana na kuimarishwa kwa shughuli za usindikaji katika baadhi ya viwanda vya hapa nchini.

Sekta ya Uvuvi:

a) Rasimu ya kwanza ya Sera ya Taifa ya Uvuvi imekamilika na itajadiliwa na wadau wa sekta kwa ajili ya maboresho.

b) Elimu juu ya uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi iliendelea kutolewa kwa jamii za wavuvi.

c) Jumla ya tani 324,830 za mazao ya uvuvi yanayokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi bilioni 371.4 yalivunwa katika maeneo mbalimbali ya uvuvi nchini. Kati ya hizo tani 43,130 zilitoka ukanda wa maji chumvi na tani 281,830 maji ya baridi.

d) Katika kudhibiti uvuvi haramu, Wizara kwa kushirikiana na nchi za Afrika ya Kusini, Kenya na Msumbiji ilifanikiwa kukamata Meli kubwa ya uvuvi iliyokuwa ikivua katika Bahari Kuu ya Tanzania tarehe 8 Machi, 2009, ambayo ilikutwa na tani 296.3 za samaki wa aina mbalimbali. Mpaka sasa jumla ya watuhumiwa 37 waliokuwa wakivua wamefunguliwa mashtaka na kesi yao ipo Mahakama Kuu ya Tanzania. Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio yaliyopatikana na inaishauri iendelee kufanya doria kwenye eneo letu la Bahari ili kuzuia vitendo vya ujangiri kama vilivyokuwa vikifanywa na meli iliyokamatwa.

e) Mafunzo kwa ajili ya wanafunzi 232 wa Uvuvi yametolewa.

f) Vipindi vya elimu kwa umma juu ya athari za uvuvi haramu viliandaliwa kwa kupitia runinga, radio, mikutano, maonesho na vipeperushi.

g) Wanavijiji 641 wa Wilaya za Ukanda wa Pwani walipatiwa mafunzo ya ufugaji wa samaki aina ya mwatiko na unenepeshaji wa kaa katika Wilaya za Lindi, Kilwa, Mafia na Rufiji.

h) Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (MACEMP) nao umesaidia katika kudhibiti uvuvi haramu kwa kuweka doria katika Ukanda wa Pwani na kusaidia shughuli nyingine za Maendeleo.

i) Mashua nne zilinunuliwa na kukabidhiwa kwa mamlaka zinazohusika kwa kazi ya doria katika Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Kila Ziwa limepatiwa mashua mbili.

j) Watumishi waliendelea kuhamasishwa kupima afya zao kupitia vikao vya wafanyakazi na mafunzo maalum. Aidha, jumla ya shilingi 1,800,000 zimetumika kulipia

posho ya lishe kwa wafanyakazi watatu waliojitokeza kuwa wanaishi na Virusi vya Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Waziri alieleza kwa kina changamoto au matatizo yaliyojitokeza katika kutekeleza bajeti ya Wizara kwa mwaka wa 2008/2009. Changamoto hizo zimekuwa zikijirudia mwaka hadi mwaka. Ipo haja ya Serikali kuchukua hatua kuhakikisha haziendelei kujirudia katika miaka ijayo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Uhaba wa maeneo ya ufugaji na miundombinu umesababisha wafugaji kuhamahama na hivyo kuleta uharibifu wa mazingira, kuenea kwa magonjwa ya mifugo na migogoro baina ya wafugaji na wakulima. Aidha, ukame umeathiri mifugo kwa kukosa maji na malisho na hivyo kulazimika kuhama.

ii) Uwekezaji mdogo katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi umesababisha ukuaji mdogo wa sekta hizi kuliko ilivyotarajiwa.

Kuwepo kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo na tishio la ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege kumeathiri pia maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini. Hata hivyo, sampuli 2,300 za ndegepori, kuku na bata zilichunguzwa na kuthibitisha kutokuwepo ugonjwa. Tumshukuru sana Mwenyezi Mungu.

iii) Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uhifadhi wa samaki na mazao ya uvuvi, uzalishaji duni na ukosefu wa masoko ya uhakika, kumepunguza mchango wa sekta hizi katika Pato la Taifa.

iv) Kutokuwepo kwa taasisi za mikopo zinazokopesha wafugaji na wavuvi kulisababisha washindwe kupata mitaji ya kuzalisha kibiashara.

v) Gharama kubwa za pembejeo za mifugo na uvuvi, zikiwemo dawa za kuogeshea na zana za uvuvi, kumesababisha wafugaji na wavuvi kushindwa kuzinunua kwa viwango vya kukidhi mahitaji yao.

vi) Tija ndogo katika uzalishaji wa mifugo hasa ya asili imesababisha sekta hii kutochangia kikamilifu katika Pato la Taifa na kutopunguza umaskini miongoni mwa jamii.

vii) Kuendelea kuwepo kwa uvunaji na matumizi ya rasilimali za uvuvi kwa njia zisizokuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, inaomba jumla ya shilingi 67,334,294,900; kati ya kiasi hiki, shilingi 37,253,454,000 ni kwa matumizi ya kawaida na shilingi 30,080,841,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 2,982,032,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 9,271,422,000 ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, kati ya

fedha za maendeleo, shilingi 9,723,810,000 ni fedha za ndani na shilingi 20,357,031,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi hayo ya fedha yatawezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali ilizojipangia. Baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

Sekta ya Mifugo:

a) Kuendelea kutoa ruzuku ya madawa na chanjo za mifugo. Jumla ya shilingi bilioni 10 zinaombwa.

b) Kutoa mafunzo kwa wanafunzi 1,200 na kutoa ajira katika Serikali za Mitaa kwa wataalam wa ugani wa Mifugo 613 waliohitimu katika vyuo vya mafunzo ya mifugo na kununua vitendea kazi kwa ajili ya wagani.

c) Kuboresha miundombinu muhimu ya mifugo ikiwa ni pamoja na kujenga masoko ya mifugo, malambo, majosho, machinjio na kukarabati vyuo vya utafiti wa mifugo na Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke.

d) Kuimarisha huduma za uhimilishaji na utafiti wa Mifugo kwa kuimarisha Kituo cha Utafiti cha Uhimilishaji cha NAIC Arusha na vituo vyote vya kanda vya uhimilishaji na kuimarisha Mashamba ya kuzalisha Mitamba.

e) Kupanga matumizi ya maeneo ya malisho ya mifugo.

Sekta ya Uvuvi:

(a) Kuimarisha miundombinu ya kupokea, kuhifadhi na kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi ikiwa ni pamoja na kujenga mialo tisa ya kupokelea samaki na kuimarisha mialo sita iliyopo, kukarabati *boat yard* tatu za Mtwara, Mwanza na Kigoma na kununua majokofu ya kuhifadhia samaki.

(b) Kudhibiti uvuvi na biashara haramu na kuhifadhi mazingira kwa kukarabati vituo 17 vya doria na kuwezesha vikundi vya wavuvi wadogo kununua zana bora za uvuvi.

( c ) Kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Uvuvi na ukusanyaji wa takwimu kwa kuendelea kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) na kuimarisha vyuo vya mafunzo ya Uvuvi ili viweze kufundisha wanafunzi wasiopungua 500 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kwa ufupi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa 2008/2009 na matarajio kwa mwaka wa 2009/2010, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Maoni ya Jumla:

a) Kutokana na umuhimu wa Sekta za Mifugo na Uvuvi katika kuchangia Pato la Taifa, kuboresha lishe ya wananchi, kupunguza umaskini na kuwapatia wananchi ajira, Kamati inaishauri Serikali, izipe Sekta hizi umuhimu wa kwanza kwa kuongeza kiasi cha fedha zinazopewa kwenye Bajeti ya Serikali.

b) Kutokana na kukwama kwa miradi mingi ya maendeleo kwa sababu ya kuchelewa kwa fedha za Wafadhili, Kamati inashauri Serikali iweke utaratibu utakaowezesha kupunguza utegemezi kwa wahisani kutoka nje.

c) Utafiti ni muhimu sana katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi. Kamati inaishauri Serikali izipe Sekta hizi kipaumbele cha juu kwenye Bajeti ya Serikali. Aidha, maslahi ya watafiti yaboreshwe ili wasishawishike kutoka nje ya nchi. Ipo haja ya kuchukua hatua za haraka kuandaa watafiti watakaojaza mapengo yaliyopo na yanayotarajiwa kuongezeka kutokana na kustaafu kwa watafiti wengi waliopo.

d) Matarajio ya makusanyo ya mapato kwa kipindi cha mwaka wa 2008/2009 yalikuwa ni shilingi 9,334,915,000. Mpaka Mei 31, jumla ya 6,191,036,863 zilikusanywa sawa na asilimia 67 tu ya lengo. Kutokana na lengo kutofikiwa, Kamati inashauri Wizara ijipange vyema ili kuhakikisha inafikia malengo ya makusanyo.

Sekta ya Mifugo:

a) Wafugaji wamekuwa wakihama kwa wingi kutoka mikoa ya kaskazini kwenda kwenye mikoa ya kusini, kufuata maji na malisho kwa mifugo yao. Kuongezeka sana kwa mifugo katika mikoa ya kusini, kunasababisha uharibifu wa mazingira na ni chanzo cha migogoro kati ya wafugaji na wakulima. Serikali inapaswa kuchukua hatua za haraka na madhubuti kukabiliana na hali hii. Kamati inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe:-

- Serikali iboreshe mazingira yaliyoko kwenye maeneo wafugaji hao wanakotoka kwa kujenga malambo na vituo vya kutibu mifugo.

- Wafugaji wafundishwe ufugaji wa kisasa wa ng’ombe wachache wanaotoa maziwa na nyama nyingi.

- Hatua zichukuliwe kudhibiti uhamishaji wa mifugo ili kuepuka migogoro kati ya wafugaji na wakulima, kuenezwa kwa magonjwa na kuharibiwa kwa mazingira.

- Wafugaji watengewe maeneo kwa ajili ya mifugo na watakiwe kuoanisha wingi wa mifugo na uwezo wa maeneo wa kulisha mifugo hiyo. Aidha, wafundishwe jinsi ya kutumia maeneo wanayotengewa kwa kulisha mifugo yao kwa mzunguko ili kuruhusu uoto wa asili na ili yatoshe kuhudumia mifugo yao kwa mwaka mzima.

- Serikali ifanye tathmini ya matumizi ya ranchi zilizobinafsishwa na zile ambazo hazitumiki kama ilivyokusudiwa zitolewe kwa wachungaji ambao wataandaliwa kuzitumia kwa ufugaji wa kisasa.
- Wafugaji na wakulima wahamasishwe kuheshimiana na watakaovuruga uhusiano kati yao kwa makusudi waadhibiwe vikali.

b) Serikali imetenga shilingi bilioni kumi kwa ajili ya ruzuku ya madawa ya mifugo. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huo. Aidha, Kamati inaitaka Wizara iweke utaratibu mzuri wa kusimamia matumizi ya fedha hizo ili ziwafikie walengwa.

c) Ngozi nyingi zinazozalishwa nchini zinauzwa nje bila kusindikwa. Kamati inarudia kuishauri Serikali ichukue hatua zinazofaa kuhakikisha kwamba, viwanda vyote vya umma vilivyobinafsishwa vinarudia kufanya kazi kikamilifu na iwapo waliovinunua wameshindwa kuvifufua, Serikali isiendelee kusita kuvichukua na kuviwekea utaratibu mpya utakaohakikisha vinafufuliwa. Kamati inahisi kwamba, viwanda hivyo vimefungwa makusudi ili kuwezesha ngozi kuuzwa nje zikiwa ghafi.

d) Kutokana na umuhimu wa zao la ngozi hasa katika Pato la Taifa, Kamati inashauri Serikali ijipange vizuri katika kuhakikisha inaendeleza viwanda vya ndani. Aidha, iweke utaratibu na ikibidi itunge sheria ambayo itahakikisha bidhaa za ngozi zinazozalishwa na viwanda vya nchini zinanunuliwa ndani (soko la kwanza). Mfano, viatu vya wanajeshi na wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari, viwe vile vinavyozalishwa na viwanda vya hapa nchini.

e) Serikali iendelee kuboresha Maabara Kuu ya Mifugo ya Temeke kwa kuipatia watumishi wenye sifa zitakiwazo, vifaa vya kisasa na vitendea kazi muhimu ili iweze kufikia kiwango cha kimataifa. Aidha, maslahi ya watumishi yaboreshwe.

f) Suala la uhimilishaji ni muhimu sana katika kuboresha mifugo na kuifanya itoe maziwa na nyama nyingi. Hata hivyo, suala hili halijapewa umuhimu unaostahili. Kamati inaishauri Serikali ilipe suala hili umuhimu unaostahili, kwa kuboresha vituo vyote vya uhimilishaji vilivyopo na kuwahamasisha wafugaji wavitumie kuboresha mifugo yao.

g) Viwanda vya maziwa vinakabiliwa na matatizo mengi ambayo yamesababisha baadhi ya viwanda hivyo kufungwa na vilivyobaki kuendeshwa kwa hasara.

Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za haraka kuvinusuru viwanda vilivyopo na kuwavutia wawekezaji wapya kujenga viwanda vya kusindika maziwa ili kuongeza kiwango kinachosindikwa sasa. Hatua zinazopendekezwa ni pamoja na:-

- Kuondoa kodi zote kwenye maziwa na mazao yatokanayo na maziwa, mashine na vifaa vinavyotumiwa kusindika maziwa, vikiwamo vifungashio, vifaa vya kuhifadhia na kusafirisha maziwa vya aina zote na kadhalika.

- Serikali ihakikishe kwamba wazalishaji wa maziwa wanakuwa na fursa za kuuza maziwa na mazao mengine ya maziwa katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki bila kuwekewa vizuizi visivyokuwa na msingi.

- Serikali iweke utaratibu wa kulinda viwanda vya maziwa, kama inavyofanyika kwa viwanda vingine, kwa kuzuia kuingizwa nchini kwa maziwa na mazao ya maziwa ambayo yanaweza kuzalishwa nchini. Baadhi ya maziwa yanatoka kwenye nchi ambako Serikali zinatoa ruzuku kwa wafugaji na viwanda vya maziwa na kuruhusu yaingizwe kunasababisha ushindani usiokuwa wa haki kwa viwanda vyetu.

- Serikali ishirikiane na wenye viwanda vya maziwa kuhamasisha unywaji wa maziwa nchini. Aidha, kwa makundi ambayo yanalishwa na Serikali, maziwa yawe sehemu ya chakula ili kuboresha lishe yao na kujenga mazoea ya unywaji wa maziwa.

- Kwa kushirikiana na Sekta ya Watu Binafsi, Serikali iweke utaratibu wa kuongeza uzalishaji na ubora wa maziwa na wa kukusanya na kusafirisha maziwa hadi kwenye viwanda vya kusindika maziwa.

Sekta ya Uvuvi:

a) Sekta ya uvuvi itaendelea vizuri endapo wavuvi watawezeshwa. Kamati inaishauri Serikali iweke mipango madhubuti ya kuhakikisha inatoa mikopo yenye masharti nafuu ya kuwawezesha wavuvi kununua zana bora za uvuvi na kwa hiyo kuzalisha kwa tija.

b) Kutokana na wakulima wa zao la mwani kuendelea kuwa na maisha duni licha ya kazi ngumu wanazofanya, Kamati inaishauri Serikali iwasaidie wakulima hawa kwa kuwahamasisha kuunda vyama au vikundi ili kuwa na sauti katika upangaji wa bei na ihamasishe ujenzi wa kiwanda cha kusindika mwani ili kuboresha na kulipa thamani zao la mwani nchini.

c) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha maslahi ya watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI). Aidha, kuna haja ya kuhakikisha Kituo cha Dar es Salaam kinaboreshwa kwa kujengewa miundombinu inayoendana na mahitaji yake na kupatiwa vifaa kwa ajili ya Utafiti.

d) Kutokana na umuhimu wa Chuo cha Mbegani katika kutoa wataalam wengi na wenye sifa zinazotakiwa, kutokana na kuwepo kwa upungufu mkubwa wa watumishi wa uvuvi katika Serikali za Mitaa na kutokana na Chuo kuchukua wanafunzi kutoka nchi mbalimbali za SADC na ukanda huu wa Afrika, Kamati inashauri mishahara na maslahi mengine kwa ujumla ya watumishi yaboreshwe, watumishi waongezwe na wapatiwe vitendea kazi muhimu kama mashua za kufundishia na kadhalika. Aidha,

Kamati inashauri Serikali iendelee na jitihada za kuboresha vyuo vyote vya uvuvi ili viweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

e) Kamati inashauri Serikali, kama ilivyoondoa ushuru kwenye zana za kilimo, iondoe ushuru kwenye zana za uvuvi, kwa mfano mashine za mashua, kamba za plastiki, nyavu *(nylon fabrics),* nyuzi, maboya, mishipi na ndoano. Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa kutengeneza zana za uvuvi humu nchini.

f) Kamati inaunga mkono jitihada za Serikali katika kudhibiti uvuvi haramu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mbadala wa kuwapatia wavuvi zana bora kwa kuwakopesha na tunaamini hatua hii itasaidia kupunguza kwa kiasi kukubwa uvuvi haramu.

g) Kamati inashauri wananchi waelimishwe kulinda na kuhifadhi mazalio ya samaki katika maziwa na bahari. Aidha, wafugaji wa samaki wapewe mwongozo wa ufugaji wa samaki ndani ya bahari na pia washauriwe kufuga samaki ambao wana soko zuri hasa katika Hoteli za Kitalii.

h) Kutokana na Sekta ya Uvuvi kutokuwa na Maafisa Ugani wa kutosha, Kamati inashauri kuwepo na ufuatiliaji wa kutosha wa miradi ya maendeleo hususan Mradi wa MACEMP. Aidha, kupitia Mradi wa MACEMP, wafugaji wa nyuki wa Ukanda wa Pwani waelimishwe ili waweze kuzalisha asali bora na wasaidiwe kupata soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Juhudi, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara, naamini vimesaidia utendaji wa Wizara. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Charles N. Keenja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia nafasi hii, kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa John P. Magufuli (Mb) na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. James M. Wanyancha (Mb), kwa ushirikianao wao mzuri ulioiwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi na kwa wakati. Aidha, nawapongeza Wataalamu wote wa Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt.Charles Nyamrunda na Naibu Katibu Mkuu, Dkt.

Jonas N. Melewas, kwa jinsi walivyofafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati wakati wa kuchambua taarifa za Wizara na mapendekezo ya Bajeti ya mwaka wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Ofisi yako, hasa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Pamela E. Pallangyo, kwa kuiwezesha Kamati kufanikisha shughuli zake kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99**,** kwa mwaka wa 2009/2010, jumla ya shilingi 67, 334, 294, 900.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Jecha.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA (MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI :** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye nguvu na hekima, ambaye ametuumba kutokana na nafsi moja tu naye ni mweza wa kuteremsha miujiza. Kwa hakika, sifa njema zote ni zake yeye Mola, mlezi wa walimwengu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 99(3) na (7), Toleo la 2007.

Aidha, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Wete, kwa kuendelea kuniunga mkono na kunipa ushirikiano mkubwa ambao umenisaidia kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Ninawaahidi kwa uwezo anaonipa Mwenyezi Mungu, nitaendelea kuwatumikia vyema, kwa juhudi zangu zote na kwamba sitowaangusha.

Kadhalika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote, hususan Wabunge wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano mkubwa wanayonipa yanayonipelekea kuifanya kazi zangu kwa wepesi na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kuwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza, kutuelekeza na kutusimamia vyema katika shughuli zetu za kila siku. Ufanisi mkubwa unaoonekana katika Kambi yetu ni kutokana na Uongozi wao mahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sitowashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa utendaji wao katika kuhakikisha Sekta hizi za Mifugo na Uvuvi inakuwa miongoni mwa sekta kiongozi katika mchango wake kwa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mkono wa pole kwa Mufti, Sheikh Mkuu Issa bin Simba na Waislamu wote, kwa kifo cha Sheikh Suleiman Gorogosi. Kadhalika, natoa pole kwa ndugu na familia ya Marehemu Profesa Haroub bin Othman, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliyefariki 28 Juni, 2009. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za Marehemu hawa peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema ufugaji kwa maana iliyo wazi na inayoeleweka na Watanzania walio wengi ni kuizungumzia jamii ya wafugaji, ambayo inaendesha ufugaji wao kwenye mazingira ya kuhama kutoka eneo moja na kwenda eneo lingine ili kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo endelevu katika sekta ya mifugo, yanatakiwa kuweka mpango mkakati utakaohusisha mahusiano katika mambo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira. Hivyo basi, sera, mkakati na mipango itayowekwa na Serikali ni lazima ihuishwe kwa kuzingatia masuala ya kijamii, uchumi na mazingira, kwa kuangalia matakwa mazima ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuielewa vizuri Sekta ya Mifugo na wafugaji kwa upana wake, kwanza, inatakiwa kufanya mapitio ya sera zetu kwa nia ya kuziboresha kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wafugaji na kuwa na uelewa sahihi kuhusu wafugaji. Kile kinachohubiriwa na baadhi ya watu kuwa wafugaji ndio waharibifu wa mazingira bila ya kuwa na ushahidi wa kisanyansi *(scientific proof)* ni kutowatendea haki wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunaashuhudia pale Mipango na Mikakati ya Serikali inayohusu wafugaji inaposhindwa kutekelezwa kutokana na kuandaliwa bila kuwahusisha walengwa, wafugaji ndio wanaoanza kulaumiwa kuwa ni watu wasiotaka kubadilika. Kadhalika hii nayo ni kutowatendea haki wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Mipango mingi inatoa miongozo ya makundi makubwa ya mifugo kuwekwa katika eneo moja la malisho kwa kipindi chote cha mwaka.

Hali hii husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na kadhalika wafugaji kupoteza mifugo yao kutokana na ukosefu wa malisho na maji.

Mabadiliko ya hali ya hewa (*ecological changes)* na umuhimu wa wafugaji kuhama hama na athari zake kwa mazingira ni jambo ambalo hadi sasa halieleweki vizuri kwa watunga sera wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema kuwa watunga sera wajitahidi kuelewa hali halisi ilivyo na kuwashirikisha walengwa. Hivyo ni muhimu sana jamii za wafugaji wakashirikishwa katika utunzi na utekelezaji wa sera zinazohusu ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kusema mara kadhaa kuwa wafugaji wamefikishwa hapo walipo kutokana na mipango ya Serikali na sera zake kwa ujumla, mfano: Kwa Serikali kuanzisha na kuendelea kuzipanua Mbuga za Wanyama *(National Parks)* na mapori ya hifadhi *(Game Reserves),* jambo ambalo linazidi kuwaathiri wafugaji katika matumizi ya ardhi na hatima yake ni kuwatenga kabisa na ardhi yao ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Serikali za kupanua kilimo kutoka mashamba madogo *(small scale farming)* kwenda kwenye mashamba makubwa (*large scale or commercial cultivation),* ukulima wa umwagiliaji wa mashamba makubwa na uchimbaji wa madini, umechukua ardhi kubwa sana iliyokuwa inatumiwa na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa, ukaribishwaji wa wawekezaji wakubwa katika sekta nzima za kilimo, maliasili na madini, maana yake ni kusukumiza pembeni jamii za asili za wafugaji katika maeneo hayo na hivyo kusababisha migongano na mifarakano kwenye matumizi ya rasilimali ardhi.

Shughuli hizi zote ambazo zinatokana na sera za serikali, zimepelekea wafugaji kutokumiliki maeneo mazuri ya malisho kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba, migogoro isiyoisha baina ya Wakulima na Wafugaji, inasababishwa zaidi na sera, sheria na mipango ya Serikali ambayo inawapendelea zaidi wanaotumia ardhi kubwa sana na kuwaacha wale wasio na uwezo wa kumiliki maeneo makubwa wakigombana wao kwa wao, yaani wakulima wadogo wadogo na wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri mambo yafuatayo katika kukabiliana na tatizo la migogoro ya matumizi ya ardhi kwa shughuli mbalimbali:-

- Kufanyika mjadala wa kitaifa kutathmini hali ilivyo sasa na hatma ya ufugaji nchini.

- Kuandaa miundombinu ya kutosha kama vile malambo, majosho, malisho na zahanati za mifugo katika maeneo yao ya asili ambayo wafugaji walihama kutokana na ukosefu wa miundombinu hiyo.

- Kadhalika miundombinu kama hiyo iandaliwe ya kutosha katika maeneo mapya yaliyoteuliwa kuhamishia wafugaji ili kunusuru uharibifu wa mazingira.

- Wafugaji waendelee kuelimishwa kuvuna mifugo yao kwa ajili ya kujiletea maendeleo ya kijamii, ikiwa ni pamoja na makazi ya kudumu, elimu, afya na kadhalika. *(Makofi*)

- Wafugaji kupatiwa mikopo ya benki kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa kisasa na kuanzisha kilimo cha mazao chakula na biashara.

- Kuimarisha minada na masoko ya mifugo pamoja na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika mashamba makubwa ya mifugo na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, mwitikio umekuwa ni mdogo sana kutokana na sababu kwamba, hakuna vivutio vya kutosha vya kuweza kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la msingi sasa kwa Serikali kuiwezesha Sekta za Mifugo na Uvuvi kuandaa mazingira mazuri yatayoweza kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa kwamba, uzalishaji wa maziwa nchini umeongezeka. La kusikitisha ni kwamba, usindikaji wa maziwa umeshuka kutoka lita 400,000 hadi lita 60,000 kwa siku.

Kupungua huku kwa usindikaji wa maziwa kunatokana na kufungwa kwa takriban viwanda 16 hapa nchini. Sababu kuu za kufungwa kwa viwanda hivyo ni kutokana na usimamizi mbaya uliopelekea kuzalisha bidhaa hafifu na hivyo kukosa soko.

Sababu nyengine ni pamoja na ukosefu wa mikopo ya benki na masoko ya uhakika.

Kwa upande mwengine viwanda vya kusindika nyama navyo ni vichache, hali inayopelekea kutoitumia vyema fursa ya biashara ya nyama na bidhaa zitokanazo na nyama ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi nchini ni miongoni mwa sekta muhimu katika kukuza uchumi wa kaya na taifa kwa ujumla. Sekta hii imechangia 1.6% ya Pato la Taifa.

Mwaka 2008, Tanzania ilizalisha jumla ya tani 324,800 za mazao ya uvuvi, zenye thamani takriban shilingi bilioni 370. Kati ya mauzo hayo, ukanda wa maji baridi ulichangia tani 281,000 na ukanda wa bahari ulichangia tani 43,000. Aidha, idadi ya wavuvi ilongezeka kutoka 163,000 hadi 170,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya, Sekta ya Uvuvi inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazorejesha nyuma maendeleo ya uvuvi hapa nchini. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na;-

- Uendeshaji wa uvuvi haramu.
- Kuendelea kuwepo uvunaji na matumizi ya rasilimali ya uvuvi isiyo endelevu.
- Ukosefu wa upatikanaji wa mitaji na mikopo kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli za uvuvi.

- Magendo ya samaki kutoka nchi moja kwenda nyingine.

- Wamiliki wa viwanda vya kusindika samaki kuendelea kuvuna samaki wachanga.

- Vikundi vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) havina zana za kutosha na za kisasa za kukabiliana na uharamia wa uvuvi haramu.

- Shughuli za kilimo na ufugaji pamoja na uchafuzi wa taka za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunasoma kupitia vyombo vya habari mbalimbali jinsi ambavyo uvuvi haramu ulivyoshamiri katika mito, maziwa na bahari hapa nchini.

Ni jambo la kusikitisha zaidi pale tunaposikia kwamba, wale ambao wana wajibu mkubwa wa kuisimamia na kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, baadhi yao ndio wanaoiendea kinyume.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja wa hivi karibuni, ulioripotiwa kwenye vyombo vya habari; Diwani wa Kata ya Ngorika Wilayani Simanjiro, Bwana Charles Kagaruki na wenzake 23, wametiwa mbaroni kwa tuhuma za kujihusisha na uvuvi haramu katika Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Vifaa kadhaa vilikamatwa vikiwemo kokoro 176, vimilia 17, vyandarua 35, tani 6.5 za samaki wakiwemo dagaa wasiostahili kuvuliwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi haramu ni tatizo kubwa na sugu ambalo linailetea hasara kubwa nchi yetu. Kambi ya Upinzani, tunalaani sana uendeshaji wa uvuvi haramu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), imeripoti kuwa kutokana na uvuvi haramu, samaki aina ya sangara katika Ziwa Viktoria, wamepungua kutoka tani 790,000 mwaka 2006 hadi tani 227,365 Agosti, 2008.

Utafiti huo umebaini kuwa sangara wanaovuliwa wanakuwa chini ya kiwango kinachotakiwa kuvuliwa, ambacho ni kati ya sentimita 50 - 55. Kiwango cha sangara wanaovuliwa kwa sasa ni kati ya sentimita 30 - 40 tu.

Hali hii haikuiathiri Tanzania pekee, bali kwa ujumla wake, viwanda 10 vya kusindika minofu ya samaki nchini Kenya, Tanzania na Uganda vimefungwa, wakati viwanda vyengine 25 vinazalisha kati ya wastani wa asilimia 30 - 40 ya uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza, hawa wavuvi wanazipata wapi zana wanazotumia kuendesha uvuvi haramu? Ni dhahiri kwamba, kuna mahali wanazipata na kwa hiyo, bado juhudi za kutosha hazijachukuliwa kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kupongezwa pale Serikali inapofanya msako mkali kukamata zana haramu za uvuvi. Kwa upande wa pili, imekuwa ni jambo la kushangaza na kuduwaza, pale serikali inaposhindwa kubaini viwanda na maduka ambayo yanauza zana na vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kufanya ukaguzi wa kina na wa kushtukiza katika viwanda na maduka yanayouza vifaa vya uvuvi na kuwachukulia hatua kali wale wanaoendelea kutengeneza na kuuza vifaa vya uvuvi vilivyopigwa marufuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi haramu unaweza kupigwa vita pale ambapo mbinu mchanganyiko zitatumika kukabiliana na tatizo hilo. Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

- Tafiti za kutosha zifanyike zitazopelekea kujua ni kiasi gani cha rasilimali ya samaki iliyopo ili kuweza kupanga mipango na mikakati endelevu ya uvunaji, utumiaji na uhifadhi wa rasilmali hiyo.

- Kuanzisha na kuimarisha taasisi za kifedha ambazo zitawapatia wavuvi mikopo yenye masharti na riba nafuu.

- Kuanzisha na kuendeleza viwanda vya kusindika samaki, hatua ambayo itapelekea wavuvi kuvuna samaki maalum kwa ajili ya soko na hivyo kupata bei nzuri.

- Sambamba na hilo, ni kuanzisha na kuendeleza ufugaji wa samaki wa aina na kabila tofauti ili kukidhi mahitaji ya soko.

- Kupunguza ukubwa na wingi wa kodi wanazotozwa wavuvi wadogo ili kupata unafuu katika gharama za uvuvi.

- Kuimarisha doria kwa kupatikana vyombo vya kutosha na vya kisasa kukabiliana na uvuvi haramu.

- Sheria na kanuni zilizotungwa kusimamia suala la uvuvi ziwe zinasimamiwa ipasavyo.

- Ili kutoa motisha kwa wavuvi wadogo kuachana na uvuvi haramu, wapewe fursa kubadilisha zana haramu wanazotumia na badala yake wapewe zana za mahususi bila malipo yoyote.
- Kuanzisha na kuendeleza viwanda vya kuzalisha zana na vifaa vya kuvulia hususan ukanda wa bahari ambako kuna kiwanda kimoja tu hadi sasa ambacho hakikidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema kwenye hotuba yetu ya Bajeti Mbadala, kuhusiana na vyanzo vya mapato kutokana na Uvuvi wa Bahari Kuu, naomba

kusisitiza yale ambayo yalisemwa na kuitaka Wizara husika itilie maanani hoja zetu hizo ili kuweza kuongeza mapato ya Serikali na kukuza uchumi wa taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi katika Bahari Kuu ni moja ya maeneo ambayo kama Serikali ingelikuwa makini na kuchukua maamuzi ambayo Kambi ya Upinzani ilipendekeza, mapato ya Serikali yangeliongezeka marudufu kutokana na kusimamia vyema shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani sio tu yanapanua wigo wa ukusanyaji wa mapato, lakini pia yanasaidia kudhibiti uvunaji endelevu wa rasilimali zetu ambapo sasa hazivunwi kwa utaratibu. Aidha ni kweli kuwa, Serikali inashindwa kununua boti yake ya kufanya doria katika Bahari Kuu na tuendelee kutegemea msaada toka kwa wenzetu wa Afrika ya Kusini? Hii ni aibu kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya wavuvi wadogo wadogo hapa nchini ni ya kusikitisha sana, kwani juhudi bado ni ndogo zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha kuwa, wavuvi hawa wanaweza kusaidiwa kupata mitaji ya kuweza kujiendeleza na kupata nyezo na vifaa vya kisasa, kwa ajili ya kukuza shughuli za uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa kina utaona kuwa, badala ya Serikali kuwawezesha Wavuvi hawa wadogo wadogo, kinachoonekana ni kuwawekea vikwazo na kodi nyingi, vinavyopelekea kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua hatua za makusudi kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kama ambavyo tumependekeza hapo juu ili waendelee kujiajiri na kuweza kukuza kipato chao kitokanacho na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mwani, inaendelea kuhamasisha kilimo cha mwani kwa lengo la kuongeza tija na kipato. Kina mama kadhaa wamejiajiri katika kilimo cha mwani, ajira hii ni zuri ikiwa biashara ya mwani itasimamiwa ipasavyo.

Kwa bahati mbaya, wakulima wa zao hili wanakabiliwa na tatizo la soko. Makampuni yanayonunua mwani yamekuwa yanajipangia bei wanazotaka wao, wakulima wa mwani hulipwa bei ndogo sana isiyolingana na bei ya soko la ulimwengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, biashara ya mwani ni huria, lakini Serikali ibebe jukumu la kuwalinda wananchi wake katika suala zima la soko la mwani. Lazima Serikali ihakikishe kwamba, wakulima wa mwani hawadhulumiwi na makampuni yanayonunua mwani na kwamba bei wanazopewa zinakuwa za maslahi na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa shukurani za dhati kwa familia yangu, wakiwemo wake zangu, watoto na familia yangu kwa ujumla, kwa kunipa moyo na kuniunga mkono kwa muda wote, nikifanya shughuli zangu za kuwawakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu.

Nikushukuru wewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti kwa kuliendesha vyema Bunge hili. Aidha, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wananchi kwa ujumla, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuwasilisha. Sasa aache kuwashukuru si wanampikia! (*Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tuna wachangiaji wengi, lakini tutatumia kipindi hiki cha asubuhi na mchana tutatumia saa moja baada ya kuanza kazi halafu tutamwita mtoa hoja. Kwa hiyo, watakaochangia kwa mara ya kwanza hapa ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa John Cheyo nafikiri utafikiwa. Nimemwita huyu kwa sababu katika wote walioandika wanaotoka CCM; ni yeye peke yake, kwa hiyo, ataitwa naye.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo, niweze kuchangia katika suala hili la bajeti ya Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mimi niseme moja kwa moja, nitajikita katika suala la mifugo. Nianze kwa kuwashukuru sana Wananchi wa Kongwa, kwa kuniamini niwe mwakilishi wao katika nyumba hii ya Kitaifa. Niwahakikishie kwamba, kazi hii ngumu waliyonipa naendelea kuifanya kwa uaminifu mkubwa, tuendelee kusaidiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, msaidizi wake, kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya katika Wizara hii mpya. Pongezi hizi ni kwa kuonesha makucha hasa katika eneo la uvuvi, wamefanya kazi nzuri sisi sote ni mashahidi katika uvuvi haramu, tunawaomba kazi hii waendelee nayo. Ushauri wangu wa mwanzo Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yenu ya wataalamu, ikiongozwa na Katibu Mkuu ni kwamba, hebu mwaka unaokuja geukeni kwenye mifugo nako muweke nguvu kubwa kwa kiwango kile kile au zaidi kidogo kama mlivyofanya kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Celina Kombani, kwa sababu kwenye Bunge lililopita hapa tulirumbana kidogo, Waheshimiwa Wabunge na Serikali, kuhusiana na masuala yaliyokuwa yakiendelea ya uhamishaji na operesheni za kuhamisha wafugaji hasa kwenye Wilaya za Kilosa na Mikoa ya Rukwa, ambako kuna dhuluma kubwa ilifanyika na Serikali ikakubaliana nasi na kutoa tamko rasmi hapa Bungeni.

Tunaomba ufuatiliaji wa karibu, kuhusiana na tamko lile bado baadhi ya maeneo wafugaji wananyanyaswa, bado hatuna hakika kama Tume ile ilishamaliza kazi na kwa

hiyo, wamemkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu ile ripoti na kama wameshamkabidhi basi yatokanayo na ripoti hiyo ni yapi na hasa tunatazamia kwamba, wafugaji waliodhulumiwa waweze kufidiwa.

Hapa ninapozungumza, kwenye *gallery* wapo wadau wengi tu wa masuala ya mifugo toka Wilaya zinazozidi 12 Tanzania nzima. Moja ya mambo ambayo wameyafuatilia ni kuona vipi mbona tamko lile na ahadi zile bado kidogo utekelezaji wake hauonekani. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama atapata fursa kesho Jumamosi mchana au jioni au keshokutwa Jumapili, kama atapata fursa akakutana na wadau ili kuweza kuzungumza kidogo, itakuwa ni jambo la faraja kubwa sana kwa wafugaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko changamoto nyingi sana. Leo nilikuwa nasikiliza vyombo vya habari; Madiwani wa Mbarali kwenye Baraza lao la Madiwani walikuwa wanaulizana wakati ule Ihefu, wafugaji wanafukuzwa wafugaji wale walipigwa faini mbalimbali kiasi cha shilingi zaidi ya milioni 200 kwa risiti za Halmashauri, wakati akiwepo DC aliyetoka. Hizi shilingi bilioni 200 zilizotoka kwa wafugaji kwa risiti za Halmashauri senti moja haijulikani iko wapi. Huo ni mfano mmoja tu, tunaomba Serikali ifuatilie mambo haya tukiendelea kuwa na utaratibu ambao una dhuluma dhidi ya aina fulani ya watu wetu, dhuluma zinazofanywa na Maafisa wa Serikali, jambo hili si sawasawa hata kidogo. Katika mambo haya, inaonekana baadhi ya Wakuu wa Wilaya wamehusika na mambo haya, adhabu yao anahamishwa tu anapelekwa mahali pengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa, DC aliyekuwa Kilosa hivi anaendeleaje kuwa Serikalini kwa mambo yaliyofanyika Kilosa, dhuluma kubwa iliyofanyika Kilosa, dhambi kwa Mungu si vizuri! Mtu anaporwa ng'ombe 300, 400 anabakia hana chochote, ushahidi upo baadhi ya Mapolisi wamehusika, baadhi ya vyombo vya ulinzi na usalama lakini hata DC wetu; halafu anahamishwa tu basi! Katika hili naomba Serikali tuwe wakali. Wakati fulani tulipokuwa tunazungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mzee Malecela akasema, jamani hivi mmewahi kuona Mmasai analia, wengi wakasema bado. Yaliyofanyika Kilosa Wazee na Morani wa Kimasai walikuwa wanalia *openly*. Ndugu zangu wa Kimasai ni watu wenye ushujaa mkubwa, unaweza ukamkata mkono na bado akashikilia akaguna tu lakini asitoe machozi. Kwa dhuluma iliyofanyika Kilosa, walikuwa wanalia kama watoto wadogo. Ushahidi upo, hatua zichukuliwe na ni vizuri watu wa Sheria wanasema ili haki itendeke ni vizuri watu wakaiona kwa macho imetendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuhudhuria kikao Kiteto cha Wilaya za Ujirani Mwema na Wilaya ya Kiteto, Simanjiro, Kilosa, Kongwa, Kondoa, Kilindi, Wilaya kama sita hivi na Kiteto yenyewe. Yule aliyekuwa DC Kiteto wakati huo, akitamba kwenye kikao kile namna walivyofanya operesheni ile na akawashawishi wenzake nao wafanye mambo kama yale. Nilisimama pale nikawaambia ni dhambi kabisa, wala hamjatumwa na Serikali kufanya mambo hayo mnayoyafanya ninyi. Kukusanya ng'ombe unaswaga kutumia Polisi wanaweka kwenye eneo *enclosure,* ng'ombe 300 mtu anaambiwa kila ng'ombe mmoja mkumbuke shilingi 30,000, ng'ombe wote wamechukua halafu wanamwambia kila ng'ombe mmoja 30,000; shilingi 30,000

mara ng'ombe 300 ni shilingi ngapi, karibu shilingi milioni 10 azitoe wapi; ng'ombe wake mmechukua halafu mnamdai hela. Dhuluma kubwa ni mbaya sana. *This is not good* na wala Chama cha Mapinduzi, hakijatuma watu wafanye mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, dira ya mifugo ni kwa ng'ombe wachache, dola endelevu watakaosaidia wananchi kiuchumi. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema wazi kwamba, tunataka mifugo ambayo itatusaidia kupunguza umaskini na kuongeza kipato. Katika hilo wakati wa awamu ya tatu, wakati wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, miaka 7 au 8 iliyopita, wako watu hapa kazi yao ni kumkejeli Mheshimiwa Mkapa tu. Mimi nawashangaa sana; Waheshimiwa Wabunge mambo kama haya uwe umetumwa na wananchi wako, usikurupuke tu unakuja Bungeni hapa kurupu kurupu; wananchi wako kweli wamekutuma uje humshutumu Mheshimiwa Mkapa hapa; kwa lipi? Nataka kuwaambia, kama hamjui wananchi watawahukumu.

Wakati wa Mheshimiwa Mkapa, liliitwa kongamano kubwa sana Arusha mwaka 2002/2003, wakati huo Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi alikuwa Mheshimiwa Edward Lowassa. Kongamano kama lile, halijawahi kutokea nafikiri katika historia ya nchi, lilikuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kongamano lile lilikaa kuangalia nini kifanyike katika Sekta ya Mifugo na moja kilichotakiwa kifanyike ni kuboresha mifugo tuliyonayo. Mifugo yetu ni midogo, isiyokuwa na kipato cha maana, maziwa kidogo, ngozi sio bora, tukakubaliana na baadhi yetu tulihudhuria katika kongamano hilo kubwa lilifanyika AICC pale. Profesa Msambichaka, nafikiri ndio aliyekuwa mratibu wa lile kongamano. Waliita wadau wote, wataalamu, watafiti, tukaweka vichwa pamoja tuboreshe mifugo yetu *artificial insemination* kutumia madume bora, itoe mifugo bora zaidi kupata mifugo bora, Wizara mpaka sasa hivi hili bado hatujaliweka sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika maazimio makubwa matano wakati ule mifugo ilikuwa kama kitengo fulani kwenye Wizara ya Kilimo, ikaazimiwa mifugo sasa iwe na Wizara Maalum inayoshughulikia masuala ya mifugo. Leo tunayo Wizara moja ya matokeo ya kongamano lile kuweka sawasawa, Mheshimiwa Mkapa huyo. Tukakubaliana katika mambo matatu makubwa muhimu ni kudhibiti magonjwa ya mifugo katika nchi hii, ndiyo mnaona leo katika malori toka Shinyanga, Dodoma kwenda Dar es Salaam kabla ya hapo ilikuwa ni kuswaga tu kila mahali ni Mheshimiwa Mkapa huyo. Ndiyo na tuendeleze sasa yale mazuri tuliyokubaliana kuhusu *control* ya magonjwa tunaweka ruzuku kiasi fulani kwenye Wizara kwa ajili ya kupambana na magonjwa, lakini bado ni ndogo, tunaiomba Serikali iangalie jambo hili la magonjwa ya mifugo. Hili jambo la magonjwa ya mifugo ndiyo linafanya hata tusiweze kuuza mifugo yetu katika soko la Ulaya, kwa sababu pakitokea ugonjwa fulani hapa tunawekewa karantini na *European Union* tofauti na wenzetu wa Botswana na Namibia, ambao wamejipanga vizuri katika eneo la magonjwa, kwa hiyo wanaweza wakauza mifugo yao kule.

Vile vile tusipoweza kuboresha mifugo yetu tukawa na kuku hawa wa kienyeji, huwezi kuuza kuku wa kienyeji Ulaya, huwezi kuuza nyama ya ng'ombe ya kienyeji Ulaya ni ngumu, hata ukiipika ngumu. Wazungu wanakula kwa uma na kijiko, wanataka nyama laini, wakikata sio mguu wa kuku unakimbia kwenye sahani unatafuta sasa hii huwezi kuuza. Kwa hiyo, lazima mifugo yetu tuibadilishe ifike mahali iendane na soko na kitu kinachotakiwa ni hicho, huwezi kulazimisha hii ya kwetu, tumezoea wenyewe kuvutana na mfupa. Wasukuma, Wanyamwezi hawa ndio kazi yao, lakini tukitaka kuwapelekea Ulaya, lazima mayai yetu ya kuku wa kienyeji huwezi kuuza Ulaya; lingine kubwa, lingine dogo, mtu akila dakika tano tumbo limejaa gesi tupu, mara yai viza; sasa haya mambo Mheshimiwa Magufuli, hebu tuyaangalie tuyaweke sawa ili tupate soko wananchi wetu waweze kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana habari ya kuimarisha masoko, viwanda vya kuchinja, viwanda vya kusindika na viwanda vya maziwa. Nitazungumzia kidogo habari ya maziwa nikipata dakika mbili au tatu hapo mbele.

La mwisho, ilikuwa habari ya umilikishwaji wa ardhi katika yale ambayo tulikubaliana Arusha miaka saba au nane iliyopita wakati wa Mheshimiwa Mkapa kwamba, wafugaji wawe na ari, wapimiwe maeneo wapewe kwa kadiri mtu ana ardhi anayoimiliki yeye mwenyewe, tunabakia na ardhi hizi ambazo ni *communal,* kila mtu anaingiza kwenye eneo lile na idadi yoyote ya ng'ombe alionao na kuongeza; haina tija, lazima tufike mahali ambapo itaeleweka eneo lile la nani ili mtu aweze kuwa na idadi ya mifugo kutegemea na eneo alilonalo apate miundombinu ya maji na kadhalika iweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mahusiano yetu na nchi jirani ya Kenya, kuna makubaliano ambayo yanafanyika kupitia Afrika Mashariki. Mfano, mwaka huu yalikuwepo makubaliano wengine wakasema bajeti yetu tumesema tuondoe VAT kwenye majerikeni, kukusanya maziwa na kadhalika. Hii haitusaidii sana. Wenzetu Kenya ni wajanja sana, bahati nzuri mimi nimewahi kutembelea Mlima Kenya, eneo lile lote nikalizunguka, nikatembelea na Kiwanda kikubwa cha Maziwa Brook Side nikaona *products* zao na wanavyofanya, walivyo na malori ma-*tanker,* sisi kila *tanker* unaloliona Tanzania linabeba dizeli au petroli, Kenya kuna *tanker* za kubeba maziwa. Uchumi ni mkubwa, akina mama wanauza maziwa asubuhi na jioni, hiyo ndio namna ya kuondoa umaskini kwa urahisi. Tukiweza kuwapa wananchi wetu ng'ombe wa kisasa, wakauza maziwa asubuhi na jioni, wanapata fedha leo leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipanda pamba mpaka uweke chini iote, palizi ya kwanza, palizi ya pili. Mzee Cheyo anapiga kelele hapa dawa, sijui kuvuna mpaka miezi minane unachelewa muda. Ukishakuwa na ng'ombe wa maziwa, unakamua asubuhi pesa, jioni pesa, kesho asubuhi pesa, mtoto wa Sekondari unamlipia, wa Chuo Kikuu unamlipia na kadhalika. Familia inaboreka; afya, *protein* na kadhalika. Haya ndiyo mambo ya kuyapa kipaumbele.

Tunaposema Kilimo Kwanza, Mifugo Kwanza pia. Hii ndio inaleta uchumi wa moja kwa moja na wa haraka kabisa. Tulitazame jambo hili na niwatahadharishe tu kwamba, wenzetu Kenya, Waziri wa Fedha ndio mwekezaji mkubwa katika *Brook Side,* ndio *shareholder* mkubwa. Kwa hiyo, tunapofanya mazungumzo ya *East Africa* hapa tusipotazama tutapigwa bao, lazima tuwe macho. Kule wenzetu wale tunaozungumza nao, ndio wawekezaji wenyewe katika mambo haya ya maziwa. Sasa wameanzisha *Brook Side Tanzania Limited,* kitu ambacho ni kizuri, naipongeza Serikali kuibana *Brook Side* iwe na *Branch* Tanzania. Wanapotaka kuingia Tanzania, wajenge viwanda vya maziwa lakini vile vile wenye viwanda vyetu vya Tanzania wanapotaka kuuza Kenya, mikiriti ni mingi; mara ooh maziwa haya leteni *sample*, maziwa haya hayatoshi! Musoma *Diary* wanatoa maziwa safi kabisa, mazuri, *long life.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Amenikumbusha siku moja kule kwetu wageni wametoka Ulaya, kuku wamepikwa ni kuku mzima mzima. Sasa Mzungu ameangalia akaona eeh haiwezekani, ikabidi aachie huko. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi ili niweze kuchangia hii hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Nianzie kwa kuishukuru Serikali yetu, kwa awamu zote nne, kwa kazi zote ambazo wamekuwa wakizifanya na mpaka hapa tulipofikia. Napenda nichukue nafasi ya pekee, kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye mimi namfananisha sawa na Mfalme Daudi wa kwenye biblia. Mfalme Daudi ni mtu ambaye alikuwa mnyenyekevu, mtulivu, msikivu, ambaye alikuwa tayari kurekebisha ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimwia Naibu Spika, lakini pia nikienda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye bajeti hii amehusika katika kuiweka katika sura iliyopo, namwona ni sawa na Nehemia Navigator. Mipango imekaa vizuri, imewaangalia wale ambao wamekuwa wakipata tabu kwa muda mrefu ambao ni wakulima, wafugaji na wavuvi na amerudisha sasa dhana ya uwezeshaji kwa wananchi, ambao wako katika kipato cha chini. Mnara huu tulioamua kuujenga ni mgumu sana, kwa sababu una ugumu katika kupima matokeo yake. Kwa hiyo, kama tumedhamiria kuujenga, basi tusiishie tu katika msingi bali tuhakikishe kwamba, mnara huu unasimama na unaweza kutoa matunda yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na msemaji aliyepita kwamba, suala la unyanyasaji la watu ambao wanafuga, halitavumilika katika nchi hii. Suala la kuwanyanyasa wavuvi pia halivumiliki. Sijawahi kuona tukichukua chakula ambacho kimetokana na nafaka, tusichanganye na nyama au samaki ambao ndio kitoweo, lakini maeneo haya yanapewa uzito ambao bado haujaridhisha. Bajeti iliyotolewa, sawa imeongezeka ukilinganisha na ya mwaka jana, lakini unakuta bajeti za matumizi ukijumlisha na OC, inakuwa ni kubwa kuliko hata ya maendeleo, hasa kwa sekta hii ambayo ilikuwa imesahaulika. Nadhani tutakuwa hatumtendei vyema Bwana Joshua, ambaye ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Huyu Bwana tulimtuma tukasema tunakuundia Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi hebu tuone ita-*perform* vipi. Joshua

amekwenda ametukamatia meli, ame-*confirm* amesema kwamba, jamani kwenye uvuvi kuna rasilimali nyingi, tumeona samaki waliokamatwa. Sasa basi tumuwezeshe ili hiyo asali na maziwa ambayo ameiona kwenye bahari na maziwa, tuweze kuvitumia na kunyanyua uchumi wetu wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika boti ambazo ametupa juzi Mheshimiwa Waziri, tunamshukuru lakini ukisikiliza sana michango mbalimbali inazungumzia boti za doria. Ina maana zitakwenda kuwakamata sasa wale wavuvi, hata kwa yale makokoro waliyokuwa wanayatumia. Kwa hiyo, ina maana tayari kuna tatizo hapo kati ya mvuvi ambaye sasa alikuwa anapata kidogo kwa njia haramu na sasa kuna boti ambayo inamwambia aah ukienda ovyo tunakukamata. Kwa hiyo, ninachoomba kazi yake ni nzuri, ameanza vizuri, lakini tunaomba hivi vitendea kazi vipatikane ili hawa wavuvi wasijikute wanaingia kwenye mtego ambao ulikuwa haujakusudiwa. Wanatamani kuhakikisha kwamba, wanaboresha maisha yao, wanachangia katika Pato la Taifa, lakini watafanikiwa hivyo endapo watawezeshwa. Katika Utawala Bora, kazi kuu ni kuhakikisha kwamba, inatimiza wajibu wake kufikia malengo au matarajio ya wananchi wake. Vile vile madaraka yatumike sawasawa katika kuhakikisha kwamba, rasilimali za nchi zinatumika ipasavyo na utekelezaji pia uwe ni ule wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzungumzia hilo, nilikuwa nasema kwamba, suala la ufisadi ambalo pia sasa hivi tumesema *governance* kwa ujumla wake ni suala mtambuka. Sasa kama ni suala mtambuka, tunategemea kwamba kila Wizara inapozungumzia iseme kwa undani. Kwenye kitabu chako Mheshimiwa Waziri, nimeona umezungumzia suala la rushwa, jinsia na UKIMWI, lakini haijitokezi sana rushwa kwa undani; unachukua hatua zipi kwa sababu kwenye maeneo hayo ndiko ambako kunalalamikiwa?

Tazama sasa hii ambayo imesemwa ng’ombe wameuzwa lakini risiti hazionekani, kwa hiyo haya ni maeneo pia ya kuangalia. Kwa sababu vita dhidi ya ubadhirifu maadili yetu au kwa lugha iliyojitokeza sana sasa hivi, ufisadi hauwezi kukoma, litajipanga tu katika sura mbalimbali na wananchi wamelipokea isipokuwa tu pale tunapokwenda tofauti kidogo. Kwa sababu tuko kwenye *transition stage*, tulianza *in freezing* ile ya kutoa *awareness* na kila mtu kutambua tuna tatizo. Sasa hivi tuko kwenye *transition,* kuna maumivu hatukubali kama kuna makosa ambayo tumekuwa tukiyatenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo maumivu hayo yanatokana na nini? Yanatokana na kwamba, sisi wenyewe kwa namna moja au nyingine tumeshiriki. Kwa hiyo, inakuwa ni ngumu kujitoa katika misingi hiyo na ndiyo maana sasa unakuta kwamba, kwa sababu katika maisha kuna suala la sehemu kuu tunazojifunza kuelimika au kubadilika, *socialisation schools* na sehemu mojawapo ni katika familia, sehemu nyingine ni katika imani zetu, Makanisa na sehemu nyingine katika jamii zetu kama hizi ambazo ni za Kiserikali. Kwa hiyo, nilikuwa nasemea hapo, nikizingatia kwamba katika Wizara hii tunaomba sana suala la ugawaji wa rasilimali ili kuifanya Wizara hii iwe endelevu na tuweze kuona matarajio yake ni muhimu sana. Suala lingine ni kwamba, nilikuwa naomba nisemee kidogo ni jinsi gani sasa Makanisa yamejikuta yakiwajibika kuingia katika sura hii ya kukemea au kusaidia mmonyoko wa maadili ya Watanzania. Kwa kuwa tunapata nafasi ya kuchangia mara moja au katika Wizara maalum, basi

naomba isichukuliwe tu kwamba nahama kwenye uvuvi bali najaribu kujiweka katika misingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi ambao tuna imani ya Kikristo, maana yake imebidi niseme hilo kutokana na mwongozo ambao umezungumziwa sana humu Bungeni. Katika Zaburi ya 15, tunaambiwa kwamba "Watu wanaotwaa fedha zao ili wapate kula riba na wanaotoa rushwa ili wawaangamize wenzao, Mwenyezi Mungu anasema kwamba hatawasamehe." Ni kauli nzito sana. Vile vile tukirudi kwenye hiyo hiyo Zaburi tena inasema kwamba, "Maana tazama wasio haki wamepinda uta wanautia mishale yao katika upote kuwapoteza gizani walio wanyofu wa moyo kama misingi ikiharibika." Kwa hiyo, nadhani haya sasa ndiyo mambo yaliyofanya Makanisa na wenzetu katika imani mbalimbali, waingilie katika kupambana na hili tatizo la mmonyoko wa maadili, hata siku zote mimi naamini walikuwa kidogo wamejisahau.

Ukisema kwamba, sasa unaingia kwenye kupambana na momonyoko wa maadili kama Kanisa, kama hakutakuwa na mwongozo maalum, watu wanaweza wakaitumia vibaya hiyo nafasi. Ndiyo maana, mimi binafsi napongeza kwamba, wamekuwa na misingi na mwongozo ambao utakuwa unaelekeza nini kinatakiwa kufanyika. Vita dhidi ya ufisadi, rushwa kwa ujumla wake sio ya mtu mmoja, sio ya kuonyosheana vidole kwamba, fulani wewe ndiyo fisadi hapana; imeanzia mbali katika misingi yetu iliyomomonyoka.

Kwa hiyo, kwa msingi huo, mimi binafsi niseme kwamba, naomba madhehebu ya dini iwe ni Wakristo au Waislam, wajue kwamba hili tatizo liko kwenye jamii yetu na uongozi ndiyo jambo pekee litakalotusaidia sisi kusimama katika misingi na uongozi. Uongozi unaanzia kwenye chaguzi zetu. Kwa hiyo ni vyema kabisa wakati wa chaguzi zetu, viongozi wetu wahamasishe na kuelimisha jamii ili tunapokuja kwenye uchaguzi, tupate viongozi ambao ni wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisimame sana katika hilo leo, kwa sababu hili ndilo lililofikisha mpaka leo wavuvi wanahangaika, wenye mifugo wanahangaika kwa sababu ya kukosa dhamira na dira ya dhati katika utekelezaji. Haiwezekani mtu anahamishwa katika eneo moja, anaambiwa nenda labda mahali kama Songea; ana ng'ombe 100 anatembea nao. Mnyama sawa ni mnyama, lakini pia kuna nafasi ya kumwonea huruma. Kuna siku nilikuwa natoka Tunduru naelekea Songea, nikakutana na mfugaji akiwa na ng'ombe wawili wamezaa saa hizo hizo na wanalazimika kutembea. Hivi kweli angekuwa mwanadamu asingesikia maumivu? Huyo ng'ombe amuache au aondoke na ndiyo utajiri wake na katika Serikali zetu tumesema tusiwatese wanyama. Kwa nini basi kama kunakuwa na sababu maalum za kuwahamisha wafugaji kwenda eneo fulani wasipangiwe kwanza eneo kwamba watakwenda kukaa mahali Fulani halafu kisha wasaidiwe kupewa usafiri ili kuhamisha hiyo mifugo lakini hatufanyi hivyo?

Wanaambiwa ninyi wenyewe nendeni mtafika mahali Fulani; mtafika vipi havieleweki, matokeo yake mtu akitembea kidogo amechoka, amepata msitu fulani hivi anajua hapa atajificha anakaa hapo hapo; iwe ni kwenye chanzo cha maji, iwe ni kwenye ardhi oevu, yeye anaona bora nikae ilimradi maisha yangu yameendelea. Kwa hiyo,

ndiyo maana basi kuna umuhimu sana wa kuwa na viongozi ambao wanaona mbali. Tuwe na macho yenye dira, tuwe na upeo wa kuwafikiria na wenzetu, tuwe na mikono inayotenda, lakini pia mipango yetu ijikite katika kuwa na maamuzi yenye uharaka na maamuzi yenye kuleta tija kwa watu wote. Bila kufanya hivyo, tutajikuta katika misingi fulani tunasahau watu wa aina nyingine. Katika hilo pia, nitaomba Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, atusaidie basi kupata sensa kamili. Hivi nchi yetu hii, wavuvi idadi yao ni wangapi na wanachukua nafasi gani katika uchumi wa taifa hili kwa namba yao? Mifugo tumesema tu ng'ombe wako kadhaa; je, ni wangapi na wanachukua nafasi gani katika jamii ili tuweze kuwasaidia kwa uzuri zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho katika sekta yako Mheshimiwa Waziri, naomba uweze kuona Wizara hiyo isije ikalemaa kwa sababu una maeneo makuu mawili; mifugo na uvuvi. Sasa unaweza ukajikuta wafanyakazi katika sehemu moja ni wengi na eneo lingine likawa wachache na hisia zangu naamini kwenye uvuvi una wafanyakazi wachache sana pengine ni *unit* ndogo tu. Sasa utajikuta unatembea kilemavu. Ni vyema basi uka-*balance,* uhakikishe hizi sehemu mbili zinakuwa na idadi ya watu wa kutosha na wote wanaweza kuwa na kazi zinazoenda kwa undani, kama ambavyo umeonesha kufanya katika hizi taarifa ulizotupa. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri, nakupongeza sana na Mungu akubariki, uendelee kuwa hivyo hivyo. *Aluta Continua. (Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi*)

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukukuru sana. Naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na kuwapongeza kwa kazi nzuri walioyoifanya, lakini pia nimpongeze Katibu Mkuu na Wataalam katika Wizara hiyo ya Mifugo na Uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tupate uhuru, mifugo haijawahi kupata mtazamo na msukumo wa kutosha kama sekta katika nchi yetu. Kwa sababu hiyo, kila mara mifugo imebebwa na kitu kingine katika ngazi ya sera. Kwa hiyo, ndiyo maana imewahi kuwekwa na Sekta ya Maji, lakini bado maji ikachukua nafasi kubwa zaidi katika kupangiwa fedha, wataalam na kadhalika. Imetokea pia mifugo ikawekwa kama kiraka kwenye Sekta ya Kilimo na hata kwa sasa tunaona pia mifugo inabebwa na uvuvi ama na samaki. Mifugo inalisha nyikani, samaki wako mitoni, ziwani na baharini; sasa hatufahamu watawabebaje hawa mifugo?

**NAIBU SPIKA:** Wote vitoweo. (*Kicheko*)

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kitoweo kama unavyosema na kwa sababu hiyo, nadhani wakati umefika sasa mifugo itazamwe kama sekta muhimu. Zaidi ya asilimia 10 ya watu wanategemea kwa kumudu maisha yao na mahitaji mengine. Pia, mifugo inachangia katika chakula kwa ujumla tukitaka kuiita ni kitoweo.

Kwa upande wa nyama, maziwa na jibini, hivi vyote vinatokana na mifugo lakini haitoshi hata humu ndani utakuta kwamba, mifugo moja kati ya mazao yake kama

mikanda na mikoba tuliyonayo humu na viatu vingi vizuri, hata tunapovaa tunaona kwamba kuna ishara ya mifugo. Kwa hiyo ni sekta moja tunayopaswa kuitazama na kuizingatia katika mipango yetu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo, unaweza ukaona kwamba, kwa sababu ya kutopewa nafasi inayostahili katika uchumi na mipango yetu ardhi inayotumika kwa upande wa mifugo, kila mara inanyofolewa na kutumiwa kwa vitu vingine. Wenzangu wametaja masuala ya Hifadhi za Taifa, lakini pia kilimo kikubwa, ardhi imechukuliwa kutoka kwenye mifugo ikaanza kutumika kwa ajili ya kilimo na sehemu nyingine imetumika kwa ajili ya madini, misitu na kadhalika. Nadhani tukitaka tunufaike na mifugo kama sekta, wakati umefika wa sera kuweka bayana maeneo ya kulishia ni haya na yanajulikana kwa sehemu kubwa, lakini maeneo hayo yakasaidiwa kuwekwa *zones* na kupangiwa na ijulikane kwamba, zao tunalotegemea kupata kutoka katika maeneo hayo ni mazao ya mifugo. Yawe katika sura ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na ngamia katika maeneo mengine. Kwa sababu kwa kufanya hivyo, itakuwa ni rahisi kupanga mipango inayokuwa bora zaidi na inayoweza kutekelezeka, lakini pia tukifanya hivyo tutakuwa tumechangia sana katika kupunguza tatizo zima la migongano na migogoro inayotokana hasa na matumizi yasiyoendana na ardhi na hasa kati ya wakulima na wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo haiwezi kustahimili na haiwezi kustawi bila kuwa na malisho ya kutosha bila kuwa na maji ya kutosha na kwa sasa katika nchi yetu, tatizo la ukame ni kubwa na kwa sababu hiyo, mifugo inahama kutoka katika kila upande kwa kutafuta malisho na maji. Tunapaswa kuona hili kama janga la kitaifa na Wizara ya Mifugo kwa kushirikiana na Wizara nyingine, kuona jinsi ya kuwawezesha wafugaji na mifugo yao haileti ukame, ambao ni tishio kwa watu wengi.

Kwa sababu hiyo, kuna haja ya kutafuta upya maeneo yenye malisho yakapatiwa maji kama programu ya dharura; kwa sababu kwa njia hii, mifugo inaweza ikaendelea kustawi vizuri hadi msimu mwingine wa mvua utakapokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni la muhimu sana, kwa sababu wafugaji wengine wapo pembezoni mwa hifadhi na malisho hayapo kwenye maeneo mengine na maji hayapo, kwa sababu wanyamapori wamekuwa katika maeneo haya. Maeneo ya Simanjiro pembeni mwa Tarangire yanayopakana na Hifadhi ya Serengeti, utakuta malisho mengine yameisha kwa sababu wanyamapori walikuwa katika maeneo haya. Walipomaliza majani na maji, wakarudi katika Hifadhi. Wafugaji na mifugo yao ikabaki mle na kunyimwa ruhusa ya kwenda kuchangia majini katika maeneo haya, pamoja na kwamba wanyama pori pamoja na mifugo ilishirikiana na kumaliza hata malisho katika maeneo haya. Hili linahitaji kutazamwa kwa namna ya pekee. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika bajeti ya sasa; kwa kweli bajeti ni ndogo na imekuwa ndogo kwa miaka yote. Ninaomba wahusika hasa majemedari katika Wizara hii, watumie bajeti hiyo ndogo katika kuweka misingi kwa maana ya sera, kanuni zake na mikakati zaidi ya kutukwamua Sekta ya Mifugo kwa kututoa mahali tulipo na kuiweka katika nafasi nzuri zaidi kwa miaka inayokuja. Hii itafanikiwa kwa kubainisha afya ya mifugo. Afya ya mifugo inapaswa kuboreshwa na haitakuwa rahisi kuiboresha bila

kuzingatia ujengaji na uendeshaji wa *veterinary centre*s, majosho lakini pia kuwaweka wataalam katika maeneo haya ili waweze kushauri wafugaji vizuri na angalau labda mkazo utakapokuwa umewekwa vizuri zaidi na fedha zaidi imepatikana katika bajeti, afya ya mifugo iweze kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji utaongezeka tu endapo malisho yatakazaniwa, maji yatakazaniwa yawepo katika maeneo haya na endepo afya ya mifugo itaboreshwa na elimu kwa wafugaji ikatolewa. Hili lingalitusaidia sana na kama wengine walivyosema, mkakati huo wa Kilimo Kwanza, Mifugo pia iwe katika mkakati huo, kwa sababu kwa njia hii nadhani mifugo itapata umuhimu unaotakiwa ili iweze pia kustawi na kuchangia zaidi katika Pato la Taifa, lakini kubwa kuchangia katika mahitaji yetu ya chakula na mahitaji ya watu wetu katika kupunguza umaskini wao.

Ni kweli kwamba, bajeti ni ndogo, lakini pamoja na udogo huu, sehemu ambazo zingalipaswa kukazaniwa zaidi ni hizo nilizosema za afya ya mifugo, malisho na maji. Pamoja na hayo ni kutazama suala zima la masoko. Ni kweli usipokuwa na namna ya kulipeleka zao sokoni ni tatizo. Miundombinu katika upande huu wa mifugo haipo inayoweza kuwezesha wafugaji kupeleka zao hilo kwenye masoko na kunufaika na mazao yao ya mifugo. Kwa hiyo, ninaomba kwa kupindi kinachokuja, maana MKUKUTA tunao kama utararibu wa kuondosha umaskini katika maeneo yote na labda Wizara ingekazana kuhakikisha masoko ya mifugo yatafufuliwa na yatahuishwa zaidi. Kwa sababu kuna *facilities* nyingi zinazotakiwa, haya masoko yaweze kuendeshwa vizuri, lakini pia wenyeji waweze kunufaika na hayo masoko. *(Makofi*)

Kwa hiyo, kuna miundombinu ya masoko na Sheria nyingine zinazowakwaza na kuwakwamisha wafugaji katika kufikia masoko haya na mifugo hii itazamwe upya ili sheria zote ziwezeshe zaidi na ziwasaidie wafugaji katika kunufaika na mazao yao na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ametoa mpango na ametoa *vision* ya Wizara. Nadhani *vision* hii ikizingatiwa na kukazaniwa, inaweza ikatufikisha mahali pazuri ambapo mwakani tutakapokuwa tunakutana tena, labda kilio hakitakuwa kikubwa badala yake kilio hicho kitakuwa kimepungua kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, wafugaji wengi waliopo hapa, wamekuja kufuatilia zaidi usumbufu wanaoupata katika maeneo mengi na hili limeongelewa. Hili litatupa faraja sana, ikitokea kwamba ahadi zilizotolewa humu katika Bunge lako Tukufu, zitafanyiwa kazi. Ni kweli taarifa tunaambiwa kwamba zimeandaliwa, taarifa hizo zitolewe ili tuone ni nini kilichotokea; matatizo yepi yaliyoibuka; na wale waliohusika wawajibishwe kwa sababu kwa njia hii moja, haki itakuwa imetendeka kwa wale wafugaji ambao wamedhulumiwa, lakini pia hii itatoa faraja kwamba, kila Mtanzania anaweza kupata haki akiwa katika kona yoyote ya nchi. Kwa hiyo, hili litazamwe na lizingatiwe bila kuchukua muda mrefu, kwa sababu tatizo lilikuwa kubwa na kwa ukubwa huo, nadhani majibu yanayostahili yanapaswa kutolewa kwa wakati ili haki ionekane imetendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mchango huo, ninakushukuru na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa nitamwita Mheshimiwa Clemence Lyamba, atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo na kufuatana na muda, Mheshimiwa Ruth Msafiri pia ajiandae.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami leo hii nitoe mchango wangu kwa hoja iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, pamoja na Naibu wake na pia Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Mikumi, kwa imani kubwa na ushauri mkubwa, wanaoendelea kunipa kwa ajili ya kutimiza majukumu mbalimbali waliyonituma. Ninawaahidi kwamba, sitakata tama, pamoja na ukubwa wa Jimbo letu, kutimiza yote na kuyawasilisha yanapotakiwa ili yapate kusikika katika nyanja za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa natoka katika eneo la wakulima ambao wameathirika sana na wafugaji, sina budi nianze kwa kusema, msema kweli ni mpenzi wa Mungu na ukweli ni kwamba, wakulima wamenyanyaswa sana na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi zimezungumzwa hapa, zipo zile za upande wa Serikali kwa kutokutekeleza yale ambayo wangefanya, adha hii wanayopata wakulima ingekuwa ndogo zaidi, lakini zipo nyingine ni mahususi zinawahusu wafugaji wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu jiulize wafugaji katika maeneo ya wakulima walitoka wapi; na kwa nini waliondoka huko? Wamefuata nini katika maeneo ya wakulima? Nafikiri jibu ni wazi kwamba, wametoka kule walikokuwa kwa sababu malisho ya mifugo yao imepungua au imekwisha. Wamekwenda huko walikokwenda bila shaka kwa sababu wameona kuna maeneo ambako kuna malisho yanayofaa kwa mifugo yao. Malisho hayo ni mazao yanayopaswa kuingia katika matumbo ya binadamu au ni mazao yanayopaswa kuingia katika matumbo ya mifugo? Hakuna majani? Hakuna nyasi? Jibu ni kwamba nyasi zipo. Hawana macho kuona mifugo inakwenda kula nyasi au inakwenda kula mazao ya wakulima. Macho wanayo, sasa kwa nini hili litendeke? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema ukweli, chanzo kikubwa cha migogoro ya wakulima na wafugaji unaweza kusema kwa kiasi fulani, kwa baadhi ya wafugaji ni uzembe. Kwa baadhi ya wafugaji ni makusudi tu na hulka ya kutokujali wakulima; kwa sababu tofauti ya nyasi na mazao ni kubwa mno na ni ya wazi. Lakini pia utakuta wafugaji wanawaachia watoto wadogo kuchunga katika maeneo nyeti ya mazao. Majani hayatembei lakini wanyama wanatembea wanapaswa kuchungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kauli hii, nasema kwa ujumla na kwa sababu pengine ya kukosa majosho na mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza, katika maeneo wanakotoka kwa wafugaji ni kweli kwamba, kuna mazingira fulani ambayo Serikali ingepaswa kuwa macho zaidi na kuyaweka ili kusaidia wafugaji waweze kuepuka kulisha mifugo yao katika maeneo ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana mkono kabisa na Wabunge wote waliotilia mkazo suala la Serikali hata kama ni kuchukua *operation* maalum katika mkakati wa kuondoa tatizo la migogoro baina ya wafugaji na wakulima *once and for all*. Wapeni fursa waingie kwenye Ranchi za Taifa, ambazo mpaka sasa bado hazijapangiwa watu kuzimiliki ili kupunguza tatizo ambalo linatutatiza hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yamezungumzwa, lawama zimetolewa za jinsi zoezi la kuhamisha wafugaji lilivyofanyika katika Wilaya ya Kilosa. Mimi ni Diwani katika Baraza la Madiwani Kilosa. Baada ya kubaini kwamba, hali ya ugomvi, vifo na majeruhi imezidi na hali ya ongezeko la mifugo katika Wilaya ya Kilosa na sehemu mbalimbali imekuwa haihimiliki, Baraza la Madiwani Tarehe 27 Oktoba, 2008 liliamua kukaza uzi, kusimamia sheria ndogo za udhibiti wa mifugo. Utaratibu ulioandaliwa ulikuwa ni mzuri na wa kisayansi kabisa katika Wilaya ya Kilosa. Takwimu na sensa imefanyika katika vijiji vyote na *data* zipo. Tume iliyokwenda kuchunguza kule inazo, Mheshimiwa Magufuli alikwenda kule ameona na Mheshimiwa Mwanri alikwenda kule pia anazo *data*. Tunajua katika kila kijiji ni ng'ombe wangapi, kondoo na hata punda; tumefanya utafiti wa kujua *stock units* kwa ajili ya malisho ni kiasi gani kilichopo. Tuna upungufu wa hekta karibu kumi na mbili elfu hizo ni kwa kukidhi mifugo ile tu ambayo ilikuwa ipo na si ile ya ziada iliyoingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira haya, ikabidi kwa kweli hakuna namna yoyote ya kunusuru mazao ya wakulima na kuepuka njaa na *inflation* ambayo mnajua inachangia kiasi kikubwa sana kama chakula kitakuwa haba, ikawa ni lazima tuchukue hatua za kuondosha mifugo ambayo imezidi uwezo wa malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa bahati mbaya sana, penye wengi pana mengi. Pakajitokeza hali kwa taarifa zilizopo, iliyoanza kwa wafugaji wenyewe wajanja, baadhi ambao waliwashawishi watendaji kuteremsha mifugo yao njiani kabla ya kufika kule ambako walipangiwa kwenda kwa kupewa pesa. Ugonjwa huu, kama magonjwa mengine, ukasambaa katika sehemu kadha wa kadha. Viongozi wa ngazi za vijiji walitoa taarifa katika ngazi ya Halmashauri na Chama cha Mapinduzi, ambacho kilikuwa kinafuatilia kwa karibu zoezi hili kwa sababu ni Serikali yake ndiyo ilikuwa inawekwa kwenye kitimoto, wakaungana pamoja kwenda katika maeneo mbalimbali ili kubaini watendaji ambao wamekiuka taratibu zilizowekwa na hivi ninavyoeleza, kuna kesi kama 42 ambazo zipo Mahakamani kabla ya Serikali kusitisha zoezi hili kwa maafisa wale ambao walibainika kwamba wamekiuka taratibu na wamefanya mambo ambayo hayakutegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwa mwonekano wa kirahisi ni kama vile wafugaji wananyanyaswa na wanaonewa, lakini nasema pia pamoja na makosa, upande fulani labda wa Serikali, lakini pia wao binafsi, maana yake hapa tatizo limeanzia katika ngazi ya mtu na mtu; yaani mkulima na mfugaji. Wafugaji wamechangia kwa sehemu kubwa, kutokana na wao kutokuwa waangalifu kudhibiti mifugo yao inayozurura maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, niungane pamoja na baadhi ya Wabunge waliochangia. Ninafikiri wakati umefika, ambapo kwanza Serikali irejee kwenye sheria inayohusu masuala ya mifugo ili hatua zifuatazo zichukuliwe:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tunaiomba Serikali itoe ripoti ya Tume ilizozituma katika maeneo haya haraka iwezekanavyo, kwa sababu hivi sasa tunavyoongea tangu zoezi la kusitisha lilipotolewa, wafugaji wamerudi pale pale katika maeneo yote ya Kilangali, Tindiga, Masanze, Rudewa, Chanzuru, Kimamba na maeneo mengine mengi, tena kwa tambo. Wanawaambia wakulima inaona sisi iliambia ninyi, tumeshinda. Mifugo imekuwa mingi mno na unyanyasaji umekuwa mwingi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi uliopita, mama mmoja alikuwa anafukuza mifugo katika shamba lake, wafugaji walikuja wakamkimbiza yule mama hadi kumvua nguo. Unyanyasaji jinsi ulivyo! Miezi michache ya nyuma, kulikuwa na mkulima ambaye alikuwa anachoma nyasi zake katika shamba anasafisha, akatokea mfugaji mmoja na ng'ombe wake anamwambia kwa nini wewe inachoma hii nyasi chakula ya ng'ombe.

Sasa jamani tuseme nini, wakulima ni watu watulivu na wavumilivu, kwa dhamira ya jinsi wanavyoangalia mazao yao kwa uangalifu kwa kutumia jembe ili mmea ukue. Ndiyo uvumilivu wao ulivyo. Kwa wafugaji; wafugaji wengine wanatembea na fimbo, wengine wanatembea na visu. Ukitishiwa kidogo lazima uogope ni silaha ile, kwa hiyo, wenzetu wana mambo ya kiamri amri, kuchunga ng'ombe maana yake mpige kwa sababu amekwenda hivi au vile, lakini wakulima ni watulivu na wavumilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwapongeze sana wakulima wote katika Mkoa wa Morogoro kwa ujumla, kwa uvumilivu mkubwa ambao wameuonesha, pamoja na matatizo yote ya kuliwa vyakula vyao katika mashamba mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la pili ni kwamba, Serikali isimamie ipasavyo sheria inayohusu mifugo na ikiwezekana iweke vipengele ambavyo vinalazimisha wafugaji wawe na uzio katika maeneo wanayofuga ili kuepusha mifugo kuvuka na kwenda kula mazao ya wakulima. Pia ichukue hatua hata kama ni operesheni, narudia kusema; ifanye operesheni ama sivyo tunaongea Kilimo Kwanza, haitafanikiwa kama tatizo hili la wafugaji halitaondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natofautina na Mheshimiwa mmoja, aliyezungumza kwamba, Kilimo Kwanza ni Mifugo Kwanza hapana; tumbo kwanza, bila tumbo kushiba hamna mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho, ambalo nalipendekeza ni kwamba, Serikali kwa kutumia Wataalam wa vyuo vya Sokoine, *Pasture Management,* watumie kuwashauri Maprofesa na Madaktari ili mifugo iweze kupata chakula katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa John Cheyo na kama nilivyosema, Mheshimiwa Ruth Msafiri atafikiwa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na karibu nyumbani, tumeku-*miss* kwa siku nyingi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! *(Kicheko)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watu wake, kwa kuweka mifugo mbele na ametupatia kitabu kizuri sana. Hongera sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, sijui kama amewahi kukaa siku moja akajiuliza thamani ya ng'ombe milioni 20 alionao, umesema hapa 19, lakini na wengine ambao wamezaliwa jana hujawahesabu; umeshafanya hesabu ukajua thamani ya ng'ombe hawa ni karibu ngapi? Ng'ombe tu peke yake, kwa bei ya sasa ya 250,000/= kwa milioni 20 ni kama trilioni tano, ambayo ni sawa sawa na nusu ya bajeti nzima ya Serikali hii. Huu ndio uzito, hatuzungumzii vitu vidogo vidogo. Mimi naona labda na Watanzania wengi hawajaona, thamani ya mali ambayo tunayo. Ukikutana na mtu ana ng'ombe 1,000 maana yake kwa bei ya sasa, huyu mtu ana zaidi ya bilioni mbili mfukoni amakaa nazo. Ndio maana tunazungumza kumaliza umaskini, huyu mtu ameshajikomboa tayari katika lindi la kuwa yeye ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia ng'ombe maana yake unazungumzia ajira ya watu zaidi ya milioni 10, ndio wanaotegemea ng'ombe. Unapozungumzia ng'ombe, unazungumzia chakula. Dar es Salaam tunakula ng'ombe 1500 karibu kila siku, kwa hiyo, wewe unaposema kwamba, tuwapunguze ng'ombe, lazima utupatie jibu; Watu wa Dar es Salaam watakula kitu gani pamoja na magonjwa mengine watakayopata?

Unapozungumzia ng'ombe, unazungumzia ukulima na ndio maana hapa nataka kusema jambo langu la pili. Hii dhana ya kusema tuna wafugaji na tuna wakulima ni potofu. Hakuna mkulima mzuri ambaye hana ng'ombe. Ukitaka kuwa mkulima utakayepata chakula cha ziada ni lazima uwe na plau. Wasukuma tunalima pamba na tumetajirika na miaka ya 1960 tulikuwa karibu na trekta kila nyumba, ilikuwa ni kwa sababu tulianza kwa kutumia ng'ombe, kwa kutumia plau sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumzia watu wanaojiita sijui *Big Six* kwa chakula, ndugu yangu amesema tumbo kwanza, wewe utalima kiasi gani kwa kutumia jembe la mkono tu bila kutumia ng'ombe? Mimi nasema neema ambayo iliwapata watu wa Kiosa, watu wa Ulanga, watu wa Mpanda na kwingine ni Wasukuma kuhamia kule na kupeleka ng'ombe na ukulima. Tatizo la Wasukuma wanalaumiwa kwa mambo matatu; Msukuma anajua kulima sana, akishalima sana, anauza ile ziada ananunua ng'ombe, akinunua ng'ombe, anaoa sana na anazaa sana. Haya ndiyo matatizo ambayo tunayo na wengi wanapotuzungmzia hapa, wanatuzungumzia kwa sababu vikabila vingine vidogo vidogo, vinaanza kumezwa na Wasukuma kwa sababu Msukuma ni mchapa kazi, ni mfugaji, anajua kufanya hilo jambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii dhana ya kwamba, tuna wafugaji, tuna wakulima, hata rafiki zangu Wamasai, siku hizi nao anakula ugali na kama wanakula ugali wanaupata wapi, sio kwa kununua, Wamasai sasa hivi wanalima.

Kwa hiyo, nataka hii dhana ya kuwatenganisha watu kwamba, mimi nashughulikia wakulima tu, nashughulikia wafugaji tu, naona ni dhana potofu na labda Serikali ikipata hilo jambo kwamba ni thamani na pili, watu wote hawa tunaozungumzia ni mtu mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu; tatizo kubwa tulilonalo ni matumizi ya ardhi. Hapa mimi nimefurahi kwamba, angalau kwa mara ya kwanza, kuna maeneo zaidi ya hekta milioni 1.4. Kitu ambacho Mheshimiwa Waziri, hajaweza kutueleza ni kwamba, watu hawa wataingia katika maeneo haya kwa utaratibu wa namna gani; wanaomba, wanahamia tu, wanahamishwa au namna gani?

Natumaini katika maelezo yako, utatueleza bayana hawa wafugaji ambao wamebanana katika sehemu mbalimbali, wataweza kwenda kule kwa utaratibu gani. Mimi nasema, kwa yote yaliyotokea Ihefu, kwa yote yaliyotokea Kilosa, katika Serikali ya Awamu ya Nne, Wazungu wanasema *this is the blackest spot,* yaani katika mambo mengi ambayo Mheshimiwa Rais amefanya, ametujengea hospitali, ametujengea UDOM, ametujengea barabara, ametujengea *secondary schools*, lakini kwa hili, tumetereza. Mimi nakubaliana na watu wote kwamba, utaratibu ufanywe kuhakikisha hakuna manyanyaso tena na watu wananyanyasika kwa sababu ya *experiments* mbalimbali au majaribio mbalimbali ya Serikali. Kila wakati Serikali zetu tangu mimi nikiwa mdogo (1964), tumejaribu jaribu. 1964 tukaanza *block farms* kule Mwanza, hamisha watu, peleka hapa, bana watu hapa, hamisha wafugaji; haya ndio matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, 1974 tumefanya tena majaribio, weka watu ndani ya vijiji, hamisha watu kwenye makao yao. Zamani watu walikuwa wanajulikana; ana heka zake 20, ana heka zake 40, anafuga, analima, lakini Serikali ikahamisha watu. Kwa hiyo, ikawa ni uholela tu, watu wale ambao sasa tunawaona Mpanda, wengi wamehama kwa sababu ya 1974 walipofukuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijaisha kufanya majaribio. Mara leo tunataka Ruaha yote iwe *Game Park*, hamisha watu, mara leo tunataka Loliondo kule iwe *Game Park*, hamisha watu. Unahamisha unapeleka wapi? Watu wenyewe tumeongezeka, tulikuwa milioni nane tulipopata uhuru na ng'ombe wetu pia wameongezeka, leo tuko milioni 40 na ng'ombe peke yake wako milioni 20. Sasa bila kupanua maeneo watu watakwenda wapi? Kwa hiyo, Serikali inapaswa kuona kwamba, kama inavyoangalia sekta nyingine kwa mfano za kilimo ni lazima tupanuke. Kule nilikozaliwa ni kwa sababu babu yangu aliingia Gambasingu Mwamomose, akafyeka na wengine akatukaribisha ndio tukawa na mahali tunapolima na mahali ambapo tunafuga. Leo tumeingiliwa na ugonjwa wa mazingira. Mazingira tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, siyo kwamba ni ku-*preserve* tu au kuweka tu; ni ku-*manage* mazingira, ndio kitu ambacho tunapaswa kufanya kwa sababu sisi ni binadamu.

Leo kila kitu ni hifadhi, pori hifadhi, wapi hifadhi, watu tunaongezeka, hatupanui maeneo. Tuangalie, tunapaswa kufyeka baadhi ya misitu ili watu waingie mle wachunge na walime. Keshokutwa tutakuwa tunazungumzia hapa kilimo, tunataka kupanua kilimo, *commercial farm*, utaipata wapi ardhi yenyewe usipokubali kwamba lazima twende sehemu fulani fulani kama ni mapori tuanze kupunguza?

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hivyo tu, kwa upande wa Ranchi, Serikali yenyewe ndio imechukua ardhi kubwa sana ya watu. Ukienda hapa Kongwa tu, rafiki yangu Ndugai alikuwa anasema jamani tugawieni, nakubaliana naye kabisa.

Ng'ombe waliomo mle ni wachache, ardhi waliyonayo ni kubwa mno, basi tukatieni baadhi ya sehemu hizo tuchunge, tufuge, kwa hali ambayo ni ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kwamba, kuna mafunzo mengi ambayo yanafanyika, lakini pia tuwafundishe watu wetu, tuwafikishe mahali ambapo wataona kwamba, kama ilivyo Amerika, unaweza ukalima kwa sababu ya ng'ombe, ukalima kwa sababu ya mbuzi, ukalima hata majani. Tufike kule basi, hata hawa watu ambao wanasema mtu ana machapa kwa sababu anakula chakula cha ng'ombe ni kwa sababu hatujafika mahali ambapo mtu anafikiri, kumbe naweza nikalima majani nikamuuzia mfugaji. Tuwafundishe watu wetu kila kitu tunacholima, kina thamani yake na kinaweza kikatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ambayo inaweza kutusaidia, tuweke viwanda. Nimeona hapa; ni kweli Mheshimiwa unataka kuweka kiwanda karibu na Dar es Salaam, lakini hicho hakitoshi, tunataka viwanda katika sehemu zote ambazo kuna wafugaji. Soko la nyama kubwa; Waarabu wanataka nyama, Commoro kama unavyojua, kila siku wanakuja hapa wanachukua ng'ombe wetu, hata sioni kwa nini wanachukua ng'ombe, watu hawa tulipaswa kuwapelekea nyama? Wewe unafahamu kwamba sasa hivi thamani ya ng'ombe ni 230,000/=, lakini ukimgeuza akiwa nyama mara moja anafika karibu 500,000/= kwa kila ng'ombe mmoja. Kwa hiyo, kuna *value added,* ambayo inaweza kupatikana. *So* tujenge viwanda, tujenge machinjio yaliyo mazuri na tuwahamasishe watu kuyatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mambo mengi sana, kuna sheria nyingi ndogo ndogo ambazo zinabana wafugaji. Akipeleka kwenye mnada, mara ukiingia kodi, ukitoka kodi, ukiwa njiani simama, unapeleka hawa ng'ombe. Tuwapende ng'ombe, ng'ombe ni mali. Tusipofanya hivyo, itakuwa kila wakati hawa watu ambao wanafuga, wajiona wao ni wanyonge sana katika Taifa hili. Mimi natoa rai, kama tusipoliangalia hili, binadamu ana hulka ya ubaguzi, hata ndani ya Bunge hili unanza kusikia watu hapa, hawa Wasukuma, hawa Wamasai, hawa wafugaji, ubaguzi ubaguzi! Mtu ukisema leo uwashukuru hawa watu kwamba,ng'ombe ni 250,000/=, tukiwapunguza wakafika milioni moja ng'ombe mmoja, hizo nyama mnazochoma mnadani mtazitoa wapi na mtazinunua kwa bei gani? Fikirieni.

Pameanza kuwa na ubaguzi, mimi nilichukia sana kusikia baadhi ya watu wananyanyaswa Mpanda. Watu wanaambiwa kwamba, wewe ulikuja hapa mwaka gani, anahesabiwa siku, anaambiwa sasa tutakuchaji shilingi 200 kwa kila kichwa kwa siku ambazo umekaa katika sehemu hii. Ukiangalia ni *group* la watu wa kabila fulani. Tukianza ubaguzi kwa kupitia ng'ombe, hapatakalika hapa Tanzania. Hawa watu walio na mizizi ya ubaguzi, nimeshawaangalia huko nyuma, hawa sio Watanzania walioachwa na Nyerere. Nyerere ametuondoshea ubaguzi, Nyerere ametuachia nchi ambayo sisi sote tunaweza kuishi mahali popote, bila kuulizana maswali wewe umetoka wapi. Hakuna mtu anayeuliza unatoka wapi. Ukiniuliza mimi natoka wapi, natoka Tanzania hapa ndio pangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ndugu yangu endelea kuendeleza mifugo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Magufuli, Waziri wa Wizara hii, kwa alivyoiwasilisha hoja yake asubuhi ya leo. Mheshimiwa Magufuli ni miongoni mwa Mawaziri wanaosifika kwa uchapa kazi, kwa ufuatiliaji na kwa kutokuwa na mzaha kwa wale ambao hawafuati taratibu za nchi na taratibu zilizowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapochangia hoja hii asubuhi ya leo, ninachangia kwa kuamini hivyo na nachangia nikiwa na mawazo kwamba, inawezekana katika baadhi ya maeneo na hasa yenye utendaji wa Kiserikali, kuna ujanja na udanganyifu fulani unaotumika na baadhi ya watendaji, kuwapotosha viongozi na hata wakati mwingine kufikia maamuzi ambayo hayako sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyosema hivyo, napenda nitolee mfano katika Ranchi ya Kagoma, ambayo mimi ni Mbunge wa Jimbo linalohusika. Tangu mwaka 2006, nimeleta kilio hiki ndani ya Bunge lako Tukufu, tangu walipokuwepo Mawaziri wote waliotangulia; Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, akaja Mheshimiwa Diallo na hata Waziri aliyepo sasa hivi. Hii si hoja mpya kwamba, naileta katika Bunge hili kwa mara ya kwanza. Nilielezea mgogoro ulijitokeza, baada ya Serikali kuwa imetenga Ranchi ndogo ndogo katika Ranchi ya Kagoma, kwa lengo la kumilikisha wawekezaji wadogo

wadogo, lakini pia wananchi waliokuwepo kuendelea na shughuli zao za maisha na maendeleo kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea nilipoiwasilisha hoja hii mwaka jana katika Bunge lako Tukufu, kumbe kulikuwa tayari kuna kesi. Mheshimiwa Waziri akanijibu kwamba, hawezi kunitolea majibu kwa sababu tayari kuna kesi. Isitoshe nilikuwa nimeshawasilisha hoja hii kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipotutembelea Mkoani Kagera; lakini naye naamini ni tatizo hili hili ambalo lilisababisha asitoe majibu ya moja kwa moja, badala yake nikapewa kazi ya kwenda kuwasiliana na wale waliopelekea kesi Mahakamani waiondoe, kusudi Serikali iweze kupata nafasi ya kutoa majibu juu ya ile Ranchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Block* 17 zinazotajwa kwamba zimetengwa, 16 wamepewa wawekezaji, moja ndiyo waliyopewa wananchi wa vijiji vya Ngenge, Lutolo na Kishuro, ambavyo vimesajiliwa. Sasa wakati nimepewa nafasi ya kwenda kuwaomba hawa watoe kesi Mahakamani, ambao hawajakubali mpaka sasa hivi, lakini tulikuwa bado tunaendelea kuwashawishi kwamba ni vizuri wakatoa kesi Mahakamani ili kuiachia Serikali iweze kufanya maamuzi yake kama ambavyo tulikuwa tumekwisha kuishauri. Katikati hapo kwenye tarehe 26 Oktoba, 2008, ikatumwa Bodi ya NARCO, ambayo na mimi nilibahatika kualikwa, nikashiriki tangu walipofika Mkoani tarehe 25 mpaka tarehe 26 walipokwenda kwenye eneo la Kagoma na kuzungumza na Meneja wa Ranchi ya Kagoma na vile vile kuzungumza na baadhi ya viongozi walioweza kufika kwa sababu walisema hatuwezi kufanya mkutano wa hadhara kwa kuwa suala hili liko Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kilichofanya nizungumze leo kwa masikitiko makubwa sana, nilipozungumza kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 25, nilizungumza hili kwa nia na makusudio ya kwamba, Serikali ijipe muda wa kwenda kuchunguza maoni yangu na kuona kama kweli maneno niliyoyasema yalikuwa ni ya kweli ili siku ya leo wakati Wizara hii inapowasilisha iweze kunipa majibu.

Badala yake, wakati nasikiliza kwa makini hapa, nikasikia katika ukurasa wa 30 wa kitabu hiki kwamba, Kampuni ya NARCO kwa sasa imekamilisha upimaji wa vitalu kwa ajili ya kuwamilikisha wawekezaji wazalendo katika Ranchi mbalimbali. Pia imewezesha upatikanaji wa hati miliki ndogo ndogo za vitalu 91, miongoni mwake ni pamoja na Kagoma vitalu 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kitu ambacho hakikubaliki. Wananchi wameshindwa kuendelea kuiomba Serikali iwape vitalu kusudi wanangoje kesi iishe, lakini Serikali inaendelea na mawasiliano na wale wawekezaji wadogo wadogo mpaka wakapewa barua za tahadhari kwamba, msipokuwa mmejenga ama mmefanya shughuli zinazotakiwa kwa miezi sita tutawafukuza, wakati huku inajua kesi iko Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Meneja wa Ranchi ya Kagoma, tulipokwenda tarehe 26 Oktoba, 2009, alitamka kwamba, hawa walikuwa hawajafanya mambo yafuatayo:-

Akasema wawekezaji hawajatekeleza ahadi zao, hawajafanya walichoahidi, hawana vibanio, hawajachimba mabwawa, hawajajenga nyumba na hawajafanya maendeleo yoyote.  Hapo ni mwezi wa kumi mwaka jana, leo hii mwezi wa saba, unasema tayari wamefanya shughuli hizi na kwa hiyo wamepewa haki ya kumiliki; ni kitu ambacho hakiwezekani!

Mawasiliano hayo waliyopewa yaliyokuwa yanafanyika kati ya NARCO na wawekezaji batili.  Tayari kuna kesi, kulikuwa na sababu ipi ya kuwafanya wawekezaji waendelee kujenga mahali ambapo tayari watu wameshtaki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi yao ni hii hapa, naomba niiwasilishe Bungeni; ni kesi namba 305 ya mwaka 2007, iliyofunguliwa Mahakama Kuu ya Kitengo cha Ardhi Dar es Salaam na kutiwa saini tarehe 19 Desemba, 2007.  Hii nakala niliipata NARCO Makao Makuu, sikuipta nje, wakati nafuatilia kama kweli kuna kesi, wakasema ni hii hapa.  Kwa hiyo, hiki kitu kinajulikana kiko wazi na kesi hii ina mambo mawili mazito; la kwanza, wananchi wanadai kwamba lile ni eneo lao.  La pili, wanadai kwamba, naomba nisome kama ilivyo inasema: *"An order of permanent injunction to restrain the defendant from trespassing on the plaintiff's premises at Ngenge, Lutolo and Kishuro Villages within Muleba District."*  Kwa hiyo, walikuwa wanasema isiendelee shughuli yoyote katika eneo hii ambalo Kagoma walikuwa wamelitoa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, waliomba *Court Injunction Order* ya kuzuia maendeleo yoyote?

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nilizonazo ni kwamba, waliomba *Court Inunction* na ndio sehemu ambayo nimeisoma, kwa sababu ya muda siwezi kuyasoma yote. Sasa kinachoshangaza ni kwamba, hizi shughuli zimeendelea kufanyika wakati tayari kuna *Order* hii na kesi iko Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachopenda kuiomba Serikali ni kwamba, hizi hati izibatilishe, imezitoa kati ya mwezi wa tano na wa sita ndio imezimalizia. Baadhi ya wawekezaji wamekwishabandika vibao kama yule wa namba tatu na ndipo kulipo na maji watu wanapochota, ndio kilipo kisima chao cha jadi. Iko ndani ya Block Namba 3 na Namba 9, wanasema mwananchi yeyote haruhusiwi kufika hapa na ifikapo tarehe 30 Julai, 2009, wananchi wawe wameondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu hiki ni kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima naiomba Serikali iangalie haki za hao wananchi, iwape nafasi kama ambavyo imefanya kwenye Blocks nyingine.  Hili zoezi halikufanyika kwenye Ranchi moja tu ya Kagoma, limefanyika kwenye Ranchi mbalimbali katika nchi hii, lakini wananchi walikuwa wanapewa nafasi, Serikali yao inapewa nafasi, wanapata nafasi na wao ya kutoa mawazo yao.  Kwa kuwa walikuwa wanaishi ndani ya eneo, wakiwapa sasa maendeleo, nani anachukia maendeleo?  Hakuna

mtu anayechukia maendeleo. Uwepo mpango ambao unaweza kutoa haki kwa yeye aliyekuwepo, utoe pia haki kwa huyu ambaye anakuja sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililotokea sote hatukuwa tunalifahamu. Mimi nimekuwa Mbunge tangu mwaka 2000, hivi vijiji vimenipigia kura mwaka 2000 na 2005. Nimekuwa navyo sambamba katika shughuli za maendeleo, lakini sikuwa nafahamu kuwa viko ndani ya Ranchi kwa sababu sikuwa naifahamu mipaka ya Ranchi na hakuna mahali palipokuwa na *demarcation* kwamba hapa Ranchi inaanzia.

Nilikuwa nafahamu jengo la Ranchi lilipo ni mbali kabisa na nilikuwa sijawahi kupatembelea, kwa kuwa nilikuwa nafahamu ni nje ya eneo langu, ni Bukoba Vijijini.

Kwa hiyo, sikuwa napenda kuona kuwa ni Bukoba Vijijini. Kumbe eneo ninaloendelea ambalo wananchi wanaishi lilikuwa ni sehemu ya Ranchi, lina wananchi wanaopata tuseme 10,000 au 11,000, kwa sbabu *population* inaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, katika hili, naiomba Serikali kwamba, iliangalie suala hili na ione kwamba kuna wananchi ambao wana hoja, hoja yao hii izingatiwe, iangaliwe, wapate haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda kuwa na mifugo endelevu katika eneo letu, lakini tunapenda pia na wananchi wasibughudhiwe. Wananchi wamechomewa nyumba, wamepigwa, wanashitakiwa, wanalishiwa mifugo yao kila siku katika mashamba yao, hapo haki ikoje?

Mimi ningetegemea ambacho kingefanyika, Serikali ingekuwa imetuma Kamati ya kwenda kuliangalia suala hili kwa ukaribu, badala ya kuachia tu kwamba, sasa paendelee tu taarifa zinazoletwa kule, taarifa hizi zina mashaka.

Tulikuwa na mashaka mengi juu ya viongozi mbalimbali, ambao walikuwa wanashiriki katika hili kwamba, wengine walikuwa wanatumia njia ambazo sio sahihi na wala hazipendezi mbele za watu na mbele za Mwenyezi Mungu. Kuhakikisha kwamba, haki za wananchi au wanyonge wasio na pesa za kushtaki wala kuhonga, ambao ndio wanapata tabu katika nchi yao, wanaendelea kunyanyaswa katika haki zao.

Unatazama sasa watu wengine eti wanaendelea kuelezea kwamba, hakuna mgogoro Kagoma mpaka zimetolewa hati. Kitengule ambako hakuna mkazi eti bado utaratibu unaendelea.

Toeni hati Kitengule, lakini wahamisheni hawa watu mliowaweka Kagoma muwapeleke Kitengule, hakuna mgogoro. Ranchi ambazo kimsingi zinaweza kubaki pengine kihalali si zaidi ya saba au nane, lakini Ranchi zipatazo sita au saba ni zile ambazo wananchi wanakaa moja kwa moja. Kwa hali hiyo, mimi ninaiomba Serikali, iangalie suala hili na ilichukue kwa taratibu zilizopo, iweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo hati iliyo mezani kwako si pekee ambayo imetolewa na hawa watu. Tatizo la hawa watu walioshtaki Mahakamani, mawazo yao

hayana ushirikiano. Nimewapigia simu, nimewaomba tukutane tuzungumze, hawapendi ushirikiano.

Wamekwishachukua hatua nyingi, wamekwishaandika barua, *Court Injunction* ipo ambayo siyo hii hapa ipo kwa Mkuu wa Mkoa, iko kwa Mkuu wa Wilaya, iko kwa watu wengine, wanasema na mimi walinipa nakala, nilipowaambia naomba nakala mliyobaki nayo.

Yote kwa pamoja yanazuia taratibu za kusaidia wananchi zisifanyike hivyo hivyo inazuia Serikali isifanye hatua nyingine. Mimi nilichokuwa naomba ni kwamba, mgogoro wa hawa walioshtaki, uishe kwanza, ukishamalizika hatua nyingine ziweze kufanyika. Isiwe sasa hawa wanaendelea kuendeleza mpaka wanapewa hati wakati wengine wanalalamika, huku wanawapiga, wanawafukuza na wanalalamika.

Sasa inaonekana Serikali yenyewe iko *clear*, taratibu zake zinakwenda, inafanya jinsi inavyoona ilikuwa imepanga. Wananchi watalalamikia wapi ama sivyo tufungue kesi nyingine sasa ya kukataa haya yaliyofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba suala hili lipewe majibu na liishe, kwa taratibu ambazo zitatoa haki kwa pande zote mbili. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kutumia muda mfupi. Suala hili nadhani Serikali imelipata na sisi karatasi tutaisoma na tutaipeleka kunakohusika, tuone inaeleza nini.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tukirudi jioni tutaweza kuwa na wachangiaji wanne tu, ambao ni Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Teddy Kassella-Bantu, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia. Hawa wanne ndiyo watakaochangia jioni, halafu tunamwita mtoa hoja na Naibu wake kwa dakika 45, basi itakuwa muda wetu umeisha.

Wakati asubuhi natambulisha wageni, tulikuwa na wageni wengine, nadhani kutoka na nafasi ilikuwa finyu hapo juu walikuwa huko *basement*. Wageni hawa ambao awali hawakupata nafasi ni wageni wa Mheshimiwa Magalle Shibuda na wageni wa Chama cha Wabunge wanaotoka maeneo ya wafugaji. Jumla yao ni 46 na wanatoka Wilaya 18 za wafugaji, ambazo ni kama ifuatavyo: Mpanda, Nkasi, Sumbawanga Vijijini, Kilosa, Ulanga, Mvomero, Sikonge, Rufiji, Kisarawe, Maswa, Urambo, Nzega, Ngorongoro, Same, Babati, Longodo, Simanjiro na Kiteto. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wanawataarifu kuwa, hawa ni wadau muhimu sana kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na wanaongozwa na Ndugu Mika Kasundwa Marwa. Naomba asimame kama yupo huyo kiongozi niliyemtaja, siyo wote. Namuhitaji Ndugu Mika Kasundwa Marwa, ndiye yupi? Hayupo! Basi tumewatambua wote hao.

Yeye ni Mwenyekiti wa Wafugaji Mpanda na pia ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya. Halafu tuna jumla ya wanafunzi 50 kutoka Chuo cha *Assemblies of God* kilichopo hapa Dodoma. Naomba wasimame walipo. Karibuni sana.

Asubuhi *gallery* yetu ilikuwa na watu wengi, kwa hiyo, mlikosa nafasi. Tunawashukuru sana, endeleeni kuliombea Taifa, tuwe na umoja, amani na upendo. Ahsanteni sana.

Baada ya kusema hayo, Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi, wana kikao sasa hivi na wanachama wengine wa Chama cha Mapinduzi humu ndani watakuwa na kikao baada ya kuahirisha kikao jioni. Kamati ya Uongozi ni sasa.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge asubuhi, niliwataja wafuatao kwamba wangepata nafasi, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, nadhani kwa muda wa saa moja, hawa wanatosha, Mheshimiwa Laizer!

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Jana Wabunge wenzangu walichangia na walipokuwa wakichangia, walikuwa wanamtajataja sana Rais wetu mstaafu. Mimi nitofautiane nao kidogo, niseme kwamba, Rais mstaafu katika Jimbo langu, mtu akimtaja vibaya, kwa kweli atapata ngeu *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Wilaya ya Longido inaitwa sasa Wilaya ya Longido kwa ajili yake, yeye ndiye ametupa Wilaya na hakuna maendeleo makubwa tuliyowahi kupata kama tulipopata Wilaya. Kwa hiyo, sisi pamoja na wapiga kura wangu tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niingie moja kwa moja kuchangia Wizara hii na mimi sana sana niguse wafugaji. Kipindi hiki kumetokea ukame, hususani katika Jimbo langu, mifugo katika Jimbo langu wamehama wako Ngorongoro, Monduli, Simanjiro, hakuna tena mifugo katika Jimbo langu na wachache waliobaki, wamekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo tulikohamia kuna unyanyasaji mkubwa sana hasa eneo la Ngorongoro. Eneo la Ngorongoro ni Hifadhi lakini kuna watu wanaoishi humo na wanaoishi ni ndugu zetu, kwa hiyo, tulivyopata janga la ukame tulikimbia, baadhi ya watu walikimbia kwao, hawakutoa maboma walikwenda ndani ya maboma ya ndugu zao lakini nashangaa wanafukuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza wafugaji wamekwenda Ngorongoro, tangu tuzaliwe na mababu na mababu hawajawahi kwenda huko. Sasa naiomba Serikali waone hali hii kwamba hali hii ni ngumu sana kwa wafugaji. Hivi jamani ukifukuzwa na simba, uingie kwa jirani halafu jirani akufukuze kwamba ondoka hivi, utaondoka na simba yuko hapo nje? Kwa hiyo na sisi tulipokimbilia kwa ndugu zetu kilichotupeleka huko, ni ukame. Kwa hiyo, tunapoambiwa ondokeni ni vigumu sana kuondoka. Utang'ag'ania, utashika kila kilichoko humo ndani, usitoke. Kwa hiyo, Serikali inapotaka kutuondoa, kwa kweli ni kama huyo simba tu, tunafukuzwa twende nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mtikisiko wa hali ya uchumi. Rais wetu alitueleza vizuri sana na Serikali ilifanya kila juhudi kutafuata fedha kuwasaidia wakulima. Imetafuta fedha kuwasaidia wakulima ambao hawakuuza mazao yao, imetafuta fedha kuwasaidia wafanyabiashara ambao wamenunua mazao na hawakuuza, imetafuta fedha kuwasaidia wafanyabiashara ambao wamekopa mabenki, Serikali ikasaidia tena fedha kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara wa madini. Serikali ilitafuata tena fedha kuwasaiadia wenye viwanda lakini naomba Serikali ikumbuke hili, katika misaada hiyo yote kusaidia killimo, imesahau wafugaji, wafugaji hawakusaidiwa, hivi mifugo wanapokufa na wafugaji kubaki maskini kwa nini Serikali isiwaone huruma, kwamba nao wako kwenye hali ngumu wasaidiwe kama watu wengine wa Tanzania wanavyosaidiwa? Wafugaji katika nchi hii wamekata tamaa. Wafugaji wanajiona kama wamenyanyaswa, wafugaji wamejiona kama wao sio Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo nitoe kilio cha waafugaji. Sisi Wabunge tuko hapa na tumetumwa na wananchi, sisi ndio sauti ya wananchi. Wananchi wote hawawezi kuja hapa Bungeni kusema matatizo yao lakini wametuchagua Wabunge mmoja mmoja kwa kila Jimbo kuwakilisha matatizo yao na mimi nawakilisha matatizo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu, wafugaji wamenyanyaswa kupita kiasi. Hivi ukinyang'anywa mifugo 400 uliyonayo ikauzwa, ukabaki maskini, ni sheria gani hiyo? Hata wangepelekwa Mahakamani, hakuna Mahakama inayomfilisi mtu ikasema kwamba ng'ombe wote 400 na mbuzi wote ulio nao ufilisiwe, hakuna Mahakama inayosema kitu kama hicho. Lakini nchi hii wafugaji wamefilisiwa na hakuna hatua iliyochukuliwa, naomba Serikali ione jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika milioni 40 ya wananchi wa nchi hii wafugaji nao wamo. Kinachonisikitisha ni swali linaloulizwa kwamba hivi wametoka wapi? Leo Mbunge mmoja amerudia kuuliza kwamba wametoka wapi. Kwanza yeye mwenyewe ajiulize yeye katoka wapi? Tumetoka Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, una shamba pale Kongwa, hivi mtu akikuuliza umetoka wapi, utamuelewa? Unakutakia nini nilikotoka? Kule kwetu tuna Wasafa kutoka Mbeya 5,000, Mheshimiwa Mwanri angekuwa hapa angesema, walikuwa kwenye msitu wa Rongai, Serikali ilipowatoa, hawakuwaambia waende Mbeya, walipewa eneo, tena

eneo walilopewa wako pamoja na wafugaji wa Jimbo langu. Kwa hiyo, ni kijiji kati ya vijiji vilivyoombwa. Hawa Wasafa wanakaa pamoja na wafugaji na kule Kaskazini katika Majimbo yetu, haijawahi kutokea vita vya wakulima na wafugaji. Mbona hamjiulizi ni kwa nini Kilosa tu? Kwa nini Mpanda tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tukisema waondoeni wakulima wote ambao wamehamia Kiteto, Simanjiro, Monduli, Longido, Loliondo, kwamba rudini mlikotoka ili na sisi turudi katika maeneo hayo, inawezekana? Kwa nini iwe Mmasai, Msukuma ndiye anaambiwa arudi alikotoka? Huu ni ukiukwaji wa Katiba na Haki za Binadamu. Tuna haki ya kiushi popote kama Katiba inavyosema. Wafugaji wakivunja Sheria, wapelekeni Mahakamani lakini sio kusema warudi walikotoka, tukiangalia sana tulikotoka, sisi tumetoka Serengeti, Ngorongoro, Manyara National Park, Tarangire, Mashamba ya *West* Kilimanjaro mpaka Kia, turudi huko tulikotoka?

Mheshimiwa Naibu Spika, nijaribu kupunguza jazba lakini hili tatizo la unyanyasaji halinifanyi nipunguze jazba. Kuna wafadhilli wanaotafutiwa maeneo, hii *Land Bank* ni kwa ajili ya wafadhili, hivi mmewatafutia kwanza wafugaji mpaka unamkumbuka mfadhili ambaye humjui jina, atakuja lini, umewatafutia wafugaji? Kuna *data* zingine zilizosomwa na Waziri sina hakika na hizo *data* lakini Mheshimiwa Magufuli anajua sana ku-*keep data* lakini *Land Bank* ni kwa ajili ya wawekezaji, naomba kwanza waangaliwe wafugaji ambao hawana maeneo, wanaorandaranda, wanaofukuzwa kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nilisema nilipochangia hotuba ya bajeti, hakuna Wizara inayoitwa Wizara ya Mifugo, hakuna. Huwezi ukatenga mifugo na majosho, majosho hayako kwenye Wizara ya Mifugo! Huwezi ukatenga mabwawa na mifugo! Siwezi kwenda kumuuliza Mheshimiwa Magufuli fedha za majosho, kwanza hana fedha, fedha iliyopo ni ya matumizi sijui ya nini? Ukiangalia shilingi bilioni tatu kwa ajili ya madawa, sensa na utafiti wa magonjwa, ndio vitu vilivyopo katika Wizara ya Mifugo ambapo madawa yenyewe hata utaratibu bado haujawekwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo nataka kulisemea ni magonjwa yanayomaliza mifugo kama *ECF*. *ECF* ina dawa lakini ni ghali, sio kila mfugaji anaweza kununua dawa hii. Jamani kama mnatoa ruzuku kwa mabilioni kwa wakulima kwa kununua mbolea hebu na sisi mtugawie hayo mabilioni tununue madawa ya *ECF*. Mnakataa tusinunue madawa ya mifugo inayokufa kila siku, kitu mnachosema, punguza mifugo, punguza mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie jamani sio kila mahali mifugo inaweza kuishi. Kwa hiyo mlipowaambia wafugaji waende Lindi, waende Mtwara, sio kila mahali mifugo inaweza kuishi, hali ya hewa inatofautiana kabisa na ndio maana hata Nyumbu hawako kule Kusini, hata Pundamlia hawapo kule Kusini, ndivyo na mifugo ilivyo. Mimi siwezi nikawapeleka ng’ombe wangu Kusini kwa sababu malisho yaliyoko pale, ni tofauti kabisa na malisho yaliyoko kwetu! Hata wanyama ndivyo walivyo. Tanzania sasa ukimtafuta Swalatwiga, anapatikana Longido tu, pamoja na ukubwa wa Tanzania, kwa

nini wasiwepo maeneo mengine? Kwa hiyo, msitulazimishe kutupeleka maeneo ambayo mifugo haistahili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe angalizo moja, zamani kwenye ramani tulipokuwa wadogo tukiwa shuleni, kuna ile Maasai *Step,* inatoka kule Longido, Ngorongoro kule, Loliondo mpaka karibu na Kongwa hapa, hivi bado ni Wamasai tu ndio wako kwenye ile Maasai *Step?* Kwa nini ni nongwa mfugaji Mmasai kuonekana katika maeneo mengine wakati eneo lao limevamiwa na wakulima, limewekwa hifadhi na kila kitu lakini akionekana sehemu nyingine, anaambiwa hutakiwi kuonekana hapa. Naomba hilo lifutwe kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu wetu yuko hapa, nilisema kabla hajaja kwamba hali ya wafugaji katika Jimbo langu, ni mbaya sana. Ukame kutoka Jimboni kwangu mpaka Kenya nzima, hali ni mbaya, mifugo imekufa imeisha. Ni ajabu mifugo iangamie huku malisho yapo kwenye hifadhi zetu. Hawa wanyama tunashirikiana malisho kila wakati inakuwaje leo sisi hatuna malisho tukaambiwa kwamba hakuna hata kumegewa kaeneo katika maeneo haya ya hifadhi ili mifugo iishi? Hivi inawezekana Serikali ikawalisha hawa wafugaji wote mifugo ikiisha? Inawezekana kweli? Kwa hiyo, ni afadhali kuokoa mifugo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA–BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Kwa sababu ni mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo na nimezungushwa na Wizara hii sehemu mbalimbali zinazoshughulika na Uvuvi na Mifugo na nimeona faida ya kupata utajiri wa mtu mmoja mmoja na utajiri wa Taifa kutokana na vitoweo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda ndani kabisa, labda nizungumzie kidogo kuhusu wafugaji kwa sababu na mimi kwenye jimbo langu la Bukene, wafugaji wako na wakulima nao pia wapo. Lakini kule kwangu waliniuliza, sasa mama tunafanyaje na wafugaji hawa, wanaoacha ng’ombe zao au mifugo yao kuja kula mazao ya mashamba yetu? Mimi nikasema, nafikiri suluhisho hapa ni sisi wenyewe kuchanga hela tuwaite watu wa Ardhi watupimie, watuwekee mipaka, shamba la mkulima mwisho wake hapa na mfugaji mwisho wake hapa na njia ya kupitisha mazao pamoja na mifugo ionekane kwa sasbabu Katiba inasema uhuru wa mtu unaisha pale unapoanza uhuru wa mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia hapa tunavyohangaika na wafugaji, tunavyohangaika na wakulima mpaka wanafika wanaumizana, nafikiri suluhisho ni utaratibu wa kugawana maeneo. Kwa hiyo, naishauri Serikali igawe maeneo ya wakulima na waweke fensi na wafugaji wasiwe wanatembea tena, kila mtu apate hati yake, mfugaji apate hati yake, ajue anafuga hapa, analima majani kwa ajili ya ng’ombe zake na kadhalika na hii inawezekana na tutakwenda kwenye ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wengi wamekwenda nchi za nje, hata mimi nimekwenda safari moja Sweden, tulikwenda kwenye semina moja ya *Democracy and Good Governance.* Lakini tukaulizwa, mnataka kutembelea nini? Tukasema tunataka

kutembelea wakulima. Tukaenda kuona wakulima *(settlers),* wanagawa mashamba yao na mifugo, inaonekana kabisa huku ni mifugo na huku ni kilimo, hawaingiliani na hakuna sababu ya kugombana. Kwa hiyo, natoa ombi langu hilo kwamba Serikali iwasaidie wananchi wetu kuwalipia Hati Miliki na na hata ikiwezekana walipe kidogo kidogo ili mradi wajue hapa ni kwangu, nikiondoka mimi ni mali ya watoto wangu, wakiondoka watoto, ni mali ya wajukuu zangu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende mbele kwenye vitoweo. Kwanza, kabla sijaingia kwenye Kamati nilikuwa nafikiri kwamba samaki wanaweza kuwekwa tu kwenye bahari au mito lakini nimeona samaki wanawekwa kwenye kitalu kama yale majaruba ya mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilisema kule kwangu Bukene kuna bwawa ambalo Marehemu Dr. Mwasela, Daktari wa kwanza Muafrika, aliyekuwa Daktari wa Nzega alikwenda kupiga bata pale, akatitia na akafa pale pale. *Historically,* tunatakiwa kulikumbuka bwawa hilo na hawa *World Vision* walishatengeneza mambo ya samaki na mimi nilizungumza na Mkuu wa Kituo cha *Research,* akaniambia kuwa atakwenda kuangalia ili aweze kusaidia, kwa hiyo, nakumbushia lile bwawa liwekwe vizuri ili tuweze kupata samaki kama kitoweo na kama ajira kwa vijana na akina mama ili waweze kuuza pale Bukene na sehemu zingine na kujipatia chochote na hivyo kuondokana na umasikini. Yale majaruba yaani vitalu (mimi naita majaruba kwani yanafanana kama majaruba ya mpunga), yanaweza kuwekwa pote sio lazima Bukene tu, Tanzania nzima tunaweza kufanya hicho kitu. Kwa hiyo, nawaomba Maafisa Samaki wasikae mezani, wapeleke elimu hii kwa wananchi vijijini ili waweze kuweka mabwawa ya samaki, ili vijana na akina mama wapate ajira na vilevile chakula yaani lishe na *protein* kama wanavyosema, ili tuweze kuwa na raia walio na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza la samaki nakuja kwenye ng’ombe. Ng’ombe ana vitu vingi sana na sisi hatuna sababu ya kuwa maskini. Kwanza ukiangalia ngozi yake, tukisema tutengeneze viatu na tuwaambie Shule zote za Msingi au za Sekondari wanunue viatu vilivyotengenezwa kwa ngozi ya Tanzania, watanunua na hivyo tutapata pato kwa ajili ya viwanda vya ngozi na vile vile pato kwa ajili ya Tanzania nzima na pato kwa wafugaji. Unaweza ukatengeneza *handbags* na vitu vingine. Kwato unaweza kutengeneza shanga, hereni na kadhalika, yote ni pesa tupu ila tuwe wabunifu na tuanze kubadilika kifikra na kuthamini vitu vyetu vya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye maziwa. Tunakasumba ya kufikiria kununua maziwa kutoka nchi za nje na tunasahau kwamba sisi tuna maziwa mengi zaidi kwa sababu tuna ng’ombe wengi zaidi katika Afrika. Sisi Tanzania ni nchi ya tatu kwa mifugo, kwa hiyo na maziwa yapo mengi, lakini sasa tunashindwa kujua kwamba ng’ombe huyu wa maziwa atatuondoaje katika umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, ukiwa na ng’ombe kumi (10) wa maziwa, kila ng’ombe akikupa lita tano (5) na kila lita unauza shilingi mia tatu (Sh.300) maana yake unapata shilingi 15, 000 kwa siku, ni kipato kikubwa sana. Halafu ukizidisha mara siku 30 maana yake kwa mwezi unapata shilingi laki nne na nusu (Sh.450,000), hilo ni

pato kubwa. Kama unafugia mjini, unaleta na ajira kama ya watu watatu au wanne, wa kwanza atakuwa yule Mkata Majani, ni ajira itakuwa imepatikana kwa yule kijana halafu mwingine wa Kuchunga, wa Kukamua na Dereva wa kupeleka maziwa kiwandani, kwa hiyo, tunatoa ajira na kila mtu anapata kitu chake. Kwa jinsi hiyo, tunaondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maziwa kama ya  Tanga *Fresh,* wale wanapata hela nyingi laki moja, milioni moja, kwa hiyo, wale na viwanda vingine vinaweza kuajiri kama watu laki tano sabini na saba elfu kwa miaka kumi, nashauri tujitahidi kuvifufua viwanda vyetu  na kuhakikisha kwamba tunavipa nguvu. Tunavipa nguvu namna gani? Ni kuhakikisha kwamba yale maziwa yanayotoka nchi za nje, tunayachaji kodi na maziwa yetu ya ndani tusiyachaji kodi, kwa hiyo, atakayetaka kununua maziwa ya nje basi ananunua kwa bei ya juu na yule anayetaka kununua maziwa ya kwetu, ananunue kwa bei ya chini, hapo tutasukuma maziwa yetu na tuwe *proud* yaani tujivunie mali yetu, tujivunie maziwa yetu ili tuweze kupata pesa na kuondokana na umaskini.

Mhesheshimiwa Naibu Spika, kwenye maziwa kuna *packing material. Packing material,* juzi hapa tulikuwa tunazungumzia mazingira, tulikuwa tunasema kuwa *plastic* zipigwe marufuku lakini zile *packing material* za maziwa zinakubalika duniani, zile zinazokuwa na 60ml, nzito zaidi kuliko zile ndogo ndogo. Kwa hiyo, tusichanganye, tuwaruhusu waendelee kama dunia nzima inavyotumia *packing material* hizo kwenye maziwa mradi iwe ile 60ml au 80ml ili waweze kupaki (kufunga) maziwa, tunywe sisi wenyewe na mengine tupeleke nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mteja wa kwanza awe ni mtoto wa shule. Tupeleke maziwa kwenye shule zetu ili watoto waweze kunywa maziwa. Mimi nakumbuka nilipokuwa nasoma *Tabora Girls,* kila siku saa nne tulikuwa tunakunywa maziwa lakini siku hizi unywaji wa maziwa umeshuka, zimetajwa hapo shule ni chache tu. Naomba turudishe *system* hiyo, watoto wa chekechea wanywe maziwa, watoto wa shule za msingi wanywe maziwa, watoto wa *High Schools* na wote kwa ujumla tunywe maziwa. Hata sisi watu wazima, maziwa, ni chakula, maziwa ni lishe, tubadilike, tuwe watu wa siku za sasa, wa leo, wa maendeleo na ufugaji wa ng’ombe wa maziwa, sio ng’ombe wengi, kumi au ishirini kwa mfano wanatosha. Kwa hiyo, tubadilishe yale mawazo yetu ili tuweze kufanya kitu, tunazalisha lakini kwa faida ya kwetu sisi wenyewe na watoto wetu na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile na zile *packing material* tunaweza kufanya *recycling.* Kampuni moja inaweza kusema zile *packet* badala ya kuzitupa ovyo unaenda kuiuza, kwa hiyo, watu watayakusanya yale yote. Kama wakati mmoja walikuwa wanasema chupa za bia au vizibo vya bia vinauzwa basi *promotion* ya namna ile iwepo kwa makusudi ili zile *packing material* ziweze kurudi kwa ajili ya r*ecycling* na kurudi tena kwenye mzunguko na kadhalika. Vilevile katika mabasi na hata daladala, tuwalazimishe waweke vikapu vya kuweka takataka. Tuanze kuanzia kwa watoto wadogo ili wanapokuwa watu wazima wanajua usafi, wanajua kuweka vitu katika usafi sio kutupa hovyo tu kama tunavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tukifanya hivyo, tutabadilika, tutakuwa matajiri, tutafurahi, tutakuwa hatuna chuki na kugombana kwa ajili ya ardhi, hatutagombana na wafugaji kwa sababu wakulima nao tunawahitaji bila kutengeneza chakula hapa, wakitugomea tutakula nini? Hivi unaweza kufanya kazi bila chakula? Haiwezekani! Kwa hiyo, wote tunawahitaji na Katiba inatuambia tuvumiliane lazima ujue mwisho wa uhuru wako kabla ya kuanza uhuru mwingine yaani ujue mwanzo na mwisho wa uhuru wako na mwanzo wa uhuru wa mwenzio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye mambo ya makusudi kabisa kuwagawia maeneo na maeneo haya yapimwe na yakishapimwa sasa na ndugu zangu tusiondoke maana tumeshapata hati, mimi nafikiri hakuna atakaye ndoka, wewe umeshapewa hati yako ya miaka 99, unaondoka unakwenda wapi? Lazima ulime majani ya ng'ombe wako kadri wanavyowahitaji na lazima kama ni maziwa au nyama, uyalete hapa machinjioni, kiko kiwanda pale machinjioni, unachinja ng'ombe wako, unauza, zinakwenda nyama kama nyama nchi za nje na nyingine tunakula hapa, yote hayo ni pesa. Kwa hiyo, tukiiweka vizuri Wizara hii hatuna sababu ya kuwa maskini na kwa kweli Mheshimiwa kaka yangu, Mheshimiwa Magufuli pamoja na Naibu wake, Kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Wanyancha, ni wachapa kazi, najua kabisa hatuwezi kurudi kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia kuna Chuo cha Mbegani ambacho kinafundisha wataalam Mabingwa wa Meli, nchi zingine wanakuja, wanasoma pale, lakini kwetu sisi wako wachache na kile chuo ni kidogo sana lakini wanaokuja kusoma pale wakitoka wakienda nchi zingine au wale Watanzania waliosoma pale wakiajiriwa na mashirika mengine ya meli vilevile wanaajiriwa kwa mishahara mikubwa sana kuliko wale wanaofundisha pale. Naomba Serikali iwatazame hao Walimu wanaowafundisha na wenyewe angalau wawe wanafanana na wale wataalamu wanaokwenda kufundishwa pale na kuingia kwenye mashirika mengine ya kimataifa ya meli, wapate mishahara mikubwa na vile vile wapanue kituo kile ili waweze kuongeza wanafunzi wengi zaidi na Watanzania waingie wengi zaidi wasome, pale ili tuweze kupata wataalamu wengi. Halafu na ile boti itengenezwe kila mara ili wanapoanza kufanya mafunzo ya kwenda baharini, waweze kwenda na wasikwame kwa sababu wanafundishwa tu *theory* bila *practical,* hivyo kila siku meli iwe katika *order* ili waweze kufanya *practical*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia kwa mia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia ajiandae

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Ngorongoro ambao nina hakika saa hizi wanatusikiliza, kwa kujua kwamba leo bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo inawasilishwa katika Bunge lako Tukufu, kama

kawaida, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yetu Mheshimiwa Magufuli, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ambaye utendaji wake wa kazi kwa kweli unajulikana na hasa katika Wizara ambazo aliwahi kuhudumu. Lakini pia nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Wanyancha, ni rafiki yangu, ni mfugaji mwenzangu lakini pia niwashukuru Wataalamu wote na watendaji wakuu ndani ya Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi nzuri waliyofanya hadi kufikisha hotuba hii ya bajeti kwa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaongelea zaidi sekta ya mifugo. Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, bajeti yake ni shilingi bilioni 67.3 na katika fedha hizo shilingi bilioni 30 ndiyo inakwenda kwenye miradi ya maendeleo katika sekta ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niipongeze Serikali kwa kutenga shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kununua madawa ya mifugo kwa sababu magonjwa makubwa ya mifugo yanasababishwa na kupe. Kwa hiyo, tukiweza ku-*control* kupe, mifugo inaweza ikastawi. Tunachoomba ni kwamba bei ya dawa hizo za ruzuku ziweze kujulikana na ziuzwe katika Vituo vya Afya za Mifugo na maduka pamoja na mawakala wajulikane na bei zijulikane, kwa sababu huko nyuma kwa kweli kuna fedha zimetengwa na zikapelekwa kwa mawakala lakini sasa wanauza hizo dawa za ruzuku wanavyotaka wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo jitihada za Serikali za kujaribu kutenga maeneo ya wafugaji ili kuondosha migogoro iliyopo kati ya wakulima na wafugaji, lakini kama alivyosema ndugu yangu, kule Kaskazini, kwa kweli hatujawahi kuwa na migogoro mikubwa, wala hakuna kabisa, ni upande huu tu na sijui ni kwa nini. Lakini jitihada za Serikali kuanzia mwaka 2006 mpaka mwaka 2009 tunaelezwa kwamba jumla ya hekta milioni moja mia tatu tisini na moja zimetengwa kwa ajili ya wafugaji katika Mikoa na Wilaya, lakini mimi ninapenda kuongeza tu kwamba katika maeneo yaliyotengwa ni vizuri ikawekwa kitu kama *fire lines* ili kukwepa pia maeneo hayo ya wafugaji kuvamiwa na watu mbalimbali na hata Serikali inavyochukua maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyofanywa katika eneo la hifadhi ya barabara imewekewa *beacon* kwamba huwezi kujenga ndani ya eneo lenye *beacon* za barabara, maeneo ya wafugaji nayo yaweze kuwekewe *fire lines* au *buffer zone*, lakini pia katika kufanya hivyo ijulikane kila eneo ni mifugo mingapi inaweza kukaa katika eneo fulani ili kukwepa kuwepo kwa mifugo mingi kuliko eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya hivyo, maeneo yale ya wafugaji ambayo yatakuwa yametengwa, tukiweza pia kutengatenga kule ndani ili mifugo itakapokuwa inachunga kule, ichunge kwa mizunguko na kwa sababu maeneo ni makubwa wakianzia upande huu mpaka waje wamalize eneo lile majani yatakuwa yameota upande mwingine. Kwa hiyo, wanaanza tena upya, hiyo inaweza ikasaidia kupunguza uhamaji wa mifugo, kwa sababu katika kufanya hivyo inaruhusu ardhi kurejesha uoto wa asili na ardhi kuendelea kuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya wafugaji na wawekezaji, maeneo haya wote tunafahamu kwamba binadamu, mifugo na wanyamapori, hawa wanazaliana na kwa hiyo wanaongezeka kwa wingi, lakini ardhi hata siku moja haiongezeki na maeneo ya kuchungia mifugo kutokana na maeneo kuchukuliwa kwa shughuli mbalimbali za Kiserikali kama maeneo yalivyotwaliwa yakafanywa kuwa Hifadhi za Taifa kama vile Serengeti, *Mkomazi Game Reserve* na maeneo mengine. Maeneo ya wafugaji kuchukuliwa kwa ajili ya kufanywa mashamba makubwa kama mashamba ya *NARCO* na BASUTO. Maeneo ya wafugaji kuchukuliwa na kupewa wawekezaji wa ndani na nje na bado yanatwaliwa na kupewa wawekezaji wawekeze katika mahoteli, wawekeze katika *camp site* na kadhalika, vitu kama hivyo kwa kweli vinabana maeneo ya malisho ya mifugo. Lipo janga la ukame ambalo limeelezwa vizuri sana ndugu yangu, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer wa Longido, hii ndiyo imefanya mifugo sasa hivi kuhamahama, walikuwa wanahama lakini imeongeza kasi ya mifugo kuhamia maeneo ambayo wanadhani yalipata mvua kidogo na kwa hiyo kuna malisho na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imesababisha mifugo kuingia katika maeneo ambayo hayaruhusiwi, kama Hifadhi za Taifa, mapori ya akiba, vitalu vya uwindaji na kadhalika. Ni shida ndiyo inalazimisha hii mifugo kuingia maeneo yale kwa sababu kuna maji na kuna majani ya kutosha. Niwambie tu kule kwangu kuna shida kubwa sana licha ya mifugo ya ndugu yangu Lekule kuja mpaka Ngorongoro, Monduli, wamekwenda Simanjiro na wa Simanjiro wakaenda mpaka Kilindi. Lakini kule kwangu kuna matatizo katika maeneo mawili, kuna matatizo katika eneo la uwindaji la *OBC*, eneo hili la huyu Mwekezaji ambaye ana leseni ya kuwinda, tumekuwa naye kwa miaka kumi na saba tangu mwaka 1992 na kila mara ana *renew* mkataba na tunaendelea naye, hatujawahi kuwa na ugomvi mkubwa sana, lakini katika kipindi hiki cha ukame na yeye anataka kuja kuwinda na anasema kwamba mifugo imejaa kule kwa hiyo anashindwa kuwinda. Mimi nilifikiri kwamba tulikuwa tumetengeneza mkataba na vijiji ambavyo vimezunguka eneo hili, tukakubaliana na tukaunda Kamati ya Kuratibu Malisho wakati hakuna uwindaji lakini wakija kuwinda Kamati hiyo itakaa chini kusema mifugo sasa ikaaje wakati mwindaji anakuja kuwinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu ulitekwa na ofisi ya *DC* na ikawa ni kazi ya Serikali na Serikali wakati mwingine kupitia Majeshi, inatumia mabavu na kwa hivi ninavyozungumza kuna operasheni kule ya kuondoa mifugo na kuondoa maboma ambayo yapo kule ndani kwa kisingizio tu kwamba mifugo ya Wakenya imejaa kule, ni kweli hiyo mifugo ilikuwepo lakini Serikali za Vijiji na viongozi wengine; kupitia kwenye Chama na viongozi wa mila, tumekaa chini tukaweka utaratibu hiyo mifugo ya Kenya ikawa *identified* na wamerudishwa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya wanathamini mifugo na wameruhusu mifugo kuingia maeneo ya Maasai Mara ambayo imetengwa kama *National Park*, wameruhusu walishe kandokando ya hifadhi ya Maasai Mara, bahati mbaya Simba wakala mifugo na Wamasai wale kwa kweli hawakuweza kuvumilia. Imeliwa mifugo kama minne lakini wakauliwa Simba sita. Bado Serikali ya Kenya imerudi ikaweka utaratibu wa kuilisha kwa vibali lakini sisi mnasema tu tuondoe mifugo, hatuwezi kwenda namna hiyo, kwa

sababu sasa hata eneo lote ambalo lipo chini ya *hunting block* ya *OBC* ni eneo zima mpaka ofisi ya DC na ofisi za Halmashauri zote ziko ndani ya eneo la *hunting block* ya *OBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukisema ondoeni sasa tunarudi nyuma kiasi gani, maana tukifanya hivyo, *then off course* tunakwenda Kenya kwa sababu ni jirani tu hapo, lakini kana kwamba hiyo haitoshi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na tulikuwa nao hapa juzi tulizungumzia habari ya ukame pamoja na watu wa Ngorongoro na wakiwepo watu wa *TANAPA* tulikubaliana huko nyuma kwamba maeneo ya tambarare kwa sababu Ngorongoro imegawanyika mara mbili, kuna *highlands* na kuna maeneo ya tambarare, tumekubaliana kwamba maeneo ya tambarare mifugo ilishwe na wanyamapori. Sasa inaonekana kama wameambizana operesheni pia ipo huko wanataka kuondoa mifugo maeneo ya Ndutu, maeneo ya Oldupai George ni eneo ambalo ni mbali kabisa na *highlands,* ni mbali na *Crater* ya Ngorongoro na ni mbali na *Nothern highlands to forest reserve*. Sasa hii mnataka kuwaambia nini wafugaji, mnawapiga kulia, kushoto, nyuma, mbele halafu wafanyeje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri watafikia mahali wafugaji hata subira itakwisha, kwa sababu danadana hii kwa kweli hatuwezi kuvumilia iendelee. Naiomba Serikali, siku zote Serikali kama ni kuweka operesheni iwe ni *last resort,* nimeongea na Mkuu wa Mkoa ananiambia anajua juu ya hiyo operesheni ina baraka ya Serikali na kwa hiyo iendelee. Nataka kutoa wito kwa Serikali kwamba yakija kutokea matatizo watu wakaumizwa, watu wakauwawa, mifugo ikachukuliwa basi tuwe tumesema hapa na Serikali itajua la kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sasa migogoro katika maeneo haya ya wafugaji. Tumesema kwamba wawekezaji wanapewa maeneo lakini bila kushirikisha sana wananchi, mimi naiomba Serikali msiendelee kuwakumbatia wawekezaji tu mkawasahau wananchi wenu. Hivi inakuwaje mnawakumbatia wawekezaji? Tuna matatizo makubwa sana na hawa wawekezaji kama ni wa madini watamaliza wataondoka, kama ni wanyama watamaliza wataondoka, tutabaki na wananchi wetu. Kazi kubwa ya Serikali katika nchi hii ni kuangalia wananchi wake na mali zao, sasa hatuoni *commitment* ya Serikali katika suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kuna operesheni sasa hivi huko, lakini hatujajua matokeo ya operesheni hii. Mimi ninaomba Waziri Mkuu na yupo hapa anatusikiliza, kama ambavyo alikuwa amesitisha operesheni ya Kilosa, asitishe hii operesheni katika eneo la *OBC* na katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro maeneo ya tambarare Ndutu. Naomba sana, kwa sababu kwa kweli hawa wafugaji hawana tena mahali pa kwenda na tukiona sasa balaa yote hii tunaletewa na wanyamapori, tutafahamu la kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwathamini viongozi wetu na sisi hatujashindwa hii kazi kama watu wanaweka operesheni kule kwa *OBC* Mbunge yupo, haelezwi, hashirikishwi wala Chama cha Mapinduzi hakishirikishwi, ni Serikali tu kwa kutumia Majeshi kwa sababu ina Polisi ina *FFU*, hatuwezi kwenda namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wametuchagua ili tuwasaidie matatizo yao na mimi nilipoingia Ngorongoro kwa awamu yangu ya kwanza hii ya miaka hii minne, tumeweka amani kati ya Wasonjo (Wabatemi) na Wamasai na Mbunge ameshughulika na hili, kwa nini hamtaki kutushirikisha katika haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu. Hakika napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu kwa hotuba hii nzuri sana hasa katika Ibara ya 120 ambako mimi ningesema ndiyo ukombozi wa Tanzania. Kwa nini? Hapa naandika Ufugaji Bora Vs Ufugaji wa Kuhamahama au Wakuchunga. Ibara hii inazungumza kwa kirefu jinsi Maafisa Ugani wanavyopelekwa katika vijiji mbalimbali kwenda kufundisha ufugaji bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikitiko langu kubwa, hawa Mabwana hawajafika Rufiji. Kwa hiyo, naomba kwanza niwaulize kwa mshangao, hivi Rufiji na sisi ni wafugaji? Kwa kweli tumeingiliwa, sisi si wafugaji. Ilivyokuja kwamba ng’ombe waende sehemu mbalimbali ya nchi, Rufiji ilikuwa na ng’ombe 50,000 tu, sasa hivi wako zaidi ya 200,000 na wamekuja kwa njia ya kijanja. Wanapewa *permit* ya kwenda Lindi, wakivuka ule Mto na majani yale wakiyakuta wanabana, usiku wanateremsha ng’ombe wale, tumepata tatizo hilo lakini kubwa ni kwamba yapo madhara, watu wa Rufiji wamechoka na madhara haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kuna *total land degradation*. Ardhi inaharibika kabisa na kwata za ng’ombe na haitafufuka ardhi ile kama ilivyokufa ya Masai *Land*.

**NAIBU SPIKA:** Wanaita kwato bwana! (*Kicheko*)

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *sorry*! Ni kwato. Kama ilivyokufa ardhi ya Wasukuma wale ndugu zangu sasa wanataka kuua na ardhi ya Rufiji vilevile. Kwa kweli hii habari ni moja kati ya jambo linalosikitisha sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama nataka kuwaambia kwamba Mungu alivyotuweka katika ardhi kulikuwa na ardhi ya kilimo tu na ardhi ya kuchungia na kufugia ng’ombe. Sasa unapopeleka ng’ombe hawa katika Bonde la ardhi bora la Rufiji wakaharibu ardhi ile na sisi tunatazama, haiwezekani! Lazima kuwe na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama kitabu cha Waziri wa Mipango, kilimo peke yake kinasaidia pato la Taifa kwa asilimia 25.7 bila *mechanization,* bila *irrigation* na tukifanya *irrigation* itapanda lakini ng’ombe mpaka leo na mifugo yote inachangia asilimia 4.6. Sasa ndugu zangu tuue hii kitu inayotupa robo ya pato la nchi kwa ajili ya hawa ng’ombe wanaotupa pato la asilimia 4.6? Hatufanyi uadilifu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani suala hili halitaki sana elimu kubwa kukumbuka historia. Historia ya Masai *steppes* ya Sukama *Land* na *the central province* ndiyo tuliyosoma katika historia hawa ndiyo wafugaji. Sasa kitu ninachotaka hapa ni *co-existence*. Ng'ombe walio Rufiji katika Bonde la Mto Rufiji lenye rutuba nyingi wahamishwe wawekwe sehemu ya juu ya Rufiji ambako hakulimwi mpunga wala hayalimwi mahindi. Kule wanaweza wakaendelea na ufugaji huo. Tunalohitaji, ni *commitment* tu. Serikali ikubali kwamba ardhi ya juu ambayo halimwi mpunga kama ikijengwa mabwawa, majosho na kukawa na mpango kamili unaosema huku marufuku kabisa kuleta ng'ombe basi watu wa Rufiji hawana ugomvi na Wasukuma wala ndugu zangu Wamasai hatuna ugomvi nao, ugomvi unapokuja wanapeleka ng'ombe hawa mashambani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshuhudia Mzee wetu namtaja hata kwa jina Mzee Mtibo wa Ikwiriri amekufa Muhimbili kwa kupigwa kwa sababu shamba lake liliingiliwa na ng'ombe na nimesoma *Yasin* pale wakati anakufa yule mzee. Uchungu mkubwa umenipata. Watu sita wamekuja Rufiji kwa ugomvi kwamba ng'ombe wanapelekwa katika mashamba ya wakulima na hili ndilo tatizo kubwa na wala asisimame mtu akasema kuna ubaguzi, hakuna. Ubaguzi ni kwamba nyie hamjali mashamba. Kwa hiyo ninaomba hivi Serikali tafadhali sana kwanza tungeomba turudie ardhi ya kilimo iwe ya kilimo tu na ardhi ya ufugaji iwe ya ufugaji tu ili hawa muwa-*contain* kule kwenye ardhi ya wafugaji *which is semi-arid* lazima kuwe na *demarcation* inayolindwa ikiwezekana na Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Rufiji matatizo bado mengi kwa sababu kumetokea wenzetu hawa ukienda nao Mahakamani kila siku wakulima wanashindwa tu. Pana nini hapo? Kesi akisimama mkulima na mfugaji, mkulima anashindwa *through out*, haiwezekani, liko jambo hapa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninaloomba ukifanya hesabu sasa hivi ya sensa ya wanyama hawa utakuta Rufuji sasa hivi wako 200,000 naweka ombi waondoshwe wabaki walewale 50,000 au ikiwezekana wote waondoshwe lakini hata hawa 50,000 wasikae katika lile bonde wapelekwe sehemu ambayo ni *plateau* ya Rufiji, ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu utakuta Lindi na Rufiji ng'ombe walioko kule ni zaidi ya 400,000 lakini kiwanda cha kusindika nyama ya ng'ombe kiko Ruvu. Sasa wazee wangu tuchinje nyama kule tulete *carcasses* Ruvu km zaidi ya 300? Kwa nini msijenge kiwanda hiki pale Rufiji basi ili iwe rahisi ng'ombe wanachungwa, wanafanyiwa mnada, wanachinjwa palepale? Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri atutafutie Kiwanda kule ambako ng'ombe wako wengi, kama hamtaki basi waondoeni ng'ombe wote. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa uamue, unataka kiwanda cha nyama au ng'ombe watoke?

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ningekuwa nachagua hayo mawili, ningeomba ng'ombe watoke. Lakini kama mnalazimisha basi naomba kijengwe kiwanda kule kwa sababu hivi sisi kweli tupeleke ile mizoga ya

ng'ombe huku Ruvu kweli hili jambo mnalofanya ni la maana? Hapa lazima Mheshimiwa Waziri utazame vizuri ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pointi ya mwisho ni hii *mentality* ya wafugaji ya kizamani ya kuwa na makundi makubwa ya ng'ombe. Ninaomba Wizara isomeshe ikiwezekana muwachukue hawa wafugaji, wapelekeni nchi za nje wakaone ng'ombe zinaweza zikafugwa bila kuwa na makundi makubwa mpaka yanatia wasiwasi. Mtu mmoja una ng'ombe 20,000 unazifanyia kazi gani? Mheshimiwa mmoja hapa, mtani wangu anasema wale ng'ombe ndiyo utajiri wanatembea na trilioni tano. Lakini wewe umeshaona hawa ndugu zangu Wasukuma wanavyotembea na wale ng'ombe, *they are the poorest people*. Wewe kawatazame wale, wanakwenda hawana viatu, wanatembea msituni, mvua zikinyesha hujui analala wapi, halafu unasema ni utajiri, huu ni utajiri gani jamani, huu ni utajiri kweli? Hii ndio maana ya maendeleo? Sio! Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali kwanza ipunguze ng'ombe walioko Rufiji na hawa 50,000 wakibaki ninaomba kiwanda kijengwe ili tusije tukabeba mizoga ya ng'ombe kuileta kusindika huku Ruvu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri John P. Magufuli (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Wanyancha (Mb), Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora unayo mabwawa matatu, nayo ni Bwawa la Igombe, Kazima na Loyo, ambayo hutoa samaki (hufugwa), kwa muda mrefu sasa hutoa samaki wadogo wadogo.

- Kwa kuwa Wizara hugawa vifaranga vya samaki aina ya perege kama inavyojieleza katika ukurasa wa 19 ni vyema Mkoa wa Tabora ukapewa kipaumbele ili uweze kukuza ubora wa samaki na kufaidika. Ombi langu ni kuomba Wizara itoe elimu kwa wavuvi wadogo wadogo wa eneo hilo (mafunzo).

- Kuongeza wataalam wa Sekta ya Uvuvi, kwani Idara hii haina wataalam wa kutosha, pia wapewe vitendea kazi. Ofisi za sekta hii ziboreshwe, kwani hazina hadhi katika Mkoa hata Wilaya. Hata moyo wa kufanya kazi haupo, kwa njia hiyo ni vyema sasa iangaliwe upya kutokana na jiografia ya nchi yetu.

- Kasma yake iongezwe ili kuiwezesha kusimamia vizuri suala la uvuvi.

- Wapewe mafunzo ya kuboresha utaalam wao kutokana na teknolojia ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji ambao wanahama hama ni vyema sasa Wizara ikatoa elimu ya ufugaji bora na kuelimishwa kupunguza Mifugo, pia vipeperushi viandaliwe kwa lugha ambayo wafugaji hao wataielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ikishirikiana na TAMISEMI, ihakikishe wafugaji wanapewa maeneo ya malisho ambayo yatatenganishwa na wakulima. Madai ya wafugaji wa Kilosa, yatolewe maelezo na wale waliohusika wachukuliwe hatua kali na kurudisha Mifugo yao.

Malembo ya Mkoa wa Tabora ni machache wakati nayo inaongoza kwa kuwa na mifugo mingi, ambayo huingia toka mikoa ya jirani, kwani si vyema kutegemea fedha za wafadhili pekee; ni wakati sasa kwa serikali kuliona hili.

Fedha iliyotengwa kukarabati majosho kwa Mkoa wa Tabora haitoshi, kwani gharama zimepanda.

Serikali ikague machinjio zilizopo kwa kushirikiana na TAMISEMI, kwa kuwa hayana hali ya kisasa kama vile machinjio ya Dar es Salaam ni machafu sana. Naomba serikali isaidie kuboresha machinjio ya Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isaidie kuongeza mitamba ya kisasa na kuwakopesha wajasiriamali wa vikundi vya ufugaji kwani Tabora wapo wengi; kuku chotara; mbuzi wa maziwa; na mashine za kutotolea vifaranga zikopeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa juhudi kubwa wanayoifanya kusimamia kazi za Wizara na kuendelea kudhibiti makosa mbalimbali yanayojitokeza katika maeneo ya Uvuvi na Mifugo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa juhudi kubwa na za dhati, ambazo zitaongeza pato la taifa. Namtakia kila la kheri, pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara. Naipongeza hotuba hii inayoonesha mwelekeo wa Wizara na kazi zote zitakazofanyika katika kipindi hiki cha mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, naomba nichangie mambo yafuatayo:-

Kwanza, naipongeza Wizara kwa juhudi inazofanya kwa kuelimisha wananchi/wafugaji na wataalam ili waelewe umuhimu wa ufagaji bora na wenye tija, kazi ambayo ikifanikiwa, itawezesha mazingira katika hali yake ya kawaida. Si hiyo tu, bali uchumi wa wananchi utaboreka. Nashauri mambo yafuatayo yafanyike:-

Wafugaji hawa baadhi yao wapelekwe na kutembelea maeneo wanayofuga vizuri, yaliyopo ndani na nje ya nchi ili warudipo wawe waelimishaji wazuri wa wenzao na wao watakuwa wafugaji wazuri. Mtu mzima ukitaka akuelewe ni kumfundisha kwa mifano ataelewa haraka.

Maeneo ya wafugaji yapimwe na mfugaji apewe eneo lake au kikundi na wamilikishwe ili wajue kwamba, eneo lake ndio alilo na haki nalo na si vinginevyo, hii itawawezesha kujiunga na ufugaji bora kwa hiari yake. Kazi hii ni nzito, inahitaji muda wa kuelimisha waelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Wizara hii ni nzuri ila tatizo ni watumishi wachache na majosho mengi ni mabovu na hayafanyi kazi na wakati mwingine ni ukosefu wa maji. Naomba serikali iangalie matatizo hayo ili yaweze kuondoka na ng'ombe wapate huduma hiyo. Majosho yaliyobaki kukarabatiwa yawekwe kwa miaka mingine, lakini hata hivyo, kila wilaya lingekarabatiwa angalau josho moja, ukizingatia ugonjwa wa Bonde la Ufa ni vizuri tukaongezewa ukarabati wa majosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua Chuo cha Mafunzo ya Kukata nyama kilichopo Dodoma kama Wizara inakijua, kwani sikusikia maelezo ya chuo hiki? Chuo hiki ni muhimu kwani wanafundishwa hapo vijana na baada ya mafunzo hayo hupata ajira. Tunaomba Chuo hiki kipanuliwe na vijana wengi wajifunze na wapate ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. BENSON M. MPYESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii. Naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii, kwa uchapaji kazi mzuri kwa malengo yaliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelekeza mchango wangu kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, 2005, kufufua viwanda Mbeya na hatimaye kuongeza ajira. Kiwanda cha Nyama cha Mbeya kipewe uzito wa hali ya juu, mashine zipo. Naomba Wizara ibebe jukumu la kukifufua kiwanda hiki. Naitaka serikali iachane na urasimu wa PSRC wa kutotaka kujibu barua toka Wizarani na kuiachia Wizara hii itafute mwekezaji na wala si PSRC.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu tuwe na mbinu za kulinda soko la ndani la mazao ya Mifugo.

Siyo busara sana kuuza ngozi ghafi nje ya nchi, kwani itafanya soko la ndani likose ngozi hiyo na tulazimike kuagiza viatu nje ya nchi. Sasa ifike wakati, serikali iandae mkakati wa kutumia ngozi yetu kwa viwanda vya ndani. Lazima wanafunzi wetu, majeshi yetu na makundi yote ya jamii, yaanze kutumia viatu, mikoba, mikanda, begi, pochi na kadhalika, ambavyo vimetengenezwa kwa ngozi yetu wenyewe. Nina imani, Waziri Magufuli, atalifanyia kazi suala hili muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa uongozi wako wa kusimamia Bunge lako Tukufu. Namshukuru Mheshimiwa

Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji, kwa kuandaa hotuba na kuisoma mbele yetu. Mchango wangu kwenye hotuba hii kama ifuatavyo:-

Hali ya Wafugaji: Ni vizuri serikali iweke mazingira mazuri ya wafugaji, kwani wafugaji bado hawajathaminiwa baadhi ya maeneo. Nashauri Wafugaji waongeze ruzuku ya madawa ya mifugo, majosho na mabwawa. Vile vile ni vizuri Halmashauri za Wilaya na Wizara, wazibane na kuzisimamia ili zihakikishe wananufaika na mifugo yao. Wafugaji watengewe maeneo, kwani wanahangaika kwa kukosa maeneo ya malisho. Kwa mfano, katika Wilaya ya Bukombe yenye 40% ya eneo la wafugaji, kilimo, madini na makazi na 60% ya eneo ni msitu; ni ngumu sana kupata eneo la malisho. Hivyo, ni vizuri serikali itenge eneo la wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya serikali juu ya wafugaji ni nzuri sana, lakini utendaji wa watendaji wake haufai.

Mheshimwa Naibu Spika, Wafugaji wa Kilosa na Mpanda, wamedhulumiwa Mifugo yao. Kwa taarifa zilizotolewa na Pingo wapo DSOs, DCs na wengine wamedhulumu. Kwa nini serikali haiwachukulii hatua watendaji wabovu?

Mheshimiwa Naibu Spika, umetokea mtindo wa wafugaji kuibiwa mifugo yao. Mfano, katika Wilaya ya Bukombe lipo kundi la wahalifu, ambao wanaandaa mipango ya kuiba ng'ombe kwa kutumia nyaraka halali. Ni vizuri serikali ifuatilie kwa makini na kuchukua hatua, kwa wale wote wanaofanya ujambazi huu, ambapo naamini serikali ngazi ya Wilaya inayo majina ya wahusika na inawafahamu. Wizara tieni msukumo wa kuhakikisha kundi hili la wahalifu, linachukuliwa hatua.

Ni vizuiri serikali iendeleze juhudi zake za kuboresha masoko ya mifugo na mazao yake. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada kubwa anazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha, anitolee ufafanuzi wa masuala yafuatayo:-

- Kwa nini serikali hatoi msukumo kwenye Halmashauri za Wilaya kwa kutenga maeneo ya malisho? Mfano Bukombe eneo la Kelezia – Runzewe au Mnyashinge - Nyarugusu?

- Je kwa nini wafugaji waliodhulumiwa huko Kilosa na Mpanda, wahusika hawajachukuliwa hatua?

- Kwa nini Serikali haiwachukulii hatua wale wote wanaojihusisha na wizi wa Mifugo Wilayani Bukombe?

- Ni lini Kiwanda cha Nyama Shinyanga kitaanza kwani kila mwaka hadithi inafanana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri serikali iongeze bajeti katika Wizara hii. Mheshimiwa Waziri na timu yake, wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mara ni Mkoa wa wafugaji, pamoja na kilimo. Hata hivyo, kama mnavyofahamu ni Mkoa ambao wizi wa Mifugo ni *rampant* hususan maeneo ya mipakani; Tarime, Serengeti na kadhalika. Kwa mawazo yangu, naamini kuwa, iwapo kungekuwa na kiwanda cha nyama, ngozi, maziwa, wafugaji wangehamisika kufuga hasa ufugaji bora, lakini pia kushawishika kupeleka ng'ombe Kenya kimagendo kungepungua kama siyo kwisha kabisa.

Naomba yafuatayo yafanyike:-

(a) Serikali ishawishi apatikane mwekezaji Kiwanda cha Maziwa cha Utegi. Kiwanda hiki kina miundombinu inayoharibika bure na iwapo kitafufuka, kitafanya makubwa ili kuboresha maisha ya wafugaji Mkoani Mara hususan Wilaya ya Tarime, Rorya na Musoma.

(b) Tujenge viwanda vya nyama na ngozi Mkoani Mara ili tamaa ya kuiba mifugo kuuza Kenya isiwe na maana tena kwa wakazi wa Mkoa huu.

Nawapongeza sana Waziri Magufuli (Mb), kwa kazi nzuri inayoonekana siku hadi siku, *keep it up.*

Kaka yangu Wanyancha umeshaizoea Wizara sasa, endelea kutusaidia. Katibu Mkuu Nyamurunda, kazi yako ni ya pekee; hivyo Mungu aendelee kukupa afya ya kuifanya.

Watendaji wote hongereni na poleni kwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii, kuitaka serikali inipe majibu yafuatayo:-

Hivi serikali haina taarifa kwamba NARCO ilishtakiwa Mahakama Kuu ya Tanzania (Kitengo cha Ardhi) Dar es Salaam tarehe 14 Desemba, 2007 kwa kesi Na. 305/2007, wakipinga shughuli yoyote kufanyika katika eneo la Ngenge, Kishuro na Rutoro katika Ranchi ya Kigoma?

Je, haikuona kipengele cha kuitaka serikali kusitisha shughuli zozote NARCO katika maeneo niliyoyataja?

- Naamini serikali hasa NARCO inajua, maana hii kopi ya kesi ninayo niliyo nayo niliipata NARCO Makao makuu katika jalada lenu kwa kupwa na Meneja (ambaye ni marehemu).

- Naamini mnajua maana tarehe 25 – 26 Oktoba, 2008, miongoni mwa kazi ilizofanya Bodi ya NARCO chini ya Mwenyekiti wake Mzee Shamte, ilikutanana na RC Kagera na Meneja wa Ranchi Kagoma na wengine tulikaribishwa na mimi nikiwepo.

- Bodi ya NARCO ilisema haina kipingamizi cha kutoa ardhi, lakini haina pa kusemea, wanashauri kwanza kesi itoke mahakamani.

- Waziri alishauri kutoa kwanza kesi mahakamani.

Kwa kujua hayo, imekuwaje NARCO kutoa hati 17 za umiliki kwa wawekezaji hao zikiwemo 16 za wawekezaji na moja ya wananchi (kilimo na makazi) na leo Mheshimiwa Waziri amesoma bajeti akielezea hivyo? Hii si halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni ufuatao:-

- Vitendo vyote vinavyoendelezwa na NARCO kwenye Ranchi ya Kagoma tangu iliposhtakiwa Desemba, 2008 ni batili. Haikuwa halali kutoa notisi ya miezi sita kwa hao watu, kwa sababu ipo *Court Injuction* ya kusitisha shughuli za NARCO katika eneo tajwa.

- Serikali isitishe hati zake zilizotoa kwa hao wawekezaji na itamke kuwa hati hizo ni batili.

- Kesi ikiisha (kwa sasa haijaamuliwa), wananchi wana hoja yao kwamba, wapewe muda/nafasi ya wao kushiriki katika mchakato kwa kupendekeza utaratibu mzuri wa kuendeleza ufugaji bora katika maeneo yao na kujiletea maendeleo.

- Naamini serikali inawapenda Watanzania/Wananchi wake, wapate makazi na kuyaendeleza, badala ya kuwabugudhi. Naishauri serikali itupatie ushirikiano, mgogoro huu uweze kumalizika kwa amani, wananchi wakiwa wameridhika na serikali imetimiza lengo lake.

Wananchi wanalalamika, wanapoona watu zaidi ya 10,000, yaani 10,033 hivi, wanateswa na kunyanyaswa na Wanyarwanda.

Tunasikitika kuona serikali haitupi nafasi ya kutusikiliza. Hivi mgogoro huu utakwishaje? Tunahisi kuna nguvu ya fedha na hasa rushwa inatumika sana katika zoezi hili. Sisi tunachotaka ni haki na amani.

Nategemea serikali itanipa jibu leo katika kuhitimisha hoja yake jioni. Ahsante. Nawasilisha.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote katika Wizara hii, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahusu bioanuai katika Bonde la Mto Kilombero. Bonde la Mto Kilombero, bioanuai yake *(biodversity)* inagusa Wizara nyingine zikiwemo Maliasili na Utalii (Hifadhi ya Selous na Kilombero Valley Game Controlled Area), Maji na Umwagiliaji (miti zaidi ya 38 isiyokauka), Wizara ya Mazingira Ofisi ya Rais (ardhi oevu, chepechepe, inayotambulika chini ya Mkataba wa Ramsar), pamoja na Wizara hii. Baada ya Ihefu, wafugaji wengi waliingia Bonde la Mto Kilombero. Wafugaji hawa wako wa aina mbili; pure pastoralist; na agro pastoralist.

Pastroralis ambao ni pure, hawana matatizo ya mazingira na mara nyingi hujitenga. Wale wanaofanya kilimo na mara nyingi ndio wanaishi jirani na wakulima na mara nyingi ndiyo wanao *clash* na wakulima

Naomba kwamba, kama nilivyowahi kuchangia hapa Bungeni, samaki katika Mito ya Kilombero wameanza kuadimika na kama watapatikana mkubwa wao huwa mdogo kwa maana ya size.

Naomba serikali kupitia TARIFI, wafanye *stock assessment,* ya kuweza baadaye kutushauri ili uvuvi uwe endelevu.

Aidha, nitaiomba Idara ya Uvuvi kupitia Sheria ya Uvuvi, kufanya doria ambayo itaweza kuangamiza *fishing gears*, ambazo zinaharibu ekolojia ya mito ile, hasa ukizingatia kuwa, samaki wengi ni wa jamii ya *cichlidae,* ambao hutaga mayai kwa kutengeneza viota chini ya maji. Viota hivi vikivurugwa, basi mazalia ya samaki pia yatakuwa yameharibiwa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wake wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, nawapongeza pia kwa changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Wizara hii, unaonekana wazi pale tutakapojiuliza maswali; je, ni fedha kiasi gani zingelihitajika kama tungeagiza kutoka nje ya nchi nyama yote, kuku wote, maziwa yote na samaki wote kwa ajili ya matumizi ya Watanzania? Jibu, tungetumia mabilioni ya fedha. Tunaishukuru Wizara kwa kuwahamasisha Watanzania wajitegemee kwa kitoweo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya MACEMP imekusudia kuwakomboa kiuchumi, wananchi wanaoishi Ukanda wa Mwambao wa Tanzania wa km. 800 pamoja na Visiwa vya Zanzibar, Pemba na Mafia. Kwa kawaida, wananchi hawa ni maskini sana

wa kipato na hivyo Miradi ya MACEMP inaweza kuwaondoa hapa walipo sasa na kuwasogeza mbele zaidi kiuchumi. Changamoto inayokabili miradi hii ni kama ifuatavyo: Bado ni vikundi vichache tu vinavyofaidika katika maeneo husika; na baadhi ya miradi ama haikufanyiwa utafiti vizuri au wanaoiongoza hawana utaalam wa kutosha wa kuiongoza.

Wavuvi wengi wanaendelea kuvua kienyeji kwa kukosa utaalam na kwa kutumia zana duni za uvuvi, kinyume na Ilani ya CCM ya 2005. Hivyo, mapato yao ya kila siku ni madogo sana na maisha yao ni duni sana. Serikali iwarahisishie wavuvi kupata mikopo ya kununulia zana bora za uvuvi na vyuo vya uvuvi viendelee kuzalisha wavuvi bora na wale waisopata elimu ya shule ya uvuvi, wapatiwe mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitishwa Sheria ya Ngozi, tunategemea uzalishaji wa ngozi utakuwa bora zaidi na viwanda vya ngozi vitafaidika zaidi. Tatizo letu ni lile lile la kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi, bila ya kuziongezea themani. Tunahitaji viwanda vya ngozi, vinavyotengeneza viatu mabegi, mikanda, mipira *(football)*, makoti na kadhalika. Viwanda hivi vitaongeza ajira nchini na vitapunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza vitu hivyo. Hata hivyo, viwanda vyetu vya ngozi vimekumbwa na mtikisiko wa uchumi duniani na vingine vimeanza kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina wastani wa ng'ombe wa maziwa wapatao 630,000, wanaotoa kwa wastani lita milioni 4.1 za maziwa kila siku, lakini maziwa yanayosindikwa ni lita 60,000 kwa siku. Hii asilimia ndogo sana (1.5%), inayosababishwa na uchache wa viwanda vya kusindika maziwa. Matokeo yake, maziwa mengi yanaingia nchini kutoka nje. Hivyo, serikali iendelee kushawishi wawekezaji wa viwanda vya kusindika maziwa, kwa kuwaondolea kero zinazowakabili kama kodi za mazao yote ya maziwa, kuondoa ushuru wa vifungashio vya maziwa na wakati huo huo, kupunguza uingizaji wa maziwa toka nje kwa kuongeza kodi ya maziwa hayo. Vile vile ni muhimu kwa serikali kuwaelimisha Watanzania, wapende kunywa maziwa kama shemu ya kuboresha afya zao.

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wataalam wa Uvuvi watufanyie utafiti wa namna gani mazao ya bahari Kusini mwa Tanzania, yanaweza kutusaidia kuinua hali za wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali isaidie kupata wawekezaji, ambao watajenga viwanda vya samaki Kusini mwa Tanzania ili kuinua hali za maisha za wavuvi wetu wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha kujenga boti cha Mikindani kinaoza na hakijafanya kazi iliyokusudiwa. Hasara kubwa itapatikana, iwapo kiwanda kitaanguka. Naomba serikali ama ikifufue au ikibinafishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake za kuona kwamba, maeneo yote ya Bahari, Maziwa na kadhalika, yanahifadhiwa.

Nawapongeza Wafanyakazi wa Mafia wa *Marine Park,* kwa kuchapa kazi kwa ufanisi; ni watunzaji wa mali ya serikali kama vile magari, maboti, majengo na kadhalika. Mahusiano yao na wananchi pia ni ya kupigwa mgano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUDOVICK MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa hongera kwa kazi anazofanya Mheshimiwa Waziri, kuzunguka nchi nzima kitoweo kinaboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uvuvi Ziwa Tanganyika, nchi yetu haijapata manufaa mengi kwa sababu hatujawekeza kama ilivyo katika Ziwa Victoria. Naomba juhudi zako zielekezwe huko na Ziwa Nyasa. Zana zipatikane kwa urahisi na *patrol* ifanyike toka Kasanga mpakani na Zambia hadi Kigoma mpakani na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni zao zuri lakini nchi hii imekuwa aibu kubwa, kwani Wizara hii imegeuza ng'ombe awe na haki zaidi ya binadanu aitwaye mkulima. Hii ni aibu ya Wizara hii, wakulima wameuawa Kilosa, Mbeya na Rukwa, kwa sababu ya wafugaji, lakini ng'ombe amepewa haki kuliko mkulima. Wizara hii lazima imheshimu mkulima ili mauaji yakomeshwe.

Tarime ugomvi wote sababu yake ni mifugo. Ng'ombe asingefugwa maeneo ya Tarime, migogoro ingekwisha. Kilosa mnaigeuza Tarime ya pili. Iringa Mbeya, Rukwa, Pwani, Lindi na Mtwara, mnataka iwe Tarime nyingine; hii ni busara gani?

Hamwoni uharibifu wa mazingira ila uongezekaji wa ng'ombe ndiyo furaha ya Wizara. Misitu inaisha, maeneo ya kilimo yanateketezwa na ng'ombe nchi yote itageuka Shinyanga au Mwanza ambako wafugaji wamekimbia baada ya kuteketeza. Dunia itawahukumu kama hamtatafuta ufumbuzi haraka.

Njaa ikitokea Mwanza au Shinyanga, kilio mnakipeleka Mbeya, Rukwa, Iringa na Morogoro, kwa nini hamchinji ng'ombe mkaenda kulisha waharibifu wa mazingira badala yake mnakwenda kwa wakulima wasio na sauti? Tanzania ikiteketea, sote tukiteketea wa kulaumiwa ni Wizara hii ya unyanyasaji wa wakulima. Tanzania imelaaniwa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Magufuli, kwa ujasiri alionao na harakati zake zinazoonekana *(Standard and Speed).*

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya uvuvi haramu hapa Tanzania, imefanyika kwa kipindi kirefu, lakini Mheshimiwa Waziri bila woga, ameweza kuliona na kuidhihirishia Tanzania kuwa, hali hii ilikuwepo lakini watendaji wake waliipuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na idara hii kuwa likizo kwa muda mrefu ni wakati muafaka kwa sasa, kuangalia mikoa inayopakana na bahari wanapatiwa mikopo ya vifaa vya uvuvi nao waondokane na umaskini; wafikiriwe kama serikali ilivyotoa kipaumbele kwa wakulima na wavuvi, nao wapate mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa MACEMP ni Mradi ambao bado haujanufaisha Mikoa ya Pwani, hivyo ni matumaini yangu kuwa, MACEMP isaidie Mkoa wa Lindi hasa Vijiji vya Pwani za Hindi navyo vifikiriwe hasa Vijiji vya Kijiweni, Ruvu, Mchinga, Mingoyo, Shuka, Nachunyu na kadhalika, nao wafaidike na Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenaa kumwomba Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kudhibiti hali ya ufugaji wa kuhamahama ili kuepusha uharibifu wa mazingira.

Hivi sasa wafugaji wengi wanaleta vurugu kubwa, uingiliaji wa kisiasa badala ya kuangalia mazingira. Je, Mheshimiwa Waziri unatoa tamko gani kuzuia wafugaji wanaohamahama na kukimbilia katika mito na kusababisha mito kukauka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi ni miongoni mwa mikoa iliyohamishiwa mifugo kutoka Ihefu. Jambo la kushangaza ni kwamba, ni lambo moja tu limejengwa; hamwoni kuwa serikali inachangia migogoro ambayo inaweza kuepukika? Ili kuepusha magomvi katika mifugo iliyopelekwa Lindi naomba yafanyike yafuatayo: Tujengewe malambo ya kutosha kukidhi mahitaji; tujengewe majosho ya kutosha ili kukidhi haja; kuhakikisha wataalam wanawekwa karibu na wafugaji ili wapate huduma muhimu; na kutoa mafunzo ya mara kwa mara ili kuleta uhusiano mwema kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, uonevu wa jeshi linalozunguka katika fukwe zetu, kwa wavuvi wadogo wadogo hata kama wavuvi wale wanakuwepo pale wakiwa na vibali na wanavua kwa dhana zinazoruhusiwa wanapora, wanawapiga wavuvi na kadhalika; ni ipi hasa kazi waliyotumwa? Nahitaji jibu nilipate leo hii. Kwa maelekezo zaidi, waulizeni Wananchi wa Mchinga Lindi nini kimetokea?

BMUs huanzishwa na nani; na kwa makubaliano ya akina nani katika eneo husika? Kwa nini maeneo mengi ambayo yameanzishwa BMUs ndani ya Maziwa na Bahari wavuvi wamekuwa na kero nyingi? Wizara itoe mwongozo sahihi ili kero hizo za unyanyaswaji wa wavuvi wadogo wadogo ziondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba Wizara igundue viwanda vinavyotengeneza nyavu zisizostahili na kuvichukulia hatua, kuliko kuwaandama wananchi wanaozitumia. Wananchi huzitoa wapi? Hutengeneza wenyewe?

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, ningependa kutoa ushauri wangu katika maeneo kadhaa ya hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni Mradi wa MACEMP. Tunaishukuru sana serikali kwa kutupatia Mradi huu, ambao kwa kiasi kikubwa, umesaidia sana kuinua kipato kwa Wananchi wa Wilaya ya Rufiji na hasa vijiji 28 vilivyo katika eneo la Delta ya Mto Rufiji. Vikundi vingi vimeanzishwa na vingi vimepata ruzuku *(grant)* na kupewa vifaa mbalimbali vya uvuvi, ufugaji wa nyuki na mashamba ya chumvi katika fukwe za bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupatiwa ruzuku hiyo, kuna dosari nyingi ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wake. Dosari hizi ni pamoja na: Fedha zinazotolewa kwenye vikundi ni ndogo na kutokidhi mahitaji halisi ya mradi unaohusika; fedha zinazotolewa zinacheleweshwa mno, kiasi cha baadhi ya vikundi kukata tamaa kuwa hawatopata na kusababisha manung'uniko makubwa; na baadhi ya vikundi havina hata mategemeo ya kupata fedha za kuanzisha miradi yao, kwani kwa sasa inaonesha kama vile mradi umesimama.

Kwa hiyo basi, ninaomba Wizara itoe ufafanuzi wa kina kuhusu Mradi huu na mgawanyo wa fedha kwa kila Wilaya ili kujua kiasi cha fedha kilichopo kwa kila Wilaya ya Mradi. Vikundi vingi vimeanzishwa na orodha yake ipo Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu Mradi wa *village Community Bank (VICOBA)*. Mradi huu ni mzuri sana na wananchi wengi wamejiunga nao. Kuna baadhi ya vikundi katika Vijiji vya Pombwe na Kiechuru, vina akiba hadi kufikia Sh. 15,000,000. Tatizo lililopo ni namna ya kuvisaidia vikundi hivi ili viwe SACCOS na viweze kukopesheka. Je, MACEMP na RUMAKI wana jitahada gani katika kuvisaidia vikundi hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mifugo hapa nchini. Kwa sasa inaonekana mifugo imepewa kipaumbele na kuruhusiwa kwenda kokote wanakotaka. Kutokana na Taarifa ya Mheshimiwa Waziri, inaonesha kuwa, Wilaya ya Rufiji imetoa vijiji 24 kwa ajili ya kufugia ng'ombe 76,807 (rejea hotuba yake ukurasa wa 106). Hivi ni nani aliyeruhusu kutoa vijiji hivyo 24 na kukaribisha mifugo iweze kuingia? Je, wafugaji hawa wameruhusiwa kuingia hata kwenye eneo zuri la kilimo la Mto Rufiji *(Rufiji Food Plain)?*

Hivi sasa ng'ombe hawa wameingia kwenye Bonde la Mto Rufiji na idadi ya Mifugo inazidi laki mbili! Kilimo kwa kiasi kikubwa, kimeathirika kutokana na wafugaji hao kutumia mashamba hayo kama maeneo yao ya malisho. Ugomvi mkubwa unatokea baina ya makundi hayo na kusababisha hata vifo. Hii ndio hali ilivyo katika Bonde hili la Mto Rufiji.

Zaidi ya hayo ni ile hali ya kulitumia eneo hilo la Bonde la Mto Rufiji kama ni eneo la kunenepesha mifugo kutokana na kuwa la kijani mwaka mzima *(evergreen).* Hali hii si nzuri, kwani inaleta matatizo makubwa na eneo hili sasa linaanza kuwa kame. Naiomba serikali iwahamishe wafugaji wote kwenye eneo hili na wapelekwe kwenye eneo ambalo Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imependekeza wapelekwe. Kinyume cha hivyo, ugomvi baina ya wakulima na wafugaji utaongezeka zaidi, kwani mifugo hiyo inaongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia hoja ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali/Wizara ifanye yafuatayo:-

Isiendelee kusikiliza kilio cha machafuko ya mara kwa mara ya wafugaji bali ifike mahali itoe suluhisho la kudumu kusaida wafugaji ili kuepuka mitafaruku kwa kuwa wote ni Watanzania. Tufike mahali tuseme imetosha.

Wafugaji wanategemea Mifugo kwa mahitaji yao yote kwa asilimia 100. serikali ibuni mikakati ya kuwawezesha wafugaji ki-uchumi. Mfumo ulioko sasa hivi haiwasaidii kabisa wala kuwalenga - hasa mkukuta hauwahusu wafugaji. Ni lini serikali itawalenga Wafugaji?

Mazao yatokanayo na Mifugo yapatiwe soko la uhakika. Kwanda cha Nyama cha Arusha, kilijengwa wakati Mkoa huo haujagawanywa na mifugo mingi wakitokea Wilaya ya Kiteto, Simanjiro, Hanang na Mbulu, ambazo sasa ni Wilaya za Mkoa wa Manyara na siyo Arusha. Tunaomba serikali itujengee Kiwanda cha Nyama (Babati) ili wafugaji wetu wapate soko la uhakika.

Serikali ipige marufuku kuswaga ng'ombe kupitia maporini ili kwenda kusaka malisho na maji kwa kuwa hicho ni kitendo cha mateso sana, wafugaji wanauawa na wezi na majambazi, wanyama wakali na kadhalika, ng'ombe kuporwa na huko hakuna waandishi wa habari na hivyo matukio haya mabaya hayana rekodi wala hayatangazwi. Serikali isaidie watu hawa (wafugaji), ifike mahali nao watulie kama Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii, nikiwa na imani kubwa kwa Mheshimiwa Waziri Magufuli na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Wanyancha, kwa usikivu wao na utendaji wao mahiri.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, pamoja na Watumishi wote kwa kutuandikia hotuba nzuri.

Serikali isimame kidete na kuhakikisha kuwa, ufugaji wa kuhamahama ukomeshwe mara moja.

Kuwe na *Land Use Plan.* Sehemu yenye rutuba ibaki kuwa ya kilimo cha chakula na biashara na sehemu ya ardhi, *semi-arid,* yaani kame, ndio iwe sehemu ya wafugaji. Bonde la Rufiji kwa mfano, liachwe na litengwe kitaifa liwe la wakulima tu.

*Land Degradation and Donflicts:* Ardhi yenye rutuba ya Wilaya ya Rifiji, inazidi kuharibika kabisa kwa kutumiwa kama malisho ya ng'ombe. Kilimo kinachangia 25.7% kwenye Pato la Taifa, lakini mifugo inachangia 4.6% tu ya Pato la Taifa. Sasa, tunaiomba serikali ikubali kuwa ardhi yenye rutuba kama Bonde la Rufiji lisitumiwe kama malisho ya ng'ombe! Kilio hiki ni kwa sababu Rufiji sasa ina ng'ombe zaidi ya 200,000. Hii ni hatari sana! Huko waliko hao ng'ombe wanakula mimea ya watu mashambani, ugomvi kati ya wakulima na wafugaji Rufiji peke yake watu sita waliuawa (kufa) katika ugomvi kati ya wafugaji na wakulima

Serikali iendeshe mjadala wa kitaifa kwamba, kuwe na kiwango cha mwicho (cha juu) cha kufuga kwa kila mfugaji. Kama hili haliwezekani, basi tuwarudishe wafugaji warudi makwao (*Pastoral Land* kama *Masai Land, Sukuma Land, Gogo Land* na kadhalika), kama wakoloni walivyowapangia.

Kama tuking'ang'ania kuwapeleka ngombe Rufifji, basi tutenge Rufiji juu (*semi-arid*) na ng'ombe wapelekwe huko. Kuwe na *strict control* ya mgawano huo. Ng'ombe wabaki katika uzio ili wasije wakaingia katika mashamba ya wakulima.

Serikali inasemaje kwa kupeleka ngombe zaidi ya laki nne Rufiji na Mkoa wa Lindi zaidi ya km 300 toka Ruvu lakini machinjio rasmi yako Ruvu? Je, ng'ombe watachinjwa huko Lindi kisha nyama isindikwe Ruvu? Maana yake serikali ijenge manchinjio mapya huko Rufiji au Lindi.

Mwisho, elimu ya ufugaji bora wala sio kuchunga na kuswagaswaga tu. Kuweko na programu ya kujenga malambo na majosho na huduma za afya ya wanyama. Vile vile tupunguze idadi ya ng'ombe kwa kila mfugaji. Watoto wa wafugaji wende shule sio kuchunga ng'ombe tu na kuishi kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Viongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa kutuongoza vizuri. Pia nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuwasilishwa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo ni mojawapo kati ya sekta muhimu, ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa, kukuza uchumi na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwepo migogogo kati ya wakulima na wafugaji, inayopelekea mapigano kati ya wakulima na wafuaji na hata kusababisha vifo miongoni mwao, ni vyema sarikali ikatenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na maeneo mengine kwa ajili ya wakulima ili kuepusha au kuzuia mapigano yasiendelee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wafugaji wabakie katika maeneo watakayotengewa ni muhimu wapatiwe mabwawa na majosho ya kutosha, ikiwa ni pamoja na kuimarisha yale yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mapigano baina ya wakulima na wafugaji yanayendelea katika baadhi ya maeneo; je, serikali imejiandaa vipi kupambana na kuondoa kabisa matatizo ya wakulima na wafugaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu inapaswa kutolewa kwa wafugaji ili wawe wafugaji bora na sio wachungaji tu; wafugaji wazalishe mifugo bora, yenye kutoa nyama na maziwa ya kutosha. Pia mifugo bora inatoa ngozi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mifugo, Sekta ya Ngozi ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi. Ngozi bora zinapatikana kutokana na mifugo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuuza ngozi nje kama malighafi haitusaidii sana. Ni vyema tukaimarisha soko la ndani, ikiwa ni pamoja na kujenga viwanda vya ngozi hapa nchini. Tukiwa na viwanda vya ngozi hapa nchini, tukaweza kutengeneza viatu, mabegi, mikanda na kadhalika na tukahamasisha taasisi mbalimbali kama vile wanafunzi mashuleni, majeshi ya ulinzi, polisi, pamoja na wananchi, wakatumia bidhaa hizo, tutaweza kukuta pato la ndani na uchumi wetu utazidi kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na viwanda vya kusindika maziwa na kuhamasisha wananchi watumie maziwa, pamoja na bidhaa mbalimbali zitokanazo na maziwa. Hii itasaidia kulinda afya za watu wetu, pamoja na kuongeza Pato la Taifa, pamoja na wananchi mbambali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi ni sekta nyingine muhimu, ambayo ikisimamiwa vizuri, inaweza kuchangia sana Pato la Taifa. Nchi yetu ina bahari, maziwa na mito, yenye samaki wengi wanaoweza kuwapatia wananchi chakula, kipato, pamoja na kuongeza Pato la Taifa. Viwanda vya kusindika samaki pia ni muhimu kwa matumizi ya ndani na zaidi kuuza nje ya nchi, kwa ajili ya kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya zana haramu za uvuvi yanaendelea kupigwa marufuku, lakini ni vyema wavuvi wakapatiwa mbadala kwa kupewa zana zinazotakiwa kwa mkopo au vinginevyo ili waepukane na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulinda rasilimali zetu za baharini hasa samaki; ni vyema serikali ikaimarisha ulinzi kwa meli au boti za kuaminika, zinazoweza kutumika kufanya doria ili majangili na maharamia mbalimbali, wasiendelee kuiba rasilimali zetu za baharini, mitoni na katika maziwa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuuze bidhaa zilizosindikwa badala ya malighafi. Ahsante.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara, kwa hotuba nzuri, inayoweka wazi juhudi za serikali katika kujaribu kukuza uchumi wa wananchi na nchi kwa ujumla kupitia mifugo na uvuvi.

Serikali iliamua kuzigawa Ranchi za Kitengule Missenyi na nyingine (Mkoani Kagera) katika vitalu na kuwagawia wawekezaji. La kusikitisha, vitalu hivyo viliingilia maeneo ya makazi ya watu hasa Ranchi ya Missenyi katika Vijiji vya Bubare Kakunyu na kadhalika. Hii imeleta mgogoro mkubwa kwa kuwafukuza wananchi katika maeneo yao, wanafukuzwa kwa kunyanyaswa na hao wawekezaji kiasi cha kuwapiga na hata kuua (sina ushahidi).

Mheshimiwa Rais, alipotembelea Mkoa wa Kagera, aliagiza kwamba kwa vile wananchi hao wanaishi katika vijiji vilivyopimwa na kusajiliwa waendelee kuishi katika vijiji vyao, ikimaanisha kwamba, vitalu vinavyoingilia vijiji hivyo vifutwe, agizo hilo halijatekelezwa na wananchi wanaendelea kunyanyaswa. Kwa nini? Agizo la Rais si ni Sheria?

Naomba maelezo, kwa nini wawekezaji wakumbatiwe na wananchi wanateseka?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa juhudi zake kubwa alizozionesha kwa vitendo katika kuinua Wizara hii. Hapo mwanzo, karibu Watanzania wengi, walikuwa hawaelewi umuhimu wa Wizara hii, lakini kwa sasa, kila Mtanzania anaitambua na kuiona ni mkombozi wa mambo mengi katika kuleta maendeleo miongoni mwa Watanzania. Hivyo, pongezi sana.

Siha haja ya kuorodhesha mema mengi (kazi), aliyoifanya Mheshimiwa Waziri, kwani mwenye macho haambiwi tazama. Ombi langu kubwa kwa serikali ni kuiongezea Wizara hii fungu kubwa ili kazi zake ziende vizuri. Pamoja na pongezi za Waziri, nisiwe mnyimi wa fadhila, nawashukuru Watendaji kwa ushirikiano mkubwa walioutoa nikianza

na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote, kila mtu kwa nafasi yake. Ushirikiano wao na umoja wao, ndio uliopelekea maendeleo yote haya ya Wizara, kwani bila wao, Waziri peke yake asingeweza. Hivyo, ninawatakia baraka za Mungu wetu, kwa yote katika mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imejitosheleza, ombi langu kubwa ni kuomba Watendaji wakaze buti tu, wafanye kazi. Mambo yafuatayo ni muhimu yaangaliwe:-

Viwanda na machinjio:-

(a) *Geographical location* ya viwanda vya nyama na machinjio yazingatie maeneo husika ili kuleta usawa kwa wafugaji, kwa ajili ya soko la karibu. Wawekezaji waelekezwe ili visije vikaendelea kurundikwa pamoja.

(b) Mkoa wa Singida tuna kuku watamu kuliko wote Tanzania na ni wengi. Tunaomba tusaidiwe kupata mwekezaji ili tupate kiwanda cha kusindika nyama ya kuku.

(c) Viwanda vya maziwa pia vitasaidia kupata soko la ndani. Serikali idhibiti maziwa mengi toka nje ili kutoa nafasi kwa wafugaji kufaidika na soko la maziwa.

(d) Serikali/Wizara, ishauriane na Wizara ya elimu ili kuwe na utaratibu wa wanafunzi kunywa maziwa shuleni angalau glasi moja kwa wiki kila motto. Hii itasaida afya kwa mtoto kwa wale wasiopata maziwa nyumbani na soko la maziwa litaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa ujasiri wake wa kuanza kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta hii muhimu sana. Niwapongeze pia Naibu wake na Wataalam wake wote, kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Napongeza Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ni nzuri sana na imeonesha masuala yote muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu, Sekta hii ya Mifugo imebaki nyuma, serikali kutotoa msukumo kuhakikisha kwamba, mifugo tuliyonayo (ambapo Tanzania ni wa tatu kuwa na mifugo mingi Africa), inachangiaje Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kunufaika sana na siasa hii ya mifugo, ikiwa tu serikali itaamamua kwa dhati, kuweka uzito wa kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hatuna maeneo ya kunywa maziwa; ni familia chache sana zinazopata angalau lita moja ya maziwa kwa siku, ukiachilia mbali wafugaji wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maziwa ni chakula pekee, chenye virutubisho vyote muhimu kwa watu wote; watoto na watu wazima. Tuhamasishe wananchi wetu wanywe maziwa kwa wingi, tukitambua umuhimu wake. Kwanza, tutakuwa tumewasaidia kujenga miili yao na kuwajengea uwezo wa akili, pia tutawezesha soko la maziwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wenzetu wafanyabishara wa nchi za jirani, wanakuja kuchukua maziwa hapa kwa bei ya chini, wanakwenda kuya-*pack* na kuyaleta hapa nchini kuuza kwa bei ya juu sana. Sisi ni soko la bidhaa za wenzetu wakati bidhaa zetu hazina masoko ya uhakika. Tubadilike, tuamke, tulisaidie taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukosa msukumo kwenye sekta hii, hakuna maeneo maalum kwa ajili ya mifugo. Wafugaji wamekuwa wanahamishwa hamishwa huku na kule, bila kuwa na mpango mzuri, wenye tija, kwa wafugaji na kwa taifa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshindwa kabisa kutafuta masoko kwa mifugo yetu hapa nchini. Serikali imeshindwa kulinda viwanda vya maziwa ndani ya nchi ili wafugaji wetu wapate soko zuri kwa mazao ya mifugo. Tulikuwa na *Tanganyika Packers,* kiwanda ambacho kilitoa soko zuri sana kwa mazao ya mifugo; leo kiko wapi? Tumekuwa na viwanda vya maziwa hapa ndani, hatuviwezeshi ili viweze kukidhi mahitaji na kujiendesha. Leo ukienda *Super Market,* utakuta maziwa *(packed milk),* kutoka Kenya, South Africa, Zimbambwe, Zambia na kadhalika. Wakati huo huo, wafugaji wetu wanakosa soko la maziwa yao, kuna wakati wanalazimika kumwaga maziwa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maziwa yanayozalishwa hapa nchini ni mazuri *(well packed),* kwa nini turuhusu maziwa kutoka nje tena *expensive* wakati tunajua tuna wafugaji wetu na wanazalisha maziwa na nyama?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunapima viatu kutoka kona zote za dunia, viatu hamna ubora sana na pia ghali sana. Hapa tuna viwanda vya ngozi, vinashindwa kufanya kazi kikamilifu, kwa sababu haviwezeshwi. Tuna ngozi nyingi sana, kuanzia zile za mifugo hadi wanyamapori; kwa nini tusivae viatu vya ngozi halisi *(pure leather)* kutokana na mifugo yetu? Kila leo makontena ya pochi za akina mama yanaingia kutoka India, Dubai, Arabs, china na kadhalika; kwa nini tusitengeneze pochi sisi wenyewe na hata tuuze nje tuongeze Pato la Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuhamisha mifugo lililofanyika maeneo mbalimbali, liliendeshwa kinyume na taratibu, liligubikwa na ukiukwaji wa haki za binadamu na Utawala Bora. Wafugaji waliporwa ng'ombe kulipishwa faini kubwa, usiojali hali halisi, kulazimishwa kuuza ng'ombe kwa bei ndogo sana ilimradi alipe faini inayotakiwa. Wamechomewa mashamba yao na nafaka zilizokuwemo na hata nyumba zao zilichomwa moto. Watendaji wametumia ubabe na ujeuri wa hali ya juu. Watu wamefilisika, wanafunzi wamelazimika kuacha masomo na hata wapo waliopoteza maisha. Hii siyo haki; hawa ni Watanzania na binadamu.

Serikali leo itoe maelezo kuhusu majibu ya timu ya wataalam, iliyoundwa na Waziri Mkuu. Watendaji waliohusika na ubadhirifu huo wamefanywa nini na nini hatma ya mali na mifugo ya wafugaji?

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli (Mb), kwa kazi nzuri anayofanya ya kuendeleza Sekta ya Mifugo na Uvuvi Nchini, bila kuwasahau Watendaji wa Wizara hii mpya, kadhalika na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Wanyancha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba serikali ione namna ya kuwasaidia wafugaji wanaonyanyasika, kama vile nchi hii sio yao. Serikali itenge maeneo ya kutosha, kwa ajili ya wafugaji pia elimu ya kuwasaidia wafugaji kupunguza mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji walioporwa mifugo yao Wilayani Kilosa, warudishiwe mifugo yao au walipwe fidia kwani hawana makosa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali yetu ina ranchi zenye mifugo ya kutosha kuanzisha/kujenga viwanda vya mazao, yatokanayo na mifugo. Ranchi zetu zinapata ruzuku kutoka serikalini, jambo ambalo halipendezi hata kidogo. Ranchi za Taifa, zijiendeshe zenyewe kutokana na kuwezeshwa kujenga viwanda vya mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika wa mifugo kuuzwa kwa mizani katika minada yetu. Wafugaji wananyonywa na wafanyabiashara, kwa mifugo yao kutouzwa kwa mizani katika minada.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri serikali, iangalie uwezekano wa kuwa na Maafisa Ugani kila Kata ili waweze kuwaelimisha wananchi, kuachana na ufugaji wa kuchunga au ufugaji wa zamani na pia mifugo iweze kuhudumiwa kwa haraka, magonjwa ya kuambukiza/milipuko yanapotokea. Kwa sasa, Maafisa Ugani wahatoshelezi mahitaji na wengine ni Maafisa Kilimo, ambao hawajawahi kusomea mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ranchi ya Kongwa ni kubwa sana, *almost* Hkt. 40,000, idadi ya mifugo katika shamba hilo ni dogo sana, *under 10,000 herds of cattle.* Baadhi ya maeneo ya Ranchi hii, yagawanywe vitalu wapewe waendelezaji wa ng’ombe wa maziwa na ng’ombe wa nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba mara kadhaa, Ranchi ya Kongwa/NARCO, wajenge japo darasa moja tu katika vijiji 13 vinavyozunguka ranchi. Jambo hilo halifanyiki, *this is a capital offence*; ni miaka tisa sasa, naomba jambo hili hamfanyi. *It is wrong*; inaniwia vigumu kuisemea Ranchi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Hapa nina machache ya kuchangia hoja hii.

Mifugo iliyokuwa katika maeneo ya Ihefu, Bonde la Rukwa na Mpanda, imevamia maeneo tengefu ya Mkoa wa Kigoma na hasa Kasulu Mashariki katika Mabonde ya Ruchugi ya Malagarasi. Mifugo hii ambayo ni kwa maelfu, inahatarisha eneo lote la Kasulu Mashariki kuwa jangwa. Je, ni namna gani Wizara hii itasaidiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kurekebisha hali hii? Je, ni lini Wizara hii itatuma Wataalam wa Mifugo Kasulu kutathmini hali hii?

Halmashauri ya Wilaya Kasulu tumejenga soko/mnada wa mifugo katika Kijiji cha Bihigwe, lengo ni pamoja na kuuza mifugo nchi jirani. Je, Wizara yako ina nafasi gani katika kusaidia kuboresha masoko haya? Bila shaka, utaalam unahitajika. Tokeni maofisini na kuja kusaidia kuboresha sekta hii katika Halmashauri za Wilaya zetu.

Je, Wizara hii ina programu gani kitaifa kusaidia wafugaji kupata mafunzo ya ufugaji wa kisasa na je, ni lini maeneo mapya kama Kasulu Mashariki yatapata msukumo toka Wizara yako?

Sekta ya Uvuvi inakua sana katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, hasa ufugaji wa samaki na uvuvi kwenye mabwawa. Je, Wizara ina programu gani kitaifa kusaidia kukuza sekta hii muhimu katika uchumi wa Taifa letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ng'ombe wengi waendao Kilwa Kusini hadi Lindi hupitia Daraja la Mkapa; na kwa kuwa maeneo mengi yaliyopo kwenye Jimbo la Kilwa Kaskazini ng'ombe wanabakia pale waonapo majani ya kutosha. Ng'ombe hao na wafugaji hao wanaharibu sana mazingira halisi ya maeneo hayo; miundombinu haikutayarishwa kiasi cha kutosha ndio maana wanashambulia hadi mashamba ya wakulima.

Tunashukuru kwamba, Watu wa Kilwa Kaskazini tumewahamasisha kiasi cha kutosha. Bila hivyo, mgogoro kati ya wakulima na wafugaji, ungepamba moto, hivyo napendekeza sheria kali itungwe ili ng'ombe hao wapakizwe kwenye magari na wapelekwe pale walipopangiwa.

Sifa kubwa ya wafugaji hawa wana tabia ya kukata miti ovyo na kuharibu mazingira oevu ya Kilwa Kaskazini; hivyo mazingira yanaharibiwa sana kwa kuchoma moto.

Mnada wa ng'ombe katika Wilaya nzima ya Kilwa upo mpakani na Wilaya ya Lindi, Mbwemkuru; hivyo, Wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, hawafaidiki kabisa na nyama ya ng'ombe, japo wanaharibu sana mazingira na maji katika jimbo hilo.

Kwa kuwa sehemu kubwa ya Kilwa Kaskazini ina miti asilia na milima mirefu, kwa hiyo, ukulima wa kutumia maksai haufanyiki na hauwezekani. Tuambuliacho sisi ni adha tu.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuisimamia na kutangaza vilivyo Wizara hii. Wizara hii ni mpya, ilikuwa haijulikani na hata wadau wake wafugaji na wavuvi, walikuwa hawana mtetezi wa kila leo. Leo wadau hawa, wameongezewa heshima kwa kuwa na Wizara yao, yenye kutetea maslahi yao na mali zao. Hotuba hii ni nzuri, inayoweka msimamo na mwelekeo wa kimaendeleo kwa wafugaji na wavuvi. Nawapongeza wote walioshiriki katika uandaaji wa hotuba hii. Hongera sana na ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, nina mchango ufuatao kwa hotuba hii:-

Sera ya Taifa ya Mifugo: Napongeza lengo kwa kutafsiri katika Lugha ya Kiswahili na kuisambaza. Hii ni hatua nzuri kwa wadau wengi ambao wengi wao hawajui kiingereza.

Sheria za Sekta ya Mifugo: Sheria zilizopo zisimamiwe ili malengo yafikiwe.

Maendeleo ya Mifugo: Tatizo kubwa la mifugo ni mahitaji ya maji, majosho na nyasi.

Ombi langu kubwa ni maeneo ya wafugaji kuongezewa malambo. Mwaka jana malambo yaliyochimwa yalikuwa machache mno. Kwa mfano, Wilaya ya Kwimba, ambayo ni Wilaya kame kuliko Wilaya zote Mkoani Mwanza ilichimba lambo moja tu. Je, kwa hali hiyo kwa nini wafugaji wasihamie maeneo yenye maji kwa ajili ya mifugo yao?

Nitashukuru kama kwa mwaka huu wa fedha, malambo mengi zaidi yangelichimbwa. Ni vyema, serikali ikaangalia njia mbalimbali za kuongeza fedha kwa Wizara hii hasa kwenye kitengo cha malambo ili maeneo yaliyo makame zaidi yaongezewe uwezo wa kuchimba malambo zaidi.

Kuhusu nyasi; naiomba Wizara hii izidishe bidii ya kusambaza elimu na mbegu za nyasi. Nafahamu elimu hiyo na mbegu hizo zinatolewa Mabuki pia. Hisia zangu zinanituma kuamini kuwa, elimu hii haijaenea vya kutosha. Sambamba na uenezaji wa nyasi kwa ajili ya mifugo, utaalam wa kunenepesha mifugo pia ni muhimu sana. Ninaamini wafugaji wengi/wote wanatamani mifugo yao kunenepa. Wanachokosa ni utaalam; ni vyema wataalam wengi wakafanya kazi karibu na wafugaji.

Ombi la mwisho ni kuendelea kama ambavyo nimekuwa nikiomba mara kwa mara; ni Wilaya ya Kwimba hususan Jimbo la Kwimba. Kuongezewa malambo zaidi.

Wafugaji wa Wilaya na Jimbo la Kwimba, kupatiwa mafunzo katika Ranchi ya Mabuki. Ninawaombea wafugaji 25, wawili wawili kutoka kila Kata (mwanaume mmoja, mwanamke mmoja na kiongozi mmoja kutoka Halmashauri ya Wilaya. Katika Jimbo la Kwimba ziko Kata 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na niliyochangia, nilisahau kitu kimoja, ambacho naamini hawa ni wataalam wa ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini kabisa, Wizara hii inaweza kuwakomboa wananchi wetu walala hoi; wa kima cha chini; yaani maafisa na wataalam wa ufuguaji wa kuku wa kienyeji, wasikae mezani, wasiwe wamangimeza. Waende kuwafundisha wananchi vijijini, jinsi ya kufuga kuku wa kienyeji kisasa na kitaalam ili vijana na akina mama wapate ajira na kipato na hivyo kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa *serious,* hatuna sababu ya kuwa maskini, kwa sababu samaki ni kitoweo na kipato; ng'ombe ni nyama na biashara ndani na nje ya nchi, ngozi, viatu, *handbags* na kadhalika, kwato ni mapambo, maziwa ni lishe na kipato; kuku wa kienyeji ni lishe na kipato. Vitu hivi vidogo vidogo vinawezekana na vinaweza hasa kututoa kwenye umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwalisha.

**MHE. ARCH FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote hapo Wizarani kwa kutuletea hotuba ya bajeti nzuri pamoja na ufinyu wa pesa, hongereni sana.

Nawapongeza pia kwa juhudi wanazoendeleanazo katika kupambana na uvuvi wa zana haramu uliokuwa umeshamiri sana na tunawatia moyo kazi iendelee. Natoe ushauri katika mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine na taasisi mbalimbali kuweka mipango thabiti na endelevu ili kutatua kabisa tatizo la malisho kwa mifugo ili kuondoa kabisa hii hali inayotokea na kujirudia katika siku za hivi karibuni, wakulima na wafugaji kupigana na kuuana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Wizara ipambane sana na hawa wahuni kutoka Kenya wanaovuruga biashara ya maziwa na badala ya kukiendeleza kiwanda cha maziwa Arusha wao wanakusanya maziwa na kuyapeleka Kenya na kuja kutuuzia tena hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri Wizara iondoe kero kubwa na isiyokuwa *'fair'* pale Watanzania wanapopata *order* za ku-*supply* maziwa huko Kenya lakini wanakutana na vizingiti vingi vya kihuni sana vinavyowakwaza ndugu zetu Watanzania. Hili lazima likemewe sana tena kwa sauti ya ukali.

Nashauri kwamba Wizara iweke mizani katika minada yetu ili wafugaji wetu wasiendelee kupunjwa; Wizara kwa kushirikiana na Halmshauri zote nchini kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa; Wizara kushirikiana na wananchi/Halmashauri ya Wilaya ya Hai kuimarisha vikundi vya maziwa na hatimaye kuwa na kiwanda cha maziwa pale Bomang'ombe ambapo ni *centre* nzuri kwa ajili ya maziwa kutoka Moshi vijijini, Siha, Arumeru na Simanjiro na mwisho, Wizara ishirikiane na Halmashauri zote nchini kuhimiza unywaji wa maziwa na ulaji wa nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Mbarikiwe sana.

**MHE. SIGFREID SELEMANI NG'ITU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kitoweo kule jimboni kwangu. Hakuna ng'ombe, mbuzi wala kondoo, ila kuku tu, nao ni wachache.

Je, Wizara haiwezi kutusaidia ufugaji wa samaki? Kwa kuanzia, angalau tungepata shamba la samaki kule Mnacho, lingine Ruangwa Mjini na kule Mandawa.

Kwa kuwa mahitaji ya kitoweo ni makubwa, naogopa sana wapigakura wangu kukamatwa na askari wa Wanyamapori kwa vile tupo karibu na mbuga ya wanyama ya *Selous Game Reserve* ambako kumejaa nyati, swala, digidigi, tohe, kongoni na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali naomba tusaidiwe mapema kabla balaa hiyo haijatukuta.

**MHE. JUMA KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru *Allah Subhana-huwataallah* katika kutujalia sisi viumbe wake kujumuika kwa pamoja katika mjadala huu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli - Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akizifanya katika sekta hizi za mifugo na uvuvi. Ukweli anastahili sifa sana.

Nampongeza pia Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha -Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa jinsi anavyomsaidia Waziri mwenye dhamana katika kuiboresha Wizara hii. Nawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote kwa namna moja ama nyingine kutekeleza sera ya mifugo na uvuvi kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanzia na suala la mifugo. Katika siku ama miaka ya hivi karibuni imeibuka tabia isiyo rasmi na ambayo inataka kufanywa kuwa rasmi ya magomvi ya kugombea ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Kwa namna moja ama nyingine tabia hii inaonekana kumea kwa sababu ya baadhi ya mamlaka (viongozi) kwa

maslahi yao wanahusika katika kusababisha migogoro hii. Nasema hivi hasa baada ya kufanya utafiti na kuona uwezekano wa migogoro hii kuchochewa sana na viongozi.

Hivi kwanini mgogoro uwe mkubwa zaidi eneo moja tu tena la Kilosa peke yake? Ajabu moja, hata wawakilishi wanaokuja maeneo mbalimbali kwa madai ya kuwasilisha matatizo ya wafugaji, wengi wao ni madalali *(middle people).* Viongozi wa Serikali za Vijiji na Kata ni miongoni mwa wachochezi wa migogoro. Naomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano na Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi ili kubaini tatizo na kulimaliza kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji hawapo Kilosa peke yake, wapo Dodoma, Singida, Shinyanga, Mwanza, Manyara, Arusha na kadhalika. Mbona kote huko hakuna matatizo? Lazima tujiulize! Kwa wafugaji wa jimboni kwangu Iramba Magharibi, naiomba Wizara kuongeza ikama ya Maafisa Ugani ili waenee katika Kata zote kwa ajili ya kutoa elimu kwa wafugaji juu ya ufugaji wa kisasa. Pia watusaidie katika kuimarisha ufugaji wa zao la kuku wa kienyeji ambao ni maarufu sana kwa Wilaya ya Iramba. Kuimarisha ufugaji wa kuku kutasaidia na kuinua kipato cha wananchi wa Jimbo langu la Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mpango endelevu wa elimu bora kwa wafugaji, naomba ujenzi wa lambo la kunyweshea mifugo kijiji cha Ujungu kilichopo Kata ya Mtekente, kadhalika josho kwa maeneo ya vijiji Ujungu, Msai, Luono na kadhalika ambavyo vinahitaji sana huduma hii katika utunzaji bora wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Uvuvi, naiomba sana Wizara kutambua nafasi ya wavuvi wadogo wadogo waliopo jimboni kwangu Iramba Magharibi, wale wa Ziwa Kitangiri ambao kwa kiwango fulani hawana stadi za kutosha za uvuvi endelevu. Aidha, suala la mitaji na matumizi ya zana bora katika shughuli za uvuvi, naomba sana Wizara kutoa kipaumbele kwa Ziwa Kitangiri pengine kutambua shughuli zinazofanywa na wavuvi hawa wa Ziwa Kitangiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika sio vibaya kama Wizara itatambua juu ya mabwawa madogo madogo yanayotoa samaki yaliyopo katika la Jimbo la Iramba Magharibi kama lile la Magungumuka na Urughu, yote ya Kata ya Urughu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu ni ya tatu Afrika kwa uwingi wa mifugo hasa ng'ombe, naiomba Wizara iendelee na kampeni yake ya kuhamasisha utumiaji wa bidhaa ya maziwa halisi yatokanayo na mifugo (ng'ombe) badala ya utamaduni wa sasa uliojengeka wa kutumia maziwa ya unga kama vile *NIDO* na kadhalika.

Kwa kuwa matumizi ya maziwa halisi unahitaji maziwa haya kuchemshwa kwa kiwango cha juu kabla ya matumizi ya binadamu, naomba Wizara kupitia mamlaka zake ihamasishe uanzishaji wa viwanda vya kusindika maziwa kwa Mikoa ya kati Dodoma na Singida ili wafugaji wauze bidhaa kama maziwa kwa viwanda hivi ili wananchi kununua maziwa yaliyosindikwa yenye ubora wa TBS.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Magufuli kwa uhodari wake na ubunifu katika kuikamata meli ya uvuvi haramu iliyokuwa kwenye kanda yetu ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kwa kuanza kutoa pongezi zangu za dhati kwa waziri, naibu waziri pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na ufinyu wa bajeti wanayotengewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi naomba nichangie machache sana katika hoja aliyowasilisha Mheshimiwa waziri wa wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wizara hii imekuwa ikipata mitihani kwa wafugaji kuilalamikia serikali juu ya mifugo yao kuchukuliwa au kunyang'anywa na baadhi ya halmashauri hapa nchini kwa visingizio mbalimbali, aidha kumekuwa kukijitokeza mapigano kati ya wafugaji hao na wakulima kitu ambacho kinakuwa kinapelekea maeneo hayo kukosa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara hii inaandaa Muswada wa Sheria wa kutenga maeneo ya malisho kwa mifugo *(Grazing land and animal feed resources Bill)* na kwa kuwa Muswada huu umekamilika kwa mujibu wa taarifa ya hali ya mazingira nchini ya mwaka 2008 *(State of environment report – 2008),* Muswada huo uwasilishwe Bungeni mapema ili utekelezaji wake uanze kufanywa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutengwa kwa maeneo ya wafugaji na yale ya wakulima kutaondosa migogoro iliyopo sasa. Hata hivyo, wasiwasi wangu ni kuwa, isije ikawa maeneo yatakayotengwa kwa ajili ya mifugo hayakubaliani na nyasi au malisho ya mifugo hiyo na hivyo kusababisha vifo vingi kwa mifugo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu mwingine ni ukubwa wa maeneo yatakayotengwa ukilinganishwa na idadi ya mifugo. Naishauri Serikali iwe makini kwa wafugaji hao kuwachanganya eneo moja hasa kwa makabila ya wafugaji wana uhasama wa kuibiana mifugo kitu ambacho kitasababisha mapigano ya mara kwa mara na hatimaye vifo kwa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara hii iweke mikakati ya kuwaelimisha wafugaji wetu hao kuanza kufuga mifugo michache kwa njia ya kisasa ili kupunguza idadi kubwa ya mifugo kama ilivyo sasa na ukizingatia kuwa idadi ya watu nayo inaongezeka kwa kasi na matumizi ya ardhi nayo yanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madawa ya mifugo na elimu ya matumizi yake kwa wafugaji ni muhimu sana kwa vile inasemekana baadhi ya dawa hizo zinaharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii muhimu katika kukuza uchumi wetu imekuwa ikichangia kwa kiasi kidogo sana katika pato la Taifa. Kutokana na Serikali kutowekeza vyema katika sekta hii, naishauri Serikali ifanye mikakati ya dhati ili kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika na sekta ya uvuvi ukizingatia kuwa nchi yetu ina mito na maziwa mengi pamoja na bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kununua boti kwa ajili ya *'patrol'* kwenye maziwa yetu, Serikali iendelee kutenga fedha dhidi ya kununua boti zaidi kwa ajili ya *'patrol'* hasa katika bahari ya Hindi ili kuwakamata wale wanaohujumu rasilimali zetu hasa majangili au wavuvi haramu kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ulinzi huo, Serikali pia ifanye mikakati ya kuwekeza katika uvuvi kama ilivyo kwa sekta nyingine. Wawekezaji hao ni wale wanaoleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano ukoje kati ya Wizara hii na ile ya SMZ kiutendaji na utoaji wa misaada ya vifaa vya uvuvi kwa upande huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii pamoja na kwamba fedha walizotengewa hazikidhi haja, hata hivyo Serikali itaendelea kutafuta namna ya kuiongezea Wizara hii muhimu kwa miaka inayofuata.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba la Ng'ombe la Kitulo lililopo Makete Mkoani Iringa ni maarufu kwa ng'ombe wa maziwa nchini. Hili ni shamba kubwa na la zamani. Kutokana na ubovu wa barabara zinazoingia na kutoka Kitulo, usafirishaji wa bidhaa ya maziwa huchukua muda mrefu na hivyo kuongeza bei kwa watumiaji. Wizara ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya barabara kwenye kitega uchumi hiki kikubwa ili kuongeza tija ya shamba hili la Kitulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la ng'ombe la Kitulo linazungukwa na vijiji vya Ujuni kata ya Matamba, Ipelele – Kata ya Ipelele na Ikuwo, Ivilikinge na Isapulano, lakini shamba hili halijasaidia kabisa wananchi hawa. Hakuna *'progrmme'* yoyote ya kuwasaidia wananchi hawa. Serikali/Wizara ieleze ni lini itaandaa mikakati ya wananchi kufaidika na shamba la ng'ombe Kitulo?

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya ng'ombe wa mitamba kwa sasa ni Sh.500,000/=, kiwango hiki ni kikubwa sana kwa wananchi wa kawaida. Lakini pia shamba hili limeshindwa kutoa ng'ombe wa kutosha kwenye soko la ndani na la nje. Mfano mwaka jana wakati wa sherehe za nane nane Mbeya shamba hili lilipewa ombi na ujumbe wa Malawi kupeleka/kuuza mitamba 500, kitu ambacho mpaka leo halijatekelezwa. Serikali ieleze mikakati ya kupanua shamba hili kwa maana ya kuongeza uzashaliji ili kukidhi soko la ndani na nje.

Kutokana na shamba la ng'ombe kuwa karibu na hifadhi ya Taifa ya Kitulo ni vizuri shamba la ng'ombe likaandaliwa ili watalii wanaokuja kuangalia maua na uoto wa

Kitulo wapate pia fursa ya kutembelea shamba la ng'ombe la Kitulo. Serikali ieleze mkakati wa kuboresha shamba ili litumike pia kama utalii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imejitahidi sana kupambana na uvuvi haramu. Naomba iangalie pia walanguzi wa madawa ya ruzuku ya mifugo. Wilaya ya Karagwe inao ng'ombe wengi pamoja na mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Ajabu ni kwamba dawa ya ruzuku ya mifugo haijawafikia wafugaji wa Wilaya ya Karagwe, kwa nini? Serikali itueleze kama wafugaji wa Karagwe hawastahili kupata madawa haya ya mifugo. Mheshimiwa Waziri Magufuli naamini anaweza kulitatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za chanjo ya mifugo yetu iko juu sana. Mfano, chanjo ya *Foot and Mouth disease (FMD)* ni Sh. 2,000/= Wilayani Karagwe. Bei hii ni kubwa sana kwa mfugaji wa kawaida. Serikali iangalie uwezekano wa kutoa chanjo ya ruzuku, kwani wafugaji wengi hawamudu gharama hizi na hushindwa kuchanja mifugo yao na matokeo yake ugonjwa hauishi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha *NAIC – National Artificial Insermination Couter* kilichopo Arusha na Mwanza kitengewe fedha za kutosha. Watumishi wa kanda ya ziwa wapewe magari ya kuwafikia wafugaji kwa ajili ya kuwapelekea mbegu na hewa ya *Nitrogen*. Kituo cha Kanda ya Ziwa cha Mwanza hakina magari ya kwenda Kagera, Mara, Mwanza na Shinyanga. Pia magari ya kusambaza hewa ya *nitrogen* Wilayani yanunuliwe.

Elimu ya uhamilishaji izidi kutolewa kwa wafugaji nchini kwa kupitia luninga, redio, magazeti, wataalam na kadhalika. Pia wataalam wenye ujuzi mzuri wazidi kuelimishwa kuajiriwa na kupelekwa vijijini (wakae/waishi vijijini kwa wafugaji). Vile vile Serikali iwapatie wafugaji mbegu za wanyama bure au kwa bei ya chini sana inayoweza kulipwa na wafugaji. Mbegu ziwe bora zenye viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenge maeneo ya ardhi yetu kwa ajili ya mifugo yetu. Wananchi wakipata maeneo yao yenye miundombinu ya kisasa yatageuka kuwa ya wafugaji badala ya wachungaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya 2008/09 tuliambiwa kuwa Serikali inakusudia kujenga kiwanda cha nyama mkoani Kagera. Naomba nielezwe suala hili limefikia wapi? Wananchi wa Kagera wanasubiri kiwanda hicho kwa hamu sana. Pia viwanda vya maziwa vinasubiriwa kwa hamu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshimia na taadhima naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza kwa kazi nzuri nzito na hasa katika kupambana na uvuvi haramu. Nawatia shime wasikatishwe tamaa kwa maneno ya ghiliba za baadhi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye mifugo mingi (ng'ombe/mbuzi/kondoo), lakini mazao ya mifugo hiyo haijawekwa kikamilifu:-

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwa na viwanda vya nyama na maziwa?
(b) Je, Wizara ina mikakati gani ya kubadilisha uuzaji wa mifugo katika minada iwe ya kutumia mizani badala ya utaratibu wa sasa wa kuangalia na kukadiria.

Mnada wa Nzega na hasa ule wa Ndala ni muhimu katika kupata soko la mifugo maeneo ya wilaya za Nzega, Igunga na Uyui. Kwa hiyo, naomba Wizara iimarisha mnada huu kwa kupandisha hadhi na kuuwekea vyombo vya kisasa.

Lingine ninalopenda kuuliza, ni kwamba:-

(i) Je, maendeleo ya ukarabati/ujenzi wa kiwanda cha nyama cha Shinyanga umefikiaje?

(ii) Unatarajiwa kuanza uzalishaji lini? Je, uwezo *(capacity)* wake ni kiwango gani?

(iii) Je kutakuwa na kiwanda cha ngozi pale pale?

**MHE. MGNA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namkupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wote wa Wizara yako kwa kazi nzuri ya mfano na ya kuigwa na kazi ambayo haijawahi kufanyika huko nyuma. Wakati wa Uongozi wao huu, ni mara ya kwanza meli kubwa ya kigeni iliyokuwa miongoni mwa meli nyingi zinazovua kwenye bahari ya Hindi kukamatwa ikiwa imesheheni samaki wengi ambao walikuwa watoroshwe. Sasa hivi doria nyingi zinafanyika kwenye maziwa na mito hapa nchini na jitihada zao na wasaidizi wao wanaendelea kufanikiwa kukamata nyavu nyingi zisizostashili kutumika kwenye uvuvi, mitumbwi na injini nyingi ambazo hazitumiki kihalali. Mmejitahidi sana kuwadhibiti wavuvi wanaovua kwa kutumia baruti na zana nyingine zote zisizoruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba shughuli nyingi za mifugo kuhamishiwa kwenye Halmashauri za Wilaya, bado nawapongeza sana kwa shughuli za kuendeleza mifugo yetu kwa kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaanza kufuga kisasa, kwa kupunguza makundi makubwa ya mifugo na kuanza kuwahamasisha ili wapate ng'ombe bora wanaotoa maziwa ya kutosha, nyama bora na kupata ngozi bora kwa ajili ya kuwaletea faida kubwa ya kipato. Naomba mwendelee kutoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna migongano mikubwa kati ya wafugaji na wakulima. Nawaomba sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake watumie busara zao kumaliza tatizo hili wakishirikiana na Wizara ya Kilimo, Ardhi na Mazingira. Umefika wakati wa kupima ardhi kutenganisha maeneo ya wafugaji na wakulima. Mgogoro huu ukiachiwa uendelee utasababisha kuvunjika kwa amani katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao ng'ombe wengi sana hapa nchini, kwa hiyo, tunaomba viwanda vya kusindika nyama vijengwe vya kutosha ili wafugaji wetu wapate masoko ya kuuza mifugo yao. Pia naomba viwanda vya ngozi vilivyoko vipanuliwe kwa ajili ya kutengeneza ngozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ijitahidi kutafuta madawa ya mifugo, maana kule katika Halmashauri zetu zinajitahidi lakini bado madawa hayatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida ni wafugaji sana wa kuku wa kienyeji na soko ni kubwa sana. Tunaomba Wizara sasa ianze kuviwezesha vikundi ili wafuge kuku wengi zaidi kwa faida ya wafugaji na walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima na afya kamili na kuweza kufika hapa Bungeni na kuweza kutoa maoni yangu ya hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge letu kwa kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitakuwa mtovu wa fadhila kwa kushindwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa jinsi walivyotayarisha hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kwa kuipongeza Serikali kwa jinsi walivyojitahidi kuikamata meli ya kigeni ambayo ilikuwa ikifanya uvuvi haramu katika bahari yetu ambayo kila siku kambi ya upinzani ilikuwa ikipiga kelele kwamba Serikali inaweza ikaongeza mapato ya Serikali kwa kutumia uvuvi wa bahari kuu, lakini nafikiri Serikali ilikuwa haipendi kuchukua mawazo ya upande wa pili kwa sababu labda hawaamini au dharau.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sasa kwamba Wizara hii nadhani itaamini maneno ya wapinzani baada ya kuona mali waliyoikamata kama kweli bahari inaweza kuchangia kwa asilimia kubwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapinzani wakichangia jambo zuri, basi Serikali yetu iifanyie kazi kwani sote ni Watanzania na hatuitakii mabaya nchi hii. Kuna maneno ya Waswahili wanasema: "Sote tunajenga nyumba moja, tusigombanie fito."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri: Je, ile shehena ya samaki tayari imeshauzwa au bado? Au itaishia hivyo hivyo tu, kila siku itapigwa mnada kesho mpaka wale samaki wasiwe na ladha tena washuke thamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi haramu, naipongeza Serikali kwa jitihada zake, lakini kwa nini wanawanyanyasa wavuvi wakati vile vitu haramu vinaletwa na wafanyabiashara wasioitakia mema nchi yetu? Kwa nini Serikali hawawazuii wafanyabiashara kabla vitu hivi havijauzwa? Wavuvi ni watu ambao hawajui nyavu hizi kama ni mbaya, wakati Serikali imeruhusu kuuza kwenye soko. Naomba Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wavuvi na wafanyabiashara kuhusu zana haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufugaji, sina budi kuishukuru Serikali kwa kutenga ardhi ya kutosha ili wafugaji waweze kufanya shughuli hiyo bila ya kutaabika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali katika nia yake hiyo nzuri ijitahidi kuzungumza na watendaji ambao mara nyingi huwanyanyasa wafugaji kwa visingizio tofauti pamoja na kuwanyang'anya mifugo yao waache mara mora ili kuepusha matatizo ambayo sio ya lazima na vile vile kuepusha vifo vya raia na kupoteza mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea Serikali isimamie kikamilifu mpango huu wa kuwagawia ardhi kwa mujibu wa sheria na sio kuwaachia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo, lazima Serikali ifanye mipango mahsusi ya kuwatafutia masoko katika nchi za nje ili wananchi wawe na motisha ya kufuga kisasa kwa kutegemea kuvuna kwa faida nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mkakati wa Wizara wazidishe jitihada ya kujenga viwanda vipya kwa kusindika mazao hayo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru sana kama Serikali itatekeleza mambo yote waliyoyaahidi.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kuamka salama. Pia nakupongeza wewe kwa kulisimamia Bunge lako kwa viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba uniruhusu nitoe mchango wangu katika hotuba iliyopo mbele yetu. Kabla sijatoa mchango wangu, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Magufuli pamoja na watendaji wake kwa kuwa wazi na wakweli katika azma yao ya kuondoa kero kwa wafugaji, pia kuisimamia bahari yetu na maziwa yetu katika uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania walio wengi ni wakulima na wafugaji mara nyingi Watanzania hawa huuana kama wanyama ukiangalia kosa ni kuingiliana katika maeneo. Wakulima hawako tayari kilimo chao kuvamiwa na mifugo na mfugaji anapokosa malisho ya wanyama wake hayuko tayari kumuacha mnyama wake afe. Kinachotokezea, mfugaji huongoza wanyama wake na hatimaye kuvamia mazao ya wakulima na hapo vita na matokeo yake vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha maamuzi haya yawe ya vitendo na yasibakie katika nia tu. Namwomba Mheshimiwa Magufuli afanye kila hila anusuru vifo vya Watanzania wenzetu. Mwenyezi Mungu atakupa uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusu uvuvi, nampongeza tena Mheshimiwa Magufuli kwa kazi zake za utendaji. Mheshimiwa Magufuli ana nia njema kwa nchi yake, ameweza kulinda uvuvi haramu na kila leo anatoa hukumu hapo hapo kwa wale wanaokamatwa na makosa hayo. Nyavu hutiwa moto, pia meli iliyokamatwa katika maeneo ya nchi yetu. Nampongeza Mheshimiwa Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahari, maziwa na mifugo ni maeneo yanayoweza kukuza uchumi wetu na kuliongezea Taifa mapato. Serikali kama iko tayari kukuza uchumi wetu, naomba Mheshimiwa Magufuli apewe meno ili aweze kuizalishia uchumi nchi yetu.

Mwisho, namalizia kwa kumpa hongera Mheshimiwa Waziri na Baraza lake kwa nia yao njema kwa kuiwezesha nchi yetu. Ahsante.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wameonekana kuzagaa nchi nzima hata katika Mikoa ya kilimo na kuleta majanga makubwa kwa ardhi, mashamba na hata kusababisha vifo vya wakulima. Ni juzi tu wafugaji walifika Bungeni kudai haki zao. Serikali inapaswa kuongeza umakini katika suala hili na kasi ya kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji na kujenga majosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kuiuliza Serikali, ni nani atawatetea wakulima ambao mazao yao yanaharibiwa/kuliwa na mifugo? Utetezi wa Serikali kwa wakulima hausikiki bayana, kwani Watanzania hawa wasio na sauti nani awawakilishe? Wafugaji wanaona wakiuza tu mifugo yao mkulima atanyamazishwa hata akifika Mahakamani! Naiomba Serikali isimame kidete kutetea na kulinda haki za wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kudhibiti uvuvi haramu katika maziwa na bahari zetu. Wachina walioshikwa na samaki, ni mfano wa kazi nzuri ya Serikali yetu. Lakini tumeona kupitia vyombo vya habari nyavu zisizoruhusiwa kutumika katika uvuvi zikichomwa moto. Umakini huo wa kuthibitisha samaki wadogo wanaachwa ziwani/baharini itasababisha uvuvi endelevu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi katika Ziwa Tanganyika unahitaji zana za kisasa za uvuvi. Kadhalika ziwa Rukwa; nachukua fursa hii kuiomba Serikali kuwasaidia

wavuvi katika maziwa yaliyotajwa ili wananchi wa Rukwa tufaidike na maziwa hayo kwa kula na kuuza samaki. Suala la Serikali kuongeza kina cha maziwa yetu kinastahili pongezi kwani ziwa Rukwa kwa mfano linazidi kujaa tope, jmbo ambalo ni hatari kwa viumbe hai na pia kwa ziwa kukauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimwa Naibu Spika, napenda kuitumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa Magufuli, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dr. Wanyancha, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye lengo la kuboresha huduma ya Wizara hii pamoja na kuinua pato la nchi kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Magufuli ambaye ameiweka Wizara hii kwenye ramani ya kujulikana kwa mambo mengi mazuri aliyoyafanya mfano kukamata meli iliyokuwa inavua samaki kwa njia ya wizi na kadhalika. Ninamwombea Mungu aendelee kumpa nguvu, afya, maisha marefu pamoja na Mheshimiwa Dr. Wanyancha na watendaji wote ili waweze kutekeleza malengo yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuijulisha Serikali kuwa Mkoa wa Singida una ng'ombe wengi sana ambao wanatoa maziwa mengi sana mpaka yanafikia hatua kukosa watumiaji. Kwa vile iko njia ya kisasa kutengeneza maziwa ili yaweze kutumika muda mrefu bila kuharibika na kupeleka hata Mikoa mingine, ninaiomba Serikali ifikirie uwezekano wa kuleta mwekezaji ambaye atajenga kiwanda cha kusindika maziwa Mkoani Singida. Nitafurahi endapo Mheshimiwa Waziri atatoa majibu kwa maombi yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kila sababu ya kujivuna, kwani kati ya Mikoa yenye mifugo mingi ni pamoja na Singida. Mifugo hii ni mingi mpaka inafikia hatua, malisho ya mifugo hii inakuwa haba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali itoe elimu kwa wafugaji namna ya ufugaji bora pamoja na kupunguza mifugo. Nina imani mifugo ikipungua itasaidia wafugaji kuweza kuihudumia vizuri ili iwe na afya nzuri jambo ambalo litaongeza soko la mifugo yetu kwa lengo la kuinua uchumi kupitia mifugo. Nina imani ushauri wangu utapokelewa na kutolewa maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida ni Mkoa wa kwanza kwa umaskini, jambo ambalo linashangaza watu wengi nikiwemo mimi mwenyewe. Katika mambo ambayo yanasababisha taarifa hii tata ni pamoja na kukosekana kwa kumbukumbu sahihi pamoja na mizani minadani ambayo itatoa uzito wa mifugo yote inayouzwa minadani ili kuleta takwimu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali sasa kuweka mizani minadani kote pamoja na Singida

Mheshimiwa Naibu Spika, nina faraja ya pekee kwani Mungu alitupa maziwa madogo madogo ambayo yamefanya Mkoa wetu kuvutia pamoja na kupata kitoweo cha samaki. Kwa kuwa samaki hawa sio wengi na maziwa haya sasa yana maji mengi yasiyopungua, ninaiomba Serikali kuelekeza wataalam sasa kupandikiza samaki kutoka maziwa mengine ili maziwa yetu ya Kitangiri, Singidani na Kindai ya Singida Mjini yaweze kuwa na samaki wa kutosha wananchi wa Singida pamoja na kuuza Mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna tatizo la vijiji mbalimbali kutokutenga maeneo ya wafugaji kulishia mifugo yao jambo ambalo linawapa kero wenye malisho, hatimaye huchungia hata kwenye mimea iliyolimwa kwa ajili ya chakula au mazao ya biashara. Ninaomba agizo hili liwe na msisitizo ili maeneo yatengwe kwa ajili ya malisho ya mifugo na kutokuingiliwa na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kuunga mkoa hoja hii mia kwa mia nikitegemea kuwa michango yangu itajibiwa. Vile vile nimalizie kwa kuwatakia kheri katika utekelezaji wa bajeti yao.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa hili linaweza kubadili mitazamo na kuangalia mifugo kama kichocheo cha maendeleo ya nchi, lakini maadam bado tunatazama mifugo kama ni tatizo, tumeshindwa kuandaa mipango ili nchi inufaike kutokana na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwepo na kutoelewana kati ya wakulima na wafugaji. Nadhani Serikali ndiyo inapaswa kulaumiwa na wala sio wafugaji au wakulima kwa kushindwa kusimamia vyema matumizi bora ya ardhi ambayo tunayo na sasa Serikali imeamua kupeleka ardhi hii mnadani kutafuta wawekezaji wakati wananchi wake wanagombana na hata kusababisha vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kama hakuna usimamizi bora tatizo hili litaendelea mwaka hadi mwaka na uharibifu wa mazingira utaendelea kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kwa sababu Serikali imeshindwa kutoa majawabu ya tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira ni jambo moja na jema kuwahamisha wafugaji katika staili; kama ile iliyofanyika Mpanda ni dhuluma na uonevu mkubwa ambao wafugaji walifanyiwa na hauvumiliki hata kidogo na hasa ukiangalia Katiba ya Nchi inatoa haki ya kumiliki mali na wala hakuna sheria ambayo imeweka kikomo cha umiliki wa mali kwa raia, pia haki ya kwenda unapotaka na maadam hakuna eneo ambalo kwa mujibu wa sheria za nchi zimepiga marufuku kupeleka mifugo katika maeneo hayo na ni dhahiri maeneo yaliyopigwa marufuku hakuna mifugo kama vile hifadhi za Taifa isipokuwa Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni dhahiri kwamba yamekuwepo malalamiko ya kweli ya wakulima juu ya uharibifu unaofanywa na wafugaji lakini kama nilivyotangulia kusema, Serikali inapaswa kubeba lawama kwa sababu imeshindwa kutenga maeneo ya wafugaji *(ranch)* na pale palipokuwa na Ranchi za Taifa wamebadili matumizi bila kuwafikiria wafugaji wakati maeneo hayo tayari yana miundombinu kwa kuhudumia mifugo.

Ni lazima sasa iwepo mipango madhubuti ya matumizi ya raslimali ardhi na kufanya mifugo kuchangia pato la Taifa kwa kuweka masoko ya uhakika ya mifugo, viwanda vya kusindika nyama na ngozi. Kutenga *Zone* za Ufugaji na idadi inayotakiwa katika *zone* hiyo na ziada yake ipelekwe katika masoko wafugaji wapewe elimu ya kutosha juu ya ufugaji bora na wa kisasa. Mipaka kati ya wakulima na wafugaji ieleweke na kuheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimalizie kuangalia uvuvi na hususan Ziwa Tanganyika. Hivi Serikali ina mipango gani ya kuwasaidia wavuvi katika Ziwa Tanganyika kwa kuwapa mikopo ili kuwa na nyenzo bora na za kisasa za uvuvi? Ziwa hili linayo hazina kubwa, pia ni lazima kuwepo viwanda ambavyo vitatumika kusindika samaki wanaovuliwa. Hivi sasa samaki wote wanapelekwa Zambia (Mpulungu) ambako wana kiwanda wakati wana eneo dogo la uvuvi, lakini samaki wa Ziwa Tanganyika wanafika sokoni Lusaka wakati sisi tunashindwa kufikisha samaki wetu Tabora, Dodoma au Dar es Salaam. Naomba Waziri atueleze mpango mahsusi kwa Ziwa Tanganyika ambao utanufaisha wavuvi na Watanzania. Wakati wa kuvuna raslimali katika ziwa hili ni sasa na uwe endelevu na sio uvuvi holela kama ulivyokuwa katika Ziwa Victoria. Ni lazima Wizara itoe kipaumbele katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. SUSAN LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa wingi wa mifugo, lakini cha ajabu, bado wananchi wake hawana uwezo wa kunywa maziwa au kula nyama kama inavyohitajika kwa kukosa fedha au elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa bidhaa hizo. Pamoja na mifugo mingi tuliyonayo, bado wafugaji wanashindwa kufuga kwa tija na badala yake kuwa na mifugo mingi bila kuwa na tija. Mara nyingi mifugo hii inakuwa dhaifu na hivyo hata ubora na mapato yenye tija hayapo. Mfugaji anakuwa hana afya bora na mifugo pia hudhoofu na kufa kutokana na kusafiri mwendo mrefu bila chakula na maji.

Ni wazi kuwa ongezeko la watu hapa nchini limefanya maeneo mengi yatumike kwa kilimo. Hali hii imeleta mtafaruku mkubwa na hata migogoro iliyosababisha vifo na mali nyingi kuharibika ikiwemo nyumba na mazao kuchomwa moto. Hali hii isipothibitiwa nchi hii inaweza kuingia katika mtikisiko na machafuko makubwa. Ni vyema basi elimu itolewe ili wafugaji wajue sehemu zao na wasivamie mashamba kwani wote tunajua kuwa wakulima na wafugaji wanategemeana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa za samaki zinatusaidia sana hasa kwa *protein*. Wote tunajua jinsi samaki walivyo na virutubisho wataalam wanasema watoto

waliozaliwa na kina mama waliokula samaki, basi *IQ* zao ziko juu sana (wana uelewa) mkubwa sana ukilinganisha na waliokula maharage. Lakini ni jambo la kusikitisha kuona jinsi wavuvi wanavyovua kwa kutumia dhana haramu kama kokoro, baruti na kadhalika. Hii ni hatari sana, kwani samaki wanatoweka lakini pia inahatarisha afya za walaji.

Naipongeza Serikali kwa jinsi walivyoweza kuikamata meli iliyokuwa inavua katika bahari yetu. Cha ajabu, hadi leo hatuambiwi ni kiasi gani kimeuzwa na je, kuna faida kiasi gani cha kuuza samaki hao ukilinganisha na gharama za kuwahifadhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba sekta ya usindikaji si bora sana hapa nchini. Viwanda vingi vya usindikaji vimekufa mfano *Tanganyika Packers* – Dar es Salaam. Toka kilipochukuliwa na wawekezaji hadi leo kimebaki gofu na hivyo kuendelea kuletewa nyama toka nje ya nchi kwa bei kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina migodi mingi ya madini tena mikubwa kama ile ya *Barrick, Geita Gold Mines,* Bulyanhulu nakadhalika. Migodi hii inaajiri watu wengi sana ambapo naamini kama bidhaa zitokanazo na mifugo zingetoka nchini, basi pato la Taifa lingepanda sana. Serikali inaweza kutueleza ni kwa nini bidhaa za nyama na maziwa kwa migodi kama *Barrick, North Mara* zitoke Kenya na sio Tanzania? Hii ni aibu kubwa sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa tufuge kisasa hasa kuwa na maeneo ya ufugaji ili migogoro hiyo ya wafugaji iishe kwani tunaweza kuingia katika vita visivyo vya lazima. Lakini pia Serikali itoe kipaumbele kwa wafugaji hasa kwa madawa na Maafisa ugani hususan mabwana afya ili wasaidie wafugaji wetu. Kilimo kwanza kitahitaji pia samadi itokanayo na mifugo. Hivyo tuendeleze mifugo yetu.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe malalamiko yangu pamoja na kumwuliza maswali mengi hapa Bungeni na kujibiwa, sioni mabadiliko yoyote, wananchi wanapata matatizo. Naomba nipate majibu ya kuridhisha kwanza wavuvi pamoja na wafugaji. Je, zana haramu wananchi wanazitoa wapi kama sio kutengenezwa na viwanda na kuziuza madukani? Ni kwanini Wizara au Serikali isidhibiti vitu hivyo viwili tuone vinatoka wapi? Je, tangu zana haramu zimeanza kuchomwa na kukamatw, ni viwanda vingapi vimesimamishwa au maduka mangapi yamekamatwa au ni wangapi walitengeneza?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu na ninaomba nifafanuliwe ni zana za aina gani za kutumia na zinapatikana wapi na ni kwanini Serikali isifanye mikakati madhubuti kwa wananchi wetu hasa masikini wenye kipato kidogo angalau wakakopeshwa, kuliko kuwapa mikopo ya pesa wakopeshwe zana hizo? Naomba wavuvi wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji Tanzania tuna ardhi kubwa sana na toka zamani wafugaji walikuwa sio wengi kama siku hizi. Hapa Wizara ifanye kazi yake

kuwatengea sehemu yake na wasikae karibu na wakulima kupunguza migogoro isiyokwisha na kuwavamia wakulima. Hayo ndiyo matatizo ya wananchi, ukizingatia sisi wote ni Watanzania, hasa sisi Wahaya huwa tunaamini tuna makazi ya kudumu, leo hii wanaleta mtu eti mfugaji, ondokeni: Je, aende wapi? Hana pa kwenda. Je, hiyo ni haki?

Naomba Wizara hii ifanye mambo yafuatayo kuunda tume kwenda Kitengule pamoja na Bubale Kakunyu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie na wasikurudishie njiani. Mchezo mchafu huo kusudi usione athari zilizoko. Naamini kaka yangu utafanya hivyo ujionee, usingoje kuambiwa. Maliza migogoro haraka ili wananchi wawe na amani na kuendelea kufanya kazi zao za kujenga Taifa. Mpaka hivi sasa hakuna chochote kinachofanyika si kulima wala kufuga. Wengine wanawekwa ndani pamoja na kupigwa, wengine ni walemavu, fika ujionee mwenyewe kinachoendelea. Wavuvi wa Mkoa wa Kagera wameunda makundi ya wajasiria lakini hawasaidiwi wala wakiomba mikopo hawapati jibu. Wanalojibiwa ni kuwa, tukiwapa pesa mtazirudisha na nini na zana zenu zinakamatwa? Je mtazitoa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba hawa watu wasaidiwe na kuhakikisha viwanda au Serikali kuleta zana halali. Majosho katika Mkoa wa Kagera yalikufa na sioni mikakati yoyote ya kuyafufua. Je, ni lini Serikali itatenga pesa ya kuyafufua?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kiwanda cha maziwa Bukoba Mjini kiboreshwe. Kikiboreshwa kitasaidia wafugaji kuuza maziwa yao kwa sasa kina sua sua. Chuo cha mifugo Maluku hivyo hivyo kinasuasua, yote hayo kazi kwako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumaini nitajibiwa kwa ufasaha.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Watendaji wa Wizara kwa ujumla kwa jitihada wanazozichukua katika kuboresha sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba sekta hii imeajiri Watanzania wengi lakini ni ukweli usiopingika pia kwamba sekta hii ni moja ya sekta inayorudi nyuma mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pato la mifugo na mazao yake katika kuchangia pato la Taifa bado ni kidogo sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mikakati mbalimbali iliyoanzishwa ili kuboresha sekta hii, lakini bado tumekuwa na mtazamo potofu wa kuiangalia sekta hii bila ya kutoa vipaumbele kwenye ile Mikoa ambayo imerekodi kuwepo kwa mifugo mingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mikoa ya Shinyanga, Arusha, Mara na Dodoma ndiyo yenye mifugo mingi ukiacha Mikoa ya Pwani. Lakini binafsi nilitegemea Mikoa hii ingesheheni nyenzo mbalimbali za kuendeleza sekta hii kama ilivyo kwa

kilimo ambapo vipaumbele vya kilimo vimeelekezwa katika Mikoa mitano tu ambayo imeonyesha uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kiwango kikubwa kuliko Mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni kwa nini vipaumbele vya mifugo, mfano viwanda vya kusindika nyama, maziwa na ngozi haivijajengwa kwenye hiyo Mikoa niliyoitaja hapo juu ili kuongeza pato la Taifa kutokana na ufugaji kwa wingi kwenye Mikoa hii??

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia Mheshimiwa Waziri anieleze, ni kwa nini mazao yetu ya mifugo hayaonekani katika *super markets* zetu kwa wingi kama mazao ya mifugo toka nchi za nje? Je, ni kwa nini turuhusu vibali vya kuingiza mazao ya mifugo toka nje wakati wafugaji wetu hawajui wapi wauze mazao yao hali inayopelekea wafugaji wetu kukata tamaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na sekta ya kilimo bado tunao upungufu mkubwa wa madaktari wa mifugo na *Animal Health Officers* na *Animal Production Officers*. Je, ni nini mikakati ya Wizara katika kuwapata wataalamu hawa hasa tukizingatia uchache wa vyuo vya mifugo hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni ipi mikakati ya kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi wa fani ya mifugo wanapatikana hasa ikizingatiwa wanafunzi wengi huikimbia fani hii kutokana na *perception* kwamba fani hii ni ngumu sana na haina *future*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na utengenezaji holela wa vyakula vya mifugo bila kuzingatia utaalamu jambo ambalo limepelekea madhara makubwa kwa walaji. Mfano, walaji wa kuku wameathirika na watoto kupevuka kabla ya umri wao na wanawake kuota ndevu, kuongezeka matiti na makalio kutokana na uchanganyaji wa vyakula hivyo na madawa yenye *hormone* mbalimbali. Je, Wizara imejipanga vipi kudhibiti tatizo hili? Kwani limeleta hofu kubwa sana katika kutumia mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze: Je, upo udhibiti kiasi gani wa nyama za mifugo zinazouzwa kwenye *butcher* zetu? Mara nyingi nyama kwenye *butcher* zetu zimeonyesha kutokufaa kwa walaj, mfano *TB* imethibitika kuenea kwa kiasi kikubwa kutokana na walaji wa nyama toka za ng'ombe mwenye *TB*, maini kwenye *butcher* zetu hukutwa na *neverflukes* waziwazi. Je, ni sheria gani imewekwa ili kuwabana hawa *meat inspectors* ambao hawatimizi wajibu wao katika suala zima la ukaguzi wa nyama kabla ya kuingia buchani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata majibu ya hayo maswali yangu hapo juu na naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu

kwa kazi nzuri za kuendeleza maendeleo ya mifugo na ulinzi na uendelezaji wa sekta ya uvuvi. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri ufuatao:-

(a) Wizara ifanye kazi karibu na Halmashauri za Wilaya zenye mifugo mingi ili kuhakikisha kuwa penye mifugo mingi ndipo pawe na malambo na majosho ya kutosha mfano Mkoani Shinyanga, Mwanza, Tabora, Dodoma na kadhalika.

(b) Wizara iongeze nguvu ya kushawishi wafugaji kuwa na mashamba ya malisho ili kupunguza tatizo la uhamaji. Halmashauri zihusike vilivyo.

*(c)* *NARCO* iwezeshwe zaidi kuweza kupata mikopo benki ili iweze kuboresha mashamba yake na mifugo yake. Kwa sasa mashamba ya *NARCO* yaliyo mengi bado siyo mazuri.

(d) Serikali ifute ushuru/tozo katika vifaa vya uzalishaji/usindikaji maziwa na vifungashio vyake na bidhaa za maziwa na nyama zinazozalishwa nchini ili kuchochea uzalishaji na ulaji/mauzo ya bidhaa hizo nchini. Kodi ibaki ya makampuni tu *(corporate tax).*

(e) Mifugo ithaminiwe kwa kuwa ni uchumi wa nchi. Kinachotakiwa ni kuuibua uchumi huu kuliko kuudharau.

(f) Hivyo, unyanyasaji wa aina mbali mbali kwa wafugaji haukubaliki, ukomeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kheri.

**MHE. ENG. DR. JAMES ALEX MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kumpongeza sana Mheshimwa Waziri John Pombe Magufuli kwa jitihada zake kubwa zinazoendelea kuboresha masuala yote ya maendeleo ya mifigo nchini pamoja na kufanya uvuvi nchini uwe endelevu na wenye manufaa kwa wavuv wadogo wadogo pia.

Pili, nampongeza sana Naibu Waziri - Mheshimiwa Dr. James Wanyancha kwa kujituma katika kumsaidia Waziri wake. Pia, nawapongeza sana Katibu mkuu na wataalamu wote wa Wizara kwa utendaji wao wakazi unaoendelea kuboreka. Hata hivyo, bado wanayo fursa na haja kubwa kuongeza juhudi hizo huku wakiweka umuhimu katika elimu na ufanisi wa wafugaji wadogo wadogo pamoja na wenzao wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na mipango na juhudi za Wizara katika kutaka kuwageuza wachungaji wetu ili wawe wafugaji. Ufugaji huo uwe wa mahali maalum (ranchi) badala ya kuwaacha wakizagaa nchi nzima kiasi cha kupelekea hata ugomvi kwa wakulima. Pia hakika kuna haja ya kuwaelimisha na baadaye kuwataka wafugaji wetu wawe, kila mfugaji ama kwa ushirika na eneo lao maalum ambalo pia watafikiwa na kupewa huduma za ugani kwa urahisi. Wakiwa katika maeneo yao (bila

kuhamahama) pia suala zima la kuongeza thamani ya mazao yao ya mifugo litakuwa rahisi kutekelezwa, kama ambavyo pia tutaondokana na tatizo la kutafuta malisho ya asili peke yake.

Mheshimiwa Spika, mifugo yetu imekuwa mingi mno lakini yenye tija kidogo sana na ubora hafifu. Tunahitaji kuona haya yanabadilika kiasi kwamba mafanikio yaweze kuhesabika kila mwaka. Vivyo hivyo tunaweza kusema kwa wavuvi wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inafurahisha kuona kuwa tuna akiba kubwa ya nyaraka, mikakati na mipango ya kufanya hivyo, inafurahisha pia kutambua mifano ya kuigwa ipo hapa nchini kupitia kwa wataalam wengi, taasisi mpya za Serikali na hata mashirika mengi yasiyo ya kiserikali ambapo uzoefu mkubwa umekusanywa. Kinachohitajika ni kusambaza haya yote ili yawafikie walengwa. Hili ndilo la kufanya kwa sasa. Tunahitaji kusambaza uzoefu huo kwa upana na kasi zaidi, lakini pia kwa msisitizo, kwa mujibu wa sheria, sheria ndogo tulizonazo katika Halmashauri za Wilaya zetu.

Hiari ya wafugaji na wavuvi wadogo bado ni muhimu sana na hasa kama inatokana na elimu inayofikishwa kwao. Lakini pia Serikali na hasa zile za vijiji katika maeneo, zinahitaji kusimamia kwa karibu hayo yote kwa kutumia sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema hapa ni kwamba, palipo na sheria, kanuni na sheria ndogo za Halmashauri, basi hizo ndizo ziwe vipimo vyetu vya usimamizi wa sekta hizi ndogo za uchumi. Muundo wa Serikali unatosheleza, watendaji wa ngazi mbalimbali wawepo na wajengewe uwezo zaidi na yote yataanza kuongeza mafanikio ya kasi inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize maelezo yangu mafupi kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, huku pia nikisisitiza kuwa tuna maandalizi ya kutosha katika kuisimamia sekta hii kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja. Nawapongeza kwa hotuba nzuri na hongereni kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhimiza utunzaji wa mali za baharini kama vile samaki na vitu vingine. Pamoja na hilo, wananchi wengi wa mwambao wa Pwani ya bahari ya Hindi hawapati samaki wengi kutokana na kuvua kwa kutumia zana za kale. Nafahamu mradi wa *MACEMP,* naomba uboreshwe na uanze sasa kutoa elimu kwa wavuvi na kuwakopesha zana bora za uvuvi kama vile nyavu zinazotakiwa, mashine za boti na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, tutaendeleza uvuvi badala ya kung'ang'ania kupambana na wavuvi hali ya kuwa hakuna juhudi za kuwaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwe na wepesi wa kujibu barua zenye mapendekezo hasa ya kuendeleza uvuvi badala ya kuelekeza upande mmoja tu. Naamini Wizara inakumbuka juhudi zangu za kumleta mwekezaji wa zana za uvuvi kutoka Japan ambapo niliwasilisha andiko mradi, mawasiliano ya Bwana Yamoto zikiwepo namba za barua na baruapepe, lakini hadi leo sina taarifa ya nini kinaendelea zaidi ya barua ya Naibu Waziri kuniomba niwe na subira na nizidi kumpatia ushirikiano. Imenishangaza kuona viwanda Mwanza na kwingineko lakini kule Tanga ikaonekana hakuna maana. Imeniuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara inunue boti ziendezo kasi ili zitumike kwenye doria baharini kupambana na wavuvi kutoka nchi jirani ambao huingia hadi bahari kuu kuvua na kuondoka hali ya kuwa wakazi wa Tanga hawapati samaki wa maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotolewa za *MACEMP* ni vyema zikapelekwa kwa wakati na kuwepo na mtiririko mzuri ili miradi iweze kuendelezwa kwa kasi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tanga umeathiriwa kwa kiasi kikubwa na mifugo ilitoka Mikoa ya Kaskazini na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, mashamba kushambuliwa na mifugo na hivyo kuhatarisha amani katika wafugaji na wakulima. Ninashauri elimu zaidi itolewe kwa kuwafundisha kuotesha majani kwenye maeneo yao ili mifugo yao isihangaike kwenda Mikoa mingine.

Aidha, ninashauri kupunguzwa kwa gharama za dawa mifugo na pembejeo nyingine ili kumotisha wafugaji nao waweze kukuza pato lao. Naamini tunaweza tunahitaji kujipanga vizuri na kujitoa zaidi kwa wananchi wetu.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa ambayo kwa hakika iliandaliwa vizuri. Nampongeza yeye binafsi, Naibu Waziri pamoja na wataalamu wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha kwa kujibu hoja za Wabunge, atoe maelezo ya kueleweka kwa wafugaji wa ng'ombe wakuu kanda ambao wamekuwa wakihangaika na mifugo yao kwa kuhamishwa kila wakati na mifugo. Sasa hivi mifugo yao inakufa kutokana na kuhamishiwa maeneo yasiyofaa kwa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wamekuwa wakija hapa Dodoma na kukutana na viongozi wa Wizara na kwa maagizo maalum tangu mwaka 2006, bila mafanikio. Mimi nikiwa mwakilishi wao, naomba Serikali itoe hatima ya wananchi hawa na mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni majuzi tu Serikali imetangaza kuwatambua wafugaji pamoja na mifugo yao. Ni matumaini yangu kuwa hawa watu watatendewa haki tofauti

na walivyotendewa kwa shinikizo la baadhi ya viongozi waliokuwa na chuki na wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaarifu wananchi hao ambao ni wafugaji wakiwa ni Watusi waliohamia miaka 40 iliyopita wasikilize kauli ya Serikali kuhusu hatima yao wakati Mheshimiwa Waziri akijibu hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji katika Mkoa wa Kigoma wanao uhaba mkubwa wa majosho. Naiomba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia kwa kujenga majosho ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa nafasi hii ili nitoe mchango wangu. Kabla ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya kusimamia rasilimali za umma, pia pongezi ziende kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa umahiri walioonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Wizara hii haipewi kipaumbele katika bajeti yake. Tunaishauri Serikali ilione hilo, bajeti ijayo ijionyeshe waziwazi kuongezewa pesa ili iweze kukamilisha mipango yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu nilichangia kwa kutaka kujua hatua za utekelezaji juu ya uonevu uliofanywa na Halmashauri za Kilosa, Mpanda, Urambo, Sumbawanga na kadhalika. Mambo yaliyojitokeza ni ukiukwaji wa Katiba na ahadi ya Serikali ilikuwa kuwarudishia pesa zao na mifugo, lakini hawajafanya hivyo. Naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyopita niliiomba Wizara itoe lambo moja, yaani Serikali kuu isaidiane na Halmashauri ili wananchi wa Kata ya Mwaniko waweze kupata maji kwa ajili ya mifugo yao. Naomba sana nifikiriwe katika bajeti hii hata kama ni kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu minada ya Upili, Misungwi inao mnada unaojengwa na Serikali kwa usimamizi wa Serikali kuu. Cha ajabu, manada huo unasuasua, wala taarifa kwa Halmashauri hakuna. Naiomba sana Serikali kuu ifuatilie ni nini kimefanyika kulingana na pesa walizotoa, huenda kuna mwanya wa matunmizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa usimamizi mzuri kwa kampuni ya *NARCO*. Kitu hiki kimepongezwa pia na Kamati ya Bunge hasa katika mchakato mzima wa ujenzi wa machinjio ya Kisasa ya RUVU. Mkataba kati ya *NARCO* na JKT ni mambo ambayo Watanzania wengi wamekipongeza kitendo hicho tunaomba sana, Serikali iwe karibu sana na *NARCO* kuhakikisha machinjio hiyo inakamilika kama

mkataba ulivyo. Hii ni kuepuka kuingia hasara kwa pande zote mbili. Tuna imani na Mheshimiwa Waziri kuwa kazi ya machinjio hiyo itakwisha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mitamba imeonekana katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, shamba la uzalishaji Mitamba la Mabuki ni kati ya mashamba yanayofanya vizuri. Naomba sana Serikali pamoja na bajeti ndogo ifikirie kuwawezesha watendaji katika shamba hilo la Mabuki ili baadhi ya matatizo yao yapunguwe. Matatizo hayo ni pamoja na kuchimba lambo kubwa kwa ajili ya mifugo ya shamba hilo na mengine kama walivyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utafiti ni tatizo kubwa hapa nchini kwa vile huwa hawapewi pesa za kutosha kufanya utafiti ikiwemo vitendea kazi pamoja na bajeti hii ndogo Wizara ione umuhimu wa watafiti ili waweze kutenda kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Wizara ni mengi, lakini kwa vile bajeti ni ndogo, tunashindwa kueleza, kwani tutakuwa tumelundika matatizo, hivyo ni vyema yaliyopangwa yatekelezwe kwa ufanisi ili mwakani tuendelee kupunguza matatizo tuliyoyatolea ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Bunge lifahamu kuwa wafugaji wamekuwa ni watu ambao Serikali yao haijawasikiliza shida zao hasa maeneo ya malisho, malambo kwa ajili ya maji ya mifugo yao masoko kwa ajili ya kuuza mifugo yao na hata soko likipatikana vizuizi vinakuwepo kukwamisha soko hilo. Naomba Serikali iliangalie suala hili kwani ni tatizo kubwa kwa wafugaji. Waandaliwe ili waweze kutoa mchango mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika mipango yake juu ya mapunjo mbalimbali ya watumishi na ni vyema ukayalipa, upandishwaji wa vyeo uendane na mishahara. Jambo hili lisije likawa kama sekta ya elimu, ni vyema kumbukumbu za watumishi wetu wa Wizara zikawa vizuri na haki zao wapatiwe kwa wakati.

Mwisho, nimtaki utekelezaji mwema Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu kwa bajeti hii mliyopewa. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kupata nafasi kwa kuchangia hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Namshukuru sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Naibu Naziri kwa hotuba yake. Napenda kumshukuru Waziri - Mheshimiwa Magufuli kwa namna anavyoongoza Wizara mbalimbali anazokuwa anapangwa. Nakumbuka namna alivyoongoza Wizara ya Ujenzi, sasa miundombinu kwa juhudi na maarifa na hekima kubwa alivyokuwa kiongozi wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kujenga kiwanda cha kusindika nyama katika Wilaya ya Tarime, kujenga kiwanda kitasaidia sana kupunguza wezi wa mifugo ambao husababisha mapigano baina ya Wilaya ya Rorya na Tarime na mapigano kati ya koo na koo. Kwa kuwa bei ya ng'ombe nchini Kenya imepanda sana,

wezi wa mifugo huiba ng'ombe Tanzania hasa katika Wilaya za Tarime, Rorya na Serengeti na kuzipeleka Kenya katika kiwanda cha *Kenya meat* ambapo kiwanda hutoa bei nzuri ambayo huhamasisha wezi kutumia silaha nzito kuibia ng'ombe, kwa kujenga kiwanda itapunguza kwa kiasi kikubwa wezi wa mifugo Wilayani Tarime.

Naushauri Serikali kuelimisha wananchi na umuhimu wa wafugaji kuwa na Bima ya Mifugo ili wafidiwe mara wanapoibiwa, magonjwa yanapotokea na kusababisha vifo. Naishauri Serikali kuwa na Wizara ya Kilimo na Mifugo, sioni sababu ya kutenganisha kilimo na mifugo. Kama kutakuwa na Waziri wa Kilimo na Mifugo ni rahisi Waziri kushughulikia ugomvi uliopo kati ya wakulima na wafugaji.

Pia nashauri Serikali iongeze kuchimba malambo kwa ajili ya mifugo ili kuepuka ukamataji wa mifugo pale panapokuwa na ukame ambapo wananchi hupeleka mifugo kutafuta malisho na maji katika hifadhi za wanyamapori hasa maeneo ya Lamwai.

Serikali iendelee kujenga mabwawa na majosho kwa ajili ya mifugo na kutoa chanjo kwa mbwa hasa chanjo ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Naishauri Serikali kuanzisha mnada wa kimataifa Wilayani Tarime ili kupunguza magendo ya ng'ombe mpakani, yaani Sirari na Isibania Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima na wafugaji hasa wafugaji watengewe maeneo ya malisho na kusaidia kufundisha wafugaji kupunguza idadi ya mifugo ili pasiwepo na ugomvi wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangua hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa Magufuli pamoja na Naibu Waziri kwa kutuletea bajeti hii, kwani inapendeza kwa maandishi, pia naomba ipendeze kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji au wavuvi wengi, ni watu wa hali ya chini sana, zana zao wanazotumia ni duni, hasa pale Serikali inaposema kuna utumiaji wa nyavu zisizofaa. Sio haki, hata na mimi naafiki hilo, kwani hakuna mtu mwenye akili timamu akatetea nyavu zisizofaa. Lakini basi tunaomba pale ambapo watu hawa wanapokamatwa na nyavu zisizofaa, ni bora wakapewa nyavu zinazofaa kuliko kusubiri kuibua kwao kwa miradi, kama ambavyo alivyojibu Naibu Waziri kwa swali la Mheshimiwa Savelina Mwijage la tarehe 30 Juni, 2009.

Wavuvi wengi sana hawana elimu ya kutosha, hawana utaalamu wa kutosha, sasa basi ni nani atawakusanya na kuwashauri kuibua miradi? Mimi naiomba Serikali kuwa wavuvi hawa wanaponyang'anywa nyavu zisizofaa, basi wakopeshwe nyavu zinazofaa ili waweze kujiendeshea maisha yao ya kila siku.

Hivi karibuni katika Mwalo wa Kabangaje kumekuja tabia kwamba, mvuvi anapohamia hapo hata kama ametokea Sengerema, Sengerema ni miongoni mwa Ziwa

Victoria na pia ni Mkoa wa Mwanza, ni vipi mvuvi huyu akatozwa ushuru Sengerema na mara afikapo Ilemela atoe ushuru tena? Hii ni dhambi kubwa kwamba baada ya mvuvi kutoa rushwa anaruhusiwa na kwa yule ambaye hana, basi atataabika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *BMU* hukusanya ushuru, lakini hata huduma za choo hakuna kama vile Mwalo wa Bwiru Mchangani na mialo mingine kama Bezi na na kadhalika. Tunawaombeni washiriki wa sera ya uvuvi mtazame utendaji wa watu wengi wa chini. Wengi wao sio waadilifu na ni mabingwa wa uonevu. Pia rushwa na oparesheni za kushitukiza ili kujitafutia rushwa. Pengine hata askari nyama hawatumiwi, ni askari wa usalama wa raia (Polisi) ndio wanaotumika. Sasa basi, pangeni utaratibu ili wavuvi waweze kujitafutia maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ngozi na kiwanda cha Ngozi Mwanza, hivi kweli chuo kiwepo na kiwanda kuuzwa na kuwa stoo: Je, suala hili limefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wafugaji wapatiwe mikopo na mafunzo ya ufugaji bora, pia unenepeshaji wa mifugo. Wakati wa Sikukuu ya Nane Nane niliona ng'ombe wenye kilo 800 hadi 870. Hivi kama unenepeshaji huu wakawafundisha wafugaji na kuwakopesha, hatuoni tutawakomboa wafugaji hawa? Ahsante.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia mada hii kwa kuanzia na wakulima wa mwani. Nitazungumzia katika jiji la Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli wengi wanaoshughulika na shughuli hii ni wanawake. Kwa kweli inaelekea wanapoteza nguvu nyingi katika kilimo hiki wakati mavuno ni machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wanalima mwani bila kuwa na elimu ya kutosha na matokeo yake mavuno yanakuwa ni madogo lakini nguvu zilizotumika ni nyingi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kutueleza ni lini wakulima hawa wa mwani wa Mtaa wa Mwambani katika Jiji la Tanga watapatiwa mafunzo yanayostahili na pia kufanyiwa ufuatiliaji *(follow up)* wa yale waliyojifunza na utekelezaji wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ukanda wa Pwani yaani Tanga, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Pwani wanavuliwa samaki wengi na wazuri kama jodari, nguru, pweza, kamba na samaki wengine, kwa nini Serikali isiwe na mikakati ya makusudi ya kushawishi wawekezaji kujenga kiwanda cha kusindikia samaki wa maji chumvi, kama ilivyo Mwanza kuwa na kiwanda cha kusindika samaki wa maji baridi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wastani wa ulaji wa mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka 2008/2009, kwa kweli walaji wa mazao ya mifugo wanahitaji sana kula mazao yao, lakini tatizo ni umaskini uliokithiri kwa walaji hao. Kuna baadhi ya wakulima wa mifugo hiyo wanashindwa hata kunywa angalau kikombe kimoja cha maziwa kwa kuhofia kukosa kipato pindi atakapoyapunguza maziwa. Tunaiomba Serikali iwahamasishe wafugaji umuhimu wa kunywa maziwa au kula nyama kutokana na mifugo yao wanayoifuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la uvuvi, Serikali ina mipango gani ya kuwawezesha wale wavuvi wadogo wadogo? Wavuvi hawa hususan wanaovua katika ukanda wa Pwani ambao wanatumia uvuvi wa jua au uvuvi wa kutumia nyavu, wananyang'anywa nyavu zao na hao watu wa mazingira. Hilo halina ubishi, lakini wavuvi wafahamishwe ni nyavu gani zinazofaa kwa uvuvi badala ya kuwachomea nyavu zao bila ya kuwapa elimu ya nyavu zipi zinazofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kuhusu meli ya kigeni iliyokamatwa. Tunaelewa kuwa kesi iko Mahakamani lakini kuna samaki tani 296.3 wa aina mbalimbali ambao wamehifadhiwa katika jokofu. Samaki hao waliohifadhiwa lazima wawe wanalipiwa gharama fulani katika hayo majokofu. Kama samaki hawa wataendelea kukaa muda mrefu katika majokofu hayo, Serikali haioni kuwa itapata gharama kubwa sana ya kulipia kuliko pesa zitakazopatikana baada ya kuwauza kwa kucheleweshwa kuuzwa kwa samaki hao. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu ucheleweshaji wa kuuzwa samaki hao? Ni kitu gani kinachofanya samaki hao wachelewe kuuzwa?

**MHE. MARGARETH S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya ngozi vifufuliwe ili vizalishe ngozi. Ngozi itumike vizuri kama Ethiopia wanakotengeneza viatu, makoti ya ngozi, mifuko na kadhalika. Watanzania wenye kutaka kutumia ngozi kwa bidhaa mbalimbali wakajifunze Ethiopia.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya maziwa vilivyokufa vifufuliwe ili tuachane na yale yanayoletwa kutoka nje.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo nikiwa na afya njema na uwezo wa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo langu la Serengeti na mimi binafsi naomba kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu Prof. Haroub Othman na Kaimu Mufti, Sheikh Gorogosi. Naomba Mola aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Ameni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza kwa dhati, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa umahiri wake katika kuliongoza Taifa letu kwa kusimamia maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Mbunge, Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge na Mawaziri wote waliokwisha kuwasilisha hoja zao kwa hotuba nzuri walizotoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuongoza Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushirikiano wanaonipa katika kipindi chote cha uongozi ndani ya Bunge na nje ya Bunge hili. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Dr. Nyamulunda na Naibu Katibu Mkuu Dr. John Mwalyosi na Wakurugenzi wote wa Idara, kwa ushauri na ushirikiano mzuri wanaonipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Serengeti, kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa na uvumilivu wao kwangu na hasa wanaponikosa kwa shughuli mbalimbali. Naomba waendelee na moyo huo, nami naahidi kuendelea kushirikiana nao na kuwawakilisha hapa Bungeni na kwingineko.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru mke wangu na watoto, kwa kunipa moyo na kunivumilia na kuniombea dua ili niweze kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, sasa naomba nirudi kwenye kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Maji, Kilimo na Mifugo na Wabunge wengine, kwa michango yao ambayo mingi imetusaidia na itatusaidia sana kuboresha mikakati ya kutoa huduma ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia muda ni mfupi, nitajibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge walizochangia leo na wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha na Uchumi na zitakazobaki, zitajibiwa au kutolewa maelezo na Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hizi ambazo nitajibu, zimejikita katika maeneo mbalimbali. Hoja ya kwanza ambayo niitaongolea, ni upungufu wa Maafisa Ugani ambao Waheshimiwa Wabunge walisema kuna haja elimu itolewe kwa wafugaji. Katika mwaka 2008/2009, wafugaji 21,312 walipatiwa mafunzo kuhusu ufugaji bora. Pili kupitia mpango maalum wa kutoa mafunzo ngazi ya Stashahda na Astashahada, jumla ya wataalam wa Ugani 1001 wamehitimu, ambapo 658 wameajiriwa kama Wagani katika

Halmashauri hivyo kupunguza pengo la Wagani kutoka 13,301 hadi kufikia 12,643 kati ya jumla ya Wagani 16,000 wanaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa juu ya viwanda vya kusindika mazao ya mifugo. Hoja hii imechangiwa na Wabunge 17 na masuala yaliyojitokeza ni kwamba usindikaji wa maziwa umeshuka, viwanda vya kusindika maziwa vifufuliwe na vipya vijengwe. Katika hoja hii, Wizara inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo. Pili, kiasi cha maziwa kinachosindikwa kwa siku kimeongezeka kutoka lita 65,930 mwaka 2007/2008 hadi lita 88,940 mwaka 2008/2009 sawa na ongezeko la asilimia 34.9. Ongezeko hili limetokana na kuimarishwa kwa usindikaji katika viwanda vilivyopo na viwanda saba vipya vimeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kwamba Kiwanda cha *Brookside* kifanye kazi. Sisi ki-Wizara tunaendelea kufuatilia mwenendo wa kibiashara wa kiwanda hiki na pale ambapo tunaona kwamba kitakuwa kimeshindwa kutimiza masharti, Serikali haitasita kukichukulia hatua na kupewa mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kwamba viwanda vya kusindika ngozi vianzishwe na nyingine ni kwamba ngozi zisindikwe hapa nchini. Serikali imeongeza kodi kutoka asilimia 20 hadi kufikia 40 kwa ngozi kavu zinazouzwa nje ya nchi. Kutokana na hatua hii, viwanda vya hapa nchini vimeongeza uzalishaji hadi kufikia takribani asilimia 80 ya uwezo wa viwanda vya kusindika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo soko la ngozi limeporomoka kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani na baadhi ya viwanda vimesimamisha uzalishaji. Hadi mwisho wa mwezi Mei, 2009, jumla ya vipande 1,514,350 vya ngozi vilishindwa kusindikwa vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.4 vimeshindikana hata kuuzwa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kuhusu maeneo ya malisho na hili Wabunge walisema kwamba kutengwe maeneo ya ufugaji ili kudhibiti migogoro ambayo inajitokeza ili kuongeza tija. Hoja hii imechangiwa na jumla ya Wabunge 31.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya hekta 460,833 zimepimwa katika vijiji 28 za Wilaya tano za Liwale, Lindi, Kilwa, Kilosa na Nachingwea katika mwaka 2008/2009. Hadi sasa, jumla ya hekta milioni 1,391,109.4 zimetengwa kwa ajili ya ufugaji. Katika mwaka 2009/2010, maeneo ya malisho katika vijiji 40 yatapimwa katika Mikoa ya Rukwa, Dodoma, Singida na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lililojitokeza, kuna Waheshimiwa Wabunge waliopendekeza kwamba ni vizuri ng’ombe wakapelekwa kuchungwa katika Mbuga za wanyama na misitu wakati wa ukame au kiangazi. Matumizi ya ardhi katika hifadhi za mbuga za wanyama na misitu, yanasimamiwa na Sheria ya Hifadhi ya Wanyama, Sura Na.283 na Sheria ya Misitu Na. 10 ya mwaka 2002. Sheria hizi nasikitika kuwa zinazuia uchungaji katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kuhusu masoko na mauzo ya mifugo, hoja hii imechangiwa na Wabunge saba, hoja ilikuwa kwamba mifugo mingi inatoroshwa na kuuzwa nje ya nchi. Ili kutatua tatizo hili, Serikali imejenga minada ya mipakani na nchi zote jirani ili kuhalalisha biashara ya mifugo, minada hiyo ni pamoja na Kanshasa, Uhigwe, Lusumo, Mtukura, Magena, Wazo Longido, Pemba, Kakonko na Kileo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali vile vile imetekeleza mfumo wa utambuzi usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa kuanzia na Mikoa ya mipakani ili kudhibiti wizi na biashara ya mifugo isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nchi za Afrika za Mashariki na pembe ya Afrika, zimeanda Itifaki ya Kuzuia Wizi wa Mifugo (*Protocol on Prevention and Combating Cattle Theft)* ambayo inapendekeza nchi kutambua, kusajili na kufuatilia mifugo kwa mfumo unaobainisha mifungo ni ya nchi gani, kwa hiyo, hili litasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilikuwa mazao ya nchi ya Tanzania kutoonekana kwenye *super market*. Baadhi ya bidhaa za mifugo za Tanzania zinapatikana katika *super market* kwa mfano wa maziwa ya *ASAS*, Tanga Fresh na nyama ya Tanzania *Pride Meat, Interchick* zinapatikana katika *super market* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kuhusu mbegu bora za mifugo na hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge watano na hoja ilihusu uzalishaji wa mbegu bora ufanyike kwa wingi na vituo vya *NAIC* na vingine vitatu vya vya uhamilishaji vimeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madume bora 12 yamenunuliwa kutoka Afrika ya Kusini na Kenya kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mbegu bora. Vituo viwili vya uhamilishaji vimeanzishwa katika Kanda ya Kati, Dodoma na Mashariki Kibaha. Aidha, vituo viwili Kanda za Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa, Mwanza vimeimarishwa. Elimu ya uhamilishaji imetolewa kuhusu *NAIC* na pia kupitia Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu uzalishaji wa mitamba kwa ajili ya maziwa, hoja hii ilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge sita. Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba mitamba 8,607 imezalishwa katika mashamba ya Serikali na watu binafsi na kusambazwa kwa wafugaji. Katika mwaka 2008/2009, mitamba 334 ilisambazwa katika Kanda ya Kaskazini chini ya mradi wa *HPI* inayojumuisha Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza, ni kuhusu uvuvi katika Bahari Kuu. Hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wanne na ilikuwa inahusu udhibiti na uvuvi haramu unaofanywa na meli kubwa na nyingine ilihusu udhibiti wa uvuvi haramu unaofanywa kwa kutumia mabomu. Kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kanuni za kutekeleza Sheria Na.6 ya mwaka 2007 ya Mamlaka

ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, umekamilika na mamlaka ya kusimamia uvuvi katika bahari kuu *deep sea* umeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika mwaka 2008/2009, jumla ya siku za kazi, doria 76 zilifanywa kwa kutumia ndege na meli kwenye bahari kuu ambapo meli ya *Tawariq1* ilikamatwa. Katika mwaka wa 2009/2010, usimamizi wa doria katika bahari kuu utakuwa chini ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu. Vile vile kuanzia mwaka 2008/2009, Wizara imeweka utaratibu wa Halmashauri zote za ukanda wa Pwani, kuimarisha doria katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na kuzuia uvuvi haramu wa kutumia mabomu kupitia vikundi vya kusimamia rasilimali BMU.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kuhusu mikopo kwa wavuvi na hili lilihusu uwezekano wa kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wavuvi. Serikali inahamasisha wavuvi kujiunga na kuanzisha Vyama vya Akiba na kukopa kwa ajili ya kupata mikopo yenye masharti nafuu. Wizara kwa kushirikiana na *WWF*, inaanda mpango wa kusaidia wavuvi kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa katika Wilaya ya Kilwa, Mafia na Rufiji. Jumla ya benki za vijiji, VIKOBA 60 zimeshaanzishwa chini ya Mradi wa Mfuko wa Japan wa Maendeleo ya Jamii. Chini ya mradi wa *MACEMP SCULT*, ipo katika mchakato wa kuanzisha Benki ya Jamii katika Wilaya Rufiji, Kilwa na Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na muda niliopewa, naona niishie hapa, nafikiri hoja nyingine Mheshimiwa Waziri wangu atazijibu, nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja inayohusu Wizara yetu. Waliochangia katika ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara zilizotangulia walikuwa Wabunge 25, waliochangia kwa kuzungumza leo hapa Bungeni ni Wabunge 13 na waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 53.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda ni mfupi kwa sababu nimepewa dakika 30 tu, lakini naomba basi niwataje waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. Ni Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Michael Lekule, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Binilith Mahenge, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Khadija Salum,

Mheshimiwa Hemed Mohamed, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Charles Mlingwa, Mheshimiwa James Msekela, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa James Shibiliti, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Salim Hemed na Mheshimiwa Mohamed Sinani. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri waliyoitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, kwa muda huu uliopo, kwa wachangiaji wengi waliozungumza, ni vigumu sana kujibu hoja zao zote kwa dakika zilizobaki. Hata hivyo, nitazungumza kwa ujumla lakini nataka nianze kwa kusema kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge wote ilikuwa mizuri sana na kwa kweli imetuelekeza zaidi ni namna gani tunaweza tukafanya kazi katika kutekeleza azma hii inayohusu masuala ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, yamezungumzwa masuala ya migogoro ambayo imekuwa ikitokea kati ya wakulima na wafugaji. Nataka nilizungumze tu hili suala kwa ufupi sana. Nchi hii wakati tukipata uhuru ilikuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 949,000 *square* kilometa, wakati huo mifugo ilikuwa ni karibu milioni nane na binadamu walikuwa kama milioni 9. Kuanzia mwaka 1961 mpaka leo, Watanzania tumeshafikia karibu milioni 40 na mifugo kwa takwimu tulizonazo sasa hivi tuna ng’ombe zaidi ya milioni 19.1 kutoka milioni 18.8 tulizokuwa nazo mwaka jana, mbuzi walikuwa milioni 13.5 sasa tuna mbuzi milioni 13.8, kondoo wao wamebaki hivyo hivyo walikuwa milioni 3.6 na mwaka huu ni milioni 3.6, nguruwe wameongezeka walikuwa milioni 1.4 sasa tuna milioni 1.6, mbwa nao wameongezeka sasa hivi ni zaidi milioni 4, kuku walikuwa milioni 53 sasa tuna kuku milioni 56 ukiachia mifugo mingine. Kwa hiyo, ardhi imekuwa ni *constant* katika miaka yote na ndiyo maana migogoro hii imekuwa sasa ikianza kujitokeza kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka mwaka juzi tulipitisha Sheria hapa ya Matumizi Bora ya Ardhi Na.7 ya mwaka 2007, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwamba ni lazima sasa kila ardhi ianze kutumiwa kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli pia kwamba tatizo la mifugo limekuwepo na tatizo la wakulima na wafugaji limekuwepo kule Kilosa. Kwa mfano katika Wilaya Kilosa pamoja na kwamba Morogoro ina mifugo isiyozidi laki sita ukilinganisha na Shinyanga ambayo inaongoza kwa kuwa na mifugo zaidi ya milioni tatu ikifuatiwa na Mwanza ambayo ina mifugo karibu milioni 2.7, Arusha milioni 1.75, Manyara milioni 1.8, Morogoro ni zaidi ya laki tano lakini pamekuwa na migogoro sana ya kati ya wakulima na wafugaji. Katika Wilaya moja tu ya Kilosa, ukichukua takwimu za kuanzia mwaka 2000 mpaka sasa hivi, zaidi ya watu 50 wamekwishauawa na wengi wao ni wakulima, hii ndiyo hali halisi. Ndio maana Serikali kwa upande wake, kwa kutambua umuhimu huu na hasa kwa sababu pia maeneo ya malisho, ni kweli kabisa maeneo ya malisho ambayo yametengwa katika nchi yetu, yanayofaa kwa ajili ya malisho ni zaidi ya hekta milioni 50 lakini zilizotengwa ni milioni 1.3. Kwa hiyo, hii ni *challenge* kwa wakulima na ni *challege* kwa Serikali nzima. Ndio maana kwa busara nzuri za uongozi wa Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliunda Tume ili kusudi masuala haya yote yatatuliwe, yachambuliwe ili kusudi Serikali ije na jibu makini la kuweza kutatua hii migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ningeomba Bunge hili tusubiri hiyo Tume ya Mheshimiwa Waziri ifanye kazi zake na bahati nzuri zimehusika Wizara zote, Wizara ya Mifugo imehusika, Wizara ya Tawala za Mikoa inahusika, Wizara ya Ardhi inahusika chini ya usimamizi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nina uhakika baadhi ya matatizo mengine yataweza kuwa *solved* na ninaamini michango hii ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli ni mizuri sana. Wabunge wa Upinzani, Wabunge wa CCM, wote yaani mpo sawasawa kabisa yaani leo wote kwa pamoja mmetekeleza Sera ya CCM. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini yote yakienda kwa pamoja tutaweza ku-*solve* haya matatizo. Kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge mtukubalie hii bajeti yetu iweze kupitia. Ni kweli sisi katika mapendekezo yetu, tuliomba karibu shilingi bilioni 800 lakini tumepata shilingi bilioni 67, hii si haba unaweza ukapata kidogo, ukakitumia vizuri na kikaleta *impact*. Sisi tunachotaka kusema, hiki kidogo tulichopangiwa kitaleta *impact* ya kweli katika sekta hii ya uvuvi na mifugo. Kwa hiyo, mturuhusu tufanye kazi, tushirikiane na Wizara zingine, nina uhakika patakuwa na mabadiliko ya kutosha na hata sasa hivi mabadiliko yameshaanza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua muda wangu ni mfupi lakini nianze kwa kuzungumza kwa haraka haraka. Mheshimiwa Keenja kwa niaba ya Kamati, ametoa ushauri mwingi tu, amesema Wizara iendelee kufanya doria, yote haya ni safi tu. Changamoto ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji, yote tunakubali kabisa. Sekta ya mifugo ipewe umuhimu na Serikali, tunakubali kabisa, wafugaji wapatiwa maeneo ya mifugo kwa ajili ya mifugo yao, tumeshapima sasa hivi zaidi ya hekta milioni 1.39 tunaendelea na Tume imeundwa na tunaendelea kushirikiana na wenzetu wa Wizara mbalimbali, nina hakika haya yote tunakubaliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ranch* ambazo zimeshindwa kutumika vizuri wapewe wafugaji wengine na sisi tumeshawapa *notice* zaidi ya *ranch* 91, ambao walikuwa

wameshindwa kuendeleza. Wengine walikuwa wanazitumia zile *ranch* kwa ajili ya kilimo, notice zile zimekaa kwa miezi sita, zimeshaisha na sasa hivi tunafuatilia utekelezaji wake. Wale watakaoshindwa kutekeleza kwa mujibu wa maamuzi wa Baraza la Mawaziri Na. 2 la mwaka 2002, watanyang'anywa lakini baada ya kuwaandikia, *ranch* hizo sasa hivi wameanza kubadilika. Kwa mfano, kama Kagera palikuwa na *ranch* zilizokuwa zinakodishwa mpaka watu wa nchi jirani, kila ng'ombe analipa shilingi 50,000 lakini haya yote tunayafuatilia ili kuhakikisha kwamba *ranch* hizi zote 124 zilizobinafsishwa kwa watu, zinatumika kwa misingi na maamuzi ya sheria tulizojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maelekezo yote na ushauri wa Kamati sisi tunakubaliana nao kwa asilimia 100 na Kamati hii kwa kweli imekuwa inatusaidia sana katika masuala mengi katika kuendeleza sekta ya maendeleo ya mifugo na uvuvi. Kwa hiyo, nisingependa niweke chumvi au nini, tunakubaliana nao asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Abbas Jecha, naye leo amezungumza yale yale, ametushauri vizuri kabisa yaani ni yale yale yaliyoko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na nampongeza Mheshimiwa Jecha kwamba ameisoma vizuri Ilani ya Uchaguzi kwa sababu ushauri huu alioutoa ndiyo uko kwenye Ilani. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe Mheshimiwa Jecha kwamba sasa hivi tukienda kwa pamoja hivi, Kambi ya Upinzani na CCM, tutaleta maendeleo ya kweli katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nakupongeza ndiyo maana umezungumza mengi, umezungumza mikopo ya benki kwa wafugaji na sisi tumekuwa tukililia kwamba mabenki yote yaliyopo 33 katika nchi hii yaanze sasa kutoa mikopo kwa wafugaji pamoja na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema pawepo na mjadala na kitaifa, hiyo wala haina tatizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaunda Tume. Amesema pia pawepo na viwanda vikubwa kwa ajili ya mifugo, tumeanza kujenga pale Ruvu na wewe tulikukaribisha siku ile na ukala nyama za Ruvu *Ranch* siku ile, kinajengwa pale, yote hayo ni sawa tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya maziwa ni vingi vipunguziwe kodi, sasa hivi sisi tumeshaandika barua kwa Waziri wa Fedha, ili kuangalia ni kwa namna gani zile kodi zinazotolewa kwenye viwanda vya maziwa zinavyoweza kupunguzwa. *Actually* lengo letu ni kwamba kodi zinazotozwa kwenye maziwa yetu zifutwe zote, ndiyo mapendekezo tunayoyapeleka, ila yale maziwa yanayotoka nje yatozwe ushuru mkubwa kweli kwa sababu Tanzania imekuwa ni *damping area* ya kuleta maziwa kutoka nje. Tanzania ni ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi lakini maziwa yanatoka nchi nyingine ambazo tunawazidi mifugo. Kwa hiyo, nafikiri haya yote ni mapendekezo mazuri tu ambayo sisi kweli tunayakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto katika sekta ya uvuvi haramu, uhutaki kabisa upande wa upinzani na sisi tunasema uvuvi haramu hatuutaki kabisa na ndiyo

maana sasa hivi zaidi ya watuhumiwa zaidi ya 184 wamekamatwa na kesi zimepelekwa Mahakamani. Tumeweza kufunga mpaka kiongozi wa CCM kwa sababu mtuhumiwa awe wa CCM, awe CUF, awe wa CHADEMA akifanya uvuvi haramu lazima ashindwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na.22 ya mwaka 2003 na Kanuni za mwaka 2005 zitumike, haya yote tunakubaliana. Ninyi mnapinga uvuvi haramu, CCM tunapinga uvuvi haramu, Ilani ya CCM inapinga uvuvi haramu kwa hiyo mambo sawa sawa, kama mambo yanavyoenda, umeshakuwa CCM. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Job Ndugai ametoa pongezi kwa Wizara, kazi hii ya kupambana na uvuvi haramu imeenda vizuri na anasema nguvu hizi pia zielekezwe kwenye ufugaji. Mheshimiwa ndugu yangu Job Ndugai nakubalina na wewe, kwamba kwa sasa hivi lazima tuchukue hatua za kuhakikisha kwamba mifugo yetu inaleta thamani kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hatupigii hesabu lakini ebu tu-*imagine* mwaka huu tutazalisha mayai bilioni 1.7. Ikiwa kila yai tungekuwa tunaliagiza toka nje na tulinunue kwa shilingi 2, uzidishe mara bilioni 1.7, zingehitajika fedha za nje kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tumezalisha tani 422 za nyama. *Suppose* hizi tani 422 za nyama tungekuwa tunazinunua, kila kilo tungeinunua kwa shilingi ngapi na hasa kwa sasa hivi ambapo ulaji wa nyama nao umeongezeka. Kila Mtanzania anakula kilo11 za nyama kwa mwaka, tofauti na mwaka jana ambapo alikuwa anakula kilo 10. Sasa kama ni kilo 11 kwa kila Mtanzania, uzidishe Watanzania milioni 40 mara kilo 11 kwa mwaka, tungehitaji trilioni ngapi kuagiza hizo kilo za nyama?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Mtanzania anakula mayai 74, tofauti na 64 ya mwaka jana, zidisha 74 kwa kila Mtanzania mara milioni 40. Uchukue samaki, kila Mtanzania sasa hivi anakula karibu kilo 8, uzidishe kilo 8 mara milioni 40 kwa Watanzania wote, tungehitaji trilioni ngapi kuagiza samaki? Bado hujaweka ngozi, bado hujaweka maziwa. Maziwa, kila Mtanzania anakunywa lita 42, hata kule kwa Mheshimwa Mizengo Pinda, bahati mbaya ameondoka, wameongeza sasa hivi badala ya kunywa lita 8.1, zimesogeasogea angalau lita 9, ni karibu lita 42 kwa kila Mtanzania. Sasa uzidishe lita 42 kwa Watanzania milioni 40, ungehitaji trilioni ngapi katika kuagiza maziwa kutoka nje? Kwa hiyo, ukijumlisha hizi fedha zote, kila mwaka Tanzania ingehitaji trilioni 35 kuagiza mazao ya mifugo (vitoweo) kutoka nje ya nchi wakati bajeti ya Bunge lako hili, ni trilioni 9.5, watu tungekufa. Kwa hiyo, mifugo, samaki ni muhimu kuliko ambavyo sisi tunafikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo nchi zinazoagiza mazao haya nje, zinatumia mabilioni ya fedha. Kwa hiyo, sekta hii ni lazima iimarishwe, lazima izingatiwe na lazima isisitizwe na iwekewe nguvu zote kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wa pande zote walivyosisitiza hapa. Kwa hiyo, nakubaliana na ushauri wenu, Serikali tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ndugai amesema kwamba baadhi ya maeneo wanasumbuliwa, ametoa mifano mingi, Serikali ifuatilie dhuluma zilizofanyika. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaunda Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine tuimarishe masoko na viwanda, vyote hivyo tunakubaliana navyo na ndio maana sasa hivi kwa sababu wafugaji hawa saa nyingine tulikuwa tukiwalaumu kwamba wana-*move from one place* kwenda kwingine lakini baada ya *Tanganyika Packers* kufa, mwaka 1975 hawakuwa na mahali pengine pa kuweza kuuza mifugo yao, ndio maana kwa sasa hivi tumeamua tuanze kujenga viwanda sisi wenyewe. Kiwanda cha Ruvu kinajengwa na tunawahamasisha wananchi wengine, wafanyabiashara na wadau wengine waendele kujenga viwanda. Sasa hivi wameanza kuonesha nia nzuri, tukishaanza kujenga viwanda vingi vya nyama, vya maziwa, vya ngozi, nina uhakika tuta-*add value* kwenye mifugo yetu na kupata fedha nyingi na kuchangia kwa kiasi kikubwa badala ya kuchangia kwa asilimia 4.7 katika pato la Taifa na uvuvi kuchangia kwa asilimia 1.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote sisi tumejitahidi kwa kuyaboresha kwa pamoja kwa kuangalia pia na Sheria zetu. Mpaka hivi sasa tumeshapitisha Sheria ya Mifugo ya mwaka 2006, Sera ya Uvuvi ya mwaka 1997 na Sheria ya Uvuvi, Na.22 ya mwaka 2003. Tumeshapitisha Sheria nyingine nyingi; Sheria ya Ngozi, Na.18 ya mwaka 2008, Sheria ya Ustawi wa Wanyama, kwa sababu ni kweli kabisa katika hatua za kuwahamisha baadhi ya wafugaji kuna mambo mengine ambayo yalikuwa yanakiukwa ikiwa ni pamoja na Sheria ambazo zimepitishwa na Bunge hili. Unawachukua mifugo, unawaweka mahali fulani wanakaa kwa saa nzima au masaa kumi, unakuwa umevunja Sheria Na.19 ya mwaka 2008 ambayo imepitishwa na Bunge hili na mambo mengine mengi. Kwa hiyo, haya yote tumeyapitisha ili kuhakikisha kwamba tunaboresha sekta hii ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sheria ya Maziwa Na.8 ya mwaka 2004, Sheria ya Nyama Na.10 ya mwaka 2006, Sheria ya *Veterinary* Na.16 ya mwaka 2003, Sheria ya Ngozi Na.17 ya mwaka 2009, Sheria ya TAFIRI Na. 6 ya mwaka 1980 na Sheria nyingine chungu nzima. Lakini kwa sasa hivi tuko pia kwenye hatua ya kupitisha Sheria ya Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo katika kulinda mifugo yetu, kuna Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji. Hizi Sheria sasa zote ziko kwenye *Cabinet*, nina hakika mwaka huu, tutazileta hapa Bungeni ili ziweze kujadiliwa, ili kusudi Sheria zetu na kazi zetu tunazozifanya katika sekta hii ziweze sasa kuboreka vizuri na kuweza kuleta *impact* kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna Bodi mbalimbali ambazo sasa hivi zimeanza kufanya kazi, kutokana na muda nisingependa kuzitaja zote.

Mheshimiwa *Engineer* Manyanya ametoa shukurani nyingi, amezungumzia juu ya unyanyasaji wa wafugaji na wavuvi na kadhalika kwamba Sheria lazima zizingatiwe na mimi nakubaliana kabisa kwamba Sheria lazima zizingatiwe. Hata kwa Mungu kuna Sheria, kuna Amri 10, kwenye *Quran* kule kuna Sheria, kwa hiyo Sheria zote zipo. Unaweza ukaambiwa usizini baadaye tena ukamwona mwanamke ukazini, lakini Sheria

zipo. Kwa hiyo, Sheria ni vizuri zizingatiwe na ndio maana tunazungumzia masuala ya Sheria na mimi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Manyanya kwamba Sheria ni muhimu na ndio maana Bunge hili lipo kwa ajili ya kupitisha Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameshukuru kuhusu boti za Ziwa Nyasa. Amesema boti zinasemwa ni za doria, tumetoa boti zile kwa ajili ya kusaidia doria lakini pia zitasaidia katika mambo mengine mbalimbali ambayo yatakuwa yakifanyika katika Ziwa Nyasa; ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wananchi kuhusu uvuvi wa kisasa ili waweze kuzalisha kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amezungumzia kuhusu usumbufu kwa wafugaji, migogoro ya wakulima ambayo tayari nimeshaizungumzia. Lakini mwisho ametoa pongezi na mimi pia namshukuru Mheshimiwa Manyanya, kwa pongezi zake lakini tunashukuru pia kwa michango ambayo ameitoa. Sisi tutaizingatia katika kuhakikisha tunaleta maendeleo ya kweli katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ole-Nangoro ametoa pongezi kwa Wizara, lakini amesema tangu tupate uhuru, mifugo haijapewa umuhimu wa kutosha. Si kweli, kwa sababu sekta ya mifugo inapewa umuhimu na ndio maana na mimi nipo hapa naitwa Waziri wa Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi. *Otherwise* ningeitwa Waziri wa Uvuvi tu, lakini sasa na mifugo ipo, ng'ombe zile ambazo ziko kule. Kwa hiyo, umuhimu upo, lakini katika kuthibitisha umuhimu huu, mwaka jana katika fedha za *EPA*, zilitolewa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kununulia madawa ya mifugo tu; wala hazikutolewa kwa ajili ya kununulia madawa ya samaki. Kwa hiyo, angalau hili basi tungeanza kushukuru kwamba Serikali imeshaanza kuona umuhimu wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia amesema mifugo ni kila kitu na mimi nakubaliana na yeye kabisa viatu, mikanda, mabegi, ardhi na kadhalika, ni kweli kabisa, lakini kwa hatua hizi ambazo tumeanza kuzichukua, nina uhakika sasa sekta ya mifugo imeanza kujitokeza na inaweza ikasaidia sana katika kuchangia pato la Taifa. Kwa hiyo, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge bado tunauchukua na tutahakikisha tunauzingatia na kuhakikisha kwamba tunashughulikia haya matatizo ambayo yamekuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amezungumzia juu ya matatizo ya malisho, maji kwa ajili ya mifugo, kwa bahati nzuri kupitia mradi wa *DADPS*, ambao upo chini ya TAMISEMI, tunashirikiana nao katika kuhakikisha kwamba yanachimbwa mabwawa ya kutosha. Lakini ni kweli katika mradi huu wa *DADPS*, baadhi ya mabwawa yamekuwa yakichimbwa, ya ajabu sana na fedha zingine zimekuwa zikiliwa huko huko. Sasa hivi tumeshapanga mikakati kwamba Wizara yangu itaanza kufuatilia, hata kama zile fedha zinapelekwa Tawala za Mikoa, lakini Serikali ni moja ili kusudi tuhakikishe yale mabwawa yanayochimbwa kule, basi ni mabwawa yanayolingana na kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa wito sasa kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri, katika nchi hii, wazitumie vizuri fedha za *DADPS* katika kuchimbwa mabwawa, kwa sababu watu wangu sasa hivi nitaanza kuwatuma, kila bwawa wanalikagua, ukisema ni la shilingi milioni 25 lakini kumbe ni la shilingi milioni tano,

tutaleta ripoti kwa waliokuajiri ili Mkurugenzi uweze kufukuzwa kwa sababu ya bwawa. Nina uwakika kwa njia hii, itawasaidia watu wanaotumia vibaya fedha za *DADPS* kujipanga vizuri na kuzitumia vizuri fedha za Serikali, ili mabwawa sasa yaweze kuonekana katika maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, umezungumzia pia suala la bajeti kuwa ndogo, mimi nakushukuru kwamba umenisemea na kweli ni ndogo tu, tulitaka shilingi bilioni 800, tumepewa shilingi bilioni 67 lakini ndio hivyo, pole pole. Tutazitumia vizuri, nina uhakika siku nyingine tutapewa nyingi na hasa kwa sababu wewe umezungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya ya mifugo ni vyema ikaboreshwa, yote haya ni michango mizuri tu. Kilimo Kwanza kiendane na Mifugo Kwanza, nafikiri hiyo ndio maana yake na ndio maana Waziri Mkuu kila siku amekuwa akizungumza, Kilimo Kwanza, Mifugo Kwanza na Uvuvi Kwanza. Kwa hiyo, hivi vyote vitaenda kwa pamoja na nina uhakika italeta *impact* nzuri katika maendeleo ya Watanzania na hasa kwa sababu wako wafugaji ambao pia ni wakulima, wako wafugaji ambao pia ni wavuvi na ni wakulima. Kwa hiyo, sekta hizi zote tatu huwezi ukazitofautisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la masoko ni vyema likaangaliwa vizuri, ni ushauri mzuri tu na mimi nakubaliana na wewe kwa asilimia 100. Ndio maana nimesema ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli ni mzuri sana na nina uhakika sisi tutaufanyia kazi katika kuhakikisha kwamba tunaboresha sekta hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Clemence Lyamba ametoa pongezi, ametoa shukurani, anasema wakulima wamenyanyaswa sana na wafugaji, msema kweli ni mpenzi wa Mungu, Kilosa ni tatizo na mimi kwa kweli kwenye suala la Kilosa, pamoja na kwamba kuna matatizo ambayo yamejitokeza, lakini nimetoa takwimu hapa kuanzia mwaka 2000 mpaka sasa hivi, watu karibu 50 wameuwawa kule Kilosa na wengi wao ni wakulima. Ukichukua kwa mfano katika kijiji cha Mwabwegere, Kilosa, walikufa watu karibu 10, mfugaji alikuwa mmoja. Kwa hiyo, ndio maana nasema haya yote yanatakiwa kuangaliwa kwa pamoja ili sisi kwa pamoja tuweze kutatua matatizo haya kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele nimeshapigiwa hapo, Mheshimiwa Cheyo naye ametoa pongezi, ushauri wake ni mzuri tu, nakubalina naye, unapozungumzia ng'ombe unazungumzia mkulima, Wasukuma wametajirika kwa sababu ya ng'ombe na hii ni kweli kabisa na wewe ni tajiri kwa sababu hata wewe una ng'ombe. Tatizo la matumizi ya ardhi umetoa ushauri, yaani leo michango yote ilikuwa ni ku-*support* tu, Mheshimiwa Cheyo, usingekubali kama ni wa *UDP*, ungeona ni wa CCM tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Cheyo, kaka yangu, ushauri wako ulioutoa, ninakubaliana na wewe na sisi tutaufanyia kazi. Hongera sana na tunakupongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, umezungumzia kuhusu Ranchi, tuweke viwanda vya nyama, yaani ushauri ni mzuri tu. Kwa hiyo, sina cha kuongeza bali nakushukuru kwa ushauri wako mzuri na tusifanye ubaguzi kwa sababu ya ng'ombe na mimi nakubaliana

na wewe kabisa. Hakuna sababu ya kufanya ubaguzi hapa kwa sababu ya ng'ombe au mbuzi au nguruwe au kondoo au nini au mbwa na kadhalika sisi wote tupo pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Msafiri, ametoa pongezi sana na mimi namkushukuru sana Mheshimiwa Mbunge lakini amezungumzia kuhusu suala ambalo linamtatiza katika maeneo yake. Naomba tu nizungumze kuhusu suala hili. Wakati wa Bunge lililopita, katika mgogoro huu, nilimwomba dada yangu, Mheshimiwa Msafiri, kwamba tungependa sana tatizo la Kagoma tulitatue *administratively* na nikawa nimemwomba na *Hansard* za mwaka jana zinasema kwamba ninakushauri wale walioishtaki Serikali, wakatoe ile kesi Mahakamani ili kusudi tuweze kulitatua tatizo hili kiutawala. Sasa ni mwaka mzima, kesi ile haijafutwa. Sasa kwa sababu kesi haijafutwa na mimi sina mamlaka ya kuingilia Mahakama, Mahakama imekuwa ikifanya kazi yake kama Mahakama na ndio maana maombi ya shauri hili yalipokelewa Mahakama Makuu, Kitengo cha Ardhi, tarehe 19 Desemba, 2007; lakini mnamo tarehe 7 Januari, 2008, Mahakama ilitoa uamuzi wa kuzuia kwa muda wadai kuondolewa kwenye ardhi yenye mgogoro mpaka shauri la maombi litakaposikilizwa tarehe 4, Februari, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niinukuu sehemu ya amri hiyo, inasema:-

*"In the mean time, status quo to be maintained pending hearing of application on 4th February, 2008"*.

Sasa ilikuwa tarehe 4 Februari, 2008 leo ni tarehe 3 Julai, 2009. Sasa mimi siwezi nikazuia maendeleo mengine yaliyokuwa yanatakiwa kufanyika. *NARCO*, yuko pale kwa mujibu wa Sheria C*ap*.212, ya mwaka 1968. Kwa hiyo njia nzuri kwa sababu wale watu wameona ni ya Mahakama, waendelee kule na *NARCO* ina mamlaka ya kushtaki au kushtakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu hili suala lipo Mahakamani na mimi nisingependa kulitolea maamuzi; wale wahusika wa Kagoma waendelee na Mahakama. Ikiwezekana waendelee kuishtaki *NARCO*, wakiamua wafungue kesi nyingine leo, waamue vyovyote, Mahakama itatoa maamuzi yake, lakini mimi hili siwezi nikaliingilia tena, kwa sababu nilitoa ushauri wangu, kwamba wale watoe kesi Mahakamani ili kusudi tulishughulikie *administratively* na tumefanya hivyo katika *West* Kilimajaro na maeneo mengine, wale watu hawakuitoa, sasa sina lingine la kusema kwa sababu suala lipo Mahakamani, tuiache Mahakama ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lekule naye amezungumzia masuala mengi tu kuhusu mifugo, wote ni ushauri mzuri kwamba tunakimbilia juu ya *land mark*, kwa nini tusiangalie kwanza wafugaji wakapata maeneo ya ufugaji? Mheshimiwa Teddy Kasella – Bantu, naye amezungumzia mambo mengi tu kuhusu mifugo. Pia amezungumzia kuhusu ufugaji wa samaki na katika kitengo chetu cha Wizara, tumetenga fedha kwa ajili ya kuanzisha ufugaji wa samaki katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, yote tu tunakubaliana nayo.

Mheshimiwa Telele naye amezungumzia mengi tu kuhusu wafugaji na ameonyesha *concern* zake nyingi na ushauri mwingi. Kwa sababu ya muda, nashindwa kuzungumza namna gani nijibu kila hoja. Ninachotaka kusema ni kwamba, haya yote tutayazingatia na tutawajibu kwa maandishi Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na waliochangia kwa kuandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Prof. Mtulia, naye amezungumzia yake mengi kuhusu mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshabonyezewa hapa kwamba muda wangu umeisha, napenda tena kukushukuru wewe, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Vyama vyote, kwa michango mizuri sana iliyotolewa katika hotuba yetu. Michango hii, itatusaidia kuhakikisha kwamba sekta ya mifugo na uvuvi inaenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja na nina kushukuru sana na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, wanipitishie hizi hela ili twende tukafanye kazi. Ahsante sana.

*(Hoja Iliamuliwa na kuafikiwa*)

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na kuungwa mkono, sasa tunaingia hatua inayofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

## FUNGU 99

## WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

*Kif. 1001 – Administration and General … .....  Shs. 3,400,038,700.00*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Zarafi Mwanawetu, Mheshimiwa Balozi Mongella, Mheshimiwa Serukamba anaanza.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiyo *programu 10,* Vote 99, *sub-vote 1001 Administration and General,* mshahara wa Waziri. Juzi Serikali imenunua boti za *patrol kwa* ajili ya Ziwa Tanganyika, Ziwa Tanganyika liko *covered* mikoa miwili kwa maana ya Rukwa na Kigoma na zimekuja boti mbili, ni jambo jema sana na tulishangilia sana lakini katika mastaajabu ya watu wa Kigoma na ambao kila siku tunaibiwa mali zetu kutoka watu wa nchi za jirani, boti zote mbili zimepelekwa sehemu moja ya Mkoa wa Rukwa. Mimi hilo sina shida nalo, nilitaka tu Mheshimiwa Waziri aniambie sasa au atupe ufafanuzi kwamba ametumia vigezo gani, ukiangalia kilomita za ku-*cover* ziwa hilo, nyingi sana ziko upande wa Kigoma lakini

boti mbili zimeenda upande mmoja wa Rukwa ambalo ni jambo jema, sasa na sisi watu wa Kigoma tutapata lini hizo boti maana inaonekana hizo mbili ziko kwa ajili ya Rukwa peke yake, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo boti ni za Ziwa Tanganyika, siyo za Kigoma siyo za Rukwa. Tulipokuwa tunazitoa siku ile ya sherehe, bahati mbaya Mheshimiwa Serukamba hakuwepo, hata Mbunge wa Kigoma alitoa maneno yake kushukuru, kwa hiyo, hizo boti zitakuwa zina-*patrol* katika Ziwa Tanganyika. Sasa kama zilifika Ziwa Tanganyika, akaziona zinaenda Rukwa haina maana kwamba zinabaki huko huko, zile ni kwa ajili ya Ziwa Tanganyika, hata hotuba yangu niliyoitoa ilizungumza hivyo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Mwanawetu.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 99, sub-vote 1001 Item 2010100.* Nilipoandika kwenye mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeelezea kuhusu unyanyasaji unaofanyika na Jeshi la Doria. Watu wote tunafahamu kwamba Jeshi, kazi yao ni kufanya doria lakini kinachofanyika sasa hivi, Jeshi lile linawanyanyasa wananchi, wavuvi wadogo wadogo na hii imetokea katika mji wa Mchinga ambako wavuvi wenye nyaraka zote zilizo halali, nyavu halali, wamekamatwa kwenye maji na kunyang'anywa shilingi laki nane ambayo waliigawa katikati na wakachukua pia samaki, wakagawa nusu pia na kuwazamisha kwenye maji mafupi. Sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, hii ndiyo Sheria ambayo Askari hawa wa Jeshi la Doria wameambiwa waifuate au ni maamuzi yao na kama si hivyo basi nataka Mheshimiwa alieleze Bunge hili kazi yao ni nini, kama siyo hiyo ya kuwanyanyasa wananchi? Ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii nimeipata leo. Lakini katika mchango wake wa maandishi tulipewa nusu saa tu, kwa hiyo nisingeweza kujibu michango yote ya maandishi ambayo ni 52. Kazi inayofanywa na Kikosi cha Doria ni kusimamia Sheria Na. 22 ya mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2005. Sasa kama yupo ambaye amefanya tofauti na hiyo, wale walioharibu na kuvunja hiyo Sheria kwa vile vyombo vya Sheria vipo wanaweza wakapelekwa Mahakamani. Kwa sababu *whether* ni Jeshi la Polisi, Jeshi la namna gani, doria anapovunja Sheria anapelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningewashauri wale walionyanyaswa, inawezekana labda wala siyo Jeshi la Doria labda hata majambazi wa Mchinga kule na kadhalika, siwezi nikafahamu. Lakini ninachosema Sheria ziko wazi kwamba mtu anayevunja Sheria awe hata Waziri anapelekwa Mahakamani. Kwa hiyo, ningekushauri wale waliodhulumiwa kama wanawatambua waliowadhulumu wawapeleke Mahakamani. Kwa sababu katika taratibu za Sheria hata anaposhikwa mtu na nyavu haramu ni lazima kwanza apelekwe Mahakamani kusudi Mahakama ikachukue maamuzi yake. Ndivyo tulivyokuwa tukifanya katika operesheni zote. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Ahsante Mwenyekiti. Fungu *99, Sub-Vote 1001 na item 200100,* nimwulize Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi kwa imani kwamba Waziri Magufuli ana uwezo wa kutatua matatizo akitaka, anao uwezo mkubwa. Mimi nina imani kwa kumpa hizi pesa hapa, itamwezesha kufanya kazi pamoja na timu yake.

Sasa mimi tangu niwe Mbunge katika Visiwa vya Ukerewe, nimefanya kazi kubwa ya kuhamasisha wavuvi waache uvuvi haramu na kuna wakati niliongeza maelezo ya kwamba wavuvi wa Visiwa vya Ukerewe wapo ambao wameanza kurudisha zana haramu kwa hiari yao hasa wa Chibasi na Chifure ambako Mheshimiwa alishafika wakamtunuku ng'ombe mweusi asiye na doa ikiwa ni ishara ya kumwamini. Mheshimiwa Waziri unieleze mradi wako huu wa doria umekuwa ni maficho ya wafanyakazi wa Maliasili pamoja na Polisi kuwavamia wavuvi na kuchukua pesa au kuchukua nyavu na kuziuza kwa watu wengine na wenyewe wanakuja kuwavamia tena? Imekuwa ni mradi, nimelalamika tangu niwe katika Bunge hili wakati wote na inatuvurugia kazi ya kupambana na uvuvi haramu. Sasa hii pia inafanya sisi tusiweze kuaminika ambao tuko pamoja nawe katika kupambana na uvuvi haramu kwa sababu ya wale wala rushwa walio katika Wizara yako wakishirikiana na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki hii nimepata simu nyingi kutoka Visiwa vinavyoanzia Ukara, Sizu, Kwelu mpaka Ilugwa, watu 21 katika Kisiwa cha Ilugwa walivamiwa na hao Wanadoria Polisi wakiwemo na Maofisa Uvuvi, wakaombwa hela za hongo. Ninaomba ufafanuzi ili uweze kupata pesa na ufanye kazi vizuri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Balozi Mongella, kwa hatua nzuri anazozichukua katika kuwahamasisha wananchi wa Ukerewe katika kupambana na uvuvi haramu. Lakini kama nilivyosema, Wizara yangu ni msimamizi wa Sheria Na.22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2005. Tunapofanya doria, pia huwa tunahusisha watendaji wengine katika Halmashauri ikiwepo Halmashauri ya Ukerewe na maeneo mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni kweli kwamba walipokwenda kushikwa walitoa rushwa na rushwa ni kosa, mimi nafikiri nitumie nafasi hii kuwaelimisha wananchi wa Ukerewe, wapiga kura wa Mheshimiwa Getrude Mongella, kama wanaombwa rushwa waende wakafungue kesi na kuwashtaki hawa wahusika na wao wasimame kupitia hata *Beach Management Units* zao ambazo kwa bahati mzuri hata Ukerewe zipo na katika Ziwa Victoria ziko zaidi ya 506 katika kuhakikisha kwamba wanapambana na vita ya rushwa. Vita ya rushwa ni ya kila Mtanzania, kila mtu ili kusudi dhuluma hii isiweze kutendeka. Kwa hiyo, naweza nikamshauri kwamba wakati wanapambana na uvuvi wa haramu waendelee pia kupambana na rushwa ambayo inaweza ikafanywa na baadhi ya Watendaji ambao siyo waaminifu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kanuni zetu za safari hii zimeleta matatizo. Ni mara moja tu. Tunaendelea, endelea Katibu.

*Kif. 1002 – Finance and Accounts ... .... Shs. 529,780,900.00*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 1003 – Policy and Planning ... .... Shs. 852,829,200.00*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nikichangia kwa maandishi, nilielezea jinsi gani zoezi la uhamisho wa mifugo lilivyoleta madhara kwa wafugaji, jinsi gani watendaji wa Serikali walivyojichukulia madaraka kunyanyasa wafugaji, kuwapora mifugo yao na kujilimbikizia mali…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya, nisikilize, hebu kaa chini. Kifungu unachoweza kusema bila kutaja kifungu kwa sababu unamwajibisha Mheshimiwa Waziri, ni hiki cha mwanzo. Ukija vifungu vingine vyote lazima utuambie *sub-item* unayozungumzia maana tunaweza tukasema maneno yote kila mahali kumbe siyo penyewe, tafadhali.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa maelekezo hayo. Ni *sub-vote 1003, item 221200 Communication and Information.*

Nilitaka nipate tu taarifa, wakati nachangia, nilielezea jinsi gani zoezi la uhamisho wa mifugo lilivyoleta matatizo kwa wafugaji na kwamba zoezi hili limepelekea wafugaji wengi kufilisika na wengine kupoteza maisha. Ninavyofahamu Serikali imeshaunda Kikundi Kazi cha kufuatilia suala hili na sasa hivi ni muda mrefu lakini taarifa...

**MWENYEKITI:** Tunaomba urudie tena kifungu, sisi hatujakupata.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** *Sub-vote 1003, item 221200 Communication and Information.*

**MWENYEKITI:** Hebu eleza sasa tukusikilize.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimeeleza kwamba wakati nachangia kwa maandishi, nimeelezea zoezi la uhamisho wa wafugaji hapa nchini lilivyoleta madhara kwa wafugaji. Watendaji wa Serikali wametumia zoezi lile tofauti na walivyopewa maelekezo, wamenyanyasa wafugaji, wamewapora ng'ombe zao na wengine mpaka leo wameendelea kupata madhara na kwamba Serikali imekwishaunda Kikundi Kazi na ni muda mrefu umepita, kwa hiyo, tungependa kujua kama taarifa ya Kikundi Kazi imetoka kwa sababu bado mpaka sasa hivi wanaendelea kunyanyasika na hawajui hatima yao. Kwa hiyo, napenda Serikali itupe majibu kwamba baada ya taarifa ile kama imekwishapatikana, nini hatima ya

wafugaji hawa na wale Watendaji ambao wamesababisha matatizo haya, wamechukuliwa hatua gani? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, umesema lakini siyo kifungu hiki. Unajua huku kwanza ni *policy issues*, sasa hapa ni *policy and planning* ya ndani ya Wizara, siyo suala tena la huko mitaani. Umesikika lakini hatutakujibu maana siyo mahali pake, tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Livestock Research and Training Institute .....................................................................Shs.5,351,401,400.00*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti, si kifungu hiki lakini kitakapokifikiwa, nitatoa maelezo kidogo, ahsante, samahani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Information, Communication and Education.…................................ Shs.171,360,000.00*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan, mbona husimami haraka?

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu maelezo kwa sababu sioni mishahara ya watu hawa, naomba kujua ni nini au hawa watu wamehamishwa?

**MWENYEKITI:** Huoni nini?

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** *Basic salaries.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri una maelezo hapa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Wapo *administration*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 1006 – National Livestock Institute – Mpwapwa …......................................... Shs. 3,474,447,400.00*
*Kif. 1007 - Internal Audit Unit …...................... Shs. 137,740,000.00*
*Kif. 1008 – Procurement Management Unit..... Shs. 201,523,000.00*

*Kif. 1009 – Legal Services Unit ................................ Shs. 133,540,000.00*

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 7001 – Veterinary Services ......................... Shs. 10, 475,776,000.00*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya taarifa tu, katika kifungu hiki cha *sub-vote 7001*

**MWENYEKITI:** 7001?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** *Sub-Vote 220400 – Medical Supplies and Services.* Kifungu hiki kinaonyesha shilingi bilioni 4.8 na kadhalika lakini wakati tukiongea na Kamati na tulikubaliana kwamba kwa sababu hizi fedha katika bajeti ya fedha za *EPA* shilingi bilioni 10 zote zilitolewa zikatumika kwa mifugo kwa ajili ya kununulia madawa. Kwa hiyo, hapa tunapunguza shilingi bilioni 1.5 ambazo zinaenda kwenye uvuvi kwa ajili ya kushughulikia doria na uvuvi na kadhalika. Kwa hiyo, tumeshawasiliana na Wizara ya Fedha na wataleta marekebisho baadaye, nilitaka nitoe taarifa kwa ajili ya Bunge hili.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo hesabu inayosomeka kifungu cha mwisho ni ngapi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Itapungua shilingi bilioni 1.5, kwa hiyo, itakuwa shilingi bilioni 4,839,000,000 kutoa bilioni 1.5.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho)*

*Kif. 7002 – Livestock Identification,*
*Registration A …................................................ Shs. 309,345,000.00*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 7003 – Pastoral System Development ....... Shs. 436,150,000.00*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote 7003,* kifungu kidogo cha *2001200 – communication and information.*

Kifungu hicho, fedha zilizotengwa ni kidogo sana ni 240,000 tu wakati kifungu hiki kinahusu kuwaelimisha wafugaji kuhusu madhara ya uharibifu wa mazingira, suala la kufuga kwa mpango, kuvuna mifugo na mambo ya namna hiyo lakini pia wafugaji wafahamu kwamba dunia hii tunaihitaji wote na ni lazima wakulima waendelee ili tuweze kupata chakula kwa ajili ya kulisha Taifa hili. Lakini pamoja na kwamba Wabunge wengi wanazungumzia kwamba wafugaji wameonewa lakini na wakulima nao pia wameonewa sana kwa sababu maeneo yao yamevamiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge…

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mimi ninachoomba ni maelezo …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, sio mahali pake, ungetaka kutupiga hotuba sisi, ungekwenda kile kifungu cha utawala, hapa uulize tu hizi shilingi 240,000 ni za kazi gani maana ni kidogo sana. Hilo ndiyo swali, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo hiki cha *Pastoral System Development*, hizi shilingi 240,000 ndizo zinazowatosha na ndiyo maana tumeweka hivyo, kwa sababu katika maeneo mengine *communication* na *information* tumezipeleka kwenye *administration* pamoja na kwenye *policy*. Kwa hiyo, tuliona hizi ndizo zinatosha kwa Kitengo hiki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7004 – *Central Veterinary Laboratories* ...... Shs. 2,631,870,000.00
Kif. 8001 – *Animal Production* ................................ Shs. 2,721,795,400.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 9001 – Fisheries Development Division........ Shs.4,775,857,000.00*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na zile fedha ambazo tulizipunguza kule, shilingi bilioni 1.5, shilingi bilioni 1 inaongezwa sasa kwenye kifungu *220300 – Fuel, Oil and Lubricants*. Kwa sababu hii itahusika na ununuzi wa mafuta na kadhalika kwa ajili ya kufanyia doria. Kwa hiyo, katika zile milioni 618,934,000 tunaongeza bilioni 1. Kwa hiyo inakuwa bilioni 1,618,934,000.

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho)*

*Kif. 9002 – Aquaculture Development Division...... Shs. 1,650,000.00*

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 99**

**WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**

*Kif. 1001 - Administration and General .............. Shs. 124,627,300.00*
*Kif. 1003 – Policy and Planning .............................. Shs. 1,670,147,100,00*
*Kif. 1004 – Livestock Research and Training Institute …............................................ Shs. 4,503,620,000.00*
*Kif. 1005 – Information, Communication and Education …...................................................................... Shs. 0*
*Kif. 1006 – National Livestock Institute – Mpwapwa …........................................... Shs. 2,011,606,200.00*
*Kif. 7001 – Veterinary Services ................... Shs. 5,097,648,600.00*
*Kif. 7002 – Livestock Identification, Registration A …..................................... Shs. 434,368,000.00*
*Kif. 7003 – Pastoral System Development ........ Shs. 651,260,000.00*
*Kif. 7004 – Central Veterinary Laboratories ...... Shs. 1,406,348,900.00*
*Kif. 8001 – Animal Production .......................... Shs. 2,828,700,000.00*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*Kif. 9001 – Fisheries Development Division .... Shs. 10,652,590,000.00*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafahamu kwa kuwa shughuli za kifungu hiki zinafanyika …

**MWENYEKITI:** Zitaje, kifungu gani?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** *Item* 9001, shughuli zake zinafanyika hasa katika fukwe za Bahari ya Hindi na kwa kuwa tatizo la mazingira liko hata kwenye fukwe za maziwa, je, Serikali ina mpango gani wa kuwa shughuli za aina hiyo zipo pia katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo ya maziwa mengine aliyoyazungumzia, tumeshamaliza kupitisha katika *Volume II, Estimates.* Hili linahusiana na mradi wa *MACEMP* ambao unafadhiliwa na *World Bank.* Kwa hiyo, ni mradi mahususi kwa ajili ya kushughulikia Halmashauri 13, kuanzia Moa hadi Msimbati zaidi ya kilometa 1,422 na wala si maji ya maeneo mengine. Maji ya maeneo mengine fedha zake tumeshazipitisha kwenye Kitabu cha *Volume II, Estimates.*

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*Kif. 9002 – Aquaculture Development Division ..... Shs. 699,624,000.00*

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na marekebisho yake niliyoyataja. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, makadirio ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi yamepita bila kupingwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili. Kwanza kesho saa tatu tutaendelea na Bunge ili kuweza kukamilisha makadirio ya Wizara ya Miundombinu.

Tangazo la pili, leo Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Faida Bakar, amefiwa na kaka yake huko Pemba, kwa hiyo, Ofisi imemwezesha kuondoka na kwa hiyo hayupo kutokana na msiba huu. Kwa hiyo, tunamwombea marehemu alale mahali pema Peponi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, sina shughuli nyingine, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.06 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumamosi tarehe 4 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*